

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Arobaini – Tarehe 31 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Arobaini.

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

### **MHE. ALOYCE J. KAMAMBA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamamba, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Katibu.

### **NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 331

**Kuunganisha Mifuko ya Mikopo Iliyo Chini ya  
Ofisi ya Waziri Mkuu**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha mifuko ya mikopo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuwezesha makundi maalum kupatiwa mikopo kwa urahisi zaidi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, VIJANA NA  
AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo yako, lakini pia kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kujibu swalii la Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaona umuhimu na kupitia Mheshimiwa Rais iliagiza na kuelekeza mifuko kuweza kuunganishwa na kufuatia maelekezo hayo, Serikali iliunda kamati ya pamoja iliyohusisha Wizara zote zinazosimamia mifuko hiyo, kwa ajili ya kufanya tathmini ya utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kupima utendaji wa mifuko na programu hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo, mapendekezo mbalimbali yametolewa kwa ajili ya kuboresha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi ikiwa ni pamoja kuunganisha baadhi ya mifuko yenye majukumu na malengo yanayoshabihiana. Taarifa ya tathmini hiyo inaendelea kufanyiwa kazi ndani ya Serikali kwa hatua zaidi ili hatimaye kuiunganisha na kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu imekwishatekeleza agizo hilo kwa kukamilisha tathmini ya mfumo wa kiutendaji wa mifuko hiyo na baada ya kuunganishwa, mtazamo mpya wa muunganiko wa programu na mifuko husika na utekelezaji wake utaanza baada ya mamlaka kuridhia, asante.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa muuza swalii, Mheshimiwa Santiel.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango wowote wa kuzigawanya fedha hizi katika Halmashauri hususan zile Halmashauri ambazo makusanyo yake yamekuwa madogo katika asilimia 10 ambazo zinatengwa. Halmashauri hizo mfano ni Wilaya yetu ya Shinyanga Vijijini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa nini Serikali isiongeze zile asilimia kutoka asilimia 10 mpaka tano kwa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

wanawake kutokana na wanawake wamekuwa ni watu wazuri sana katika marejesho? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Pascal Katambi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inayo mpango wa kuweza kufanya mapitio na kuweza kuweka maboresho zaidi kwenye mifuko hii kwa sababu ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya Halmashauri nyingine zenyе kipato cha chini zile asilimia nne kwa wanawake, nne kwa vijana na mbili kwa watu wenye ulemavu kwenye maeneo mengine wanapata pungufu zaidi ya hapo. Kwa hiyo, hilo nalo ni jambo ambalo tumeshalichukua kama Ofisi ya Waziri Mkuu na limekwisha kuanza kufanyiwa vikao vya tathmini na kuweza kuangalia namna gani tutaweza kuboresha ikiwa ni sambamba na ule mjumuisho wa mifuko hii inayoshabihiana.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo lingine tumeona kwamba mikopo inayotolewa kwenye Halmashauri tunajaribu kuangalia zaidi tija, vikundi vimeduwa vikijiunga kwa ajili ya lengo la kupata mikopo ile, lakini baada ya hapo vinasambaratika na hawaendi kufikia azma ya kukopea mikopo hiyo na mpaka sasa tukisema katika mifuko tu ya fedha za Halmashauri ni mabilioni mengi ambayo bado hayajaweza kufanyiwa marejesho. Na kwa Ofisi ya Waziri Mkuu peke yake tuliwahi kutoa shilingi bilioni 4.9 lakini katika fedha hizo, ni shilingi milioni 700 tu ambazo ziliweza kurudishwa, zaidi ya shilingi bilioni nne bado hazijaweza kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili Mheshimiwa Santiel Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum kwamba kuona ongezeko la asilimia; hili ni eneo pia nalo ambalo tumekuwa tukilifanyia kazi kuweza kuona namna gani tunaweza tukaboresha Zaidi hasa kwa wale waliokuwa waaminifu katika kukopa kwa sababu lengo la Serikali na llani ya Chama

cha Mapinduzi ni kuwawezesha wananchi hawa kiuchumi wanapokopa hizi fedha waweze kuzirudisha ili watu wengine waweze kufanya biashara zaidi. Na tunategemea waweze *ku-graduate* kwenye hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli tunalifanyia kazi na tunatarajia hivi karibuni hasa kwenye mwaka huu wa fedha, fedha hizi zinazotolewa tuone ile tija na hasa twende hata kwenye kukopesha vifaa kuliko fedha ambapo mara nyingi zimekuwa zinatumika vibaya. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mbunge wa Rarya, Mheshimiwa Jafari Chege.

Na. 332

### **Hospitali ya Wilaya ya Rarya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, ni lini Hospitali ya Wilaya ya Rarya itaanza kutoa huduma?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rarya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Rarya ambapo kati ya mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021 Serikali imeipatia shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tisa na shughuli za ujenzi zinaendelea ambapo ujenzi wa majengo saba ya awali umekamilika na tangu Juni 2020 inatoa huduma ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

wagonjwa wa nje (*OPD*). Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Rorya

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya inatarajiwa kuanza kutoa huduma za upasuaji wa dharula na kulaza wagonjwa ifikapo Disemba, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Rorya, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na nishukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba nipate nafasi sasa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambayo kimsingi yanatokana na jibu la swali la msingi.

Swali langu la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mwaka 2020/2021 kiasi cha shilingi milioni 500 kilichangwa kwa ajili ya kununua vifaa tiba, lakini sasa tumebakiza mwezi mmoja unaokuja wa sita.

Je, ni lini Serikali sasa hii milioni 500 iliyokuwa imetengwa itaweza kufika kwenye hospitali hii ili kuweza kununua vifaa tiba hivi ili kuongeza wigo wa utoaji huduma katika hospitali ile?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kwa kuwa Serikali imekiri mwezi Disemba mwaka huu hospitali ile itafunguliwa kwa ajili ya kutoa huduma lakini pia inakiri kwamba hatuna jengo la upasuaji na wala halijaanza kujengwa; je, jengo hili ni lini litaanza kujengwa ili itakapofika mwezi Desemba hospitali ile iweze kutoa huduma inavyotakiwa? (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rarya kama ifuatavyo:-

Kimsingi tumetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya hospitali zote 67 za Halmashauri za awamu ya kwanza ikiwepo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Rarya na fedha hizo tayari zimeshapelekwa Bohari Kuu ya Madawa (*MSD*) kwa ajili ya kununua vifaa tiba ambavyo Halmashauri ya Rarya wameainisha kwamba ni mahitaji yao ya kipaumbele.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizo tayari zimekwishatolewa kwa ajili ya Hospitali ya Rarya ana tayari zimekwishawasilishwa *MSD*, taratibu za manunuzi ya vifaa tiba zinakamilishwa na vifaa tiba vitaletwa katika Halmashauri ya Rarya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na jengo la upasuaji; hospitali ile tayari ina majengo saba, tunaendelea na ujenzi wa majengo tisa na kati ya majengo saba ambayo tayari yamekamilika kwa asilimia 98, jengo la akina mama wajawazito linaungana na jengo la upasuaji. Kwa hiyo, tayari tuna jengo la upasuaji la kuanzia katika Hospitali ya Wilaya ya Rarya. Mpango ni kuendelea kujenga majengo mengine ya upasuaji katika mwaka wa fedha ujao, lakini hili halitaathiri kuanza kutoa huduma za upasuaji ifikapo Disemba mwaka huu 2021, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, bado tupo TAMISEMI swalii la Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini.

Na. 333

### **Ujenzi wa Kituo cha Afya Bashnet - Babati Vijijini**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Bashnet baada ya Serikali ya Kijiji kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi huo?

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mpango wa kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Babati kupitia mapato yake ya ndani imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Bashnet katika eneo lenye ukubwa wa ekari 12.6 lilitotengwa na Serikali ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi huo utaanza katika mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyopangwa.

**SPIKA:** Ah Daktari majibu yako nimeyapenda siku hizi yaani, moja kwa moja kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mbunge wa Babati Vijijini bado una swali la nyongeza kweli?

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yanayotia moyo, lakini naomba niulize swali moja tu dogo la nyongeza.

Je, Serikali ipo tayari kuongeza wataalam wa afya katika Kituo cha Afya cha Ufana ambacho kipo jirani na Bashnet ili wananchi wa Bashnet wapate huduma ya afya wakati wanasubiri kujengewa kituo cha afya? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo moja, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kuongeza watumishi katika kituo cha afya katika ajira hizi za watumishi 2,726 zilizotangazwa, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa tuendelee na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Na. 334

### **Upungufu wa Watumishi wa Afya Jimbo la Kilwa Kaskazini**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuiliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka watumishi wa Idara ya Afya katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ambalo lina uhaba mkubwa wa watumishi kiasi cha kufanya baadhi ya zahanati kutoa huduma duni na nyingine kuchelewa kufunguliwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 60 zikiwemo

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

hospitali mbili, vituo vya afya vitano na zahanati 53. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi Desemba, 2020, Serikali imeajiri na kuwapanga watumishi 108 wa kada mbalimbali za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Aidha, mwezi Mei, 2021 Ofisi ya Rais-TAMISEMI imetangaza nafasi 2,726 za ajira za kada mbalimbali za afya. Watumishi hao watapangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kutoa kipaumbele kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vyenye upungufu mkubwa wa watumishi ikiwemo baadhi ya vituo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya na kuwapangia katika vituo Wilayani Kilwa na kote nchini kwa ujumla, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa Kaskazini uliza swali lako.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Hospitali ya Kipatimu ambayo imekuwa ikiendeshwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na taasisi ya Kanisa Katoliki imekuwa na changamoto kubwa ya mtaalam wa mashine ya *x-ray*. Itakumbukwa kwamba mwaka 2017 Serikali ilitumia jumla ya shilingi milioni 60 kuleta mashine ya *x-ray* katika hospitali ile lakini mpaka leo hatujawa na mtumishi wa kitengo hicho.

Je, katika hizi ajira chache 2,726 ambazo zimetangazwa hivi karibuni, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kunihakikishia kwamba moja kati ya watumishi hao atapelekwa katika Hospitali ya Kipatimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri wa TAMISEMI lini atakuwa tayari kutembelea Wilaya ya Kilwa ili kutambua changamoto mbalimbali zinazowakabili

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawahakikishieni kabisa kwamba Mheshimiwa Francis Ndulane anaona kama kawaida; yupo vizuri kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, mwaka 2017 ilipeleka mashine ya *x-ray* na mpaka sasa utaratibu wa kumpata mtumishi kwa maana ya mtaalam wa *x-ray* upo hatua za mwisho na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira hizi ambazo tumezitangaza, tutakwenda kuhakikisha tunapata mtaalam wa *x-ray* kwa ajili ya kwenda kutoa huduma katika Hospitali ya Kipatimo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kufanya ziara katika Jimbo la Kilwa mara baada ya kumaliza *session* hizi za Bunge Juni 30, 2021. Ninakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho kwa TAMISEMI leo wana maswali mengi sana wana maswali manne, Mheshimiwa Regina.

Na. 335

**Kupeleka Vifaa Tiba na Watalaam katika Vituo vya Afya**

**MHE. REGINA N. QWARAYaliuliza:-**

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Je, ni lini Serikali itapeleka na kuongeza vifaa tiba na wataalam katika vituo vya afya ilivyojenga vikiwemo vifaa tiba maalum kama vile "*incubator beds*" na taa maalum kwa ajili ya kukabiliana na homa ya manjano kwa watoto njiti?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibuu:-**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa vituo vya afya unaenda sambamba na mpango wa ununuzi wa vifaa tiba. Kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2020/2021 Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 68.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya afya vilivyojengwa na kukarabatiwa ili kuwezesha utoaji wa huduma za dharura na upasuaji kwa akinamama wajawazito na wananchi kwa ujumila. Vifaa vilivyonunuliwa vinajumuisha vifaa kwa ajili ya kusaidia watoto wanaozaliwa kabla ya muda (*Infant Radiant Warmers*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoa shilingi bilioni 34 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali mpya 67 za Halmashauri zilizojengwa kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mei, 2017 hadi Mei, 2020 Serikali imeajiri na kuwapanga watumishi 9,531 wa kada mbalimbali za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, mwezi Mei 2021 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetangaza nafasi 2,726 za kada mbalimbali za afya. Wataalam hao watapangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini na kipaumbele kitakuwa kwenye vituo vyenye uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma za afya nchini kwa kuboresha miundombinu, kununua vifaa tiba na kuajiri wataalam wa kada mbalimbali za afya kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tayari kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa vifaa tiba lakini pia bado kuna tatizo la ukosefu wa vyumba vya kuhudumia hawa watoto njiti katika vituo vyetu vya afya pamoja na Hospitali zetu za Wilaya.

Je, Serikali inamkakati gani katika kuhakikisha kila Hospitali yetu ya Wilaya navituo vya afya inakuwa na vyumba hivyo kwa ajili ya kuhudumia watoto hao?

Mheshimiwa Spika, swali lapili pale Mererani tuna kituo kikubwa cha afya ambacho kinahudumia kata zaidi ya nne katika Wilaya ya Simajanjiro na Wilaya za jirani kama Hai na Arusha DC, lakini tatizo kubwa liliopo pale hawana kabisa chumba maalum cha kuhifadhi maiti, hivyo ndugu zetu wanapotangulia mbele za haki ndugu wanahangaika kuwasafirisha kwenda *Mount Meru* na Himo.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kukamilisha jengo liliojengwa tayari ili huduma hiyo iweze kupatikana pale katika Kituo cha Afya cha Mererani? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Dugange, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa majengo ya huduma ya afya ya uzazi na mtoto ambayo yanaendelea nchini kote hivi sasa ramani zile zimezingatia *provision* ya kuwa na chumba kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya muda wao maarufu kama njiti. Kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika michoro ya sasa ramani zetu zimezingatia kuwa na vyumba ambavyo vitakuwa mahsusini na vitawekewa vifaa tiba zikiwemo *Radiant Warmers* kwa ajili ya kusaidia watoto wanaozaliwa kabla ya muda wao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali imeendelea pia kuhakikisha inaelimisha jamii kuhusiana na *kangaroo mother care* kwa maana ya huduma mwambata pamoja na kuwa vyumba hivyo. Kwa hiyo tutaendelea kuhakikisha kwamba vyumba hivyo vinakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pili chumba cha kuhifadhi maiti katika kituo cha afya cha Mererani ni muhimu sana na mimi ninaomba tulichukue hili tutawasiliana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa maana ya Simanjiro lakini na sisi kama Serikali kuu tutaona njia bora zaidi ya kuhakikisha tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga chumba cha kuhifadhi maiti. Ninakushukuru sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilombero nilikuona, Mheshimiwa Abubakari Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, Kituo cha Afya cha Kidatu Nyandeo kina uhaba mkubwa sana wa jokofu la kuhifadhi milli ya marehemu na mara ya mwisho tuliwasiliana na *MSD* wakasema kwamba wangepeleka jokofu hilo lakini mpaka sasa hawajapeleka.

Je, lini Serikali itapeleka Jokofu katika Kituo cha Afya cha Nyandeo Tarafa ya Kidatu Jimbo la Kilombero?

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka mipango ya kupata vifaa tiba na vifaa mbalimbali yakiwemo majokofu ya kuhifadhia maiti, lakini pamoja na jitihada za Serikali tumeendelea pia kuhakikisha tunawaelekeza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha katika mapato ya ndani kununua baadhi ya vifaa tiba na baadhi ya vitendea kazi katika hospitali zetu yakiwemo majokofu ya kuhifadhia maiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nichukue nafasi hili kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kwa sababu majokofu haya ni kati ya Milioni 12 hadi Milioni 30; fedha hili ipo ndani ya uwezo wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilombero na hivyo ninamuelekeza katika mwaka ujao wa fedha wahakikishe wanaweka *provision* ya kununua jokofu la kuhifadhia maiti katika kituo cha afya. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Kilimo Waheshimiwa Wabunge, swali litaulizwa Mheshimiwa NusratShaaban Hanje.

Na. 336

### **Hitaji la Upatikaji wa Mbegu Bora za Alizeti-Singida**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je Serikali ina mpango gani wa kutumia mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora hususani za alizeti ambayo ndio zao la uti wa mgongo wa uchumi wa mkoa wa Singida?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhalii.

## **NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa zao la alizeti katika kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kula hapa nchini ambapo asilimia 68 ya mafuta ya kula yanatokana na zao hilo ikilinganishwa na mazao mengine ya yanayochangia asilimia 31.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za mafuta nchini kwa kutenga fedha jumla ya shilingi bilioni 40 katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya uzalishaji wa mbegu ya Wakala wa Mbegu wa Serikali ili kuzalishaji mbegu za alizeti na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo kutawezesha kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti kutoka tani 538 katika msimu wa 2019/2020 hadi kufikia tani 10,000 za mbegu bora za alizeti mwaka wa fedha 2019/2030 ambazo zitatosha kutumika katika eneo la hekta milioni 1.2 zinazoweza kuzalisha tani 500,000 za mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini umuhimu wa zao la alizeti, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kugundua na kuzalisha aina mpya ya mbegu bora za alizeti zenye sifa ya kutoa mavuno na mafuta mengi na zenye ukinzani dhidi ya magonjwa kutoka aina 1 hadi 17 za zao la alizeti katika msimu wa 2019/2020.

**SPIKA:**Mheshimiwa Nusrat swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoa na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

na upatikanaji wa mbegu ya alizeti kwa wananchi wa Mkoa wa Singida naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Singida wamekuwa wakilima kwa utaratibu wa kawaida kabisa ule ambao wanalima wakimaliza wanaweka mbegu baada ya kuuza wanabakiza kidogo kwa ajili ya kwenda kulima tena mwakani ndio utaratibu wanaoutumia mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri sasa yupo tayari kwa ajili ya kwenda kukutana na wakulima wa alizeti wa Mkoa wa Singida hususan jimbo la Singida Magharibi kwenye kata za Mwaru, Mgungia, Muhintiri, Minyukhe kwa ajili ya kwenda kuzungumza nao sasa kuona namna gani ambavyo ku-*in cooperate* mawazo yao na ya Wizara kwa ajili ya kuhakikisha kwamba upatikanaji wa mbegu ya alizeti, zinapatikana zenye tija ili walime kilimo ambacho sio cha desturi? Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mimi nilifikiri utamwalika ufuatane naye huko, maana hajui. Mheshimiwa Waziri labda unakujuua huko, majibu tafadhali. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hanje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenda ku-*visit* tupo tayari na tutafanya hivyo na Mwenyezi Mungu akijaalia mwezi huu wa Juni tutakuwa na Mkutano mkubwa utakaoongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mkoa wa Sindhiga kwa ajili ya suala la zao la alizeti na kukutana na wazalishaji na wakulima wa alizeti. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, ndio nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Itigi.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, naomba *commitment* ya Serikali au itusaidie Serikali kuona namna iliyobora hasa kwa mbegu ambayo inaitwa *Hysun* inauzwa shilingi 35,000 kwa kilo mbili.

Je, Serikali sasa ipo tayari kuingiza ruzuku kwa mbegu hii ili uzalishaji wa mafuta uwe bora zaidi katika Mkoa wa Singida na mikoa mingine ambayo inalima alizeti?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba gharama ya mbegu za *highbred* za alizeti ni kubwa sana na sio rahisi mkulima wa kawaida kuweza kuzinunua. Kwa hiyo, mpango wa Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha baada ya kupitishiwa bajeti yetu hapa ni kwamba tukimaliza mukutano wa kukutana Singida na wazalishaji wote wa viwanda vyta kulizisha mafuta mpango wetu ni kutengeneza *subsidy*, ruzuku ili bei ya mbegu hizo kwa utaratibu tutakaoweka kwa wasambazaji ili wakulima bei yao iweze kupungua.

Kwa hiyo huo ni sehemu mpango wetu na tunaamini tutautumia katika mwaka ujao wa fedha ili kuweza kupunguza bei ya mbegu za alizeti.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa na Wizara ya Maji swali litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza.

Na. 337

**Ujenzi wa Mradi wa Maji-Bukoba Vijijini**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

(i) Je, ni lini ujenzi wa mradi wa katika Kata za Izimbya, Kyaitoke, Ruhunga, Mugajwale, Katoro na Kaibanja utaanza na kukamilika?

(ii) Je, ni lini mradi wa maji wa Kata za Kemondo, Katerero na Bujugo utaanza na kukamilika?

(iii) Je, ni lini mradi wa maji wa Kata za Karabagaine, Maruku na Kanyangereko utaanza na kukamilika?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuanza utekelezaji wa miradi ya maji ambayo itahudumia Kata za Izimbya, Kyaitoke, Ruhunga, Mugajwale, Katoro na Kaibanja katika mwaka wa fedha 2021/2022 na muda wa utekelezaji ni miezi 12 na mradi utakamilika mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Kemondo – Maruku umeanza kutekelezwa ambapo kwa sasa upo katika awamu ya kwanza iliyoanza mwezi Januari, 2021. Utekelezaji wa mradi huu utatumia miezi 18 hivyo utakamilika mwezi Julai, 2022. Kupitia mradi wa Maji Kemondo – Maruku; Kata za Kemondo, Katerero, Bujugo, Maruku, Kanyangereko na Karabagaine zitanufaika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza nimekuona uliza swali lako.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, majibu haya ni mazuri kuyasikia

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kwenye masikio na yanafurahisha, lakini siamini kama kuna ukweli wa kutosha kwasababu kwa mfano hili swalii (c) kuhusu Mradi wa Maji Karabagaine nimewahi kuliuliza humu ndani majibu yakawa ni haya haya kwamba mradi huu utaanza, lakini mpaka leo haujaanza. Sasa leo nitaaminije kinachosemwa hapa ni kweli?

**SPIKA:** Jibu la swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri unamuaminisha vipi Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nipende kujibu swalii la Mheshimiwa Jasson Rweikiza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara tupo katika mageuzi makubwa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali na mradi kama huu wa Karabagaine ni mradi wa muda mrefu lakini ni katika ile miradi ambayo tayari tupo katika mpango wa kuona kwamba utekelezaji wake unafikia sasa mwisho.

Mheshimiwa Spika, hivyo nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo ameshafuatilia kwa muda mrefu na jitihada kubwa namna ambavyo tumeweza kushirikiana pamoja nikuhakikishie mradi huu unakwenda kutekelezwa katika mwaka wa fedha huu 2021/2022 na itawezekana kwa sababu tumedhamiria kuleta mageuzi makubwa.

**SPIKA:** TAMISEMI sijui mna mpango gani majina magumu magumu haya kuyafanyia utaratibu mkayapunguza punguza ili yatamkike hata na Wamakonde na watu wengine, majina mrefu mrefu Kanyangangerero Karabaka nanii, halafu kuna mengine tena. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ester Bulaya nimekuona.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa swalii dogo la nyongeza; wewe ni shahidi mradi wa Bunda umechukua muda mrefu sana takribani miaka 13; lakini moja katika makubaliano kwenye mkataba wa mradi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ule ni kujenga vitu kabla mradi haujafika Bunda Mjini kwenye eneo linalotoka kule Nyabeu.

Sasa nataka kuuliza maeneo yanayopita mradi kama Gushigwamara, Kinyambwiga, Tairo, Guta na Bunda Store kabla hayajafika *centre*; ni lini mtaweka vituo ili wale wananchi wa maeneo yale wasisikie tu mradi umetoka chanjo cha maji vijiji ambavyo vinapita havijapata maji? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tayari tunaendelea na kuona kwamba maeneo ya miradi ambayo imekaa muda mrefu inakamilika, na sera ya maji inataka pale kwenye chanzo na kadri ambavyo mradi unakwenda tunaendelea kusambaza maji. Yule wa karibu ya chanzo ataendelea kupata maji kwa kwanza kulikoni aliyekuwepo kule mbali. Hivyo nikuhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba maeneo yote ambayo umeyataja yatazingatiwa katika kuona kwamba miundombinu ya usambazaji maji inawafikia. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga nilikuona.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali.

Serikali imekamilisha mradi wa maji katika Mji wa Kateshi mradi wenye thamani ya shilingi billioni 2.5 lakini mpaka sasa mradi huo haujaanza kufanya kazi.

Je, ni lini Serikali itaanza kusambaza maji ili wananchi wa mji wa Kateshi lakini maeneo ya Mogito ambayo chanzo

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kimeanzia pamoja na maeneo mradi unapopita watanufaika na maji haya katika miji hii na kata hizi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wowote ukishakamilika sisi kama Wizara tunapenda kuona maji yanawafikia wananchi kwenye vituo vya kuchotea maji, hivyo mara miundombinu yote itakapokamilika maji mara moja yataanza kutoka katika mradi huu wa Katesh. Tunafahamu tumeshatumia fedha nyingi za Serikali ambazo ni jasho la wananchi, hivyo hatuko tayari kuona fedha imeshatumika halafu kile tunachokitarajla kisipatikane. Pia niendelee kukupongeza Mheshimiwa Asia mwendo wako ni mzuri wewe unawakilisha vizuri vijana na sisi kama Wizara hatutakuwa kikwazo kuona kwamba unafika mbali. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga swali la mwisho la nyongeza kwenye Wizara ya Maji.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona kunipa swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika miradi 28 ambayo inatakiwa ipelekewe maji na Mji wa Makambako ni miongoni katika miji hiyo 28; ni lini mradi huo utaanza katika mji wa Makambako?

**SPIKA:** Majibu ya Mradi wa Maji Makambako, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sanga Mbunge wa Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yote ya miji 28 mpaka dakika hii taratibu zote zimeshakamilika hivyo wakati wowote ule miradi hii katika miji yote 28 tunakwenda kuanza kufanya kazi mara moja.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi swalii litaulizwa na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga. Mheshimiwa Kiswaga tafadhalii.

Na. 338

**Wabunge kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawafanya Wabunge kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi kutokana na ukweli kwamba migogoro mingi ya ardhi na mashamba hupelekewa kesi wao?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Naibu Waziri, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu namba 27 cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura Namba 216, baadhi ya watu wenye madaraka kama vile Wabunge, Wajumbe wa Halmashauri za Wilaya, Kata na Vijiji hawana sifa ya kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Lengo la kifungu hiki ni kuwezesha mgawanyo wa madaraka na utendaji kazi katika Serikali.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi wote katika maeneo yao endapo Mheshimiwa Mbunge atakuwa Mjumbe wa Baraza la Ardhi, wakati wa kutoa maoni ama maamuzi yanayompa ushindi mwananchi wa upande mmoja na kumnyima ushindi mwananchi wa upande wa pili suala hili linaweza kusababisha malalamiko yanayohusu mgongano wa maslahi kutokana na nafasi zao.

Aidha, Wizara yangu inaendelea kutoa elimu kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Umma kwa ujumla kuhusiana na taratibu za utatuzi wa migogoro ya ardhi zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga nimekuona umesimama, uliza swali lako.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; kwa kuwa katika bonde lililoko katika Kijiji cha Nyenza kata ya Mabolilwa kumekuwa kuna mgogoro ambaao umechukua miaka mitatu pale kwenye Mabaraza la Ardhi. Sasa kwa kuwa na wananchi wangu wameendelea kusumbuliwa kwenda na kurudi nilikuwa naomba kuuliza swali; je, sheria inampa mamlaka gani Waziri ya kuingilia kati endapo mgogoro umechukua muda mrefu kama huu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ardhi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Sura Namba 216 ambayo ndiyo inashughulika na utatuzi wa migogoro, Mheshimiwa Waziri hapaswi kuingilia maamuzi yanayotolewa na vyombo vyaya utoaji haki. Kama kuna changamoto yoyote ambayo inatokea katika maeneo hayo mlalamikaji anayo nafasi ya kumuona Msajili wa Mabaraza ya Ardhi kuweza kupeleka kero yake na atamsaidia hatua ya kwenda mbele zaidi.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Tunaenda Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Minza Simon Mjika. Mheshimiwa Minza tafadhali.

Na. 339

### **Ujenzi wa Barabara ya Kolandoto - Meatu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara kutoka Kolandoto hadi Meatu itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge Viti Maalum, Simiyu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandoto hadi Meatu ni sehemu ya barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti hadi *Oldeani Junction* yenye urefu wa kilometra 328. Upembusi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ulishakamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 5,000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kolandoto – Mwanhuzi yenye urefu wa kilometra 62.5 na kipande cha Lalago – Ng’oboko – Mwanhuzi yenye urefu wa kilometra 74.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa Daraja la Mto Sibiti pamoja na barabara unganishi kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometra 25 mpakani mwa Wilaya ya Meatu Mkoani

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Simiyu na Wilaya ya Mkalama Mkoani Singida ni hatua za awali za ujenzi wa barabara hiyo ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru sana kwa majibu ya Waziri, lakini sasa napenda njue ni lini zoezi hili litaanza la ujenzi wa hiyo barabara? Naomba kupatiwa majibu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa *Engineer Msongwe*, tafadhalii

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Minza Mjika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeainisha kwamba tayari tumeshaanza ujenzi kwenye baadhi ya maeneo na katika bajeti tutakayoanza kuitekeleza ambayo Bunge lako limepitisha, tumetenga fedha, kwa hiyo, mara tu bajeti itakapoanza kutumika barabara hiyo itaanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Nimekuona Mbunge wa Longido uliza swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilianza ujenzi wa barabara ya lami inayotoka Sanya Juu kwenda Kamwanga ambapo ingeungana na nyingine inayotoka Rombo kuja mpaka Kamwanga na barabara hii imesimama ujenzi wake pale Kijiji cha Elerai wakati zimebaki zimebaki kilometra 42.8 tu kukamilika.

Naomba kufahamu Serikali itaendeleza lini ujenzi wa barabara hii ambayo sasa ni mwaka wa pili tangu isimame?

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara ambazo zimeainishwa kwenye bajeti yetu na kama tulivyoahidi kwenye bajeti zetu tuna uhakika bajeti itakavyoanza kutekelezwa basi itaendelea kutekelezwa kama tulivyoahidi kwenye bajeti yetu ambayo imepitishwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi swali la nyongeza

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, wananchi wa Jimbo la Mlimba ukiwaauliza tatizo lao kubwa ni barabara unaweza kuacha yote lakini barabara ni kipaumbele cha kwanza.

Naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo kwa niaba ya wananchi wa Mlimba; ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi rasmi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Ifakara - Ng'ambo - Mto Lumemo mpaka Lupembe Madeke yenye urefu wa kilometra 223? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ambayo ambayo ameitaja inayoanzia Mikumi, Ifakara, Mlimba, Madeke hadi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Lupembe na hadi *Kibena Junction* ni barabara inayounganisha mikoa miwili na imetengewa fedha kwenye bajeti ambayo itaanza kutekelezwa kuanzia upande wa Njombe na kuanzia upande wa Jimbo lake kwenye sehemu mbili.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mara bajeti itakapoanza kutumika kama tulivyoahidi kwenye bajeti barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Esther Midimu, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ya kutoka Bariadi - Itirima - Mwandoya mpaka Isibiti Iguguno ni kilometra 289 na iko kwenye llani. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya barabara inayoenda Gambosh, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayoisema inatoka Mwandoya *junction* kwenda Mwandoya ni barabara ambayo ilikuwa bado haijafanyiwa usanifu wala upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha huu barabara hii imepangwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili iwe sasa tayari kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nikisikia barabara inayotoka Simiyu kuja Kolandoto ni kama inanitonesha vile kidonda. Mheshimiwa Naibu Waziri ulisema *tenderitatangazwa*; je, lini mnatangaza *tender* kwa barabara hii?

**SPIKA:** Ni lini *tenderitatangazwa*, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayoisema ya Mbulu na hasa Mbulu Hydom yenye kilometra 50 ipo kwenye mpango wa kutangazwa kabla ya mwisho wa bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, taratibu zote za manunuzi zote zinakamilisha, muda wowote barabara hii itatangazwa kabla ya kuanza bajeti ya mwakani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ambayo pia Mheshimiwa aliombea kupiga sarakati itatangazwa kabla ya mwisho wa mwaka huu, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Swalii la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge, litaalizwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri.

Na. 340

**Serikali Kujenga Nyumba za Viongozi Waandamizi Dodoma**

**MHE. MARIAM D. MZUZURI** aliuliza:-

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za viongozi waandamizi wa Serikali kama Makatibu Wakuu na Mawaziri katika Mji wa Dodoma kwa ajili ya makazi ya viongozi hao?

**SPIKA:** Tunaomba majibu ya swali hilo muhimu sana kwa siku ya leo. Yajibewe kwa uhakika. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali kuhamishia shughuli zake makao makuu ya Serikali hapa Jijini Dodoma kumekuwepo na juhudhi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa viongozi waandamizi wa Serikali wanapata makazi bora ya kudumu na yenye usalama. Katika kutekeleza hilo, Serikali imeanza mkakati wa kujenga nyumba za viongozi katika jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Sekta ya Ujenzi, imetenga kiasi cha shilingi bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 20 za viongozi na shilingi billioni nne kwa ajili ya ukarabati wa nyumba 40 za viongozi jijini Dodoma. Hivi sasa kwa kutumia Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) hatua za ubunifu na usanifu wa nyumba hizo pamoja na makadirio ya gharama za ujenzi zimekamilika. Aidha, ukarabati wa nyumba za viongozi jijini Dodoma unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Sekta ya Ujenzi, imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba 20 za viongozi jijini Dodoma. Aidha, pamoja na ujenzi wa nyumba hizi, Serikali pia imetenga fedha kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa nyumba nyingine 40 za viongozi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

zilizopo jijini Dodoma katika maeneo ya Kisasa, Area D na Kilimani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Ditopile nimekuona.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Spika, niseme wazi tu sijaridhika na majibu ya Serikali kwenye swali hili ambalo ni la mkakati na lina umuhimu sana na niseme tu mimi kama Mbunge mwenyeji nimeshafuatwa sana na Naibu Mawaziri huku kuwatafutia nyumba za kuishi na kwa kweli wanatusababishia mtaani watu wengi kukosa.

Mheshimiwa Spika, iliwezekana Dar es Salaam kule Masaki, kule Mikocheni kujengwa nyumba kwa ajili ya viongozi. Kwa nini ishindikane mbona mji wa Serikali tumeujenga? Kwa hiyo naomba kwa kweli nitakuja kulirudia hilli swali na lije na majibu yanayoeleweka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumeona jitihada za Serikali katika ujenzi wa makao makuu katika kuendeleza miundombinu yetu.

Maswali mawili ya nyongeza; la kwanza naomba kuuliza je wamefikia hatua gani katika ujenzi wa *airport* ya kule Msalato? Lakini la pili katika ujenzi wa barabara ya mzunguko kwenye Jiji letu la Dodoma? Nnashukuru.

**SPIKA:** Hili la mabarabara sjui ni *Engineer Msongwe?* Yeye mwenyewe tena bado. Kweli nilitaka kusahau Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara majibu ya maswali hayo muhimu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Mariam Ditopile kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wameleta maombi mbalimbali ya nyumba pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali. Lakini tumeshatoa maagizo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwa Meneja Mtendaji Mkuu wa *TBA* na kuna viongozi wengine ambao walishastaafu yaani walikuwa Wabunge siyo Wabunge tena hapa Dodoma. Wengine walikuwa ni viongozi wa Serikali siyo viongozi wa Serikali walikuwa wanatumia hizo nyumba mpaka tunavyozungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wameshapewa *notice* nadhani ndani ya wiki mbili zijazo utapata taarifa halisi na baadhi ya Wabunge watapata nafasi ya nyumba hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini maswali yake mawili kama ifuatavyo; la kwanza ni kweli kwamba Kamati ya kwako ya Kudumu ya Miundombinu, mwezi huu unaoishia walitembelea eneo la uwanja wa ndege wa Msalato, lakini pia na barabara za mzunguko hapa Dodoma naomba niseme tu kwamba fedha zipo za kulipa fidia. Pale Msalato kuna baadhi ya wananchi ambao hawakuwepo wakati wa fidia, fedha zipo zoezi linafanyika ndani ya muda mfupi sana zoezi litakamilika.

Mheshimiwa Spika, kujenga uwanja wa ndege wa Msalato pamoja na *ring roads* ni ahadi ya Serikali na Mheshimiwa Rais Mama Samia ameshatoa maagizo na maelekezo tutasimamia na itatekelezwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Vita Kawawa uliza swalilako.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; kwa nini Serikali isijenge nyumba ambazo watakuwa wanaweka mkataba kwa Wabunge kila baada ya miaka mitano ambao wanaendelea wataendelea kukaa kwenye nyumba hizo, lakini ambao watakuwa hawaendelei basi nyumba hizo Wabunge wapya wanaokuja wakaweza kukaa. Kwa nini Serikali isiwe na mpango wa kujenga nyumba namna hiyo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swalilako hilo Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali hizi nyumba zimekuwa na matumizi ambayo ni mabaya na tumekuja kugundua kuna baadhi ya watu wana nyumba zao hapa kwa sababu hizi za Serikali gharama ni chini kidogo wanapangisha za kwao hizi wanakaa nazo.

Mheshimiwa Spika, tumeshatoa maelekezo *TBA* kwamba wapitie na kimsingi ni nchi nzima ikiwepo ni madeni ambayo ni makubwa yapo watu wanadaiwa hawajalipa fedha ya Serikali na kupelekea wanashindwa hata kukarabati nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pilli kwamba kama kuna mtu alikuwa ni Mbunge hapa Dodoma, ameshamaliza kipindi chake ile nyumba inapaswa irejeshwe au alikuwa ni mtumishi wa Serikali hizi nyumba zinapaswa kutumiwa na viongozi waliopo kwa wakati huu katika nafasi zao. Wazo lako ni jema Mheshimiwa Mbunge tulipokee tutalifanyia kazi ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeisha sasa naomba tuendelee na kuwataja wageni tulionao pamoja na kusisitiza hili swalii la mwisho ambalo Mheshimiwa Waziri amelijibu.

Ndugu zetu wa Wizara ya Ardhii, *National Housing* inajenga nyumba kule, juzi nilitembea kule lyumbu, lakini mna *concentrate* kujenga vijumba vidogo vidogo, nyumba viwili na sebule, kwa nini nyumba za Mawaziri za Makatibu Wakuu za viongozi wakuu wa Serikali hamzijengi Dodoma? (*Makofi*)

Kwa nini mnang'ang'ania hizi nyumba za vyumba viwili na sebule, vyumba vitatu na sebule haiwezi kuwa makao makuu bila *senior officers* kuhamia Dodoma. Kwa hiyo hebu *National Housing* tubadilike twende tu *bridge gap* ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Dodoma kitu gani kinakosekana Dodoma ndiyo tukifanye, itatusaidia zaidi, ahsante sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni viongozi kutoka Wizarani na Watendaji Wakuu wa Taasisi, tunaye Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbas, karibu sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Ally Possi, karibu sana. (*Makofi*)

Mkurugenzi Idara ya Habari Maelezo Gerson Msigwa, huyu bwana huyu akikutokea saa saba usiku hatari. (*Makofi*)

Pia yupo Katibu Mkuu *TFF* Wilfred Kidau, popote ulipo karibu, Yahya Olly - Katibu Mkuu *TPRC*, Richard Mganga Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, karibuni popote pale mlipo. (*Makofi*)

Yupo pia Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *TBC* Martha Swai, hongera sana *TBC* tuko nanyi. (*Makofi*)

Katibu wa Kamati wa Olympiki - Ndugu Filbert Bayi karibu sana, Kaimu Katibu Mtendaji BAKITA - Ndugu Consolatha Mushi, Kaimu Katibu Mtendaji BASATA - Ndugu Matiko Mniko, Kaimu Katibu Mtendaji Filamu - Dkt. Kiagho Kilonzo, ahsante. (*Makofi*)

Yupo pia Mtendaji Mkuu *COSOTA* - Ndugu Doreen Sinare, Mtendaji Mkuu *TaSUBa* - Dkt. Herbet Makoye, Rais wa Shirikisho la Kikapu Tanzania Ndugu Phares Magesa. (*Makofi*)

Mgeni mwengine wa Mheshimiwa Waziri ni mke wake Ndugu Jennifer Bash karibu sana shemeji yetu, karibu sana Mama Alaska, karibu Bungeni. (*Makofi*)

Wageni wengine 12 wa Mheshimiwa Bashungwa ni wawakilishi wa sekta ya michezo nchini wakiongozwa na Refa wa Kimataifa wa Mchezo wa Ngumi za Kulipwa Ndugu Pendo Njau, ahsante sana. (*Makofi*)

Pendo Njau mwenyewe yuko wapi? Jamani huyu Refa wa Ngumi yaani na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda *promoter* wa ngumi yuko hapa, wajibu wangu ni kuwakumbusha Waheshimiwa Wanaume mambo haya tunazidi kuzidiwa kila upande. Sasa hata kwenye ngumi wameingia, hongereni sana. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Bashungwa ambao ni wawakilishi wa Mashirikisho ya Sanaa ni Rais wa Shirikisho la Filamu Tanzania, Ndugu Elias Mjata, Rais wa Shirikisho na Ufundı (*TAFCFA*) Ndugu Adrian Nyangamalle, Rais wa Shirikisho la Muziki Ndugu Addo Novemba, Rais wa Shirikisho la Sanaa za Maonesho Tanzania, Ndugu William Chitanda, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine watano wa Mheshimiwa Bashungwa ni Wawakilishi wa Vyombo vyta Habari nchini wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (*TEF*) Ndugu Deodatus Balile, karibuni sana (*Makofi*)

Lakini kwenye Jukwaa la Spika ninao wageni ambao ni Wawakilishi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), nitawatambulisha mmoja mmoja yupo Katibu wa CWT wa Mpwapwa - Ndugu Pancras Ngamesha, Mwenyekiti wa CWT Mpwapwa - Ndugu Daniel Tito, Katibu wa CWT Bahi - Mwalimu Kemirembe, Mwenyekiti wa CWT Bahi - Ndugu Mahagi Mapesi, Katibu wa CWT Kongwa - Ndugu Damari Semango, Mwenyekiti CWT Kongwa - Ndugu Samuel Malecela, Mwenyekiti wa CWT Jiji - Ndugu Prosper Mtungi, lakini yupo Kaimu Mwenyekiti CWT Mkoa wa Dodoma - Ndugu Elia Kumbulusa, karibuni sana. Wamefatana na Katibu Mkuu wa CWT Taifa - Mwalimu Deo Self, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Wageni wengine ambao tunao leo ni wageni 42 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro - Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni Watendaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kutoka Arusha. Wale Watendaji wa Ngorongora, ni wageni wa Waziri, mmebadilika kweli siku hizi, hongereni sana. Nasema hivyo mimi ndugu yao, wao wenyewe

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

wanajua, ahsanteni sana. Muendelee kulinda hifadhi yetu ya kidunia, *best park in the world. (Makofi)*

Wageni 42 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaao ni wanafunzi na walimu wa sekondari ya Maria De Mattias wakiongozwa na mwalimu wao Ndugu Paulo Mathew, De Mattias, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambaao hamfahamu Dodoma hapa tuna shule nzuri sana, shule mbalimbali nzuri sana *the best*. Kwa hiyo, mkiwa na watoto mnawezza mkawasogeza katika shule za karibu hapa wakapata elimu sawa sawa au nzuri zaidi hata mahali ambako labda mnawapeleka huko mbali, moja ya shule hizo ni hii ya Maria De Mattias, ahsanteni sana, karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ni wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Pomerini, Kilolo Mkoani Iringa, wakiongonzwa na Ndugu Erasto Kalolo. Wale wa Pomerini Kilolo, hongereni sana kutoka Kilolo, hivi nani yule anasema elimu Tanzania imeshuka, hivi mambo haya kweli elimu imeshuka hii, elimu imepanda sana viwango, karibuni sana vijana wetu. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wanaotoka Jimbo la Mbongwe, Mkoani Geita wakiongozwa na Ndugu Silvester Musa, karibuni sana kutoka kule Mbogwe, msikimbilie kuchimba dhahabu, msome shule, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 57 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaao ni Waheshimiwa Madiwani, viongozi wa Chama ngazi ya Wilaya na watendaji kutoka Jimboni Nyamagana Jijini Mwanza, wakiongozwa na Mstahiki Meya wa Jiji la Mwanza ambaye nitamtaja baadaye, Madiwani kutoka Mwanza, viongozi wa Chama kutoka Mwanza, mnawezza mkaa karibuni watani zetu, karibuni sana.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Meya Sima Constantine, karibu sana. Lakini pia tunaye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Nyamagana Ndugu Zebedayo Athumani, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaao ni marafiki zake kutoka jijini Dar es Salaam, Ndugu Matola Mohamed na Ndugu Hemed Hemed, karibni sana. (*Makofii*)

Baada ya matangazo hayo sasa naomba tunendelee na utaratibu, Katibu.

### **NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea, Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane nina wageni maalum kabisa ambaao ningependa kuwatambulisha kwenu nao si wengine bali nitaanza na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Ndugu Stephen Kagaigai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Kagaigai naomba uendelee kusimama; kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge hawa nitoe shukrani za kipekee sana kwako na kwa familia, lakini pia tumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kukupa heshima kubwa ya kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Tutaendelea kukumbuka kazi yako uliyofanya hapa Bungeni na mara kwa mara tutakapo kuita usisite kujunga nasi hapa Dodoma. (*Makofii*)

Lakini pia amefuatana na mwenyeji wake ambaye ni Katibu mpya wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi ambaye alikuwa msaidizi wako Ndugu Kagaigai kwa muda mrefu, tunaamini umemfundisha vyatutoshana na yeye tunamkaribisha katika kazi hizi mpya ambazo ameaminwiwa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

na Mheshimiwa Rais ya kuwa Katibu wa Bunge, ahsanteni sana nyote wawili, mbarikiwe sana na ahsante sana. (*Makofii*)

Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Innocent Bashungwa, karibu tafadhalii kwa hotuba yako na una nusu saa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, awali ya yote niombe hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge yaani *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa buheri wa afya na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano na upendo. Nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuapishwa kwake kushika nafasi hiyo kufuatia kifo cha mpwendwa wetu aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Natoa pole kwa Mheshimiwa Rais, familia, wadau wa sekta za Wizara na Watanzania wote kwa ujumla kufuatia kifo cha mpwendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuendelea kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Sita. (*Makofii*)

Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kuteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali katika awamu hii. Vilevile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioaminiwa na kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kuwa Naibu Spika. (*Makofii*)

Vilevile nawapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao ili kuliwezesha Bunge hili kutekeleza majukumu yake. Ni imani yangu kuwa uzoefu, umahiri, hekima na busara zenu katika kuliongoza Bunge hili zitaendelea kutumika katika kuhakikisha nchi yetu na watu wake wanapata maendeleo yanayokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuisimamia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kumuhakikishia Mheshimiwa Rais utendaji bora na uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu niliokabidhiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, chanda chema huvikwa pete, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki kwa kupokea, kujadili na hatimaye kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2021/2022, Wizara itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwenda tezi na omo marejeo ngamani, sasa niwashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika utekelezaji wa shughuli za kuwaletea maendeleo Wanakaragwe, ninawahidi utumishi uliotuka pamoja na ushirikiano wa dhati katika kipindi chote nitakachokua nikiwakilisha katika Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru familia yangu mke wangu Jennifer Bash aka Mama Alaska na wanangu Santo, Solana, Sankala na wanafamilia wote kwa upendo wao na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, figa moja haliinjiki chungu, natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nianze kwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Pauline Gekul Mbunge wa Babati Mjini, Naibu Waziri, kwa msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. (*Makof*)

Nimshukuru Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu; Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Niwashukuru pia watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma ili kuleta tija na ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio na ya utekelezaji ya majukumu kwa kipindi cha mwaka 2020/2021; Wizara ilikadiriwa kukusanya shilingi 960,000,000 ambapo shilingi 1,080,109,491 sawa na asilimia 113 ya lengo zimesanya hadi Mei, 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadirwa kukusanywa ni jumla ya shilingi 40,694,484,000 ambapo hadi mwezi Mei, 2021 jumla ya shilingi 18,663,436,283 zilikusanywa sawa na asilimia 45.8 ya lengo la mwaka. katika mwaka 2020/2021 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 40,782,209,00 ambapo shilingi 29,636,664,259 sawa na asilimia 72.6 zilipokelewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango hati mwezi Mei, 2021 kwa mchanganuo ulibainishwa katika sehemu ya 3.1.2 ya hotuba yangu ukurasa wa tano mpaka wa saba.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi Mei, 2021 umeelezwa kwa kina katika sehemu ya tatu ukurasa wa saba mpaka wa 48 wa hotuba yangu kwa muktasari utekelezaji wa majukumu ya kupita sekta na taasisi zilizo chini ya Wizara ullikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari; Wizara iliendelea na utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016 ambayo pamoja na mambo mengine inaelekeza kuanzishwa kwa Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari. Bodi ya Ithibati itakuwa na jukumu la kutoa ithibati na vitambulisho kwa wanahabari wenyewe sifa, kusimamia maadili na nidhamu kwa wanahabari mionganoni mwa wanahabari, kuishauri Serikali kuhusu elimu ya kitaaluma, mafunzo ya wanahabari na kuhakikisha wanahabari wanazingatia sheria, kanuni na maadili ya uandishi wa habari katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa sasa Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha bodi hii.

Mheshimiwa Spika, Baraza Huru la Habari litaundwa baada ya Bodi ya Ithibati kuanza kazi, kwa kuwa Baraza hili litaundwa na wanahabari wenyewe watakaokuwa wamepewa ithibati na bodi. Pamoja na majukumu mengine, Baraza hili litakuwa linashughulikia malalamiko na kutoa maamuzi kuhusiana na ukiukwaji wa maadili katika uandishi wa habari. Kwa upande wa Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari, mfuko huo utawezesha waandishi wa habari

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kupata mafunzo yaani *capacity building* na kufanya tafiti katika uandishi wa habari na mawasiliano ya umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hii waajiri wanatakiwa kuwakatia bima wanahabari na inaifanya taaluma ya habari kutambulika kisheria badala ya kila mtu kufanya kazi ya habari, kuweka misingi mizuri na kusimamia maadili ya taaluma ya habari nchini.

Mheshimiwa Spika, wigo ya vyombo vya habari umeendelea kuongezwa hili kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya Kikatiba ya kupata taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kuflikia mwezi Mei, 2021 Tanzania ilikuwa na jumla ya magazeti na majalida yaliyosajiliwa 257 ambapo 206 yanamilikiwa na sekta binafsi na 51 yanamilikiwa na Serikali, vituo vya televisheni 43 ambavyo vya Halmashauri za wilaya ni vitatu, umma vitatu, na vya binafsi 37, vituo vya redio 200 ambapo za Halmashauri za Wilaya ni vinne, vya umma viliwli na vya binafsi 194 hadi sasa Tanzania ina televisheni mtandao 451, redio mtandao 23, blog 122 na jukwaa mtandaoni tisa.

Mheshimiwa Spika, idadi hii ya vyombo mbalimbali vya habari inaonesha namna nchi yetu inavyoendelea kuimarisha uhuru na upatikanaji wa habari kwa wananchi kurahisisha upatikanaji wa habari na kushirikisha sekta binafsi na wadau wengine katika uwendeshaji wa sekta ya habari na utangazaji. Nitoe wito kwa wadau na wawekezaji kuendelea kuchangamikia fursa zilizopo katika sekta hii. Serikali tutaendelea kuimarisha zaidi mazingira ya kisera na kisheria kwa maendeleo na ukuwaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wa Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma ili kuhakikisha taarifa za utekelezaji wa kazi za Serikali inawafikia wananchi kwa wakati na ufanuzi wa hoja za

wananchi unatolewa na Serikali kwa wakati ili kufikia azma hiyo mwezi Mei, 2021 kulifanyika Mkutano wa Maafisa hao Mkoani Mbeya ambapo pamoja na mambo mengine Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alielekeza umuhimu wa kutoa taarifa kwa umma kwa wakati badala ya kusubiri mpaka wananchi walalamike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, usikivu wa redio za *TBC* umeendelea kuimarishwa katika Wilaya za Same, Sikonge, Kahama, Bunda, Nkasi, Kasulu na Karagwe ambapo ufungaji wa mitambo ya kurusha matangazo unatarajija kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2021. Kazi ya ujenzi wa mitambo kwa ajili ya kuongeza mawanda na usikivu katika Wilaya za Ngara, Kyela, Ruangwa, Kilombero na Ludewa unaendelea na unatarajija kukamilika mwezi Juni, 2021. Vilevile ujenzi wa mitambo ya redio ya *FM* katika Wilaya za Tanganyika, Makete, Uvinza, Mbinga na Ngorongoro unaendelea na unatarajija kukamilika mwezi Agosti, 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kutohana na hatua zinazochukuliwa na Serikali, usikivu wa redio umeongezeka kutoka Wilaya 87 mwaka 2017 hadi Wilaya 102 mwaka 2021. Miradi inayoendelea kutekelezwa kwa sasa ikikamilika, usikivu utaongezeka na kufikia Wilaya 119 kati ya Wilaya zote nchini 161 sawa na asilimia 74 na matarajio ya Serikali ni usikivu wa redio kuzifikia Wilaya 134 sawa na asilimia 83 za Tanzania Bara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mpango wa Serikali ni kufunga mitambo ya redio kwa ajili ya usikivu kwa Wilaya 27 zilizosalia ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kupitia *TBC* cimeanzisha channeli ya televisiuni yani *TBC2* ikiwa ni utekelezaji wa azma ya kuendelea kupanua wigo wa kupeleka habari kwa umma, inayoendana na mahitaji ya walaji kwenye soko hasa vijana na wapenda burudani. Studio hii itatumika kwa ajili ya kuandaa na kurusha vipindi vya habari, elimu na burudani kwa vijana, kuandaa vipindi vya biashara, kuendesha

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

midahalo mbalimbali na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vyaa habari.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) iliendelea kujiimarisha kibashara kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuboresha magazeti yake kimuonekano na Kimaudhui. Taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya *TSN* ni kama inavyoonekana katika sehemu ya 3.12 ya hotuba yangu.

*Mheshimiwa Spika*, sekta ya maendeleo ya utamaduni; Serikali imeanzisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania ambao ulisajiliwa tarehe 30 Septemba, 2020. Mfuko huu unalenga kuwawezesha watendaji wa kazi za kiutamaduni na kisanaa kimitaji na kuwajengea uwezo wa kitaalam ili kuwawezesha kuandaa bidhaa bora zinazomudu ushindani kitaifa na kimataifa. Utekelezaji wa majukumu ya mfuko huu na hivyo kuwawezesha walengwa kupata manufaa yanayokusudiwa utaanza mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kinaombwa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Kiswahili hivi sasa yanaongezeka kwa kasi duniani. Kukubalika kwa lugha hii kunachagizwa na mambo kadha wa kadha ikiwemo msukumo wa kustawisha lugha hiyo ndani na nje ya nchi uliofanywa na unaoendelea kufanywa na viongozi wetu wa kitaifa. Juhudi hizo zimefanywa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na watangulizi wake na kwa sasa zinaendelezwa kwa kasi na Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali za kuendeleza na kubidhaisha Kiswahili kitaifa na kimataifa zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kufungua kituo cha kufundisha kutaini na kupima ujuzi wa lugha ya Kiswahili kwa wageni kilichopo katika ofisi ya BAKITA, Dar es Salaam, kuititia kituo hiki tayari mafunzo yametolewa kwa watu mbalimbali kama inavyobainishwa katika sehemu ya 3.21 ya hotuba yangu ukurasa wa 18. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua zingine zilizochukuliwa na sekta hii kuitia BAKITA katika kikitangaza kukiendeleza na kuklibidhaisha Kiswahili kitaifa na kimataifa ni kuendesha mafunzo ya kufundisha Kiswahili kwa wageni yanayoambatana na usajili wa wataalam hao katika kanzidata ambayo hadi sasa ina wataalam 1,318; kutambua na kutoa ithibati kwa vituo mbalimbali vya kufundisha Kiswahili kwa wageni, na kuwezesha idadi ya vituo hivyo kufika 15 hadi sasa; kutoa mafunzo ya msasa yaliyoambatana na upimaji wa kiwango cha weledi kwa ukalimani wanafunzi 11 wa lugha za Kiingereza, Kireno na Kiarabu. Hadi mwezi Mei, 2021 idadi ya wakalimani waliosajiliwa imefikia 45 ambapo 20 ni wakalimani waliobobea na 25 wanahitaji mafunzo zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu utekeleza wa Programu ya Urithi ya Ukombozi wa Bara la Afrika ambapo hadi sasa tayari mashuhuda walioshiriki na kushuhudia harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika yaani Maktaba Hai 2,027 wamehojiwa na nyaraka 6,782 za harakati hizo zimekusanya na kuhifadhiwa. Tarehe 21 Mei, 2021 kulifanyika kongamano lililolenga kutambua kuenzi na kuelimisha jamii kuhusu Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika uliopo nchini ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kongamano hili liliazimia kufanyika kwa tathmini katika maeneo ya Urithi wa Ukombozi wa Bara yaliyopo nchi ili yakarabatiwe na kuifadhiwa, kuingizwa katika Gazeti la Serikali maeneo yanayokidhi vigezo vya kuwa uUrithi wa Taifa ili yalindwe kisheria, kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa kutambua mchango wake katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na kuhamasisha ujifunzaji wa historia hiyo mashulenii.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa sanamu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika Jijini Addis Ababa, Ethiopia uliendelea kuratibiwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano

wa Afrika Mashariki. Ujenzi wa sanamu hiyo kwa kutumia malighafi ya shaba nyeusi yaani *bronze* kwa gharama ya dola za Marekani 267,992.60 ambayo imetengwa na SADC, unalenga kuenzi mchango wa viongozi wa Afrika katika mapambano ya kuzikomboa nchi ya Bara hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya maendeleo; maendeleo ya sanaa; majukumu yaliyotekelawa katika kipindi hiki katika sekta hii ni pamoja na kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wasanii na wadau wa sanaa ambapo taasisi zinazowahudumia wasanii za BASATA, Bodii ya Filamu na COSOTA zimiwekwa katika eneo moja yani *One Stop Center* kwenye Jengo la Utumishi liliopo Kivukoni. Hatua hii ni pamoja na mambo mengine itawapunguzia muda kadhia na gharama wasanii wetu na wadau wengine wanaohudumiwa na taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuikuza sekta kuikuza sekta ya sanaa ili iendelee kutoa ajira kwa makundi mbalimbali ya jamii kama inavyoolekezwa katika Ibara ya 241 ya llani ya CCM ya mwaka 2020-2025, Wizara inaendelea kupitia sheria na kanuni zake ili kuziboresha ziendane na mahitaji na hali ya sasa. Mwezi Mei, 2021 Wizara ilifanya kikao na wadau kuhusu kanuni ya 25 ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa iliwayahimiza kuwasilisha kazi zao kwa ajili ya uhakiki kabla ya kurushwa kwenye vyombo vya habari ili kudhibiti masuala ya kimaadili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza pande zote mbili, yaani Wasanii na BASATA, Wizara iliamua kusitisha utekelezaji wa kanuni hiyo ili kutoa nafasi kwa wadau kutoa maoni kuhusu namna bora ya kuitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara imelekekeza BASATA kusimamia uandaaji wa mwongozo utakaotumiwa na wazalishaji wa kazi za sanaa na Idara za Muziki za vyombo vya habari ili kuhakikisha masuala ya kimaadili yanazingatiwa katika kazi za sanaa. Wizara inaendelea kuwashimiza wasanii wetu kuendelea kuzingatia sheria za nchi na kulinda maadili yetu wakati wa kuandaa na kushiriki shughuli za sanaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta tija katika sekta ya sanaa, Wizara pia ipo katika hatua za awali za kuandaa sera ya sanaa ili kuendana na hali halisi ya maendeleo ya kisekta. Wizara inatambua kuwa sanaa sasa imekua, na ipo haja ya kuweka misingi ya kisera inayoitambua kama Sekta rasmi inayoweza kuwanufaisha wadau kiuchumi kama zilivyo shughuli nyingine rasmi na kwa kuzingatia pia maelekezo ya Ibara ya 241 ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 yanayoitaka Serikali kuendesha sekta hii kibashara.

Mheshimiwa Spika, ili kuenzi mchango wa wasanii mashuhuri katika Taifa letu na kutunza kazi zao kwa matumizi ya kizazi cha sasa na kijacho, Serikali inaandaa kanzidata ya wasanii hao itakayowezesha kazi zao kuhifadhiwa katika mfumo wa kidijiti. Lengo hapa ni kutafiti, kutambua, kuhifadhi na kutangaza wasanii na kazi zao za sanaa zilizowahi kuvuma na kuwa na mguso na mchango chanya katika jamii ya Kitanzania kwa wasanii wote walio hai na wale waliotangulia mbele ya haki. Hatua hii sio tu itatambua mchango wa walengwa katika kukua sekta kwa sanaa hapa nchini bali pia itarahisisha kazi ya kusimamia mapato yatokanayo na matumizi ya kazi zao kwa manufaa ya wasanii wenyewe wategemezi wao na hata warithi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yaliyotekelizwa katika sekta hii ni mfumo wa usajili wa usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa ulianza kuandaliwa na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021. Mfumo huu utaimarisha na kurahisisha usajili wa wasanii na kuwezesha utoaji wa vibali vya wasanii kwenda nje ya nchi kufanya kazi za sanaa kwa njia ya kieletroniki na hivyo kupunguza gharama na urasimu. Wizara kuitia BASATA ipo katika maandalizi ya utoaji wa tuzo za muziki nchi ambazo zinatarajiwa kutelewa ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia *COSOTA* na kushirikiana na wadau imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha mapato ya wasanii yanaimarika na mchango wa shughuli za sanaa katika pato la Taifa unaimarika. Hatua

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

hizo ni kama inavyoonekana katika aya ya 104 na 105 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, upande wa taasisi ya sanaa na utamaduni Bagamoyo yaani *TaSuBa* taasisi hiyo iliendelea kutoa mafunzo ya utamaduni na sanaa ambapo wanachuo 397 walisajiliwa. Ili kuhakikisha kuwa vijana wengi wenye vipaji vyta sanaa ambaao hawana vigezo vyta elimu vyta kujunga na mafunzo ya sanaa kupita mfumo wa *NACTE* wanapata mafunzo Wizara ina mkakati wa kuanzisha ushirikiano kati ya Taasisi ya Sanaa na utamaduni Bagamoyo na Vyuo vyta *VETA* vilivyopo nchi nzima katika kutoa mafunzo hayo kwa kuanzia na vituo vichache vitakavyoteuliwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maendeleo ya michezo; nchi yetu imeendelea kuwa na wachezaji wanaocheza katika michezo mbalimbali nje ya nchi ambayo ni fursa ya ajira kwa wanamichezo wetu kimataifa hadi kufikia mwezi Mei, 2021 Tanzania ilikuwa na jumla ya wachezaji 54 wanaocheza michezo mbalimbali nje ya nchi ambapo mpira wa miguu ni 32 mpira wa kikavu ni 16 mpira wa wavu ni wanne na mchezo wa kabati ni wawili.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wananchi katika michezo uliendelea kuimarike ambapo baraza la michezo la Taifa (BMT) lilisajili vyama 12 vilabu 89, taasisi tano za kimichezo, wakuzaji wa vipaji vyta michezo 11, vituo vyta michezo vinne na mawakala wa michezo 21. Watala wa michezo waliendelea kuzalishwa ili kuendana na mahitaji kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya ambapo mafunzo ya muda mrefu yaliyotelewa kwa wanachuo 244.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni hatua ya kuendeleza michezo nchini Wizara ilikamilisha rasimu ya mkakati wa Taifa wa maendeleo ya michezo, mkakati huo umeweka malengo mbalimbali ya kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya michezo ikiwa ni pamoja na kuimarike miundombinu ya michezo, kuimarike vyanzo vyta mapato ya kugharamia michezo, kuwa na wataalam wa michezo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wanaokidhi mahitaji kwa michezo mbalimbali na kuimarisha michezo mashulenii.

Mheshimiwa Spika, malengo mengine ni kuimarisha uteuzi wa wachezaji na maandalizi ya timu za Taifa, kuwa na utaratibu bora wa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo, kuimarisha ushiriki wa umma katika kufanya mazoezi, pamoja na kuimarisha utawala bora michezoni. Mkakati huo ambao unabainisha pia majukumu ya wadau mbalimbali katika kuendeleza michezo nchini unatarajiwaa kuzinduliwa mwezi Julai, 2021.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Baraza la Michezo la Taifa na Mashirkisho/Vyama ya Michezo iliendelea kuratibu ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa na kupata mafanikio mbalimbali. Mafanikio hayo ni pamoja na timu ya Tanzinia *Tanzanite* kutoa kombe la COSAFA nchini Afrika Kusini mwezi Novemba, 2020; *Taifa Stars* kufanikiwa kushiriki mashindano ya CHAN nchini Cameroon mwezi Januari, 2021; timu ya kwa wachezaji wenye umri chini ya miaka 20 (*under 20*) kushiriki fainali za AFCON kwa mara ya kwanza mwezi Februari, 2021.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika mpira wa miguu ni Kablu ya Simba kuingia robo fainali katika mashindano ya Klabu Bigwa Barani Afrika na timu ya Namungo kushinda mechi mbalimbali katika hatua za awali za Kombe la Shirikisho Barani Afrika, kupitia Bunge lako Tukufu nipongeze Klabu ya Simba na Klabu ya Namungo kwa mafanikio haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo wa ngumi kumekuwepo na mafanikio mbalimbali kama inavyoonekana katika aya ya 119 ya hotuba yangu, niwapongeze mabondia wetu kwa kuwakilisha vyema Taifa letu katika masumbwi ikiwemo Hassan Mwakinyo na Ibrahim Class kwa ushindi walioupata katika mapambano yao ya tarehe 28 Mei mwaka 2021. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya ni dhamira ya Serikali kwa kushirikiana na vyama vya mashirikisho ya michezo kutekeleza mikakati mbalimbali itakayowezesha kuongeza ushiriki wa jamii katika michezo katika ngazi za jamii na shule yaani *sports for all* ili kupitia ushiriki huo viibuliwe vipaji vitakavyoendelezwa na kuwezesha ongezeko la ajira kwa wachezaji ndani na nje ya nchi kwa maana ya *professional sports*.

Mheshimiwa Spika, mikakati itakayotelekezwa ni pamoja na kuimarisha ugharamiaji wa michezo kwa kuibua vyanzo vipyta vya mapato, kuendeleza michezo katika shule na taasisi za elimu, kuimarisha miungombinu ya michezo na vifaa vya michezo katika ngazi mbalimbali na kuboresha utaratibu wa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali. Mikakati mingine ni kuimarisha ushirika wa wananchi wa makundi mbalimbali katika michezo na kuanzisha na kuendeleza shule za michezo yani *sports academies*.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wachezaji wa zamani wa soka, ngumi na riadha waliowakilisha nchi yetu vyama katika mashindano ya kimataifa, kwa uchache wa wachezaji hawa ni kama inavyoonekana katika aya ya 122 na mia 123 ya hotuba yangu.

Napenda pia kuchukuwa fursa hii kuupongeza uongozi mpya wa *Bunge Sports Club* uliochaguliwa hivi karibuni unaohusisha Waheshimiwa Wabunge wafuatao kwa nafasi zao; Mheshimiwa Tarimba Abbas - Mwenyekiti; Mheshimiwa Esther Matiko - Makamu Mwenyekiti na Mheshimiwa Seif Gulamali - Meneja wa Klabu. (*Makof*)

Mheshimiwa spika, niwapongeze pia wajumbe wa klabu hiyo Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Rose Tweve, Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Aeshi Hilary, napenda kuuhakikishia uongozi huu na Waheshimiwa Wabunge kuwa Wizara itaendelea kuwapa ushirikiano wa dhati ili kutimiza malengo yanayokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa spika, kuhusu changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kukubiliana nazo, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2021 pia kulikuwepo na changamoto mbalimbali kama inavyoonekana katika sehemu ya mme ya hotuba yangu ukurasa wa 49 mpaka 50.

Mheshimiwa Spika, utandawazi na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani kuna athiri ya uzingatiwaji wa tamaduni mila na desturi za mtanzania hususani kwa vijana na baadhi ya wasanii wetu wamekuwa na hulka la kuiga mambo ambayo yanafanyika katika mataifa mengine kwa lengo la kushindana na soko la kazi za sanaa duniani.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wasanii wetu ili wazalishe kazi zinazoendana na misingi, mila na desturi na utamaduni wetu, ibara ya 32, 125, 239, 241 na 243 za ilani za uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 zinaielekeza Serikali kuchukuuwa hatua mbalimbali za kuendeleza sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo ili kuimarisha mchango wa sekta hizo katika maendeleo ya Taifa letu ikiwemo kuzalisha ajira hususani kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, maelekezo hayo ni pamoja na kuhakikisha wasanii wetu wanazingatia mila na desturi za jamii za Tanzania kwa ajili ya kulindwa na kuhifadhiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Spika, mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Wizara na taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kama ilivyoelezewa kwa kina na kisekta katika sehemu ya tano ya hotuba ya tano yangu ukurasa wa 51 mpaka 61.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaratibu uundwaji wa vyombo vyao kutekeleza Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016 yaani Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, miradi na programu mbalimbali zinazotekelizwa, kusajili vyombo vya habari na kuimarisha usikivu wa *TBC* katika maeneo mbalimbali nchini yasiyo na usikivu au wenye usikivu hafifu kama ilivyofafanuliwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara itawajengea uwezo wasanii wetu kimitaji na mafunzo kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, hatua ambayo itaongeza tija, ubora na ushindani wa kazi za sanaa na wabunifu wetu kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili Kitaifa na klmataifa pamoja na kufanya tafti kuhusu utamaduni, mila na desturi za jamii mbalimbali kwa lengo la kuzihifadhi na kuzienzi kwa kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika itaendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya hali ilivyo katika maeneo 260 ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika yaliyopo nchini ili yaweze kuhifadhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara itakamilisha uundwaji na kuanza matumizi ya mifumo mbalimbali ya kisasa ya kielektroniki ya kuwashudumia wasanii na wadau wengine wa sanaa ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma, kurahisisha urasimishaji wa sekta ya sanaa na shughuli za ubunifu na kuongeza mapato ya wasanii na Serikali kupitia ukusanyaji wa mirahaba.

Mheshimiwa Spika, mifumo hiyo ya kufuatilia matumizi ya kazi za sanaa, hususan muziki na filamu katika vyombo vya habari, mfumo wa kusambaza kazi za wasanii *online platform* kama ilivyo *Netflix*, na mfumo wa usajili na usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa sanamu ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika, Addis Ababa, Ethiopia, utaendelea kuratibiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Filamu itaendelea kuimarisha mazingira ya wadau wa filamu kushiriki katika kazi za filamu, kuhakiki filamu na kuzipanga katika madaraja na kutoa vibali vyta uoneshaji wa filamu kwa umma. BASATA itaendelea na zoezi la urasimishaji wa sekta ya sanaa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuweka mazingira bora ya kisheria na kikanuni, na *COSOTA* itaendelea kusajili wabunifu wa haki miliki na haki shirikishi, kukusanya mirahaba na kuigawa kwa wabunifu. *TaSuBa* itaendelea kudahili na kutoa mafunzo ya sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, Wizara itaendelea kuimarisha uibuaji na uendelezaji wa vipaji kuititia michezo shulenii, mashindano ya Taifa (*Taifa Cup*) kwa michezo mbalimbali na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Vipaji vya Michezo (*Sports Academy*) katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia itaendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji katika uanzishaji wa vituo vyta kukuzia vipaji vya michezo, kugharamia maandalizi ya ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali kwa kushirikiana na wadau na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika michezo.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango wa fedha kwa mwaka 2021/2022; ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2021/2022 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 ya jumla ya shilingi 54,741,802,000 ambapo shilingi 19,146,653,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 14,880,149,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ni shilingi 20,715,000,000. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, mwisho na shukrani; mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2020/2021 yametokana pia na ushirikiano wa wadau mbalimbali. Nitoe shukrani zangu za dhati kwa wanahabari kwa kuendelea kuwawezesha wananchi kupata haki yao ya Kikatiba ya kupata habari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nilipongeze Baraza la Habari Tanzania (*MCT*), Jukwaa la Wahariri, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania, *Press Clubs*, Vyuo vya Kati vya Uandishi wa Habari, magazeti, redio, televisheni na taasisi za kihabari kama Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira, kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuendeleza sekta ya habari nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wasanii wetu kwa kuendelea kuitangaza vyema sanaa ya Tanzania kitaifa na kimataifa na pia timu na wanamichezo wote walolilletea Taifa letu sifa kimataifa. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo ya Taifa letu na watu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho chambilecho wahenga, jifya moja halinjiki chungu na umoja ni nguvu. Niwashukuru wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wa ndani ambao kimsingi ni wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wadau wa nje, nazishukuru Nchi za China, Japan, Korea Kusini, Usvisi na Ujerumani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (*JICA*). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara kwa anuwani za [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz) na [www.maelezo.go.tz](http://www.maelezo.go.tz).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**HOTUBA YA MHE. INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB.),  
WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO,  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/22 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

- 1. *Mheshimiwa Spika*,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.
- 2. *Mheshimiwa Spika*,** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa buheri wa afya na kuendelea kujalia nchi yetu amani, utulivu, mshikamano na upendo. Aidha, nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa.
- 3. *Mheshimiwa Spika*,** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kwake kushika nafasi hiyo kufuatia kifo cha mpPENDWA wetu, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Natoa pole kwa Mhe. Rais, familia, wadau wa Sekta za Wizara na Watanzania wote kwa ujumla kufuatia kifo cha mpPENDWA wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Aidha, nampongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- 4. *Mheshimiwa Spika*,** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuendelea kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Sita. Fauka ya hayo, nawapongeza Waheshimiwa mawaziri wote kwa kuteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali katika Awamu hii. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioaminiwa na kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kuwa Naibu Spika. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao ili kuliwezesha Bunge hili kutekeleza majukumu yake. Ni imani yangu kuwa uzoefu, umahiri, hekima na busara zenu katika kuliongoza Bunge hili Tukufu zitaendelea kutumika katika kuhakikisha nchi yetu na watu wake wanapata maendeleo yanayokusudiwa.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** kwa namna ya pekee nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuisimamia Wizara hii yenye dhamana ya kuratibu na kuendeleza Sekta za Kimkakati za Uraghibishi (*soft powers*) za nchi ambazo ni Habari; Utamaduni, Sanaa na Michezo. Naomba kumhakikishia Mhe. Rais utendaji bora na uliotukuka katika utekelezaji wa majukumu niliyokabidhiwa.

**7. *Mheshimiwa Spika*,** "Chanda chema huvikwa pete", ningependa kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2021/22 kupitia Kikao kilichofanyika tarehe 28 Machi, 2021. Wizara itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2021/22.

**8. *Mheshimiwa Spika*,** "Mwenda tezi na omo marejeo ngamani", sasa niwashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe

kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika Jimbo hili na kuwaleta maendeleo wana Karagwe. Ninawaahidi utumishi uliotukuka pamoja na ushirikiano wa dhati katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Aidha, naishukuru familia yangu kwa upendo wao na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu.

**9. *Mheshimiwa Spika*,** "Figa Moja Halinjiki Chungu", natambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nianze kwa kumshukuru kwa dhati Mhe. Pauline Gekul (Mb.), Naibu Waziri, kwa msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu; Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zillizo chini ya Wizara. Niwashukuru pia Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma ili kuleta tija na ufanisi.

**10. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka 2020/21 Bunge lako Tukufu liliwapoteza wabunge wenzetu, Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Muhamawe (CCM), Mhe. Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (CCM) Mkoa wa Manyara na Mhe. Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Konde (ACT Wazalendo). Nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuwapoteza wawakilishi wao hawa. "Hakika sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea". Aidha, nitoe pole kwa familia ya aliyekuwa Katibu Mtendaji wa BASATA, Hayati Godfrey Mngeze na wasanii kwa ujumla kwa kuondokewa na kiongozi huyo aliyetoea mchango mkubwa katika maendeleo ya sanaa nchini.

**11. *Mheshimiwa Spika*,** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-25; ahadi na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 - 2025/26 na

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 katika maeneo yanayohusu Sekta za Wizara. Aidha, Hotuba hii imezingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2020/21 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2021/22.

**12. *Mheshimiwa Spika*,** Hotuba hii imegawanyika katika sehemu nane (8): Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2020/21 na Sehemu ya Nne inaeleza Changamoto zilizojitokeza na Hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/22; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2021/22; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2021/22 na Sehemu ya Nane ni shukurani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

### **2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA**

**13. *Mheshimiwa Spika*,** Dira ya Wizara ni kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lili loshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za Sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo.

**14. *Mheshimiwa Spika*,** Dhima ya Wizara ni kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa Habari, kukuza Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.

**15. *Mheshimiwa Spika*,** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kusimamia na kuratibu kazi za Msemaji Mkuu wa Serikali; kuratibu na kusimamia Vyombo vya Habari; kuendeleza shughuli za sanaa, michezo na utamaduni na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza.

Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Raslimali watu ya Wizara na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodii ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Pia, Wizara inaratibu na kusimamia Sekta ndogo ya Utangazaji na Kamati ya Maudhui kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

### **3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2020/21**

#### **3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA**

##### **3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**16. *Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2020/21, Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Milioni Mia Tisa Sitini (Sh. 960,000,000) kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo viingilio katika Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, ukodishwaji wa kumbi za mikutano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, malipo ya usajili wa magazeti na majorida pamoja na mauzo ya vitambulisho vya waandishi wa habari na picha mbalimbali za Viongozi wa kitaifa. Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Themanini, Mia Moja na Tisa Elfu, Mia Nne Tisini na Moja (Sh.1,080,109,491) sawa na asilimia 113 ya lengo zimesanywa. Ongezeko hili linatokana na mauzo ya picha ya Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na kuimarika kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru kupitia Kituo cha Taifa cha Uhifadhi Data (NIDC) tangu Oktoba, 2020.

**17. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa taasisi nane (8) zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriva kukusanya njumla ya Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Sita Tisini na Nne, Mia Mia Nne Themanini na Nne Elfu (Sh.40,694,484,000) ambapo

hadi mwezi Mei, 2021 jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Sita Sitini na Tatu, Mia Nne Thelathini na Sita Elfu, Mia Mbili Themanini na Tatu (Sh.18,663,436,283) zilikusanywa sawa na asilimia 45.8 ya lengo la mwaka.

### **3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha**

**18. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21 Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja Arobaini, Mia Sita Arobaini na Moja Elfu (Sh.40,140,641,000) kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi. Kati ya fedha hizo Mishahara ni Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tisa Sabini na Tisa, Mia Mbili Thelathini na Moja Elfu (Sh.20,979,231,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nne Arobaini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.11,446,410,000) na Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Kumi na Tano (Sh.7,715,000,000). Aidha, mwezi Julai, 2020 Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ilihamishiwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, ikiwa na Bajeti ya Mshahara wa Shilingi Milioni Mia Tatu na Moja, Mia Tano Sitini na Nane Elfu (Sh.301,568,000) na Mradi wa Maendeleo (Mradi wa Kuwezesha Taasisi (*Institutional Support*) Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini (Sh.340,000,000). Hivyo, bajeti ya Wizara ya mwaka 2020/21 baada ya COSOTA kuhamia Wizarani ni Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Saba Themanini na Mbili, Mia Mbili na Tisa Elfu (Sh.40,782,209,000) ambapo Mishahara ni Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Mbili Themanini, Mia Saba Tisini na Tisa Elfu (Sh.21,280,799,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nne Arobaini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.11,446,410,000) na Miradi ya Maendeleo Shilingi Bilioni Nane, Milioni Hamsini na Tano (Sh.8,055,000,000). Miradi hiyo ni:

- a) Kuungeza Mawanda ya Usikivu wa TBC uliodhinishiwa Shilingi Bilioni Tano (Sh.5,000,000,000);
- b) Habari kwa Umma, uliodhinishiwa Shilingi Bilioni Moja (Sh.1,000,000,000);

- c) Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika ulioidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Tano Kumi Tano (Sh.515,000,000);
- d) Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo ulioidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Mbili Hamsini (Sh.250,000,000);
- e) Ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya ulioidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Tatu (Sh.300,000,000);
- f) Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam ulioidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Sita Hamsini (Sh.650,000,000); na
- g) Kuimarisha Taasisi ya COSOTA uliodhinishiwa Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini (Sh.340,000,000).

**19. *Mheshimiwa Spika*,** hadi mwezi Mei, 2021 Wizara ilipokea kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Shilingi Bilioni Ishirini na Tisa, Milioni Mia Sita Thelathini na Sita, Mia Sita Sitini na Nne Elfu, Mia Mbili Hamsini na Tisa (Sh.29,636,664,259) ambayo ni sawa na asilimia 72.6 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Sita Ishirini na Moja, Mia Sita Sitini na Nne Elfu, Mia Mbili Hamsini na Tisa (Sh.23,621,664,259) ambayo ni sawa na asilimia 72 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Katika Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyopokelewa, Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Moja Themanini na Mbili, Mia Nne Ishirini na Tisa Elfu, Mia Mbili Hamsini na Tisa (Sh.14,182,429,259) ni Mishahara sawa na asilimia 66.6 ya bajeti ya Mishahara na Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nne Thelathini na Tisa, Mia Mbili Thelathini na Tano Elfu (Sh.9,439,235,000) ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 82 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo.

**20. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, hadi mwezi Mei, 2021 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Sita, Milioni Kumi Tano (Sh.6,015,000,000) sawa na asilimia 74.6 ya Bajeti. Miradi iliyopokea fedha na kiasi kilichopokewa ni ifuatayo:

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- a) Kuongeza Mawanda ya Usikivu wa TBC Shilingi Bilioni Tano (Sh.5,000,000,000), sawa na asilimia 100;
- b) Habari kwa Umma, Shilingi Milioni Mia Tano (Sh.500,000,000), sawa na asilimia 50; na
- c) Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika Shilingi Milioni Mia Tano Kumi na Tano (Sh.515,000,000), sawa na asilimia 100.

Kwa upande wa miradi ambayo haijapata fedha ambayo inahusu ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo; ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya; ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam na kuimarisha Taasisi ya COSOTA, Wizara imekwishawasilisha maombi ya fedha hizo Wizara ya Fedha na Mipango na inatarajiwa zitapatikana kabla ya mwishoni mwa Juni, 2021.

### **3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2020/21**

#### **3.2.1 SEKTA YA HABARI**

**21.** *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya Sekta hii inayohusisha Idara ya Habari-MAELEZO, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (kwa upande wa maudhui ya utangazaji), ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu na Miradi imbalimbali ya kuwaleta wananchi maendeleo inayotekelizwa na Serikali.

**22.** *Mheshimiwa Spika*, Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016 inaelekeza kuanzishwa kwa Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari pamoja na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari. Bodi ya Ithibati itakuwa na jukumula la kutoa ithibati na vitambulisho kwa wanahabari wenye sifa,

kusimamia maadili na nidhamu miongoni mwa waandishi wa habari, kuishauri Serikali kuhusu elimu ya kitaaluma na mafunzo ya wanahabari na kuhakikisha wanahabari wanazingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya uandishi wa habari katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa sasa Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha Bodi hii.

Aidha, Baraza Huru la Habari litaundwa baada ya Bodi ya Ithibati kuanza kazi, kwa kuwa Baraza hili litaundwa na wanahabari wenyewe watakaokuwa wamepewa ithibati. Pamoja na majukumu mengine, Baraza hili litakuwa linashughulikia malalamiko na kutoa maamuzi kuhusiana na ukiukwaji wa maadili katika uandishi wa habari. Kwa upande wa Mfuko wa Mafunzo kwa wanahabari, Mfuko huo utawezesha waandishi wa habari kupata mafunzo, kusaidia kuboresha na kuendeleza maudhui ya ndani pamoja na kufanyika kwa tafiti katika uandishi wa habari na mawasiliano ya umma.

**23. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016 kutoa fursa ya kuwajengea uwezo wanahabari kimafunzo kupitia Mfuko huu, Sheria hii inawataka pia waajiri kuwakatia bima Wanahabari, kuifanya taaluma ya habari kutambulika kisheria badala ya kila mtu kufanya kazi ya habari na kuweka misingi mizuri na kusimamia maadili ya taaluma ya habari nchini.

**24. *Mheshimiwa Spika***, wananchi waliendelea kuhabarishwa kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2021 alifanya jumla ya mikutano 11 na vyombo vya habari. Kupitia mikutano hiyo, Msemaji Mkuu wa Serikali alizungumzia na kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa miradi, programu na mikakati ya Serikali. Vilevile, alifanya mahojiano na vyombo mbalimbali vya habari (Redio na Televisheni) vya ndani na nje kama vile Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), China Global Television Network (CGTN), Deutsche Welle (DW) na vingine vingi ambapo alizungumzia na kufanua masuala mbalimbali yaliyohitaji ufanuzi.

**25. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika**, Wizara ilianda jumla ya habari 1,453 zilizochapishwa katika magazeti mbalimbali zilitoa taarifa kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa kazi za Serikali. Aidha, jumla ya habari picha za video 2,342 na mnato 1,389 na vibango 1,503 ziliandaliwa na kusambazwa kupitia televisheni mtandao na mitandao ya kijamii ikiwemo *blogs, twitter, facebook, Youtube* na *Instagram* pamoja na Majarida ya Mtandaoni 40 yalichapishwa na kusambazwa.

**26. Mheshimiwa Spika**, wigo wa vyombo vyahabari umeendelea kuongezwa ili kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kupata taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli zao, ambapo katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Mei, 2021 jumla ya magazeti na majarida mapya 14 yalipatiwa leseni ambapo magazeti saba (7) ni ya wamiliki binafsi na saba (7) ni ya Serikali. Aidha, leseni 26 zilihuishwa zikihusisha leseni 25 za wamiliki binafsi na leseni moja (1) ya Serikali. Hadi kufikia mwezi Mei 2021, Tanzania ilikuwa na magazeti na majarida yaliyosajiliwa 257 ambapo 206 yanamilikiwa na Sekta Binafsi (80.16%) na 51 yanamilikiwa na Serikali (19.84%).


Aidha, katika kipindi hicho TCRA ilitoa leseni katika vituo saba (7) vya redio vyote vikiwa vinamilikiwa na watu binafsi, vituo vitano (5) vya televisheni ambapo vinne (4) vinamilikiwa na watu binafsi na kimoja cha Umma. Kwa upande wa maudhui mtandaoni, vituo 117 vya watoa huduma za televisheni kwa njia ya mtandao (*Online TV*) vilipewa leseni na vituo vinne (4) vya redio mtandaoni (*Online Radio*) vilipewa leseni. Vilevile, vituo 16 vya huduma za blogu mtandaoni pamoja na mtoa huduma mmoja wa Jukwaa Mtandaoni (*Online forum*) vilipatiwa leseni.

**27. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei, 2021 Tanzania ilikuwa na jumla ya vituo vya televisheni arobaini na tatu (43) ambapo vya Halmashauri za Wilaya ni vitatu (3), umma vitatu (3) na vya binafsi 37. Kwa upande wa redio, kuna jumla ya vituo 200 ambapo vya Halmashauri za Wilaya ni vinne (4), vya umma ni viwili (2) na vya binafsi ni 194. Aidha, televisheni


mtandao ni 451, redio mtandao ni 23, blogu ni 122 na jukwaa mtandaoni ni 9. Vyombo vyote vya utangazaji mtandaoni vilivyo na leseni vinaendelea kutoa huduma za utangazaji kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta. *Kiambatisho Na. 1* kinabainisha mwenendo wa usajili wa Vyombo vya Habari hadi Mei, 2021. Kwa upande wa vitambulisho vya waandishi wa habari, jumla ya vitambulisho 838 vilitolewa kwa waandishi wa habari wa ndani katika kipindi cha Julai 2020 hadi Mei, 2021.

**28. *Msheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa habari ambapo Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na wadau wengine wa habari kwa pamoja waliandaa na kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani tarehe 3 Mei, 2021 iliyoadhimishwa Kitaifa jijini Arusha.


**Kielelezo Na. 1: Magazeti na Majorida Yaliyosajiliwa hadi Mei, 2021**



**Kielelezo Na. 2: Vituo vya Televisheni Vilivyopewa Leseni hadi Mei, 2021**



**Kielelezo Na. 3: Vituo vya Redio Vilivyopewa Leseni hadi Mei, 2021**



### 3.2.1.1 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)

**29. Mheshimiwa Spika**, TBC ni Shirika la Utangazaji la Umma lenye majukumu ya kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha, kutafakarisha, kuendeleza utamaduni na kulinda taswira ya nchi. TBC inamiliki Redio (*TBCTaifa*, *TBCFM*, na *TBCInternational*); studio za redio za Kanda (Kigoma, Arusha, Dodoma na Songea); Televisheni (*TBC1*, *TBC2*, na *TBC3*)

(*Tanzania Safari Channel*); na TBC Mtandao (Tovuti ya [www.tbc.go.tz](http://www.tbc.go.tz), Programu Tumizi ya TBC Live; Mitandao ya kijamii ikiwemo Facebook, Instagram, Twitter na Youtube. Aidha, Shirika lina Tovuti na Programu Tumizi ya *Tanzania Safari Channel* ([www.tanzaniasafarichannel.go.tz](http://www.tanzaniasafarichannel.go.tz)).

**30. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TBC imeendelea kuchukua hatua za kuhakikisha usikivu wa redio za TBC unaimarika katika maeneo mbalimbali nchini yenye usikivu hafifu au kutokuwa na usikivu. Katika kipindi hiki, ujenzi wa mitambo ya kurusha matangazo ili kuongeza mawanda na usikivu wa redio za TBC uliendelea katika Wilaya za Same, Sikonge, Kahama, Bunda, Nkasi, Kasulu na Karagwe na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2021. Aidha, kazi ya ujenzi wa mitambo kwa ajili ya kuongeza mawanda na usikivu katika Wilaya za Ngara, Kyela, Ruangwa, Kilombero na Ludewa unaendelea kupitia ufadhilli wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021. Vilevile, ujenzi wa mitambo ya redio ya FM katika Wilaya za Tanganyika, Makete, Uvinza, Mbinga na Ngorongoro kupitia ufadhilli wa UCSAF unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2021. Vilevile, ujenzi wa jengo la kituo cha kurushia matangazo ya FM katika eneo la Kisaki, Morogoro ulikamilika mwezi Desemba, 2020 na ufungaji wa mitambo ulikamilika mwezi Mei, 2021. Matangazo ya redio za TBC katika kituo hiki yanapatikana katika masafa ya 87.9MHZ kwa TBC<sub>Taiifa</sub> na 89.9MHZ kwa TBC<sub>FM</sub>.

**31. Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutohana na hatua zinazochukuliwa na Wizara, usikivu wa redio umeongezeka kutoka Wilaya 87 mwaka 2017 hadi Wilaya 102 mwaka 2021. Miradi inayoeendelea kutekelezwa kwa sasa ikikamilika, usikivu utaongezeka na kufikia Wilaya 119 kati ya Wilaya zote 161 sawa na asilimia 74 na matarajio ya Serikali ni usikivu wa redio kuzifikia Wilaya 134 (83%) za Tanzania Bara pamoja na visiwa vya unguja na Pemba kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mpango wa Serikali ni kufunga mitambo ya redio kwa ajili ya usikivu kwa Wilaya 27 zilizosalia ifikapo mwaka 2025.

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**32. *Mheshimiwa Spika*,** ukarabati w a vyumba vya studio na kufunga mitambo ya redio katika Jiji la Dodoma umekamilika mwezi Mei, 2021 ambapo studio mbili za kuandalia vipindi zimejengwa, moja ya kurushia matangazo pamoja na Redio ya Jamii itakayorusha matangazo yake kupitia masafa ya 93.7MHz. Redio hii itawezesha kuandaa na kurusha vipindi vya redio kutoka Makao Makuu Dodoma pamoja na kurusha habari za kikanda na hivyo kuleta uelewa kwa wananchi kuhusiana na kazi wanazozifanya.

**33. *Mheshimiwa Spika*,** TBC inatarajia kufunga mitambo na vifaa vya kisasa vya kidijiti katika studio za redio (TBC *Taifa*, TBCFM na TBC *International*) zilizopo Barabara ya Nyerere, jijini Dar es Salaam. Ufungaji wa mitambo mipyua unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2021.

**34. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea pia kuimarisha studio za televisheni za TBC ambapo katika kipindi hiki ujenzi wa jengo la ghorofa moja lililopo Mikocheni, Dar es Salaam kwa ajili ya studio za TBC, lilikamilika. Aidha, mitambo na vifaa muhimu vya studio hiyo vilifungwa mwezi Februari, 2021 na utaratibu wa ufungaji wa vizuia mwangwi katika studio pamoja na ununuzi wa samani unaendelea na unatarajia kugharimu Shilingi Milioni Mia Nne Hamsini na Mbili (Sh. 452,000,000). Mradi huu ambao unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Tanzania na Korea Kusini, hadi sasa umegharimu Shilingi Billioni Tatu, Milioni Mia Mbili Hamsini na Saba, Mia Moja Themanini na Nane Elfu, Mia Nne Hamsini na Nane (Sh. 3,257,188,458) ambapo kati ya fedha hizo, Serikali ya Tanzania imetoa Shilingi Milioni Mia Sita Themanini, Mia Tano Themanini na Moja Elfu, Mia Mbili Kumi na Moja (Sh. 680,581,211). Aidha, mafunzo ya uendeshaji wa studio hiyo kwa wataalamu wa TBC yalitolewa mwezi Februari, 2021.

**35. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia TBC imanzishza channeli ya Televisheni ya TBC2 ikiwa ni utekelezaji wa azma ya kuendelea kupanua wigo wa kupeleka habari kwa umma, inayoendana na mahitaji ya walaji kwenye soko hasa vijana na wapenda burudani. Studio hii itatumika kwa ajili ya kuandaa na kurusha vipindi vya habari, elimu na burudani

kwa vijana; kuandaa vipindi vya biashara; kuendesha midahalo mbalimbali na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vya habari.

**36. Mheshimiwa Spika**, Shirika pia lilinunua mitambo na vifaa kwa ajili ya studio, *Fly away*, *LIVE-U* na studio j o n g e v u vyenye thamani ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Tisini na Moja, Mia Tano Sitini na Saba Elfu, Mia Sita (Sh. 2,491,567,600) kwa ajili ya Chaneli ya *Tanzania Safari* iliyoanzishwa mahususi kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo nchini. Vilevile, watendaji 58 kutoka mikoa yote ya Tanzania walipata mafunzo ya kuboresha uandaaji wa maudhui. Mafunzo hayo yaliendeshwa na mtaalamu mbobezi wa Kitanzania ambaye huandaa vipindi vya "National Geographic" na kampuni za kimataifa. Chaneli ya *Tanzania Safari* kwa sasa inapatikana katika visimbuzi vyote vilivyomo nchini bila kulipia (*free to air*) na katika chaneli za kimataifa za DSTV na ZUKU na pia inaendelea kuandaa maudhui yatakayorushwa kwa lugha za kigeni ikiwemo Kichina, Kijerumani, Kiingereza na Kireno ili kutangaza utalii katika mataifa mbalimbali ya kigeni.

**37. Mheshimiwa Spika**, kuwepo kwa chaneli hii kumeweza kwa Watanzania na nje ya nchi kufahamu vivutio vya utalii vilivyopo nchini, pamoja na kutangaza utamaduni wa Mtanzania ikiwemo historia ya ukombozi wa nchi zilizoko kusini mwa Afrika. Matokeo ya vipindi vinavyorushwa na chaneli hii yamekuwa na mwitikio chanya ndani na nje ya nchi. Mathalan, hivi karibuni chaneli ya *Tanzania Safari* iliandaa na kurusha vipindi vinavyohusiana na historia ya ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika ambapo baadhi ya familia za wapigania uhuru walioishi katika kambi ya Mazimbu iliyopo mkoani Morogoro ziliweza kuunganishwa na ndugu zao waliopo nchini Afrika Kusini.

### **3.2.1.2KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)**

**38. Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa na la msingi la Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ni kuwa chombo cha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi na pia wananchi

na Serikali yao. Jukumu hili linatekelezwa kupitia magazeti ya Daily News, Sunday News, HabariLeo na SpotiLeo na pia kwa kutumia njia za kielektroniki kama vile tovuti na mitando ya kijamii ikiwemo *Twitter*, *Instagram*, *Facebook* na *Youtube*.

**39. Mheshimiwa Spika**, TSN iliendelea kujiimarisha kibashara ili kukabiliana na ushindani mkubwa katika soko la habari chapishi (*print media industry*) na kuendelea kushuka kwa biashara ya magazeti kutokana na kushamiri kwa habari mtando, kwa kuboresha magazeti yake kimwonekano na kimaudhui na pia kwa kubuni, kuanzisha na kuendeleza vyanzo vipyta vya mapato. Vyanzo hivyo ni pamoja na utoaji wa ushauri wa kimedia (*media consultancy*), huduma za uchapaji kibashara, upigaji pitcha kibashara (*commercial photography*), huduma za uhariri na usanifu, huduma za uhakiki maandishi (*proofreading*) na uandaaji na uendeshaji wa majukwaa ya fursa za biashara na uwekezaji.

**40. Mheshimiwa Spika**, hatua hizi zimeiwezesha TSN kuendelea kujijenga kama Kampuni inayotoa huduma za habari kwa upana wake na hivyo kupanua wigo wa mapato lakini bila kusahau jukumu lake la msingi. Mathalan, katika kipindi hiki, Kampuni ilianza kutoa huduma za uchapaji kibashara kwa kutumia mtambo wake wa kidijiti (*digital printing machine*) ambazo ziliingiza jumla ya Shilingi Bilioni 1.027 na pia ilioa huduma ya Ushauri wa Kitaalamu kuhusumedia (*Media Consultancy*) kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na kuingiza kiasi cha Shilingi Milioni 314.

**41. Mheshimiwa Spika**, pia, TSN iliandaa na kuchapisha Matoleo Maalumu (*special supplements*) saba yaliyoangazia masuala mbalimbali ya Kitaifa ambayo, mbali na kuongeza maudhui ya magazeti, pia yalichangia katika kuongeza mapato kwa kuiingizia Kampuni jumla ya Shilingi milioni 892.9.

**42. Mheshimiwa Spika**, vilevile, TSN iliendelea kujiimarisha katika habari mtando kwa kuimarisha kitengo husika kwa kikipatia vifaa na nguvukazi na pia kuboresha uuuzaji wa magazeti yake kwa njia ya mtando kupitia Programu Tumizi za simu (*mobile apps*). Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 jumla ya

wasomaji 9,422 walikuwa wamejisajili kutumia huduma hii ambapo wasomaji 2,038 walijisajili kati ya mwezi Julai, 2020 na Mei, 2021 na wameilingizia Kampuni mapato ya Shilingi Milioni 34.23.

**43. Mheshimiwa Spika**, Kampuni pia iliongeza upatikanaji wa habari katika mitandao ya kijamii na hivyo kuvutia wasomaji na wafuatilaji. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Mei, 2021 jumla ya watu milioni 68.4 wameweza kuangalia video au kusoma habari kwenye kurasa za TSN na chaneli ya YouTube. Aidha, TSN inaendelea na juhudzi za kuanzisha studio ya kisasa (*multimedia studio*) kwa ajili ya kutengenezea vipindi na kumbukumbu za picha. Studio hii ambayo itagharamiwa kwa fedha za ndani ya Kampuni inatarajiwa pia kuwa chanzo cha mapato ya Kampuni kwa kufanya kazi za wateja mbalimbali.

**44. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, TSN pia imeendelea na juhudzi za kupata mtambo mpya na wa kisasa wa uchapaji ili kuondokana na mtambo uliopo wa kuchapa magazeti ambao umekuwa na ufanisi hafifu kutoptana na uchakavu na hivyo kuathiri ubora wa magazeti na kusababisha kupoteza wateja wa matangazo hasa ya rangi na pia kuongeza gharama za uendeshaji kwa kuharibika mara kwa mara na kuwa na matumizi makubwa ya mali ghafi. Taratibu za kupata fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 16 kwa ajili ya ununuzi wa mtambo huo zinaendelea katika Wizara ya Fedha na Mipango na utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka 2021/22. Mradi huu utakapoanza utakuwa chanzo kingine kikubwa cha mapato ya kampuni, sio tu kwa kuongeza biashara ya magazeti na matangazo kwa kuchapa magazeti yenye ubora wa hali ya juu, bali pia kwa kutoa huduma za uchapaji wa machapisho mbalimbali ndani na nje ya nchi.

### **3.2.1.3 MAMILAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

**45. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuititia Kamati ya Maudhui ina jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana ya Habari kuhusu utekelezaji wa

Sera ya Utangazaji, kusimamia na kufuatilia maudhui ya vituo vya utangazaji, kushughulikia malalamiko kutoka kwa watangazaji na watumiaji wa huduma za utangazaji pamoja na kuhakikisha kuwa Kanuni za Utangazaji zinafuatwa.

**46. *Mheshimiwa Spika*,** Kamati ya Maudhui ya TCRA iliendesha semina kwa Wahariri Wakuu na Waandaaji wa vipindi (Watozi) vya Redio na Televisheni kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuandaa vipindi bora vinavyozingatia maadili, weledi na Kanuni za Utangazaji. Jumla ya Wahariri 62 na Watozi 120 walishiriki kwenye semina hizo. Wizara kwa kushirikiana na TCRA itatekeleza Mpango maalumu wa kutoa elimu kwa watoa huduma za maudhui mtandaoni ili kuwajengea uwezo wa kutoa maudhui bora, yanayozingatia weledi na maadili ya utangazaji.

### **3.2.2SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI**

**47. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuwa na miongozo madhubuti ya kusimamia na kuendeleza utamaduni na inayoendana na wakati na mahitaji ya sasa, Wizara iliendelea kufanya mapitio ya Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997. Tayari rasimu ya Sera ya Utamaduni iliyohuishwa imeandaliwa na kwa sasa wadau wanaendelea kushirikishwa kutoa maoni na mapendekezo yao ili kuhakikisha Sera hiyo inazingatia mahitaji na matakwa ya jamii ya Watanzania. Kukamilika kwa Sera hii pamoja na mambo mengine, kutatoa fursa ya kuwa na Sera inayoendana na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na teknolojia yaliyotokea tangu kutungwa kwa Sera ya sasa ya Utamaduni miaka 24 iliyopita.

**48. *Mheshimiwa Spika*,** ikiwa ni hatua ya kuhakikisha watendaji wa kazi za kiutamaduni na sanaa wanapata mitaji ya kuimarisha kazi zao pamoja na kuzalisha bidhaa bora zinazomudu ushindani kitaifa na kimataifa, Serikali imeanzisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania ambao ulisajiliwa tarehe 30 Septemba 2020. Kuanzishwa kwa Mfuko huu kutakuwa chachu ya maendeleo katika Sekta za Utamaduni na Sanaa, kwa kutatua changamoto zinazozikabili Sekta hizo

na wadau wake na hivyo kuimarisha zaidi mchango wa Sekta hizo katika Pato la Taifa na ajira.

**49. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa Mwaka 2003 kuhusu Kulindwa kwa Urithi wa Utamaduni Usioshikika. Taarifa hiyo ambayo iliwasilishwa Makao Makuu ya UNESCO Paris, Ufaransa tarehe 15 Desemba, 2020, inaelezea pamoja na mambo mengine, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mkataba huo pamoja na vipengele muhimu vya Urithi wa Utamaduni Usioshikika unaopatikana nchini na inabainisha mikakati ya kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau ili kulinda na kuhifadhi urithi huo.

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mkataba huo ni pamoja na kutolewa kwa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi urithi wa utamaduni usioshikika, kuwajengea uwezo maafisa utamaduni na kubainisha vipengele vya urithi huu vyenye sifa ya kuingizwa katika orodha ya urithi wa Taifa na Kimataifa. Aidha, ubainishaji wa vipengele hivi umefanyika kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Manufaa ya utekelezaji wa Mkataba huu ni pamoja na nchi yetu kunufaika na fursa za mafunzo na uwezeshaji wa kifedha kupitia Mfuko wa Mkataba huu. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Mikakati itakayotekelezwa ili kuhifadhi urithi huu ni pamoja na kufanya tafiti katika jamii kabla ya kuondoka kwa maktaba hai (wazee), kuendeleza urithi huu ili kuvutia utalii wa kiutamaduni na kuongeza kipato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya Habari vikiwemo redio, televisheni na mitandao ya kijamii kuhusu kuzingatia mila na desturi za Mtanzania, kuhimiza uzingatiaji wa maadili na utamaduni wa Mtanzania hususan kwa vijana ili kuthamini na kuendeleza utamaduni wetu na kuurithisha kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**50. Mheshimiwa Spika**, fauka ya hayo, Wizara iliratibu Kikao kazi cha Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo kutoka katika Mikoa na Halmashauri zote nchini kilichofanyika tarehe 22-23 Mei, 2021. Lengo la Kikao kazi hicho lilikuwa ni kujadili

maendeleo, fursa na changamoto zinazozikabili sekta za utamaduni na michezo na kuweka mikakati ya utatuzi wa changamoto zilizopo kwa maendeleo ya Sekta hizo.

Fursa muhimu zilizotokana na kikao hiki ni pamoja na Maafisa hao kupata elimu ya uendelezaji wa amali za urithi wa utamaduni, ushirikishwaji wa Maafisa Utamaduni katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili, miongozo ya utekelezaji wa Sera na uboreshaji wa Muundo wa Utumishi wa Maafisa Utamaduni. Kikao hiki kilibainisha changamoto kubwa inayowakabili Maafisa Utamaduni kuwa ni upatikanaji wa bajeti ya kutekeleza shughuli za kiutamaduni katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na ukosefu wa uwakilishi stahiki katika vikao vya maamuzi ili kuhakikisha uzingatiwaji wa masuala ya utamaduni katika vipaumbele vya mamlaka hizo. Changamoto hizi zitatatuliwa kwa kuboreha Muundo wa Maofisa hao, zoezi ambalo limekwishaanza katika hatua za awali.

**51. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kuzingatia kuongezeka kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa, vifaa vya ukalimani vya kisasa vimenunuliwa kwa ajili ya kufundishia wakalimani kwa vitendo. Hatua hii itawezesha kukidhi mahitaji ya wakalimani wenye sifa za Kimataifa na kuimarisha ajira za wakalimani wanaoandaliwa nchini.

Ununuzi wa vifaa hivi utawezesha taifa kuzalisha wakalimani wengi zaidi na wenye weledi, kwani kwa muda mrefu wanafunzi wanaohitimu katika vyuo hawapati fursa ya kutumia vifaa hivi kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo, kwa kuwa hakuna chuo chochote hapa nchini ambacho kina vifaa hivi. Hivyo, itakuwa ni fursa muhimu kwa wahitimu hawa kupata mafunzo ya vitendo kabla na baada ya kuhitimu.

**52. *Mheshimiwa Spika*,** Matumizi ya Kiswahili hivi sasa yanaongezeka kwa kasi duniani. Kukubalika kwa lugha hii kunachagizwa na mambo kadha wa kadha ikiwemo msukumo wa kustawisha Kiswahili ndani na nje ya nchi uliofanywa na unaoendelea kufanywa na viongozi wetu wa

kitaifa. Juhudi hizo zimefanywa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na watangulizi wake, na kwa sasa zinaendelezwa kwa kasi na Rais wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Villevile, nitambue mchango wa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) Bi. Stergomena Lawrence Tax ambaye kwa kushirikiana na Serikali amewezesha lugha hiyo kukubalika katika SADC kama lugha rasmi ya umoja huo. Aidha, baada ya Kiswahili kuwa moja ya lugha za Umoja wa Afrika, mchakato unaendelea wa kuifanya lugha hiyo kuwa lugha ya kazi katika Umoja huo.

### **3.2.2.1 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)**

**53. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu ya BAKITA ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kuimarisha lugha ya Kiswahili kitaila na kimataifa.

**54. *Mheshimiwa Spika*,** katika kubidhaisha Kiswahili kitaifa na kimataifa, BAKITA limefungua kituo cha kufundisha, kutahini na kupima ujuzi wa lugha ya Kiswahili kwa wageni kilichopo katika Ofisi zake. Kituo hiki tangu kilipoanza kutoa huduma mwaka 2020 kimetoa mafunzo ya Kiswahili kwa watu mbalimbali wakiwemo raia wawili wa Polandi, wawili wa Jamhuri ya Cheki, mmoja wa Uingereza, na mmoja wa Kanada. Aidha, BAKITA limepima ujuzi wa Kiswahili kwa mabalozi wawili wa nchi za Polandi na Italia, wafanyakazi wawili mmoja wa Ubalozi wa Uingereza na mwingine wa Ubalozi wa Italia. Pia, huduma hiyo imetolewa kwa raia mmoja wa India na mwingine wa Uganda. Hata hivyo, wingi wa wageni waliokuwa wakitarajiwa kujunga na kituo haukufikiwa kutohana na mlipuko wa ugonjwa wa Korona.

Aidha, katika kukabiliana na hali hiyo programu maalumu inayoitwa *SWAHILI PRIME* imeandaliwa na itaanza rasmi kutumika kufundishia Kiswahili kwa njia ya mtandao mwezi Juni, 2021. Fauka ya hayo, taratibu na majadiliano ya kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili kwa wageni katika balozi za Tanzania yameanza na kwa kuanzia, kipaumbele kimewekwa katika nchi za China, Ethiopia, Afrika Kusini,

Zimbabwe na Msumbiji kutohana na nchi hizo kuonyesha mahitaji makubwa zaidi ya kuifahamu lugha ya Kiswahili. Mpango uliopo ni kuhakikisha balozi zetu zote zinakuwa na vituo nya kufundisha Kiswahili.

**55. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Mwongozo wa Kitaifa wa Kufundisha Kiswahili kwa Wageni unaolenga kuboresha na kuweka ufananivu wa ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni umeandaliwa. Mwongozo huu tayari umeanza kutumiwa na vituo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni ndani na nje ya nchi. Pia, umesambazwa kwenye balozi za Tanzania katika nchi za Namibia, Burundi na Korea Kusini. Balozi hizi ni zile ambazo tayari zimeanzisha vituo au zipo katika maandalizi ya kufungua vituo hivyo.

**56. *Mheshimiwa Spika*,** ili kufanikisha ubidhaishajikatika uwanja wa ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni yalitolewa kwa wataalamu 48 wa mkoani Dar es Salaam na Tanga. Mikoa mingine iliyokwishapatiwa mafunzo hayo tangu mwaka 2018/2019 ni Dar es Salaam (awamu 14), Mwanza (awamu 2), Mbeya (awamu 2), Arusha (awamu 1), na Iringa (awamu 1). Aidha, hadi sasa idadi ya wataalamu waliosajiliwa ni 1,318. BAKITA litaendelea kutoa mafunzo haya katika Mikoa mingine katika mwaka 2021/22.

**57. *Mheshimiwa Spika***ili kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika mikutano na shughuli mbalimbali za kitaifa na kimataifa, huduma ya ukalimani ilitolewa katika mikutano kadhaa ikiwemo mikutano mitatu ya Asasi za Kiraia zinazojihusisha na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto na masuala ya afya ya akili. Vilevile, huduma hii ilitolewa katika shughuli nyingine za ndani ya nchi kama vile dhifa za kitaifa.

**58. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuimarisha huduma ya ukalimani, mafunzo ya msasa yaliyoambatana na upimaji wa kiwango cha weledi wa ukalimani yalitolewa kwa wakalimani wanafunzi 11 wa lugha za Kiingereza, Kireno na Kiarabu. Hadi Mei, 2021 idadi ya wakalimani waliosajiliwa imefikia 45

ambapo kati ya hao, 20 ni wakalimani waliobobe na 25 wanahitaji mafunzo zaidi. Kwa sasa Tanzania inahitaji wakalimani wapatao 70 wa kuhudumu katika lugha mbalimbali, hivyo wakalimani watandelea kupatiwa mafunzo na kuimarishwa zaidi katika lugha rasmi za Jumuiya za kikanda na kimataifa, mathalan SADC na Umoja wa Afrika.

**59. *Mheshimiwa Spika*,** huduma ya tafsiri kwa mashirika, idara, wizara, ofisi za balozi na watu binafsi ilitolewa kwa nyaraka 738. Tafsiri hizo zililhusisha lugha za Kichina, Kituruki, Kiingereza, Kiarabu, Kihispaniola, Kijerumanji, Kireno na Kifaransa

**60. *Mheshimiwa Spika*,** ili kukieneza Kiswahili kitaifa na kimataifa, Kamusi ndogo ya semi za kila siku ya *Kiswahili – Kiingereza - Kireno* na *Jarida la Lugha Yetu* vilichapishwa na tayari vimeanza kutumiwa. Pia, Kitabu cha *Furahla Kiswahili* kinachotumiwa kufundisha Kiswahili kwa wageni hatua ya awali kimepitiwa kwa lengo la kukiboresha na kukifanya kiendane na *Mwongozo wa Kitaifa wa Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni* na kinatarajiwu kukamilika na kuchapishwa ifikapo Machi, 2022.

**61. *Mheshimiwa Spika*,** ili kusimamia ubora wa mafunzo ya Kiswahili kwa wageni, utambuzi na ithibati imetolewa kwa vituo vitano vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambavyo ni Nuru Cultural and Swahili Training Solution (Dar es Salaam), Modern Linguistics and African Cultural Promotion Centre - MOLAC (Arusha), UPI Innovations and Development (Dar es Salaam), Kituo cha Kufundisha Kiswahili kwa Wageni Tanga na Swahili Community Centre. Hadi sasa jumla ya vituo 15 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni vimekwishatambuliwa rasmi.

Vituo vingine ambavyo tayari vilishasajiliwa ni Swahili Dar Language School (Dar es Salaam), Leam Swahili (Dar es Salaam), Peace Corps Tanzania (Dar es Salaam), Chuo cha Maendeleo na Ushirkiano wa Kimataifa - MS TCDC (Arusha), South Africa Fellowship of Churches (Afrika Kusini), Isiders Languages Center (Dar es Salaam), Lilinga Swahili School

(Iringa), Kiswahili na Utamaduni – KIU (Dar es Salaam), Swahili Hub ( Dar es Salaam) na Italy Swahili Language School (Italia).

**62. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhakikisha Kiswahili kinasheheni msamiati mpya na unaokidhi matumizi na mahitaji katika nyanja mbalimbali, jumla ya msamiati 216 wa mazingira na 103 wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO 19) ulipitishwa (kusaniifishwa). Aidha, vifungu 100 vya maneno kwa ajili ya tovuti ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania navyo vilisanifishwa na kwa ujumla wake kufanya matumizi ya Kiswahili yaende sawia na mambo yanayoibuka katika jamii pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Baadhi ya msamiati huo umepata mashiko makubwa Kitaifa na Kimataifa na mionganoni mwake ni matumizi ya neno barakoa (mask), kiambukuzi/kipukusi (*sanitizer*) na UVIKO 19 (*COVID 19*) kwa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Korona. Vilevile, kwa upande wa Mazingira matumizi ya maneno kama vile mvuaasidi (*acid rain*), uasilishaji (*adaptation*) na vichafuzi hewa (airborne particulates); nayo yametandawaa Kitaifa na Kimataifa.

**63. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na usanifishaji huo, kumekuwepo na maneno magumu ambayo mara nyingi wananchi hushindwa kuyaelewa kiurahisi. Katika kutatua changamoto hiyo, BAKITA inaendeleza jitihada za kupata maneno rahisi ili kupata mashiko ya kimatumizi. Hata hivyo, yapo maneno yenye maana maalumu katika uwanja fulani ambayo hayawezi kufanana na maneno ya kawaida hivyo kitakachofanyika ni kuyafafanua kwa wataalamu na wanajamii.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili, vipindi 583 vya kuelimisha umma viliandaliwa na kurushwa hewani kuititia redio na televisheni za ndani na nje ya nchi. Aidha, makala 32 zinazotoa elimu ya sarufi, fasih, historia na maendeleo ya Kiswahili ziliandaliwa na kuchapishwa katika gazeti la HabariLeo ambalo lina mkataba na BAKITA tangu 2018. Vilevile, makala mbili (2) zilichapishwa katika gazeti la Mwananchi.

Pia, elimu ya lugha ilitolewa kuititia mitandao ya kijamii ya *YouTube, Twitter, Facebook na Instagram*. Halikadhalika, ilitolewa semina kwa waandishi na watangazaji wa radio, televisheni na magazeti katika mikoa ya Morogoro, Mtwara na Tanga. Semina iliyolenga matumizi ya lugha pamoja na uzingatiaji wa adabu ya lugha ilitolewa pia kwa wasanii kuititia Jukwaa la Wasanii linaloandaliwa na Baraza la BASATA. Aidha, BAKITA lilitoa ithibati ya matumizi ya lugha katika vitabu 103 ambapo vitabu 36 vimeandikwa na Taasisi ya Elimu Tanzania na vingine 67 vimeandikwa na waandishi mbalimbali.

**65. *Mheshimiwa Spika*,** katika kukturangaza Kiswahili ndani na nje ya nchi, Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili (MASIKI) yaliandaliwa na kufanyika Jijini Dodoma tarehe 1920 Januari, 2021. Katika maadhimisho hayo aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alitunukiwa Nishani ya Juu ya Shaban Robert kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kuendeleza Kiswahili.

Maadhimisho haya yaliwakutanisha wataalamu, wadau na wapenzi wa lugha ya Kiswahili wapatao 520 na hivyo kupata fursa ya kujadili mada mbalimbali zinazohusu Kiswahili na hasa mbinu za ubidhaishaji wa Kiswahili na kuweka Mikakati ya kuendeleza lugha hiyo ndani na nje ya nchi kama vile kuimarisha taaluma ya ukalimani na tafsiri, uandaaji wa walimu na vitabu vya kufundisha Kiswahili kwa wageni na kuimarisha stadi za kufundisha kwa kutumia mtandao. Aidha, katika maadhimisho hayo michango na jithada za wadau mbalimbali katika kuendeleza lugha hiyo zilitambuliwa.

### **3.2.2.2 PROGRAMU YA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA**

**66. *Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2011 Tanzania ilikabidhiwa na Umoja wa Afrika (AU) kuititia Azimio Namba 357 {Assembly/AU/Dec (XVI)} jukumu la kuratibu Programu ya Afrika iitwayo “Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (African Liberation Heritage Programme)” yenye jukumu la kukusanya,

kuhifadhi na kutangaza kumbukumbu kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ikiwemo nyaraka, makaburi, majengo, mahandaki, silaha, sare, hotuba na magari kwa matumizi ya vizazi nya sasa na vijavyo. Nchi yetu ilipewa jukumu hilo ikiwa ni hatua ya kutambua mchango wake wa kupigiwa kifani katika harakati za kuzikomboa nchi za Afrika, hususani Kusini mwa Bara hilo. Utekelezaji wa Programu hii unalenga pia kujenga Kituo cha Kikanda (*Regional Centre*) cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika Jijini Dar es Salaam kitakachokuwa na makumbusho, maktaba, kituo cha utafiti na ukumbi wa maonesho.

**67. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza Programu hii tayari mashuhuda walioshiriki na kushuhudia harakati za ukombozi wa Bara la Afrika (Maktaba Hai) 227 wamehojiwa na nyaraka 6,782 za harakati hizo zimekusanya na kuhifadhiwa. Aidha, ukarabati wa jengo liliokuwa linatumilwa na Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika ya OAU liliopo Dar es Salaam unaendelea kwa ajili ya kuwa kituo cha kitaifa cha maonesho ya historia ya harakati za ukombozi wa Afrika na kuhifadhi historia ya jengo hilo.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania ina maeneo ya urithi wa ukombozi zaidi ya 260. Haya yanajumuisha majengo na maeneo ya wazi, ambapo majengo yaliyo mengi yanahitaji ukarabati wa haraka ili kutopoteza tunu na kumbukumbu hizi muhimu kwa Taifa letu kwa vizazi nya sasa na vijavyo kuhusu historia ya Taifa letu na mchango wake katika kuzikomboa nchi za Afrika.

Hivyo, katika kutatua changamoto hii, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI zimeanza kufanya tathmini ya hali ilivyo na gharama za ukarabati kwa maeneo yote yaliyopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili taarifa ya tathmini hiyo itumike kuwashirikisha wenzetu wa Nchi za Kusini mwa Afrika kuyakarabati ili yatumike kama kivutio cha utalii wa kiukombozi. Hatua hii pamoja na mambo mengine, itaimarisha vivutio nya utalii vilivyomo nchini pamoja na kuhifadhi historia ya Taifa letu.

Halikadhalika, Programu kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii imebainisha maeneo 15 ya kuyatangaza kuwa sehemu ya urithi wa Taifa kwa kuyaingiza katika Gazeti la Serikali ili yalindwe kisheria.

**69. Mheshimiwa Spika**, ikiwa ni hatua ya kutangaza, kuhamasisha na kuelimisha jamii umuhimu wa kujivunia na kuenzi urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika uliopo nchini, Wizara iliendesha kongamano liliolenga kutambua na kuenzi mchango wa Tanzania katika harakati za kulikombua Bara la Afrika. Katika kongamano hilo liliolofanyika tarehe 21 Mei, 2021, jamii ilielimishwa kuhusu namna nchi yetu ilivyojitoa kwa hali na mali kuhakikisha Bara la Afrika linakuwa huru. Elimu hiyo ilitolewa kuititia mada mbalimbali zilizowasilishwa na wabobezi wa masuala ya historia ya nchi yetu, ikiwamo mashuhuda walioshiriki katika harakati hizo.

**70. Mheshimiwa Spika**, kongamano hili la kihistoria lilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo aliweka mkazo wa kuhakikisha urithi na tunu hizi za Afrika zinalindwa na kuhifadhiwa ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu muhimu kwa Taifa na Bara zima.

Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kufanya tathmini ya hali ilivyo katika maeneo ya urithi wa ukombozi yaliyopo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuzishirikisha nchi wanachama wa Umoja wa Afrika hususan nchi za Kusini mwa Afrika kushirikiana na Tanzania kuyaendeleza kwa kuyakarabati maeneo na majengo ya urithi.

Maelekezo mengine yaliyotolewa ni Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuyatambua maeneo yanayokidhi vigezo vyta kuingizwa katika gazeti la serikali na kuwa urithi wa Taifa ili yalindwe kisheria kama llani ya CCM ya mwaka 2020-2025 inavyoelekeza. Pia ilielekezwa Programu hii ianze kutoa elimu mashulenii na kufungua klabu za ujifunzaji wa somo la historia kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Elimu.

**71. *Mheshimiwa Spika*,** kongamano hili, liliolahudhuriwa na washiriki zaidi ya 720 lilijikita katika kuhamasisha umma juu ya ukombozi wa kiuchumi na kifikra ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono falsafa ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya “*Kazi iendelee*”. Kongamano hili liliweka mikakati kabambe ikiwamo: uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kwa kutambua umuhimu wake katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na Makongamano kama haya kuendeshwa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhifadhi historia na kutangaza utalii wa kiukombozi uliopo nchini.

**72. *Mheshimiwa Spika*,** kwa muda mrefu tumekuwa na kasumba ya kutumia vitabu vyta historia ya nchi yetu vilivyoandikwa na wageni wasio Watanzania ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakipotosha historia ya nchi yetu. Katika kutatua kasumba hii, Programu kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu nchini, imefanikiwa kuandaa rasimu ya mihitasari ya somo la historia na vitabu vyake vyta shule ya msingi na sekondari vyenye maudhui na historia halisi ya mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika. Lengo ni kuongeza uzalendo na utaifa kwa vijana ili walinde na kuendeleza historia tukufu ya Tanzania.

### **3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA**

**73. *Mheshimiwa Spika*,** moja ya majukumu makuu ya Wizara ni kusimamia Maendeleo ya Sekta ya Sanaa nchini kuititia Idara ya Maendeleo ya Sanaa na Taasisi zilizo chini yake ambapo masuala ya Filamu yanasmamiwa na Bodii ya Filamu Tanzania kwa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya mwaka 1976; masuala ya hakimiliki na hakishiriki yanasmamiwa na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999. Masuala mengine kama vile muziki, Sanaa za Maonesho na Sanaa za Ufundi, yanasmamiwa na BASATA kwa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya mwaka 1984 ikisomwa kwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019.

**74. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Wasanii na wadau wa Sekta hii wanapata huduma kwa wakati, bila kadhia na kwa gharama nafuu, na ikiwa pia ni utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (*Blueprint*), Wizara imeziweka Taasisi zake zinazowahudumia Wasanii za BASATA, Bodi ya Filamu na COSOTA katika eneo moja katika jengo la UTUMISHI liliopo Kivukoni kama sehemu ya mpango wa muda mfupi wa kuanzisha Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja kwa Wadau wa Sanaa (*One Stop Center*). Wizara inaendelea na mipango ya muda mrefu ya kuwa na kituo hicho Jijini Dodoma, kupitia ujenzi wa Ofisi za kisasa za Mfuko wa Utamaduni na Sanaa katika Jiji hilo. Jengo hilo litawezesha huduma zote za kisekta kama vile vibali, ithibati na usajili kupatikana katika eneo moja.

Aidha, ili kuhakikisha changamoto za kiuratibu kwa Wasanii zinaondolewa, Wizara illanzisha mpango wa kuziunganisha huduma za BASATA na Bodi ya Filamu Tanzania. Hatua hii ilitokana na ukweli kwamba, wakati BASATA imepewa jukumu la kukuza maendeleo na uzalishaji wa kazi za sanaa, Bodi ya Filamu imepewa jukumu hilohilo lakini kwa sehemu ya wasanii ambaao ni wanatasnia ya filamu. Hata hivyo, kwa sasa wapo wasanii wengi ambaao wanafanya kazi za Sanaa ya Filamu na wakati huo huo ni wasanii wa Sanaa za Muziki, mitindo ya mavazi na ulimbwende ambayo iko chini ya BASATA na hivyo Wasanii hao kulazimika kuwa na usajili wa BASATA na Bodi ya Filamu.

**75. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya mwaka 1984 imeondoa picha jongevu na michezo ya kuigiza kati ya mambo inayoyashughulikia, hali hii imejenga dhana kuwa filamu na michezo ya kuigiza sio sehemu ya sanaa ili hali wadau wa filamu na michezo ya kuigiza wanajitambua kama wasanii. Mambo mengine ya kiuratibu yanayowakwaza wasanii ni pamoja na tozo mbalimbali ambazo hutozwa na taasisi zetu na kujenga taswira kuwa Serikali inawatoza tozo zilezile zaidi ya mara moja. Kwa sasa Wizara inaendelea na hatua za kupata maoni ya wadau kuhusu suala hili.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Vilevile, katika hatua za kuikuza Sekta ya Sanaa ili iendelee kutoa ajira kwa makundi mbalimbali ya jamii kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 241 ya llani ya CCM ya mwaka 2020-2025, Wizara inaendelea kupitia Sheria na Kanuni zake ili kuziboresha ziendane na mahitaji na hali ya sasa. Mwezi Mei, 2021 Wizara ilifanya kikao na Wadau kuhusu Kanuni ya 25 ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa iliyowahimiza kuwasilisha kazi zao kwa ajili ya uhakiki kabla ya kurushwa kwenye vyombo vya habari ili kudhibiti masuala ya kimaadili. Baada ya kusikiliza pande zote mbili, yaani Wasanii na BASATA, Wizara iliamua kusitisha utekelezaji wa Kanuni hiyo ili kutoa nafasi kwa wadau kutoa maoni kuhusu namna bora ya kuitekeleza.

Aidha, Wizara ilieelekeza BASATA kusimamia uandaaji wa mwongozo utakaotumiwa na wazalishaji wa kazi za Sanaa na Idara za Muziki za vyombo vya habari ili kuhakikisha masuala ya kimaadili yanazingatiwa katika kazi za Sanaa. Wizara inaendelea kuwahimiza wasanii wetu kuendelea kuzingatia sheria za nchi na kulinda maadili yetu wakati wa kuandaa na kushiriki shughuli za sanaa.

**76. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuleta tija katika Sekta ya Sanaa, Wizara pia ipo katika hatua za awali za kuandaa Sera ya Sanaa ili kuendana na hali halisi ya maendeleo ya kisekta. Wizara inatambua kuwa sanaa sasa imekua, na ipo haja ya kuweka misingi inayoitambua kama Sekta rasmi inayoweza kuwanufaisha wadau kiuchumi kama zilivyo shughuli nyingine rasmi na kwa kuzingatia pia maelekezo ya Ibara ya 241 ya llani ya CCM ya mwaka 2020-2025 yanayoitaka Serikali kuendesha Sekta hii kibiashara. Mazingira ya kisera yaliyopo sasa yanatoa fursa finyu ya kuendesha Sekta ya Sanaa kibiashara, kwani makuzi katika Sekta hiyo sasa yanapishana na muktadha wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 na ni vigumu masuala ya Sanaa hasa za kisasa ambayo yanatoa fursa kubwa ya kiuchumi kwa vijana wetu kuendelea kuwa sehemu ya Sera ya Utamaduni.

**77. *Mheshimiwa Spika*,** ikiwa ni hatua ya kuenzi mchango wa viongozi wa Afrika katika mapambano ya kuzikomboa

nchi za Bara hili, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliendelea kuratibu ujenzi wa Sanamu ya Mwl. Julius Kambarage Nyerere katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Sanamu hiyo itakayojengwa kwa kutumia malighafi ya shaba nyeusi (*bronze*) kwa gharama ya USD 267,992.60 ambayo imetengwa na SADC, inasimamiwa na Meneja Mradi kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**78. *Mheshimiwa Spika*,** tayari Mpango Kazi wa Usimamizi wa Mradi huu umeandaliwa na Kamati za Maandalizi zimeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania ya Kuwaenzi Waasisi wa Kitaifa ya mwaka 2004 na kufanya kazi ya kuchambua picha za Mwl. Nyerere kwa ushirikiano na familia yake ili zitumike wakati wa Ujenzi wa Sanamu inayohusika. Bajeti ya shughuli hii imehamishiwa mwaka wa fedha 2021/2022 baada ya Kampuni iliyokuwa imeshinda zabuni kujiondoa kwa kushindwa kutimiza masharti ya SADC. Kwa sasa, SADC inaendelea na zoezi la kupata Kampuni itakayohusika katika ujenzi wa Sanamu hiyo na matarajio ni Sanamu inayohusika kuzinduliwa katika maadhisho ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa Mwalimu Nyerere Aprili, 2022.

**79. *Mheshimiwa Spika*,** tayari zabuni hii imetangazwa na SADC kupitia tovuti yake [www.sadc.int](http://www.sadc.int) kwa nchi wanachama ili Msanii au kampuni yenye sifa iweze kuomba. Naomba nitumie nafasi hii kuwahamasisha Wasanii wote wenye sifa nchini kuomba zabuni hii mapema kwani, "Chelewachelewa utakuta mwana si wako". Wizara tayari imewasiliana na wadau wa Sanaa hapa nchini kupitia BASATA na Shirikisho la Sanaa za Ufundı (TAFCA) ili waweze kuchukua hatua za haraka kupitia taasisi zao ambazo tayari zimesajiliwa kisheria kutekeleza miradi kama hii.

**80. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuenzi mchango wa wasanii mashuhuri katika taifa letu na kutunza kazi zao kwa matumizi ya kizazi cha sasa na kijacho, Serikali inaandaa kanzidata ya Wasanii hao itakayowezesha kazi zao kuhifadhiwa katika mfumo wa kidijiti. Tayari Andiko la kanzidata hiyo

limeandaliwa na kazi zitakazofanyika ni pamoja na kutafiti, kutambua, kuhifadhi na kutangaza wasanii na kazi zao za Sanaa zilizowahi kuvuma na kuwa na mguso pamoja na mchango chanya kwa jamii ya Kitanzania kwa wasanii wote walio hai na wale waliotangulia mbele ya haki. Hatua hii, sio tu itatambua mchango wa walengwa katika kukua kwa Sekta ya Sanaa hapa nchini, bali pia itarahisisha kazi ya kusimamia mapato yatokanayo na matumizi ya kazi zao kwa manufaa ya wasanii wenyewe, wategemezi wao au hata warithi wao.

Vilevile, kwa kuwa kazi za nguli hao wa Sanaa zimesheheni ubora, Wasanii wa sasa nao wataweza kupata mahala pa kujifunza namna ya kuzalisha kazi bora zaidi za Sanaa. Katika kazi hizi, na hasa za muziki, filamu na michezo ya kuigiza yamo mafunzo mbalimbali ambayo yataweza kutukumbusha tulikotoka pamoja na kutumika kuhamasisha uzalendo kwenye jamii, na kuitangaza na kuipa heshima nchi yetu kitaifa na kimataifa.

**81. *Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendelea na jitihada za kuibua vipaji na kutangaza kazi za wasanii ambapo katika kipindi hiki liliifanyika Tamasha la Sanaa la Serengeti (*Serengeti Festival*) katika Uwanja wa Uhuru tarehe 26 Desemba 2020; katika viwanja vya Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) tarehe 27 Desemba, 2020 na katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma tarehe 6 Februari, 2021. Tamasha hilo lilihusisha shughuli mbalimbali za Sanaa ikiwemo michezo ya jukwaani, michezo ya jadi, ngoma za asili na muziki wa kizazi kipyaa. Kati ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika tamasha hili lililusisha wasanii wakubwa, wa kati na wachanga zaidi ya 150 ni pamoja na ushiriki mkubwa wa wananchi hasa katika Mkoa wa Dodoma waliofikia zaidi ya 10,000 na kuwarudisha katika taswira ya muziki baadhi ya Wasanii wakongwe waliokuwa wameanza kukata tamaa.

Lengo la Serikali ni kuendesha matamasha kama haya kila mwaka kwa kushirikiana na wadau na kupanua wigo wa ushiriki katika nyanja za kitamaduni, sanaa na ubunifu. Aidha,

Wizara iliratibu ushiriki wa vikundi vyaa sanaa na burudani kutoka Tanzania Bara na Zanzibar katika matukio mbalimbali ya kitaifa, ikiwemo ya uapisho wa viongozi wa kitaifa.

**82. *Mheshimiwa Spika*,** vikundi hivyo ni pamoja na Kikundi cha Taifa cha Utamaduni cha Zanzibar; Bendi ya TOT – DSM; Kikundi cha Ngoma cha JKT Makutopora Dodoma; Kwaya ya Chuo cha Utumishi wa Umma Dar es Salaam; JW Mlalakuwa; JKT – Barabara ya Kilwa; na Polisi – Barabara ya Kilwa. Vilevile, Wasanii wakubwa kama Diamond, Harmonize, Ali Kiba na Nandy walishiriki na Wasanii wengine wa Muziki wa Kizazi Kipy 27 walitunga na kuimba wimbo Maalumu wa pamoja unaoitwa *MAGUFULI MITANO TENA*. Vikundi hivyo vilifanyiwa tathmini ya mahitaji yao, kukaguliwa maudhui ya nyimbo zao, kukagua uchezaji wa ngoma i n a y o husika kwa kufuata taratibu na miongozo pasi na kukiuka maadili. Pia, Wizara iliratibu shughuli za Sanaa za maombolezo kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli mwezi Machi, 2021 ambapo Wasanii 20 walitunga na kuimba wimbo wa maombolezo wenye jina la *HAYASAHAULIKI* na Wasanii wengine kutunga na kuimba nyimbo binafsi.

### **3.2.3.1 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**

**83. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu ya BASATA ni pamoja na kuendeleza kazi za Sanaa, kutoa ushauri na utaalamu wa kiufundi kwa wasanii na wadau wa sanaa, kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu maendeleo ya sanaa nchini na kuratibu na kusimamia maonesho, mashindano, matamasha, makongamano na warsha mbalimbali zinazohusu kazi za Sanaa.

**84. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuimarisha na kurahisisha usajili wa wasanii ikiwemo wachongaji, wachoraji, wanatasnia ya filamu na muziki, michezo ya kuigiza na ulimbwende, BASATA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) linaandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili na usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa. Mfumo huu ambaao unatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2021 utatumika kwa

shughuli za usajili na utoaji wa vibali kwa njia ya kielekitroniki kwa wadau wa sanaa wanaokadiriwa kufikia zaidi ya milioni 4 nchini na hivyo kuimarisha mapato yatokanayo na usajili na kuimarisha urasimishaji wa Sekta ya Sanaa. Kwa kuwepo kwa mfumo huu, mdau wa sanaa hatahitajika kufika katika Ofisi za BASATA ili kujisajili au kupata kibali cha kufanya shughuli ya sanaa, hivyo kuwapunguzia usumbu na gharama za usajili wadau hao.

**85. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara, kupitia BASATA ipo katika maandalizi ya utoaji wa tuzo za Muziki nchini. Tuzo hizo zinatarajiwu kutolewa ndani ya mwaka wa fedha wa 2021/2022. Aidha, Baraza limefanya mukutano na wasanii pamoja na wadau wa sanaa kwa lengo la kupata changamoto zinazoikabili Sekta ya Sanaa na kuweka Mikakati ya pamoja ya kuendeleza Sekta hiyo. Mikakati hiyo inajumuisha kuendesha programu za pamoja kati ya Serikali na wadau wa Sanaa pamoja na kuimarisha mifumo rasmi ya mawasiliano kati ya Serikali, wasanii na wadau wa sekta ya Sanaa nchini. Mukutano huo ambaeo ulihudhuriwa na wadau wa sanaa 102, ulihuisha BASATA na watendaji Wakuu wa taasisi mbalimbali zikiwemo Bodii ya Filamu Tanzania, TaSUBA, BAKITA, Idara ya Sanaa Bunifu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau wengine.

**86. *Mheshimiwa Spika*,** kazi ya kusajili wasanii nchini iliendelea ikiwa ni hatua za kurasimisha kazi zao ambapo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi kufikia mwezi Mei, 2021 jumla ya wasanii na wadau wa Sanaa 890 walisajiliwa. Wadau hawa wanajumuisha Wasanii binafsi, Vikundi, Kampuni na Taasisi zinazojishughulisha na shughuli za Sanaa, Kumbi za starehe na burudani na Studio za muziki. Zoezi hili limefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Iringa, Njombe, Manyara, Shinyanga, Dodoma na Morogoro. Idadi hii ya usajili bado ni ndogo ikilinganishwa na wasanii na wadau wa sanaa waliopo nchini kutokana na kutokuwepo kwa mfumo rahisi wa kuwafikia wasanii na wadau wengi katika maeneo yote nchini. Hivyo, mfumo wa usajili wa wasanii na utoaji wa vibali unaoandaliwa utakuwa mwarobaini katika kupatia ufumbuzi changamoto hii.

**87. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wasanii na wadau wa sanaa wanaandaa kazi za sanaa zilizo bora na zinazomudu ushindani kitaifa na kimataifa, Baraza limetoea ushauri kwa wasanii na wadau wa sanaa 1,892 kutoka katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, ili kuwafikia wasanii na wadau wa sanaa wengi zaidi, Serikali imeweka mkakati wa kutoa taarifa zaidi za upatikanaji wa huduma hii ambayo hutolewa bure na BASATA. Ushauri uliotolewa ulihusu masuala ya maadili, masoko ya kazi za Sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji fedha kwa vikundi na taasisi pamoja na masuala ya usajili na vibali.

Aidha, Baraza liliandaa midahalo mitatu (3) ya Jukwaa la Sanaa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Njombe iliyohusisha jumla ya wasanii na wadau wa Sanaa 316. Mkakati wa BASATA ni kuongeza idadi ya washiriki katika midahalo hii, kwa kuitangaza programu ya Jukwaa la Sanaa pamoja na kuyafika maeneo mengi zaidi nchini katika kuendesha midahalo ya jukwaa hilo. Katika majukwa hayo, wasanii na wadau hao walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Sanaa, ikiwa ni pamoja na fursa na changamoto zinazowakabili katika kufanya shughuli za Sanaa na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi.

**88. Mheshimiwa Spika**, Baraza lilitoa pia elimu na ushauri kwa wasanii na wadau wa sanaa kupitia vyombo mbalimbali vyahabari kuhusu masuala yanayohusu sanaa. Vyombo hivyo ni pamoja na Channel Ten, Sunrise Radio (Arusha), Dodoma FM (Dodoma), Redio 5 (Arusha), Boma FM (Kilimanjaro), Highland FM (Mbeya), TBC FM, Star Tv na Clouds FM. Elimu hiyo ililenga kuhimiza wasanii na wadau wa sanaa kuzingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania katika uandaaji na usimamiaji wa kazi za sanaa pamoja na kuhamasisha wasanii kuongeza ubunifu katika kazi za sanaa ili kuimarisha ubora na ushindani wa kazi hizo ndani na nje ya nchi.

**89. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendelea kutoa vibali kwa Wasanii wanaoingia na wanaotoka nje ya nchi kwa ajili ya kuendesha shughuli za sanaa. Katika kipindi cha Julai, 2020

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hadi Mei, 2021 Baraza limetoa jumla ya vibali 50 kwa wasanii wa Tanzania kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za sanaa. Katika kurahisisha utoaji wa vibali hivi, Serikali inaendelea na maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali ambao utapunguza ghamama na urasimu uliopo sasa. Vilevile, Baraza limetoa vibali 16 vya kuingiza wasanii kutoka nje ya Tanzania kufanya shughuli za sanaa nchini, baadhi yao wakiwa ni Koffi Olomide (Congo DRC), Eric Omondi (Kenya) na Fire Boy (Nigeria).

Hali kadhalika, Baraza liliendelea kuratibu na kutoa ushauri juu ya uendeshaji wa matukio ya sanaa yanayofanywa na wadau ili kuhakikisha kazi za sanaa zinazingatia miongozo na taratibu zilizopo ili kuimarisha ubora wa kazi za sanaa. Baadhi ya matukio hayo ni pamoja na Bongo Star Search 2020, Miss Utalii 2020, Ongala Music Festival, The 2020 Time 2Dance, Miss Tanzania na Stand Up Comedy.

Fauka ya hayo, BASATA lipo katika hatua ya kukusanya na kupokea maoni ili kukamilisha zoezi la kuhuisha kanuni Na.43 za mwaka 2018 ili ziweze kuleta tija na kukidhi mahitaji ya wadau wa sanaa. Katika kuhamasisha utekelezaji wa marekebisho ya Kanuni hizi, kilifanyika kikao kati ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na viongozi wa wasanii na kujadili namna bora ya kufanikisha urekebishwaji wa kanuni tajwa.


### **3.2.3.2 BODI YA FILAMU TANZANIA**

**90. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu ya Bodi ya Filamu ni pamoja na kusimamia utayarishaji wa filamu; kuzihakiki na kuzipanga katika madaraja; kusimamia usambazaji na uoneshaji wa kazi hizo na kutoa ithibati kwa miundombinu, kampuni na wadau wa filamu na michezo ya kuigiza.

**91. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Mei, 2021 Bodi ilitoa jumla ya vibali 108 vya kutayarisha filamu ambapo vibali 46 ni kwa watayarishaji wa ndani na vibali 62 kwa watayarishaji kutoka nje ya nchi. Aidha, Bodi ilihakiki, kupanga katika madaraja na kutoa vibali kwa jumla

ya filamu 1,456 ambapo filamu 1,388 ni za ndani na 68 kutoka nje ya nchi. Madaraja hayo yalihusu umri wa hadhira inayopaswa kutazama filamu inayohusika na katika filamu zote zilizohakikiwa, hakukuwa na filamu iliyokataliwa kibali cha maonesho kwa umma. *Kiambatisho Na.2* ni mwenendo wa vibali vya utayarishaji wa filamu na picha jongevu vilivyotolewa na *Kiambatisho Na. 3* ni mwenendo wa filamu za ndani na nje ya nchi zilizohakikiwa na kupewa vibali.

#### **Kielelezo Na. 4: Filamu za Ndani na Nje ya Nchi Zilizohakikiwa na Kupewa Vibali, Mwaka 2015/16 - 2020/21**



**92. Mheshimiwa Spika,** Bodii iliendelea kutoa leseni za ithibati za uendeshaji wa shughuli na biashara za filamu ambapo jumla ya leseni 50 zilitolewa na vitambulisho 121 vilitolewa kwa wadau wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza katika mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, Bodii ilibadilisha aina ya vitambulisho vinavyotolewa kwa wadau wa filamu ambapo kwa sasa inatoa vitambulisho vya kisasa aina ya *Smart Card*. Vitambulisho hivyo siyo tu kwamba vina hadhi na uwezo wa kudumu kwa muda mrefu zaidi ya vile vya awali (ambavyo vilikuwa katika mfumo wa karatasi na hivyo kuharibika kirahisi), bali pia vinaendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia kimatumizi kwa kuruhusu taarifa za wanatasnia kuingizwa kwenye kanzidata ya Serikali na kuwaunganisha katika mifumo mingine ya huduma kama vile NIDA, TRA, Uhamiaji na taasisi za fedha. Hatua hii itaimarisha kuwarasimisha na kuwatambua wadau wa filamu kwa kuzingatia usoefu, ubobevu na taaluma zao katika tasnia.

**93. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhakikisha uzingatiwaji wa sheria na taratibu za uendeshaji wa shughuli za filamu na vilevile kulinda kazi za wanatasnia, Bodi iliendesha jumla ya operesheni 35 katika maeneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam na Arusha katika hatua ya awali ambapo mikoa hiyo ilionekana kuwa na uzalishaji mkubwa zaidi wa filamu na kiini cha changamoto ya ukiukwaji huo wa sheria. Operesheni hizi ni endelevu, hivyo mpango uliopo ni kuhakikisha maeneo yote nchini yanafikiwa.

Kupitia operesheni hizo, wadau na wamiliki wa kazi za filamu waliobainika kukiuka taratibu za kisheria waliwajibishwa kwa mujibu wa Sheria na kuelekezwa kuwasilisha kazi zao Bodи ya Filamu kwa ajili ya kupatiwa vibali na uhakiki. Vilevile, elimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza na Kanuni zake kwenye uandaaji na usambazaji wa filamu pamoja na uendeshaji wa shughuli hizo imeendelea kutolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano na wadau wa filamu na kipitia vyombo vya habari.

**94. *Mheshimiwa Spika*,** Bodи ya Filamu iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwajengea uwezo wanatasnia ya filamu ili kuwawezesha kuzalisha kazi bora zinazomudu ushindani kitaifa na kimataifa. Hatua hizo ni pamoja na:

i. Kuratibu na kutoa miongozo ya uendeshaji wa matamasha ikiwemo kuwizesha kufanyika kwa tuzo za wanafunzi wa Vyuo vikuu (UNI AWARDS), ambapo kilele cha shughuli hii kilikuwa tarehe 18 Desemba, 2020 katika ukumbi wa mikutano wa Mwl.J. K. Nyerere, Jijini Dar es Salaam. Tuzo hizo zililenga kutambua na kuibua vipaji vya Sanaa kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini;

ii. Kuanzisha mchakato wa kuziwesha filamu za kitanzania kuingia katika tuzo za kitaaluma maarufu kama *tuzo za Oscars* ambapo tayari majina yatakayounda kamati ya kitaifa ya tuzo hizo yameshawasilishwa kwa waandaaji nchini Marekani ikiwa ni mahitaji ya awali kwa ajili ya maandalizi ya tuzo hizo.

iii. Kuendesha mafunzo kwa wanatasnia ya filamu 440 kwa njia ya vitendo (*taylor-made training*) na kipitia programu

ya uchambuzi (*film screening*) katika mikoa ya Dar es Salaam na Geita ili kuongeza weledi katika filamu zinazozalishwa hapa nchini. Mafunzo haya yalishirikisha wataalamu kutoka Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Kampuni ya Wanene Entertainment na Kampuni ya Like Brothers ya nchini Uingereza. Mafunzo haya yalinufaisha wanatasnia 110 katika maeneo ya uandishi wa miswada, uongozaji wa filamu, uigizaji, upigaji picha, sauti katika filamu na uhariri na kupitia mafunzo hayo filamu fupi iitwayo PAMELA iliandaliwa na wanafunzi hao. Mafunzo haya yataendelea kutolewa katika mwaka 2021/22 ili kuifkia mikoa mingi zaidi.

Kwa upande wa pogamu ya kutazama na kuchambua filamu (*film screening*) mafunzo yalishirikisha wataalamu na waandaaji wa filamu inayohusika. Kupitia programu hii, wadau 330 walinufalka ambapo filamu 33 ziklwemo tamthiliya zilizooneshwa na DSTV na Azam Tv kama vile Huba, Nyavi, Slay Queen, Karma pamoja na filamu nyingine zilichambuliwa. Programu hii imekuwa na mtazamo chanya na mwitiko kutoka kwa wadau wa filamu na imeongeza weledi na ujuzi wa watayarishaji wa filamu ikiwemo kupunguza upungufu wa kiufundi uliokuwa ukijitokeza katika utayarishaji wa filamu; na

iv. Kuratibu na kuwezesha kufanyika kwa mikutano na vikao kazi vya wadau wa filamu kupitia Shirikisho la Filamu Tanzania na Vyama vinavyounda Shirikisho hilo. Kupitia vikao hivi, Bodi inakuwa karibu zaidi na wadau wake, kufahamu changamoto zinazowakabili na kuweka mikakati ya pamoja na kuzipatia ufumbuzi kwa maendeleo ya tasnia ya filamu. Aidha, Bodi iliratibu na kuwezesha kufanyika kwa chaguzi za viongozi wa Shirikisho hilo pamoja na vyama tisa (9) vinavyounda shirikisho hilo. Lengo na hatua hizi ni kuliongezea nguvu Shirikisho na vyama vyake ili viweze kuhudumia wadau wake kiufanisi zaidi.

**95. *Mheshimiwa Spika***, jithada za kufufua utamaduni wa Watanzania kuangalia filamu katika kumbi za sinema ziliendelea kutekelezwa ambapo iliundwa Kamati

Ilioanda vigezo vya kutumika kupata filamu bora zitakaooneshwa kwenye kumbi za sinema. Kupitia Kamati hiyo iliyozindulwa tarehe 4 Agosti 2020, filamu mbili (NYARA na BINTI) zilikidhi vigezo vilivywewekwa na kupidishwa kuoneshwa katika kumbi za sinema zilizopo Jijini Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Mwanza, Dodoma na Zanzibar. Mathalani, filamu ya NYARA ilioneshwa katika kumbi hizo kwa muda wa wiki moja, kuanzia tarehe 29 Desemba 2020 ambapo jumla ya tiketi 471 ziliuzwa.

Vilevile, kutokana na kukidhi viwango vya kuoneshwa katika Kumbi za Sinema hapa nchini, filamu hiyo iliwavutia wapenzi wa filamu wa nchi za jirani na kuoneshwa pia katika kumbi za Sinema nchini Kenya na Uganda kwa muda wa wiki mbili. Kwa vigezo hivyo hivyo, filamu ya BINTI ilipata fursa ya kuoneshwa nchini Marekani kwenye matamasha ya *Pan-African Film Festival* na *American Film Institute* tarehe 28 Februari hadi tarehe 14 Machi, 2021.

**96. Mheshimiwa Spika**, ili kuwatambua wanatasnia ya filamu nchini, Bodi ya Filamu kwa kushirikiana na BASATA na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ilianza kuanda Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa watendaji na wadau katika Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini. Lengo la mfumo huu ni kuwatambua kwa kuwasajili kidijiti wadau wote wa filamu nchini na kuwapatia vitambulisho vya kisasa (*Smart Cards*) vitakavyokuwa vinasoma katika mfumo huo ili kurahisisha utendaji na kuwashudumia kwa ufanisi na tija mahali popote mdau wa filamu alipo bila kulazimika kufika ofisi za Bodi kwa ajili ya huduma hizo. Uundwaji wa mfumo huu upo katika hatua za mwisho na utafanyiwa majaribio mwezi Juni, 2021.

**97. Mheshimiwa Spika**, jitihada za uboreshwaji wa mazingira ya uwekezaji hasa kwa sekta binafsi kwenye masoko na usambazaji wa kazi za filamu zimeendelea. Katika kipindi hiki, kumekuwa na ongezeko la kampuni za uzalishaji na usambazaji wa filamu vikiwemo vituo vya televisheni vinavyonunua na kuonyesha (kusambaza) filamu za kitanzania (Bongo Movie) kwa saa ishirini na nne kama vile

DSTV, Azam Media, Star Swahili, Zuku TV, pamoja na televisheni mtandao kama vile, Swahiliflix, MamboTV, Inalipa App, Airtel TV na Lipia App.

Vituo vingine vya Televisheni vinavyorusha na kuonesha filamu za Kitanzania na zinazotumia lugha adhimu ya Kiswahili ni EATV, Clouds Plus na ITV. Aidha, Kampuni ya Azam Media, DSTV na Startimes zimeongeza uwekezaji wa mitaji kwa lengo la kukuza Sekta ya Filamu nchini kwa kutoa ufadhili wa uandaaji wa kazi za filamu. Uwekezaji huo umechochea uzalishaji wa filamu bora na hivyo kupelekea kuongezeka kwa idadi ya ajira na mapato yatokanayo na kazi za filamu pamoja na kuchochea maendeleo ya sekta nyingine mtambuka kama vile sekta ya Usafirishaji na Uchukuzi, Utalii, Hoteli na Huduma.

**98. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuhakikisha wasanii wanapata haki zao, Bodi ya Filamu imeratibu vikao vya Kamati ya Haki za wasanii ambayo kwa kipindi hiki pekee Kamati hiyo imepokea na kushughulikia malalamiko 19, ambapo kiasi cha Sh. 38,218,000 zimeshafidiwa kwa walalamikaji wakiwemo wasanii wa filamu, muziki na sanaa za ufundi. Baadhi ya wasanii walionufaika ni pamoja na Young Dee (David Genz Mboli), Duma (Daudi Tairo), Mary Patrick, Getrude Marekani, John Samweli Isike, Ibrahim Mzonge, Edwin Musiba, Asha Ismail na Husein Juma Nguya.

**99. Mheshimiwa Spika**, jitihada za kuongeza wigo wa uhusiano wa kikanda na kimataifa kwenye tasnia ya filamu zimefanyika. Katika kipindi hiki Bodi ya Filamu imeanzisha uhusiano na Nuella TV kutoka nchini Uhlanzi ambapo hadi sasa filamu nne za Kitanzania zimeshatumwa na filamu moja tayari imeshaanza kuoneshwa kupitia kituo hicho.

### **3.2.3.3 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)**

**100. Mheshimiwa Spika**, majukumu ya COSOTA ni pamoja na kusimamia masuala ya Hakimiliki katika kazi za sanaa na ubunifu ikiwemo kukusanya na kugawa mirabaha kwa wadau wa kazi hizo. Vilevile, taasisi hii ina jukumu la kutunza

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

rejista za kazi, usanii na vyama vya watumzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa na watangazaji na wachapishaji.

**101. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Mei, 2021 COSOTA imesajili kazi za sanaa na ubunifu 2,132 zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999. Aidha, katika kipindi hicho COSOTA imesajili wasanii na wabunifu 1,668 na imetoa vyeti vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki 1,907. Kufuatia usajili huu, wasanii na wabunifu wanapata manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutambuliwa na umiliki wa kazi zao ndani na nje ya nchi, kupata elimu ya hakimiliki na mikataba, uthibitisho wa kazi zao, kazi kurushwa katika vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kulipwa mirabaha.

### ***Jedwali Na.1: Usajili wa Wanachama na Kazi za Sanaa/ Ubunifu katika Kipindi cha Julai, 2020 hadi Mei, 2021***

<b>Na.</b>	<b>Fani za Sanaa/Ubunifu</b>	<b>Wanachama Waliosajiliwa</b>	<b>Kazi Zilizosajiliwa</b>
1.	Maandishi	824	493
2.	Filamu	460	1,282
3.	Muziki	384	357
<b>Jumla</b>		<b>1,668</b>	<b>2,132</b>

**102. Mheshimiwa Spika**, kuitia ukusanyaji wa mirabaha na usajili wa kazi za hakimiliki, COSOTA ilitoa leseni 300 kwa watumiaji wa kazi zenye hakimiliki na kukusanya jumla ya Shilingi 196,642,009. COSOTA iliendelea na utatuzi wa migogoro ya Hakimiliki katika kazi za sanaa na ubunifu ambapo katika kipindi hiki migogoro 27 ilipokelewa na kufanyiwa kazi, ambapo 18 imemalizika na 9 inaendelea kufanyiwa kazi.

**103. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, Kanuni ya Ufifilishaji wa Makosa ya Hakimiliki (*compounding of offences*) za mwaka 2020 zilikamilishwa na kuanza kutumika. Kanuni hizi

pamoja na mambo mengine, zinawezesha kutoza faini bila haja ya kwenda mahakamani punde mtuhumiwa anapokiri kosa la kukiuka Sheria ya Hakimilili na hivyo kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani zinazohusiana na ukiukwaji wa hakimilili. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na wadau wengine, zoezi la kurekebisha Kanuni za Maonesho kwa Umma, Utangazaji na Mawasiliano kwa Umma lilitifanyika na Kanuni mpya zinatarajiwu kuanza Julai, 2021. Kukamilika kwa Kanuni hizi kutaimarisha mapato ya wasanii kwa kuwezesha makusanyo kukusanywa katika maeneo mbalimbali ikiwemo baa, hoteli, kumbi za disko, televisheni, redio, mitandao ya kijamii na simu za mikononi.

**104. *Mheshimiwa Spika*,** ikiwa ni hatua ya kuongeza wigo na makusanyo ya mirabaha, COSOTA imeunganisha Kanuni iliyokuwa inaandaliwa ya Kazi za Mikono Zinazouzwa kwa Mara ya Pili (*Resale Right*) na Kanuni ya Maonesho kwa Umma, Utangazaji na Mawasiliano kwa Umma. Kwa kufanya hivi, mbunifu wa kazi za mikono atapata nafasi ya kupata mrabaha iwapo kazi yake itauzwa kwa mara ya pili katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Aidha, COSOTA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ipo katika hatua za mwisho za kuweka mfumo wa kisheria utakaowezesha kupatikana kwa tozo ya *Blank Tape Remuneration/Levy* kutokana na vifaa vinavyobeba, kuhifadhi na kuzalisha kazi za ubunifu ambapo sehemu ya mapato yatakayopatikana yatagawiwa kwa wasanii na katika Mfuko wa Maendeleo wa Utamaduni na Sanaa wenye lengo la kuwajengea uwezo wadau hao kimitaji na mafunzo.

**105. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na wadau na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilianza zoezi la kuimarisha mifumo ya kufuatilia matumizi ya kazi za sanaa hususani muziki na filamu katika vyombo vya habari. Aidha, kwa kushirikiana na TTCL unaandaliwa mfumo wa kielektroniki (*online platform*) kwa ajili ya kusambaza kazi za wasanii. Kukamilika kwa mifumo hii kutaimarisha makusanyo ya mirabaha kwa wasanii na hivyo kuwawezesha kunufaika zaidi na kazi zao na vilevile kuimarisha mchango wa Sekta ya

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Sanaa katika Pato la Taifa na kuibua ajira hususani kwa vijana.

**106. Mheshimiwa Spika**, ikiwa ni hatua ya kuhakikisha wadau wanazingatia matakwa ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 na vilevile kuwalinda wasanii, waandishi na wabunifu wetu dhidi ya vitendo vyta kuhujumiwa katika kazi zao, COSOTA kwa kushirikiana na MultiChoice Tanzania iliendesha semina kuhusu hakimiliki na hakishiriki kwa wadau 273 wa mikoa ya Mwanza (35), Arusha (115), Dodoma (89) na Mbeya (34).

**107. Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba 2020 ilitolewa elimu ya hakimiliki kwa wabunifu wa Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yallyoandaliwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ambapo wabunifu mbalimbali walihudhuria. Vilevile, mwezi Novemba, 2020 na Aprili 2021 yalitolewa mafunzo ya hakimiliki kwa wakufunzi na watafiti wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambapo wakuu wa Idara na Vitengo walihudhuria. COSOTA, pia imetoa elimu ya masuala ya hakimiliki kuititia vyombo mbalimbali vyta habari ikiwa ni pamoja na Uhai Redio, Clouds FM, Clouds Tv, Channel Ten, Magic FM. Times FM, TBC<sub>FM</sub>, TBC<sub>1</sub>, Midundo Online Radio na Boresha Online Radio.

**108. Mheshimiwa Spika**, ili kudhibiti uharamia na matumizi ya kazi za wasanii na wabunifu yasiyozingatia Sheria ya Hakimiliki, kulifanyika operesheni kwa wadau wa televisheni za kebo (cable tv) katika Mikoa ya Manyara, Ruvuma, Songwe, Kagera, Mwanza, Kilimanjaro, Lindi, Arusha na Mtwara. Katika operesheni hizo, hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa elimu kwa watuhumiwa waliobainika kukiuka sheria ya hakimiliki, kutozwa faini ya jumla ya Sh.11,000,000 na kuharibiwa kwa vifaa ilivyotumika kurushia matangazo bila ya kibali na kesi kupelekwa mahakamani.

### 3.2.3.4 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**109. Mheshimiwa Spika**, TaSUBa ni Taasisi inayotoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusu Sanaa na utamaduni. Mafunzo yanayotolewa na Taasisi hii ni Astashahada ya Sanaa na Maonesho na Ufundı (*Certificate in Performing and Visual Arts*); Astashahada ya Teknolojia na Muziki na Sauti (*Certificate in Music and Sound Design*) na Astashahada ya Picha Jongevu na Uzalishaji wa Vipindi nya Televisheni (*Certificate in Film and TV Production*). Kwa upande wa Stashahada Taasisi inatoa Stashahada ya Sanaa na Maonesho na Ufundı (*Diploma in Performing and Visual Arts*), Stashahada ya Teknolojia na Muziki na Sauti (*Diploma in Music and Sound Design*) na Stashahada ya Picha Jongevu na Uzalishaji wa Vipindi nya Televisheni (*Diploma in Film and Television Production*).

**110. Mheshimiwa Spika**, TaSUBa iliendelea kutoa mafunzo ya utamaduni na sanaa ambapo wanachuo 397 walisajiliwa. Taasisi pia iliendesha kongamano/mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wake kama ifuatavyo:

- a) Mafunzo kuhusu Utunzi Mwafaka na Uandishi wa Muziki kwa kutumia teknolojia ya kompyuta yaliyofanyika kwa wadau kutoka Madhehebu ya Wasabato tarehe 5 hadi 31 Oktoba, 2020;
- b) Mafunzo ya muziki kwa njia ya mtandao (*music online*) yaliyoendeshwa kwa Wanachuo 8 kutoka TasUBa ambayo yaliwezeshwa na Taasisi ya Kijerumani ya *Music for Better Life*, Chuo Kikuu cha Munich cha Ujerumani na *Goethe Institute* (Tanzania). Mafunzo hayo yalifanyika mwezi Novemba-Desemba, 2020; na
- c) Kongamano la Nne la Mwaka kuhusu Sanaa kwa Mabadiliko ya Jamii lilihofanyika kwa kushirikiana na Taasisi ya Walimu wa Sanaa (*Teachers Arts Institute*) ya Marekani ambapo washiriki 20 walitoka nchi za Marekani na Uganda. Kongamano hilo ambalo lilihofanyika tarehe 13-15 Novemba, 2020 lilihusisha washiriki 80 kutoka Jumuiya ya TaSUBa.

*Kiambatisho Na. 4* ni idadi ya wanafunzi waliohitimu Astashahada na Stashahada TaSUBa katika vipindi mbalimbali.

**111. *Mheshimiwa Spika*,** TaSUBa kwa kushirikiana na wadau, huendesha Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo kila mwaka. Tamasha hilo linalenga kupima kiwango cha maendeleo ya usanii na utamaduni; kuibua, kuendeleza na kutangaza vipaji na kazi za wasanii na kuhamisha au kurithisha utamaduni na thamani yake kwa vizazi vyaa sasa na vijavyo. Tamasha la 39 la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo lilifanyika tarehe 27 Desemba, 2020 na kuhudhuriwa na vikundi 47 vyaa sanaa za jukwaani na 16 vyaa sanaa za ufundi kutoka ndani ya nchi. Aidha, Tamasha hilo lilihudhuriwa na watazamaji zaidi ya 8,000.

### **3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO**

**112. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu ya Sekta hii ni pamoja na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu na wataalamu wa michezo kwa kushirikiana na wadau, kuhamasisha umma kushiriki katika michezo na kuhakikisha Timu za Taifa na wachezaji wanafanya vyema katika mashindano ya Kimataifa kwa kushirikiana na wadau.

**113. *Mheshimiwa Spika*,** ikiwa ni hatua ya kuimarisha michezo nchini, Wizara ilikamilisha rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Michezo. Mkakati huo umeweka malengo mbalimbali ya kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Michezo ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya michezo, kuimarisha vyanzo vyaa mapato ya kugharamia michezo, kuwa na wataalamu wa michezo wanaokidhi mahitaji kwa michezo mbalimbali na kuimarisha michezo shulenii.

Malengo mengine ni kuimarisha uteuzi wa wachezaji na maandalizi ya timu za Taifa, kuwa na utaratibu bora wa kuibua na kuendeleza vipaji vyaa michezo, kuimarisha ushiriki

wa umma katika kufanya mazoezi pamoja na kuimarisha utawala bora michezoni. Mkakati huo ambao unabainisha pia majukumu ya wadau mbalimbali katika kuendeleza michezo nchini, unatarajiwa kuzinduliwa mwezi Julai, 2021.

**114. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Mashirikisho/Vyama ya Michezo iliendelea kuratibu ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa na kupata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:

- a) Katika Mashindano ya COSAFA ya Wanawake wenye Umri Chini ya Miaka 17 yaliyofanyika nchini Afrika Kusini mwezi Novemba, 2020, Timu ya Tanzania (*Tanzanite*) ilitwaa Kombe la COSAFA baada ya kuzichabanga Timu kutoka Comoro (mabao 5-1), Afrika Kusini (mabao 6-1), Zimbabwe (mabao 10-1) na Zambia (mabao 2-1);
- b) Timu ya Taifa (*Taifa Stars*) ilishiriki katika fainali za mashindano ya wachezaji wanaocheza ligi za ndani ya nchi (CHAN) yaliyofanyika mwezi Januari, 2021 nchini Cameroon. Timu hiyo ilishiriki katika fainali hizo kwa mara ya mwisho mwaka 2009;
- c) Wanariadha wawili Ignasi Mtweve na Sauda Saidi kwa watu wenye ulemavu walishiriki katika mashindano ya kufuzu michezo ya Paralimpiki nchini Dubai mwezi Februari, 2021 na Tunisia mwezi Machi, 2021. Kupitia mashindano hayo, Ignasi Mtweve amefuzu kushiriki mashindano ya michezo ya Olimpiki yatakayofanyika Tokyo, Japan kwa michezo wa kurusha Kisahani na Sauda Saidi amefuzu kushiriki michezo ya Paralimpiki kwa michezo wa kurusha Tufe. Hivyo, kufanya idadi ya wachezaji waliofuzu kushiriki michezo ya Olimpiki kufikia watano (5) ambao ni Felix Simbu, Failuna Mataga, Gabriel Geay, Iganas Mtweve na Sauda Saidi;
- d) Timu ya Taifa kwa Wachezaji Wenye Umri Chini ya Miaka 20 kwa mara ya kwanza, ilishiriki katika fainali za Kombe la Afrika (AFCON) zilizofanyika nchini Mauratania mwezi Februari, 2021;

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- e) Timu ya Taifa ya Mchezo wa Tennis ya Walemavu ilishiriki katika michezo ya kufuzu mashindano ya Dunia nchini Msumbiji mwezi Mei, 2021;
- f) Wanariadha wawili Gabriel Geay na Natalia Sule walishiriki katika mashindano ya Milan Marathon yaliyofanyika nchini Italy mwezi Mei, 2021 ambapo mwanariadha Gabriel Geay amefanikiwa kufuzu kushiriki Michezo ya Olimpiki nchini Tokyo Japan 2021;
- g) Timu ya Taifa ya Mpira wa Wavu ilishiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika yaliyofanyika nchini Tunisia mwezi Aprili, 2021; na
- h) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Ufukweni (*beach soccer*) imefuzu kwa mara ya pili kushiriki katika mashindano ya Bara la Afrika kwa mchezo huo yatakayofanyika nchini Senegal kuanzia tarehe 23/05- 29/05.

**115. *Mheshimiwa Spika*,** mafanikio mengine makubwa yaliopatikana katika mpira wa miguu ni Klabu ya Simba kuingia robo fainali katika mashindano ya Klabu Bingwa Barani Afrika. Klabu hii imeonyesha soka la hali ya juu katika mashindano hayo kwani ilizichakaza Klabu kubwa Barani Afrika kama vile FC Platinum ya Zimbabwe goli 4-0, Al Merreikh ya Sudan goli 3-0, As Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo goli 4-1, Al Ahly ya Misri goli 1-0 na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini goli 3-0. Aidha, timu yetu ya Namungo ilifanikiwa kuiwakilisha vyema nchi yetu kwenye Kombe la Shirikisho Barani Afrika ambapo katika hatua za awali ilizichabanga Al Rabita ya Sudan Kusini goli 3-0, Al Hilal Obeyid ya Sudan goli 5-3 na De Agosto ya Angola goli 75.

**116. *Mheshimiwa Spika*,** kwa heshima na taadhima, kupitia Bunge lako Tukufu, niipongeze Klabu ya Simba na Klabu ya Namungo kwa mafanikio makubwa zilizoyapata ambayo ni kielekezo kuwa soka la Tanzania limeendelea kukua na kutoa upinzani Kimataifa, na salamu kwa Vilabu vikubwa Barani Afrika kuwa Timu za Tanzania siyo uchochoro wa kupita. Mafanikio haya kwa pamoja yameipa nchi yetu fursa ya

kutoa Vilabu vinne (4) vitakavyotuwakilisha katika Klabu Bingwa Barani Afrika na Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Serikali itaendelea kuweka mazingira bora zaidi yatakayochochea mafanikio makubwa zaidi ya mpira wa miguu na michezo mingine katika nyanja za Kimataifa.

**117. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara iliendelea kuratibu usimamizi na utunzaji wa Uwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru pamoja na miundombinu mingine ya michezo ambapo hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kufunga lifti mpya katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Aidha, ikiwa ni hatua ya kumuenzi Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin Mkapa, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliamua Uwanja wa Taifa ubadilishwe jina na kuitwa rasmi Uwanja wa Benjamin Mkapa (*Benjamin Mkapa Stadium*).

**118. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuimarisha michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA inayolenga kuibua vipaji vya michezo kwa vijana wetu walioko shulenii, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilikutana na kufanya vikao mbalimbali vya watalaam, Makatibu Wakuu pamoja na Mawaziri wa Wizara hizo ili kushauriana kwa kina juu ya kuendeleza michezo mashulenii na vilevile kuimairisha mashindano ya wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Kabla ya Vikao hivyo usimamizi wa michezo hususan katika ufundishaji wa michezo na usimamizi wake katika Shule ulikuwa umelegalega.

Kufuatiavikao hivyo na maelekezo yaliyotolewa, Wizara hizo kwa pamoja zimekubaliana kuongeza ushirikiano katika kusimamia na kukuza michezo mashulenii na kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na zifuatazo:

a) Kuandaa Mwongozo wa uendeshaji wa michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA ambao utakuwa unatumika kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano badala ya kutoa Mwongozo kila mwaka. Hatua hii itawezesha kuimarisha maandalizi ya michezo hiyo na kuondoa tatizo la

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ucheleweshaji wa mwongozo ambao kimsingi unaathiri maandalizi. Mwongozo mpya utaanza kutumika katika mashindano yajao ya mwaka 2022.

b) Kushirikiana kwa pamoja katika kutafuta wadhamini wa kudumu ili kuimarisha ugharamiaji wa mashindano hayo;

c) Kuundwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu maandalizi na uendeshaji wa michezo ya UMISSETA na UMITASHUMITA kwa kuhusisha Wizara zote tatu kuanzia michezo ya mwaka huu wa 2021.

d) Kuratibu na kusimamia kwa pamoja michezo ya UMISSETA na UMITASHUMITA itakayofanyika mkoani Mtwara mwezi Juni, 2021.

**119. *Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa michezo wa ngumi, mabondia wa Kitanzania wa Mchezo wa Ngumi za Kulipwa wameshiriki Mashindano 21 ya kimataifa na kushinda mapambano saba (7) kama ifuatavyo:

a) Bruno Tarimo alimtwanga Bondia Kye Mackenzi wa Australia na kushinda mikanda ya *IBF International Super Feather* na *IBO Intercontinental Super Feather* mwezi Aprili 2021;

b) Ibrahim Class alimtandika bondia Denis Mwale kutoka Malawi na kunyakua Mkanda wa *WBF Intercontinental Light* mwezi Januari 2021;

c) Shabani Jongo alimchakaza Bondia Shawn Miller kutoka Marekani na kufanikiwa kushinda mkanda wa *WBF Internationa Cruiser* mwezi Januari 2021;

d) Bondia Tony Rashid alimfumua Hassan Milanzi Kutoka Zimbabwe na kufanikiwa kutwaa mkanda wa *ABU Super Bantamweight* mwezi Desemba, 2020;

- e) Ibrahim Class alimgaragaza Bondia Simon Ngoma kutoka Zambia na kufanikiwa kushinda mkanda wa *GBC World Super Featherweight* mwezi Novemba 2020;
- f) Salim Jengo alimtwanga bondia Eduardo Masinto kutoka nchi ya Thailand na kufanikiwa kutwaa mkanda wa *UBO World Lightweight* mwezi Novemba, 2020; na
- g) Hassan Mwakinyo alimtandika bondia Tshibangu Kayembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kutwaa mkanda wa *WBF Intercontinental Super Welterweight*.

**120. *Mheshimiwa Spika*,** nchi yetu imeendelea kuwa na wachezaji wanaocheza katika michezo mbalimbali nje ya nchi ambayo ni fursa ya ajira kwa wanamichezo wetu kimataifa. Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 Tanzania ilikuwa na jumla ya wachezaji 54 wanaocheza michezo mbalimbali kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo:

***Jedwali Na 2: Idadi ya Wachezaji wa Tanzania Wanaocheza Michezo Mbalimbali Nje ya Nchi***

Na.	Aina ya Mchezo	Idadi ya Wachezaji
1.	Mpira wa miguu	32
2.	Mpira wa kikapu	16
3.	Mpira wa wavu	4
4.	Mchezo wa kabaddi	2

**121. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na mafanikio haya, ni dhamira ya Serikali kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo kutekeleza mikakati mbalimbali itakayowezesha kuongeza ushiriki wa jamii katika michezo katika ngazi za jamii na shule (sports for all) ili kupitilia ushiriki huo, viibuliwe vipaji vitakavyoendelezwa na kuwezesha ongezo la ajira kwa wachezaji ndani na nje ya nchi (*professional sports*). Mikakati itakayotekelozwa ni pamoja na kuimarisha ugharamiaji wa michezo kwa kuibua vyanzo vipyta vya mapato, kuendeleza michezo katika shule na Taasisi za elimu; kuimarisha miundombinu ya michezo na vifaa vya michezo katika ngazi

mbalimbali na kuboresha utaratibu wa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali. Mikakati mingine ni kuimarisha ushiriki wa wananchi wa makundi mbalimbali katika michezo na kuanzisha na kuendeleza shule za michezo (*sports academies*).

**122. *Mheshimiwa Spika*,** napenda kuwapongeza wachezaji wetu wa zamani waliotoa mchango mkubwa na kulipa Taifa letu heshima katika mashindano ya Kimataifa. Kwa uchache niwapongeze wachezaji wa riadha waliofiletea heshima Taifa letu ambao ni Filbert Bayi (Medali ya dhahabu aliyopata katika mashindano ya Jumuiya ya Madola mwaka 2008) na Suleiman Nyambui (Medali ya Fedha mwaka 1980 katika mashindano ya mita 5,000). Wachezaji wengine ni Juma Ikangaa aliyepata Medali ya Fedha katika mashindano ya Jumuiya ya Madola Mwaka 1996; Samwel Mwera aliyepata Medali ya Dhahabu katika michezo ya *All African Games* katika mbio za Mita 800 na Gidamis Shahanga aliyepata Medali ya Dhahabu katika mashindano ya Jumuiya ya Madola mwaka 1978. Wengine ni Christopher Iswege aliyeshinda Mashindano ya Dunia ya Riadha mwaka 2006 (*World Athletics Championship*) na Theresia Dismas aliyepata Medali ya Shaba mwaka 1965 katika Mchezo wa Kurusha Mkuki na kuwa Mtanzania wa kwanza kuliletea Taifa letu Medali ya kwanza.

**123. *Mheshimiwa Spika*,** niwapongeze pia wanamasumbwi Habibu Kinyogoli, Rashidi Matumla, Emanuel Mlundwa na William Isangura kwa kuliletea Taifa letu medali mbalimbali katika mashindano ya kimataifa ya masumbwi. Kwa upande wa soka, sina budi kuwatambua wachezaji nguli waliofiletea heshima kubwa Taifa letu kwa kutuwezesha kuingia kwa mara ya kwanza kwenye Fainali za Kombe la Afrika nchini Nigeria mwaka 1980. Kwa uchache, wachezaji hao ni wazee wetu akina Leodger Tenga, Peter Tino, Ahmed Amasha, Juma Pondamali, Leonad Mukebezi, Daud Salum, Jela Mtagwa, Mtemi Ramadhan, Mohamed Husein na Husein Ngulungu. Wachezaji hawa wa zamani ni hazina kubwa katika maendeleo ya michezo nchini na kupitia Kikao nilichofanya

nao, nimepata maoni mengi ya msingi yatakayowezesha kufanya maboresho katika uendelezaji wa michezo nchini.

**124. *Mheshimiwa Spika*,** napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza waheshimiwa wabunge ambao wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza Agizo la Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kufanya mazoezi kila Jumamosi ya pili ya mwezi. Naupongeza uongozi mpya wa Bunge Sports Club uliochaguliwa hivi karibuni unaohusisha Waheshimiwa wabunge wafuatao kwa nafasi zao: Mhe. Abbas Tarimba – Mwenyekiti, Mhe. Esta Matiko – Makamu Mwenyekiti na Mhe. Seif Gulamal – Meneja wa Klabu. Niwapongeze pia wajumbe wa Klabu hiyo Mhe. Ridhiwan Kikwete, Mhe. Anna Lupembe, Mhe. Rose Tweve, Mhe. Stanislaus Mabula na Mhe Aeshi Hillal. Napenda kuuhakikishia uongozi huu na Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara itaendelea kuwapa ushirikiano wa dhati ili kutimiza malengo yanayokusudiwa.

Vilevile, kipekee niwapongeze wananchi wote waliojiunga kwenye makundi mbalimbali ya mazoezi (*jogging clubs*) kwa ajili ya kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao. Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Afya ili kuendelea kuhamasisha wananchi wote kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara kwa lengo la kulinda afya zao na kujiepusha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo shinkizo la damu, kisukari na unene uliopitiliza.

### **3.2.4.1 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)**

**125. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu ya BMT ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo; kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Michezo; kuidhinisha mashindano na matamasha ya Kitaifa na Kimataifa yanayoandaliwa na Mashirikisho/Vyama vya Michezo na Taasisi ili kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo na kusajili vyama, vilabu na mashirikisho ya michezo nchini.

**126. Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu la BMT ni kuhakikisha shughuli za michezo zinarasimishwa na kutambulika na katika kutekeleza jukumu hilo, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Mei, 2021 Baraza lilisajili Vyama 12, vilabu 89, Taasisi 5 za kimichezo, wakuzaji vipaji nya michezo 11 vituo nya michezo 4 na mawakala wa michezo 21. *Kiambatisho Na. 5* ni usajili wa Vyama, Vilabu, Vituo nya Michezo na Wakuzaji/ Mawakala wa Michezo. Aidha, marekebisho ya Katiba ya Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Vyama nya michezo vinne (4) ambavyo ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Shirikisho la Riadha Tanzania, Chama cha Michezo ya Jadi Tanzania na Chama cha Mpira wa Miguu cha Wilaya ya Mpanda zilipitiwa, kuboreshwa na kuidhinishwa na Msajili wa Vyama nya Michezo.

**127. Mheshimiwa Spika**, ikiwa ni hatua ya kuimarisha michezo katika jamii na kupunguza tatizo la uhaba wa wataalamu wa michezo, mafunzo kwa walimu wa michezo 48 katika Mkoa wa Songwe yalitolewa. Mafunzo hayo yalihusu uratibu wa matukio ya kimichezo, huduma ya kwanza katika michezo, Sheria za Mchezo wa Netiboli, Mpira wa Mikono, Mchezo wa Riadha na namna ya uendeshaji wa mazoezi ya viungo nya mwili (*aerobics*). Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu na makocha wa shule ili kuwawezesha kufundisha masuala hayo kwa wanafunzi, jamii na wadau wengine. Pia katika kuhakikisha Vyama na Mashirikisho ya Michezo yanaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, mafunzo ya uongozi na utawala bora yalitolewa kwa Viongozi 42 wa Vyama na Mashirikisho ya Michezo ya watu wenye Ulemavu.

**128. Mheshimiwa Spika**, katika kuhahakisha michezo inafanyika kikamilifu na kwa kufuata utaratibu, matukio mbalimbali ya michezo yaliidhinishwa ambapo jumla ya vibali thelathini (30) vilitolewa kwa matukio ya kitaifa na Kimataifa kama vile mapambano ya ngumi na mbio za barabarani.

**129. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia BMT imeendelea kuwezesha Vyama nya Michezo na Timu za Taifa kifedha na ushauri wa kitaalamu ikiwa ni hatua ya kuhakikisha timu

zinaandaliwa vyema ili zifanye vizuri katika mashindano ya kimataifa. Katika mwaka 2020/2021 Vyama na Mashirikisho sita (6) ambayo ni Kamati ya Paralimpiki, Mpira wa Miguu, Mpira wa Wavu, Michezo wa Riadha, Netiboli na Mpira wa Miguu kwa watu wenyewe ulemavu yaliwezeshwani. Aidha, katika kuhakikisha Timu za Taifa zinafanya vizuri BMT limeendelea kuweka mikakati ya kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo nchini ambapo kwa mwaka 2020/2021 mfuko huo umekusanya kiasi cha Shilingi Milioni 87 kutoka katika makusanyo ya ndani tofauti na miaka ya nyuma ambapo mfuko huo haukuwa na vyanzo nya mapato.

Hali kadhalika, BMT kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Michezo na Wizara ya Fedha na Mipango zinaendelea na majadiliano yatakayowezesha Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Michezo (*Sports Betting*) kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo ya Michezo pamoja na kuchezeshwa kwa Bahati Nasibu ya Taifa ambayo kwa mujibu wa Sheria, asilimia 50 ya mapato yatokanayo na Bahati Nasibu hiyo yanapaswa kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo ya Michezo. Inatarajiwa kuwa vyanzo hivi vikianza kufanya kazi, vitakuwa muarobaini wa changamoto ya fedha za kugharamia timu za Taifa.

**130. *Mheshimiwa Spika***, Serikali iliendelea kuchukua hatua za kuhahakisha jamii inashiriki kikamilifu katika shughuli za michezo na mazoezi ya viungo nya mwili ili kuimarishe afya na kupunguza tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo kisukari, shinikizo la damu na unene uliopitiliza. BMT kwa kushirikiana na Kamati za Michezo za Mikoa na Wilaya, limeendelea kuratibu na kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za michezo na mazoezi ya viungo ikiwa ni hatua ya kuhakikisha wananchi wanashiriki katika mazoezi ya viungo ili kuimarishe afya zao.

### **3.2.4.2 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA**

**131. *Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Chuo hiki ni kuandaa wataalamu wa michezo kwa kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya ufundishajji wa fani mbalimbali za michezo;

kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya fani za Michezo; na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu michezo. Chuo kinatoa stashahada tatu ambazo ni Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo (*Diploma in Sports Management and Administration*), Stashahada ya Ufundishaji Michezo (*Diploma in Sports Coaching Education*) na Stashahada ya Elimu ya viungo vya mwili katika michezo (*Diploma in Physical Education and Sports*). Pamoja na mambo mengine, katika mwaka 2020/2021 Chuo kimetekeleza majukumu yafuatayo:

- a) Kimehuisha mitaala ya ufundishaji ili iendane na mahitaji ya soko la michezo nchini, ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya michezo inayofundishwa ikiwemo mpira wa kengele kwa ajili ya watu wenye uoni hafifu, mpira wa meza, vinyoya na *tennis*. Aidha, katika kuhuisha mitaala chuo kimeongeza moduli ya ufundishaji uamuzi (*refereeing*) kwa ajili ya mpira wa miguu.
- b) Kimeanzisha Mtaala wa Astashahada ya Elimu ya Viungo vya Mwili katika Michezo (*Certificate in Physical Education and Sports*). Mtaala huu ni fursa pekee kwa wahitimu wa kidato cha nne kuweza kupata mafunzo ya michezo ambapo baada ya kuhitimu ngazi hii watajumuishwa katika ngazi ya tano na sita ili kupata sifa ambayo itawapatia stashahada ya michezo.
- c) Kimeingia makubaliano na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ya utoaji wa mafunzo ya michezo.
- d) Kimeanzisha vituo vya mafunzo ya Michezo jijini Dar es Salaam, na Mkoani Ruvuma katika Halmashauri ya Tunduru kwa ajili ya kutoa mafunzo katika kanda ya mashariki na kanda ya kusini. Kituo cha Dar es salaam kimeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kuwapatia wadau wa michezo ujuzi mbalimbali ili kupanua wigo wa utoaji wa mafunzo ya michezo nchini. Katika kipindi hiki, washiriki takriban 204 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya michezo katika Kituo hiki.

Aidha, Chuo kilitoa mafunzo katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma na kuhudhuriwa na washiriki kama ifuatavyo: Tunduru

274, Namtumbo 164, Songea 164, Songea Vijijini 168, Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga 217, Halmashauri ya Mji wa Mbanga 126, Nyasa 168 na Madaba 70. Vilevile, mafunzo yalitolewa Mkoani Rukwa katika Wilaya ya Kalambo ambayo yalihusisha washiriki 74.

e) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo 244. *Kiambatisho Na. 6* ni mwenendo wa usajili wa wanafunzi katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

### **3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU**

**132. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha nguvukazi yake na kuboresha mazingira ya kufanya kazi. Katika kipindi hiki nafasi za ajira mpya zilizo jazwa ni tisa (9) na watumishi 10 walihamishiwa Wizarani. Aidha, nafasi za viongozi sita (6) wa Wizara zilliazwa. Vilevile, kulifanyika mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi ikiwa ni hatua ya kuwashirikisha watumishi katika utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa kushirikiana na uongozi. Pia, jumla ya watumishi 16 waliwezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 40 mafunzo ya muda mfupi.

### **4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO**

**133. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2020/21, pia kulikuwepo na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Wizara ni kama ifuatavyo:

a) Kutokana na utandawazi unaosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, kumekuwa na mmonyonyoko wa maadili na kutozingatiwa kwa mila na desturi za Tanzania hususan kwa vijana. Aidha, wasanii wetu wamekuwa na hulka ya kuiga mambo ambayo yanafanyika katika mataifa mengine kwa lengo la kushindana na soko la kazi za sanaa duniani. Hali hiyo inasababisha uvunjifu wa maadili kwani mila na desturi zetu hazifanani na za mataifa mengine ambako wasanii wetu wanaiga namna ya

uendeshaji wa kazi zao. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wasanii wetu ili wazalisho kazi zinazoendana na misingi ya mila, utamaduni na desturi zetu.

b) Kuongezeka kwa ushindani katika biashara za huduma za utangazaji na uchapishaji kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya mawasiliano ikiwemo habari mtandao, tovuti, blogu, majukwaa na mitando ya kijamii. Hatua hii inaathiri mapato ikiwemo ya TSN kupitia magazeti inayozalisha. Kama ilivyobainishwa awali, mikakati inayotekelezwa ni pamoja na kujiimarisha ili kuendana na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia katika tasnia ya habari na utangazaji, na kutumia kikamilifu fursa zitokanazo na teknolojia hizo kujiimarisha kiutendaji na utoaji wa huduma unaoendana na mahitaji ya wateja.

c) Uhaba wa watumishi wa Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na uwepo wa Miundo ya Kiutumishi isiyoakisi utekelezaji wa majukumu yanayohusu Wizara kwa tija na ufanisi katika mamlaka hizo. Katika kutatua changamoto hii, Makatibu Wakuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, OR-TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumisha wa Umma na Utawala Bora walikutana tarehe 22 Mei, 2021 ambapo baada ya kupokea changamoto za kimuundo zinazowakabili maofisa Utamaduni na Michezo walliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Kikao kazi cha Maofisa hao, walikubaliana kuanza mara moja kwa zoezi la kupitia Miundo husika ili kutatua changamoto hiyo ipasavyo.

d) Upungufu wa miundombinu ya michezo inayokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali katika ngazi mbalimbali. Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995, inabainisha kuwa suala la ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya michezo ni jukumu la wadau mbalimbali ikiwemo Serikali za Mitaa; Sekta Binafsi; Mashirika ya Umma; Vyama, Vilabu na Mashirikisho ya Michezo na wananchi kwa ujumla. Pamoja na maelekezo haya, bado kuna uhaba mkubwa wa miundombinu ya michezo. Wizara imeendelea kuhamasisha

wadau kujenga viwanja vya michezo na pia kutoa utaalamu kuhusu ujenzi wa miundombinu ya michezo katika Halmashauri mbalimbali na wadau wengine.

Wizara inatoa wito kwa waheshimiwa Wabunge kuendelea kuhamasisha Halmashauri zao kuweka kipaumbele katika kutenga maeneo ya michezo, kuyaendeleza na kuyalinda maeneo hayo ili yasivamiwe na kubadilishwa matumizi. Aidha, Wizara inakishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kuwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika Sekta ya Habari, na ni matarajio kuwa uwekezaji huu utaendelea kufanyika katika ukarabati na uendelezaji wa viwanja vyake vya michezo.

e) Upatikanaji wa mitaji nafuu na ya uhakika kwa wasanii, pamoja na mafunzo ili kuwawezesha kuzalisha kazi zenye ubora na viwango vinavyomudu ushindani katika masoko ya kimataifa. Kuanza kwa utekelezaji wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa katika mwaka 2021/22 kutawezesha kukabiliana na changamoto hii.

f) Athari za UVICO 19 katika Sekta za Wizara hususani sanaa ambapo watayarishaji wa picha za filamu na wasanii kutoka nje ya nchi walishindwa kuja nchini kwa ajili ya shughuli hizo na hivyo kuathiri mapato. Aidha, wasanii wetu walikosa fursa ya kufanya matamasha katika nchi mbalimbali kutokana na nchi hizo kutoruhusu watu kuingia na mikusanyiko kutokana na ugonjwa huo;

## **5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

**134. *Mheshimiwa Spika*** katika mwaka 2021/22 Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-25; ahadi na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 - 2025/26; na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26. Aidha, utekelezaji wa majukumu utazingatia pia malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya

Mwaka 2030 katika maeneo yanayohitaji kuchukuliwa hatua na Wizara.

**135. *Mheshimiwa Spika***, Ibara za 32, 125, 239, 241 na 243 za llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 202025 zinailelekeza Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kuimarisha mchango wa Sekta hizo katika maendeleo ya Taifa letu, ikiwemo kuzalisha ajira hususan kwa vijana. Maelekezo hayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa urahisi zaidi; kufanya tafiti za lugha, historia, mila nzuri na desturi za jamii za Tanzania kwa ajili ya kulinda, kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho; kuliimarisha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na kutekeleza programu maalum ya kikitangaza Kiswahili duniani.

**136. *Mheshimiwa Spika***, maelekezo mengine ni kuwahamasisha na kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika utamaduni, michezo na sanaa kwa ajili ya kuongeza ajira na kipato; na kuimarisha michezo, ikiwa ni pamoja na michezo ya kulipwa, kuanzisha shule maalum za kukuza vipaji vya wanamichezo (*sports academy*), kuhamasisha wananchi kushiriki katika michezo na kuimarisha miundombinu ya michezo. Aidha, Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprilli, 2021 alibainisha Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi wa masuala ya Hakimiliki ili wasanii waweze kunufaika na kazi zao; kuhuisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwasaidia wasanii wetu, ikiwemo kupata mafunzo na mikopo na kutenga fedha kwa ajili ya kuziandaa Timu zetu za Taifa, zikiwemo za wanawake.

**137. *Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza maelekezo haya, katika mwaka 2021/22 Wizara itaratibu uundwaji wa vyombo vya kutekeleza Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016, kusajili vyombo vya habari na kuimarisha usikivu wa wa TBC katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara itawajengea uwezo wasanii wetu kimitaji na mafunzo kuititia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, hatua ambayo itaongeza

tija, ubora na ushindani wa kazi za sanaa na wabunifu wetu kitaifa na kimataifa. Vilevile, Wizara itakamilisha uundwaji na kuanza matumizi ya mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya kuwahudumia wasanii na wadau wengine wa sanaa ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma, kurahisisha urasimishaji wa Sekta ya Sanaa na shughuli za ubunifu na kubwa zaidi, kuongeza mapato ya wasanii na Serikali kuitia ukusanyaji wa mirabaha. Mifumo hiyo ni ya kufuatilia matumizi ya kazi za sanaa hususani muziki na filamu katika vyombo vya habari, mfumo wa kusambaza kazi za wasanii kama ilivyo Netflix na mfumo wa usajili na usimamizi wa taarifa za wasanii na wadau wa sanaa.

**138. *Mheshimiwa Spika***, katika nyanja za michezo, Wizara itaendelea kuimarisha uibuaji na uendelezaji wa vipaji kuitia michezo mashulenii, mashindano ya Taifa (Taifa Cup) kwa michezo mbalimbali na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Vipaji vya Michezo (*Sports Academy*) katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Wizara pia itaendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji na uendeshaji wa vituo vya kukuzia vipaji vya michezo pamoja na kuimarisha vyanzo vya mapato ya kuendeleza michezo.

**139. *Mheshimiwa Spika***, Kisekta, Wizara itatekeleza majukumu mbalimbali kama inavyofafanuliwa hapa chini.

## **5.1 SEKTA YA HABARI**

**140. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wa Idara ya Habari-MAELEZO na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali ili iweze kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hususani katika kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelizwa na Serikali; kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari; kuchapa na kutoa kwa wadau picha za viongozi wa kitaifa; kuchapa na kutoa leseni za magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari, kutoa mwongozo na kutathmini utoaji wa taarifa kwa umma kuitia Taasisi za Serikali.

Majukumu mengine yatakayotekelezwa ni kukusanya na kusambaza habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya Serikali, kuratibu mkuutano wa mwaka wa Maofisa Mawasiliano wa Serikali na pia kushirikiana na Vyama vya Wanahabari kama Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA Tan), Baraza la Habari na Waandishi wa Habari kwa ujumla katika kutangaza shughuli za maendeleo.

### **5.1.1 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)**

**141. *Mheshimiwa Spika***, TBC itaendelea na majukumu ya kufunga mitambo ya masafa ya FM katika mikoa ya Njombe, Songwe na Simiyu pamoja na Wilaya za Kilwa na Serengeti; upanuzi wa usikivu wa redio katika maeneo ya Unguja na Pemba; kuendelea na ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya TBC katika eneo la Vikonde Jijini Dodoma na kuimarissha Chaneli ya Tanzania Safari kwa kununua mitambo na vifaa vya uandaaji na utangazaji mahususi kwa ajili ya vipindi vya utallii (kamera za kisasa, drones, LIVE U, magari, vifaa vya kurekodi sauti za wanyama na ndege na vifaa vya kuhariri picha za video).

Aidha, Shirika litafunga mitambo ya televisheni kwa ajili ya kuunganisha studio za TBC<sub>1</sub>, na TBC<sub>2</sub> na kutoa mafunzo kwa watendaji kuhusu uandaaji bunifu wa vipindi vya redio na televisheni. Vilevile, katika kutimiza jukumu lake la kuelimisha, kuhabarisha na kuburudisha, TBC kuititia TBC<sub>2</sub> imedhamiria kuwafikia vijana na kukidhi mahitaji ya kundi hilo kwa kuandaa vipindi vyenye vionjo vya burudani zaidi pamoja na vipindi vinavyohusu midahalo kutoka vyuoni na mashulenii ambavyo vitafundisha masomo mbalimbali. Vilevile, TBC<sub>2</sub> itatoa fursa kwa vijana wa vyuoni kufanya mazoezi kwa vitendo, itaandaa matamasha ambayo yatasaidia kuibua vipaji vya wasanii wadogo, kuhakikisha vijana wanaelewa mila na desturi za kitanzania, kuimarissha uwezo wa vijana kusimamia masuala ya ulinzi na usalama wa nchi na kuzingatia maadili ya Mtanzania katika jamii.

### **5.1.2 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)**

**142. *Mheshimiwa Spika*,** TSN itaendelea kuboresha uwezo wa Taasisi kiutendaji na kibiashara kwa kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma za Kampuni na kupanua wigo wa biashara kwa kuendelea kubuni vyanzo vipyta vyta mapato na kuendeleza vile vilivyopo. Aidha, Kampuni itaanza utekelezaji wa mradi wa ununuzi wa mtambo mpya na wa kisasa wa uchapaji na itawekeza zaidi kwenye habari mtandao kwa kuajiri nguvu kazi, kupata vifaa vyta kisasa na kuanzisha studio ya kisasa (*multimedia studio*).

Vilevile, TSN itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake wakiwemo wahariri pamoja na waandishi wa habari, kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ndani na nje ya nchi na itaongeza nguvu katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi ikiwemo maslahi, pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi ili kubakiza vipaji vyta kitaalamu vilivyopo na kuvutia vipaji na umahiri zaidi katika kampuni kutoka katika soko la ajira za wanahabari nchini. Lengo ni kuongeza ufanisi na ubora wa bidhaa za kampuni kwa kuchapisha habari zilizoandikwa, kuhaririwa na kusanifiwa kwa ubora wa hali ya juu unaoendana na mahitaji ya soko.

### **5.1.3 MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

**143. *Mheshimiwa Spika*,** TCRA itaendelea kuweka mazingira maridhawa ya kuendeleza Sekta ya Habari na Utangazaji kwa kuititia Kanuni mbalimbali zinazosimamia sekta ya Utangazaji kwa ajili ya kuboresha huduma za Utangazaji nchini. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara itafanya kazi hoja 13 kutoka kwa wadau ambazo zimekuwa changamoto katika utoaji wa huduma za utangazaji nchini. Hoja hizo ni pamoja na kuhakikisha kuwa Wasanii, Wabunifu, na wale wasiojihusisha na masuala ya utoaji wa Habari (*news and current affairs*) mtandaoni wanatoa huduma mtandaoni na wanapata fursa ya kuimarisha maudhui ya ndani ikiwa ni pamoja na Wasanii kutangaza kazi zao bila tozo zozote ili mradi wanazingatia sheria za nchi.

Hoja nyingine za kufanyiwa kazi ni pamoja na kuimarisha Muundo wa TCRA ili uweze kusimamia ipasavyo masuala ya utangazaji; kupunguza gharama za tozo kwa televisheni za mtandaoni na watoa huduma wengine wa mitandaoni; kuwa na kisimbuzi kimoja; kuangalia suala la adhabu kali zinazotolewa kwa vituo vya redio/televisheni kupitia Kamati ya Maudhui; pamoja na vyombo vya habari vya dini kuchukuliwa kuwa ni vya kibiashara na wengi kucheleweshwa kuruhusiwa kuongeza ukubwa wa leseni zao (mfano kutoka leseni ya wilaya hadi leseni ya kitaifa). Hoja nyingine ni kuimarisha usalama wa akaunti za wasanii wenye wafuasi wengi ili zisiweze kuibawa na kuuzwa (*hacked*) na kukamilisha Mfumo wa wa Pamoja wa Kufuatilia Haki za Wasanii katika televisheni na redio.

## **5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI**

**144. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa kwa kushirikiana na wadau na kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kwa kutoa mikopo kwa wanatasnia na kuwajengea uwezo wa kuzalisha kazi bora na zenye ushindani kitaifa na kimataifa pamoja na kuanza ujenzi wa ofisi za Mfuko. Utunishaji wa mfuko huu utategemea ruzuku ya serikali, sehemu ya tozo mbalimbali zinazotokana na kazi za tasnia pamoja na michango ya wahisani. Vilevile, Wizara itakamilisha uhuishaji wa Sera ya Maendeleo ya Utamaduni ya mwaka 1997; kuchapisha na kusambaza kitabu cha Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Taifa na kuratibu Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika iliy oasisiwa na azimio la Umoja wa Afrika mwaka 2011.

Majukumu mengine ni pamoja na kufanya tafiti kuhusu mila na desturi za jamii mbalimbali; kuandaa na kuorodhesha vipengele vya urithi wa utamaduni wa Taifa usioshikika na kuratibu maonesho na shughuli za kiutamaduni za kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, utamaduni wa Mtanzania utaendelea kuenezwa kupitia ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa kuwa ufundishaji wa lugha huambatana na ufundishaji wa utamaduni.

Kuhusu utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika yenye lengo la kutambua, kuhifadhi, kulinda na kutangaza amali za urithi wa ukombozi wa Afrika zinazoshikika na zisizoshikika zilizopo nchini, Wizara itaendelea kuratibu tathmini ya hali ilivyo katika maeneo 260 ya Urithi wa Ukombozi yaliyopo nchini na kuzishirikisha nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika hususani Kusini Mwa Afrika katika kuyahifadhi. Katika kufanya tathmini hiyo, Wizara itashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na OR-TAMISEMI na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi, Agosti, 2021.

### **5.2.1 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)**

**145. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu yatakayotekelawa ni pamoja na kuendeleza mikakati ya kikitangaza na kubidhaisha Kiswahili kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na kufunga mfumo wa vifaa vya kisasa vya kufundisha ukalimani. Vilevile, tafsiri ya Sheria, Kanuni na nyaraka mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali itafanywa; na elimu ya matumizi sanifu na fasaha ya lugha itatolewa kupitia redio na televisheni na kuchapisha makala za mada mbalimbali katika magazeti. Pia, Sheria ya BAKITA ya mwaka 1967 itapitiwa ili kuhakikisha inaendana na mahitaji ya Kiswahili ya sasa.

**146. *Mheshimiwa Spika*,** BAKITA pia litaendelea kutoa mafunzo kwa wageni kupitia kituo kilichopo katika ofisi za BAKITA na kwa njia ya mtandao. Vilevile, litachapisha vitabu vitatu (3) ambayo ni *Furahia Kiswahili Toleo la Pili*, Kitabu cha *Sarufi Sahilli* na *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili Sanifu*. Aidha, mafunzo ya msasa ya kupima weledi wa wakalimani yatatolewa kwa wakalimani 50.

### **5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANA**

**147. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itaendelea kuratibu maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Sanaa ili kuweka misingi thabiti ya kuiendesha Sekta kwa manufaa ya Wasanii na Taifa kwa ujumla; kufanya tathmini ya utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazohusika na masuala ya Sanaa kwa ajili

ya kuziimarisha ili zikidhi matarajio ya wadau na pia kuwa na msingi wa kufanya mageuzi ya kisekta. Vilevile, Wizara inatarajia kuzisimamia Taasisi zake na kuhakikisha mifumo ya kisasa ya ukusanyaji mirabaha na usajili kwa njia ya kidijiti inakamilishwa sambamba na kuanzisha tuzo za Kitaifa katika Sekta ya Sanaa hapa nchini. Kwa mwaka 2021, tuzo hizi za Kitaifa zinatarajiwa kutolewa mwezi Desemba.

**148. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kukutana na Balozi mbalimbali kupitia utaratibu iliyojiwekea ili kuhakikisha ushirikiano wa kisekta unaimarishwa kwa malengo ya kujenga mshikamano mionganoni mwa mataifa rafiki. Baadhi ya maeneo ambayo Wizara inaona ni muhimu kwa ushirikiano ni pamoja na ushirikiano wa kitaalam katika sekta, makusanyo na ugawaji mirabaha, udhamini katika mafunzo ya Sanaa na vifaa husika, uwekezaji katika miundombinu na vifaa vya uzalishaji Sanaa, kubadilishana uzoefu kupitia matamasha na maonesho mbalimbali na kuwa na mialiko ya ushiriki katika shughuli za Sanaa.

Mathalani, Wizara ina mpango wa kuwa na maktaba itakayowawezesha Wasanii, hasa wa muziki na filamu kuazima vifaa vya kisasa ili kuzalisha kazi bora na zenye ushindani kitaifa na kimataifa. Natoa wito kwa balozi zetu, kuona umuhimu wa kuthamini mpango huu kwani sio tu utaleta tija katika kuzalisha kazi za Sanaa zenye ubora bali pia kuwapa fursa Wasanii wetu kujifunza kutumia zana za kisasa na kuvutia soko la kiushindani.

**149. Mheshimiwa Spika**, Wizara hii imepewa jukumu la kutoa mafunzo na kuwawezesha kimitaji Wasanii na wadau wengine wa Utamaduni na Sanaa kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. Kupitia Mfuko ulioanzishwa, Wizara inalenga kuanza kujenga jengo la kisasa Jijini Dodoma lenye Ofisi za Mfuko, BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania, COSOTA na BAKITA na kuanza kuwawezesha kimitaji na mafunzo wadau wa mfuko huo ambao katika mwaka 2021/22 unaombewa kiasi cha Shilingi Billioni Moja na Milioni Mia Tano (Sh.1,500,000,000) na Mkakati wa Wizara ni kuutunisha kupitia vyanzo mbalimbali nje ya ruzuku kutoka Serikalini. Baadhi ya

vyanzo hivyo ni tozo ijulikanayo kama *Blank Tape Remuneration* iliyowasilishwa Serikalini kwa maamuzi, ambapo sehemu ya fedha itakayokusanya kutokana na mirabaha ya wasanii itaingia kwenye Mfuko. Aidha, sehemu ya makusanyo yatakayotokana na mfumo (*platform*) wa kusambaza na kuuza kazi za Wasanii unaoundwa na Serikali yataingizwa kwenye mfuko na washirika wa maendeleo na wadau mbalimbali watahamasishwa kuchangia katika Mfuko.

Mfuko huu ukianza kutoa huduma, kilio cha muda mrefu cha wadau kuhusu ukosefu wa mitaji na mafunzo kitakuwa kimetatuliwa na hivyo kuchochaea uzalishaji wa kazi bora za Sanaa, kuibua ajira mpya na kuimarishe uchumi wa msanii mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

**150. *Mheshimiwa Spika***, jukumu jingine ni kuandaa Siku Maalumu ya Msanii Tanzania, ambapo mafanikio yatabainishwa na changamoto katika Sekta zitajadiliwa kwa mapana ili kuwa na mikakati ya pamoja ya namna ya kusonga mbele kufuatia mabadiliko makubwa yanayoendelea kutokea katika utoaji mafunzo, uzalishaji, usambazaji, urasimishaji na ulinzi wa kazi za Sanaa. Majukumu mengine ni kuratibu shughuli za burudani katika matukio ya kitaifa ikiwemo Sherehe za Uhuru na Muungano na shughuli nyingine zitakazojitokeza; kuratibu Tamasha la Sanaa la Serengeti (Serengeti Arts Festival) na kuendesha matamasha, maonesho na maadhisho mengine yatakayojitokeza; kutoa elimu kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kwa kushirikiana na wadau kuratibu na kuendesha Programu ya Uzalendo (Nchi Yangu Kwanza). Programu hii iliyanza mwaka 2017 inalenga kuhamasisha wananchi, hasa vijana kuipenda na kuitumikia nchi yao Tanzania.

Aidha, Wizara itaandaa makala (*documentary*) ya kutangaza kazi za Sanaa kama vile kazi za uchongaji, kazi za ubunifu wa mavazi, michoro, ngoma, muziki na maigizo zinazozalishwa hapa nchini kwa lengo la kuisambaza katika tovuti za Serikali na Balozi za Tanzania kwenye nchi mbalimbali ikiwa ni mkakati wa kuzitangaza kazi hizo katika masoko ya

kitaifa na kimataifa. Pia, Wizara itaratibu maandalizi na ushiriki wa Tanzania katika Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST); na kusimamia ujenzi wa Sanamu ya Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika, Addis Ababa, Ethiopia.

### **5.3.1 BODI YA FILAMU TANZANIA**

**151. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu yatakayoteklezwa ni pamoja na kuimarisha mazingira ya wadau wa filamu kushiriki katika kazi za filamu ikiwemo kuwajengea uwezo; kuratibu uendeshaji wa matukio, matamasha na tuzo za filamu na kuwawezesha wadau hao kupata mikopo/mitaji kuititia mfuko wa Utamaduni na Sanaa na wadhamini wengine. Vilevile, Bodi itaendelea na jukumu la kuhakiki, kupanga katika madaraja na kutoa vibali vya uoneshaji wa filamu kwa umma; kutoa vibali vya utayarishaji wa filamu na Michezo ya Kuigiza, kubaini na kutangaza maeneo ya upigaji picha za filamu. Lengo la kubaini na kutangaza maeneo hayo ya upigaji picha ni kuvutia makampuni ya kutengeneza filamu kutoka nje ya nchi ili yaje kutengeneza filamu katika maeneo yetu, hatua ambayo itaiongezea nchi mapato kutohana na tozo za vibali zitakazotozwa kwa makampuni hayo, pamoja na kuongeza ajira kwa wataalam na wacheza filamu wa ndani watakaotumiwa na makampuni hayo wakati wa uandaaji wa filamu hizo.

Majukumu mengine yatakayoteklezwa ni kufanya operesheni ili kudhibiti uendeshaji wa shughuli za filamu usiozingatia Sheria na Taratibu na kutoa elimu ya masuala ya kisheria. Aidha, Bodi itatoa ithibati na leseni za uendeshaji wa shughuli za filamu pamoja na vitambulisho kwa wadau wa filamu na kuimarisha elimu kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa na Bodi.

### **5.3.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**

**152. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu yatakayoteklezwa ni pamoja na kuendelea na zoezi la urasimishaji wa Sekta ya Sanaa nchini; kuimarisha mifumo ya kuhudumia wadau

pamoja na mifumo ya huduma za dawati la msaada wa kisheria kwa wasanii na wadau wa Sanaa nchini. Aidha, Baraza litaimarisha ukusanyaaji wa mapato kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaopanua wigo kwa kuwafikia wadau wa maeneo yote ya Nchi wanaohitaji kupata huduma za usajili na vibali, pamoja na kufanya tafiti za vyanzo vipya vya mapato sambamba na zoezi la uhuishwaji wa Kanuni za Baraza za mwaka 2018. Pia, Baraza litaimarisha utoaji wa taarifa na ushawishi kwa umma kuhusu masuala ya Sanaa.

Vilevile, Baraza limejipanga kutoa vitambulisho kwa wasanii na kuondoa utumiaji wa vyeti ambavyo vinatolewa kwa sasa. Vitambulisho hivyo vitawarahisishia wasanii kupata huduma mbalimbali kama vile Bima za afya na huduma za kifedha kwani vitambulisho hivyo vitaunganishwa na mifumo ya taasisi zingine.

### **5.3.3 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)**

**153. *Mheshimiwa Spika***, majukumu yatakayotekelizwa ni pamoja na:- kukamilisha marekebisho ya Kanuni ya Maonesho kwa Umma, Utangazaji na Mawasiliano kwa Umma; kuweka mfumo wa kisheria utakaowezesha kutozwa kwa tozo ya *Blank Tape Remuneration/Levy*; kukamilisha mfumo wa kufuatilia matumizi ya kazi za sanaa hususan muziki na filamu katika vyombo vya habari na kukamilisha mfumo wa kielekroniki (*online platform*) kwa ajili ya kusambaza kazi za wasanii. Majukumu mengine ni kuendelea kusajili wabunifu na kazi zao kwa njia ya mtandao; kutoa elimu ya hakimiliki kwa kutumia vyombo vya habari, semina na mikutano; kuboresha mfumo wa usajili wa wabunifu; kukusanya mirabaha na kuigawa kwa wabunifu na kufanya operesheni dhidi ya wanaokiuka Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999.

### **5.3.4 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)**

**154. *Mheshimiwa Spika***, TaSUBa itaendelea kudahili na kutoa mafunzo ya sanaa na utamaduni; kusajili mitaala mipya

NACTE ambayo ni Kiswahili, Sanaa za Ufundı, Tamthilia na Ngoma na kuendesha Tamasha la 40 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Majukumu mengine ni kukarabati miundombinu ya Taasisi na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, Taasisi itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya Chuo ili kuwafikia vijana wengi zaidi wenye vipaji na kiu ya kupata mafunzo ya sanaa.

Taasisi imejidhatiti kuwafikia vijana hao kwa kuimarisha kozi fupi fupi ambazo zitatolewa kwa kushirikiana na wadau wengine nchini yakiwemo mashirikisho yote ya sanaa, vyama vya wasanii, BASATA, Bodi ya Filamu, COSOTA na maafisa utamaduni. Mathalan, tayari Taasisi imeingia makubaliano na taasisi ya Tanzania House of Talent (THT) ya ushirikiano kwenye eneo la utoaji wa mafunzo ya muda mfupi ya muziki kwa vijana wenye vipaji.

Pia, TaSUBa imepanga kutuma wakufunzi wake katika halmashauri za miji, majiji, manispaa na wilaya mbalimbali ili kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya sanaa mbalimbali kadri ya mahitaji ya wasanii wenyewe. Mpango huu utasaidia kuwafikia vijana wengi wenye vipaji kwa gharama nafuu ikilinganishwa kama wangelifuata mafunzo hayo kwenye Taasisi, Bagamoyo.

#### **5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO**

**155. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaratibu mashindano ya Taifa Cup kwa michezo sita ya kipaumbele ambayo ni Soka, Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu, Ngumi na Riadha ambayo itafanyika mwezi Desemba 2021 ili kuibua vipaji vya michezo kwa vijana; kuanzisha Tamasha Maalumu la Michezo ya wanawake ili kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michezo na kuibua vipaji vyao na kuzindua Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Michezo na kusimamia utekelezaji wake. Vilevile, Wizara itaratibu utungwaji wa Sheria ya Kusimamia Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni na kuratibu na kugharimia ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo ya Olimpiki Tokyo, Japan.

Majukumu mengine ni kusimamia uendeshaji wa viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru.

**156. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara itaendelea kuzisimamia Shule maalumu za michezo zitakazotengwa kwa ajili ya michezo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na kusimamia ufundishwaji wa somo la michezo mashulenii ikiwa ni pamoja na Tahsusizi zilizoanzishwa ili kukuza taaluma ya michezo nchini. Fauka ya hayo, michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA itaendelea kuratibiwa kwa kushirikiana na Ofisi ya RaistAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na kuratibu Siku Maalumu ya Michezo Kitaifa ikiwa ni hatua pia ya kuhamasisha michezo kwa jamii.

**157. *Mheshimiwa Spika*,** majukumu mengine yatakayotekelawa ni kuendelea kutoa mafunzo ya michezo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na kusimamia ujenzi wa madarasa, mabweni na kituo cha ukuzaji vipaji vya michezo (*sports academy*) katika chuo hicho. Lengo la kuanzisha Kituo hiki ni kukuza vipaji vya michezo ambapo vijana watakuwa wanachaguliwa kutoka katika maeneo mbalimbali nchini na kupelekwa katika kituo hicho ili kuendelezwa vipaji vyao vya michezo kupitia watalaam wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hatua hii itasaidia kuimarisha timu zetu za Taifa kwa kupata wachezaji wenye vipaji na weledi na hivyo kuongeza ajira kwa vijana wetu wanaocheza michezo ya kulipwa katika nchi mbalimbali.

Aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kunakuwepo na vyanzo madhubuti vya fedha za kuendeleza michezo, ambapo itaendelea na majadiliano na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuwezesha kuendeshwa kwa Bahati Nasibu ya Taifa (*National Lottery*) na kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha sehemu ya mapato yatokanayo na Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Michezo (*Sports Betting*) kutumika kugharamia maendeleo ya michezo.

#### **5.4.1 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)**

**158. *Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika*,** BMT itaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za michezo kwa kusajili vyama, vilabu, vituo, wakuzaji na Taasisi za michezo; kutoa mafunzo ya utawala bora katika michezo kwa viongozi wa vyama vya michezo; kutoa elimu ya michezo kwa walimu wa michezo, kuratibu na kugharimia maandalizi na ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano ya Kimataifa kwa kushirikiana na wadau. Baraza litatoa pia vibali vya ushiriki wa timu na wachezaji katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aidha, program za kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo zitatekelezwa ambapo BMT kwa kushirikiana na wadau kama vile JICA litaendesha Tamasha la michezo ya wanawake katika michezo mbalimbali na kutoa mafunzo ya Uongozi na Utawala katika Michezo kwa wanawake ili kuwajengea uwezo wa kushika nafasi mbalimbali katika Uongozi wa Michezo.

#### **5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA**

**159. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara itaendelea kuweka mazingira bora ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi muhimu; kuajiri na kupandisha vyeo watumishi na kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuimarisha uwezo wao kiutendaji. Aidha, ikiwa ni hatua ya kuimairsha ushiriki wa watumishi katika kupanga na kutekeleza majukumu ya Wizara, kutafanyika mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi na pia watumishi watawezeshwu kushiriki katika matukio mbalimbali ya kitaifa, ikiwa ni pamoja na Sherehe za Mei Mosi, Siku ya Wanawake Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Michezo ya SHIMIWI.

### **6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

#### **6.1 MAPATO**

**160. *Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika*,** mwaka 2021/22 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia

Tisa Sitini (Sh.960,000,000) kupitia Idara za HabariMAELEZO na Maendeleo ya Michezo. Vyanzo vyatapato hayo ni pamoja na viingilio katika matukio ya michezo yanayofanya katika viwanja vyatapato Benjamin Mkapa na Uhuru, leseni za usajili wa magazeti na ada za vitambulisho kwa wanahabari. Aidha, kwa upande wa Taasisi nane (8) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokadiriwa kukusanya na Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Nane Sitini na Sita, Mia Nne Arobaini na Nne Elfu (Sh.33,866,444,000).

Kiambatisho Na. 7 ni mchanganuo wa tapato yanayotarajiwa kukusanya na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2021/22. *Kiambatisho Na. 7* ni mchanganuo wa tapato yanayotarajiwa kukusanya na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2021/22.

## **6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO**

**161. *Mheshimiwa Spika*,** Mwaka 2021/22 Wizara imetengewa bajeti ya **Shilingi Bilioni Hamsini na Nne, Milioni Mia Saba Arobaini na Moja, Mia Nane na Mbili Elfu (Sh.54,741,802,000)**. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Moja Arobaini na Sita, Mia Sita Hamsini na Tatu Elfu (Sh.19,146,653,000)**, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Nane Themanini, Mia Moja Arobaini na Tisa Elfu (Sh.14,880,149,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Saba Kumi na Tano (Sh.20,715,000,000)**. *Kiambatisho Na. 8* kinaonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

## **7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2021/22**

**162. *Mheshimiwa Spika*,** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2021/22 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22 ya jumla ya **Shilingi Bilioni Hamsini na Nne, Milioni Mia Saba Arobaini na Moja, Mia Nane na Mbili Elfu (Sh.54,741,802,000)** ambapo **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni**

**Mia Moja Arobaini na Moja, Mia Sita Hamsini na Tatu Elfu (Sh.19,146,653,000) ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi Bilioni Kumi na Nne Milioni Mia Nane Themanini, Mia Moja Arobaini na Tisa Elfu (Sh.14,880,149,000) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Saba Kumi na Tano (Sh.20,715,000,000).**

## **8.0 MWISHO NA SHUKURANI**

**163.** *Mheshimiwa Spika*, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2020/21 yametokana pia na ushirikiano wa wadau mbalimbali. Nitoe shukrani zangu za dhati kwa wanahabari kwa kuendelea kuwawezesha wananchi kupata haki yao ya kikatiba ya kupata habari. Aidha, nilipongeze Baraza la Habari Tanzania (MCT) na wanachama wake ikiwemo Jukwaa la Wahariri, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Press Clubs, Vyuo vya Kati vya Uandishi wa Habari, Magazeti, Redio, Telesheni na Taasisi za kihabari kama Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira, kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuendeleza Sekta ya Habari nchini.

Niwashukuru wasanii kwa kuendelea kuitangaza vyema sanaa ya Tanzania kitaifa na kimataifa na pia timu na wanamichezo wote waliolilettea Taifa letu sifa kimataifa. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo ya Taifa letu na watu wake.

**164.** *Mheshimiwa Spika*, mwisho chambilecho wahenga, "Jifya moja haliinjiki chungu na "Umoja ni nguvu". Niwashukuru Wadau wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wa ndani ambao kimsingi ni wengi. Kwa upande wa wadau wa nje, nazishukuru nchi za China, Japan, Korea Kusini, Uswisi na Ujeruman, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA).

**165.** *Mheshimiwa Spika*, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**VIAMBATISHO**

**Kiambatisho Na. 1**

**VYOMBO VYA HABARI (MAGAZETI, REDIO NA TELEVISHENI) VILIVYOSAJILIWA MWAKA 2010 – MEI 2021**

Mwaka	Idadi ya Magazeti na Majarida	Idadi ya Vituo vya Redio	Idadi ya Vituo vya Televisheni
2010	8	14	1
2011	41	12	-
2012	29	12	-
2013	36	4	-
2014	23	8	3
2015	39	22	1
2016	26	23	6
2017	161	6	3
2018	42	8	3
2019	23	23	8
2020	24	8	2

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kiambatisho Na. 2

### VIBALI VYA UTAYARISHAJI WA FILAMU NA PICHA JONGEVU VILIVYOTOLEWA MWAKA 2011/12 – 2020/21

Mwaka	Kampuni za Kitanzania	Kampuni za Wageni	Jumla
2011/12	21	84	105
2012/13	30	123	153
2013/14	33	125	158
2014/15	36	133	169
2015/16	31	137	168
2016/17	30	123	153
2017/18	46	137	183
2018/19	38	133	171
2019/20	24	84	108
2020/21 <sup>1</sup>	46	62	108

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania

---

<sup>1</sup>Kuanzia Julai, 2020 hadi Mei, 2021

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Kiambatisho Na. 3**

**FILAMU ZILIZOHAKIKIWA NA KUPEWA VIBALI MWAKA 2011/12 – 2020/21**

Mwaka	Filamu za Kitanzania	Filamu za Kigeni	Jumla kwa Mwaka
2011/12	206	12	218
2012/13	414	12	426
2013/14	1,181	58	1,239
2014/15	1,339	61	1,400
2015/16	653	114	767
2016/17	706	92	798
2017/18	762	148	910
2018/19	832	158	990
2019/20	686	119	805
2020/21 <sup>2</sup>	1,388	68	1,456

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania

---

<sup>2</sup> Kuanzia Julai, 2020 hadi Mei, 2021

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Kiambatisho Na. 4**

**WANAFUNZI WALIOHITIMU ASTASHAHADA NA STASHAHADA TaSUBa MWAKA 2010 - 2021**

Mwaka	Wanaume	Wanawake	Jumla	% Wanaume	% Wanawake
2010	28	14	42	67	33
2011	27	8	35	77	23
2012	25	10	35	71	29
2013	32	12	44	73	27
2014	23	12	35	66	34
2015	37	23	60	62	38
2016	31	19	50	62	38
2017	38	6	44	86	14
2018	96	22	118	81	19
2019	112	35	147	76	24
2020	157	44	201	78	22
2021	48	19	67	72	28

**Chanzo:** Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kiambatisho Na. 5

VYAMA, VILABU, VITUO VYA MICHEZO NA WAKUZAJI/MAWAKALA WA MICHEZO WALIOSAJILIWA KUANZIA MWAKA 2010 – 2021

Mwaka	Vilabu vya Michezo	Vyama vya Michezo	Vituo vya Michezo	Wakuzaji/ Mawakala wa Michezo
2010	272	9	-	-
2011	168	5	-	-
2012	339	-	-	-
2013	285	37	12	-
2014	464	17	7	-
2015	224	15	12	-
2016	331	9	15	-
2017	288	29	13	14
2018	212	23	18	29
2019	231	18	21	19
2020	110	12	5	26
2021 <sup>3</sup>	23	2	3	14

**Chanzo:** Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Michezo (BMT)

---

<sup>3</sup>Julai 2020- Mei, 2021

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Kiambatisho Na. 6**

**WANAFUNZI WALIOSAJILIWA KATIKA CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA 2010 - 2020**

Mwaka	Wanaume	Wanawake	Jumla
2010	NA	NA	NA
2011	25	14	39
2012	NA	NA	NA
2013	26	14	40
2014	NA	NA	NA
2015	29	24	53
2016	31	15	46
2017	94	31	125
2018	110	31	141
2019	91	22	113
2020	70	26	96

**Chanzo:** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Kiambatisho Na. 7**

**MADUHULI YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2021/22**

**a) Maduhuli Yatakayokusanywa na Wizara**

**i) Idara ya Maendeleo ya Michezo**

<b>Kijifungu</b>	<b>Maelezo</b>	<b>Makadirio ya Mapato Mwaka 2020/21 (Sh.)</b>	<b>Makadirio ya Mapato Mwaka 2021/22 (Sh.)</b>
140259	Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Benjamin Mkapa)	439,995,000	470,200,000
140315	Ada za Mafunzo	270,000,000	312,000,000
140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	1,000
140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	1,000
<b>Jumla Ndogo</b>		<b>709,997,000</b>	<b>782,202,000</b>
<b>ii) Idara ya Habari</b>			
140387	Vitambulisho vya Waandishi wa Habari	24,500,000	20,000,000
140202	Machapisho ya picha, mabango na majarida	15,500,000	15,500,000
140265	Ukumbi wa Mikutano	1,000	1,000
140264	Usajili wa Magazeti	55,000,000	42,295,000
140310	Ada ya mwaka ya Magazeti	155,000,000	100,000,000

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	1,000
140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	1,000
<b>Jumla Ndogo</b>		<b>250,003,000</b>	<b>177,798,000</b>
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>960,000,000</b>	<b>960,000,000</b>

**b)Maduhuli Yatakayokusanywa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

<b>Na</b>	<b>Jina la Taasisi</b>	<b>Makadirio ya Mapato 2020/21 (Sh.)</b>	<b>Makadirio ya Mapato 2021/22 (Sh.)</b>
1.	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	13,792,639,000	14,044,500,000
2.	Kampuni ya Magazeti ya Tanzania (TSN)	22,684,519,000	14,343,823,000
3.	Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)	398,339,000	558,630,000
4.	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)	500,000,000	700,000,000
5.	Bodi ya Filamu Tanzania	1,313,574,000	1,413,572,000
6.	Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	1,382,193,000	1,480,919,000
7.	Baraza la Michezo la Taifa (BMT)	100,000,000	300,000,000
8.	Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA)	523,220,000	1,025,000,000
	<b>JUMLA</b>	<b>40,694,484,000</b>	<b>33,866,444,000</b>

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Kiambatisho Na. 8**

**MGAWANYO WA BAJETI YA WIZARA YA MWAKA 2021/22 KWA IDARA NA VITENGO, TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA NA MIRADI YA MAENDELEO**

**a)Mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo**

Kifungu	Idara/Kitengo	Makisio ya Bajeti Mwaka 2021/22		
		Mishahara (PE) (Sh.)	Matumizi Mengineyo (Sh.)	Jumla (Sh.)
1001	Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu	818,312,000	4,142,223,000	4,960,535,000
1002	Fedha na Uhasibu	235,366,000	81,594,000	316,960,000
1003	Sera na Mipango	258,628,000	174,688,000	433,316,000
1004	Mawasiliano Serikalini	125,897,000	117,356,000	243,253,000
1005	Ununuzi na Ugavi	147,160,000	74,080,000	221,240,000
1006	Ukaguzi wa Ndani	19,920,000	65,550,000	85,470,000
1007	TEHAMA	93,840,000	179,578,000	273,418,000
1008	Huduma za Sheria	61,368,000	22,650,000	84,018,000
6001	Maendeleo ya Utamaduni	203,412,000	379,717,000	583,129,000
6004	Maendeleo ya Michezo	711,495,000	942,897,000	1,654,392,000
6005	Maendeleo ya Sanaa	225,001,000	529,251,000	754,252,000

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

7003	Habari	640,929,000	1,369,195,000	2,010,124,000
<b>JUMLA</b>		<b>3,541,328,000</b>	<b>8,078,779,000</b>	<b>11,620,107,000</b>

**b) Mgawanyo wa Bajeti kwa Taasisi Zilizo Chini ya Wizara**

Jina la Taasisi	Makisio ya Bajeti Mwaka 2021/22		
	Mishahara (PE) (Sh.)	Matumizi Mengineyo (Sh.)	Jumla (Sh.)
<b>6001-26311266</b> Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)	588,828,000	172,289,000	761,117,000
<b>6005-26311352</b> Bodi ya Filamu Tanzania	602,080,000	128,717,000	730,797,000
<b>6005- 26311267</b> Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	868,800,000	105,497,000	974,297,000
<b>6005-26311234</b> Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA)	423,732,000	1,500,000,000	1,923,732,000
<b>6005 – 26311267</b> Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)	1,112,300,000	122,289,000	1,234,589,000
<b>6004 – 26311273</b> Baraza la Michezo la Taifa (BMTL)	476,079,000	422,289,000	898,368,000
<b>6004 – 26321387</b> Chuo cha Maendeleo ya Michezo-Malya	-	150,289,000	150,289,000

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

<b>7003 – 25110113</b> Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	8,564,346,000	4,200,000,000	12,764,346,000
<b>7003 – 26311487</b> Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)	2,969,160,000		2,969,160,000
<b>Jumla</b>	<b>15,605,325,000</b>	<b>6,801,370,000</b>	<b>22,406,695,000</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>19,146,653,000</b>	<b>14,880,149,000</b>	<b>34,026,802,000</b>

### c) Miradi ya Maendeleo

<b>Na.</b>	<b>Jina la Mradi</b>	<b>Makisio ya Bajeti 2021/22</b>
<b>Idara ya Maendeleo ya Utamaduni</b>		
1.	6293 – Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika	515,000,000
2.	6502 – Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania	1,500,000,000
<b>Jumla ya Idara</b>		
<b>Idara ya Maendeleo ya Michezo</b>		
3.	6385 – Ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya	1,300,000,000
4.	6503 – Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma	1,000,000
5.	6523 – Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam	648,000,000
6.	6504 – Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi	10,500,000,000
<b>Jumla ya Idara</b>		
<b>Idara ya Maendeleo ya Sanaa</b>		
7.	4353 – Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo	250,000,000

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

<b>Jumla ya Idara</b>		<b>250,000,000</b>
<b>Idara ya Habari</b>		
8.	4279 – Upanuzi wa Usikivu TBC	5,000,000,000
9.	6505 – Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji	1,000,000
10.	6567 – Habari kwa Umma	1,000,000,000
<b>Jumla ya Idara</b>		<b>6,001,000,000</b>
<b>JUMLA KUU YA WIZARA</b>		<b>20,715,000,000</b>

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako nzuri, ahsante sana. (*Makofii*)

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kamamba, karibu tafadhali.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni...

**SPIKA:** Mwenyekiti akimaliza hotuba yake, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali atafuatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** ...pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard*.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ni maelezo kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Upuzi wa Usikivu wa *TBC* (*Expansion of TBC Coverage*) ambao kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa kiasi chote cha fedha yaani jumla ya shilingi bilioni tano, sawa na asilimia 100 kilipokelewa na *TBC*, utekelezaji wa miradi iliyopangwa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya kijinsia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, uwiano wa wanawake na wanaume katika ngazi za uongozi umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, pili, kuna ukosefu wa miundombinu kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa jengo lenye ghorofa moja na halikuwa na *lift*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zote za Mradi wa Usikivu nchini kiasi cha shilingi bilioni tano. Aidha, inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika kwa wakati ili usaidie katika kuongeza usikivu nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo:-

(a) *TBC* iendelee kuboresha maudhui ili yaendane na mahitaji ya walaji;

(b) *TBC* ishirikiane na Balozi zetu ili *channel* ya *TBC* iweze kuonekana nje ya nchi;

(c) Chaneli ya utalii ya *Safari Channel* iboreshwe ili kuongeza vipindi vya lugha mbalimbali ili kuvutia watalii ambao wanatoka maeneo mbalimbali duniani;

(d) *TBC* ipewe haki na uwezo kurusha mechi za mpira ndani na nje ya nchi ili wananchi waweze kunufaika na chombo chao cha umma badala ya kutegemea vyombo binafsi;

(e) *TBC* iwezeshwe na Serikali kupata haki za kutangaza ligi za ndani na nje ya nchi yakiwemo mashindano ya UMITASHUMTA, UMISETA na kadhalika maana huko ndiko kunakopatikana vipaji;

(f) *TBC* iboreshe ofisi za kanda ili ziendane na mabadiliko makubwayaliyopo kwa sasa; na

(g) *TBC* ihakikishe inafanya kazi kibiashara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021; utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; kwa kiasi Wizara imetekeleza maoni ya Kamati. Aidha, kwa maoni ambayo hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati itaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/2021 makadirio ya Wizara yalikuwa ni kukusanya shilingi billioni 41.6 kutoka vyanzo mbalimbali viliwyopo chini ya Wizara. Kufikia Februari, 2021 makusanyo yalikuwa shilingi billioni 15.3 sawa na asilimia 36.9 ya lengo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makusanyo madogo zaidi ya asilimia 3.6 ni kutoka kwenye usajili wa magazeti. Kamati ilihoji sababu ya makusanyo hayo madogo na ilielezwa kuwa ni kutohana na wateja wachache walijitokeza kusajili na kuhuisha leseni za mwaka za magazeti. Si hivyo tu, pia ukuaji na ufanisi wa teknolojia ya mawasiliano ya kielektroniki katika kupashana habari na kutangaza biashara kumeathiri soko la bidhaa za magazeti na majarida.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia kuwa Kampuni ya Magazeti ya Tanzania (*TSN*) na Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) makusayo yao kufikia Februari yaliikuwa chini ya asilimia 30 ya lengo. Kamati ilihoji na kuelezwu yafuatayo:-

(a) Kwa upande wa *TSN* ni kutokana na uchakavu wa mtambo uliopo na kutopatikana kwa mtambo mpya ambao iliutegemea; na

(b) Kwa upande wa BASATA ni kutokana na kutozinduliwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Vibali ambao ulichelewa kutokana na zoezi la upembuzi yakinifu wa mahitaji ya mfumo (*system requirement specifications*) kuchukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa mwaka 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 40.4 zenye kujumuisha mishahara asilimia 52, matumizi mengineyo (*OC*) asilimia 28 na miradi ya maendeleo asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, kufikia Februari, 2021 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 24.3, sawa na asilimia 60.1 ya bajeti iliyoidhinishwa. Mishahara ilipokelewa kwa asilimia 53.5, matumizi mengineyo (*OC*) 66.2 na miradi ya maendeleo asilimia 68.3, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara ya watumishi ni asilimia 53.5 wakati ilitarajiwa kuwa kufikia Februari iwe asilimia 66. Kamati ilihoji na kuelezwu kuwa mishahara iliyotoka haikuzingatia upandishwaji wa vyeo uliokusudiwa pamoja na ajira mpya zilizopangwa kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa rai wa Serikali kuhakikisha inatoa fedha hizi za Wizara ili watumishi wanaostahili kupandishwa vyeo waweze kupandishwa na

ajira mpya zitolewe ili kuondoa changamoto ya uhaba wa watumishi ambayo Wizara na taasisi zake inakumbana nayo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; sehemu ya tatu, ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 34.8 kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 3.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya mwaka 2021/2022 yamepungua kwa asilimia 16.35 ambapo upungufu ni zaidi katika vyanzo vya taasisi na hususan katika Shirika la Magazeti (*TSN*) kwa 36.77.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu za kushuka kwa makadirio ya makusanyo ya *TSN* na ilielezwa ni kutokana uchakavu wa mitambo uliopo pamoja na kutopatikana kwa mtambo mpya wenye gharama ya shilingi bilioni 16. Kamati ilielezwa kuwa Wizara inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha za kununua mtambo mpya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ikiwa ni pamoja na kufuatilia madeni ya takribani shilingi bilioni tisa ambayo *TSN* inazidai taasisi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusositiza Serikali kuhakikisha inahakiki madeni ya taasisi za umma ili yalipwe kusaidia kununua mitambo mipya.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, uchambuzi umebaini kuwa makadirio ya makusanyo ya Baraza la Sanaa (BASATA) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yameongezeka kwa asilimia 7.14 licha ya kuwa ukusanyaji wa mwaka 2020/2021 kufikia Februari ulikuwa asilimia 28.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu ya ongezeko hilo na ilielezwa kuwa ni kutokana na matarajio ya kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa usajili wa vibali. Ni imani ya Kamati kuwa mfumo huu utaanza kutumika na lengo hili la makusanyo litafikiwa. Kielelezo Na. 4 kinaonesha

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ulinganisho wa maduhuli ya Fungu 96 kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 54.7; mishahara ya watumishi asilimia 35, matumizi mengineyo asilimia 27 na miradi ya maendeleo na asilimia 38 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 35.2 kutoka shilingi bilioni 40 hadi shilingi bilioni 54.7. Ongezeko zaidi linaonekana katika fedha za matumizi mengineyo kwa asilimia 30 na miradi ya maendeleo kwa asilimia 157.2 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo limechangiwa na bajeti ya ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzika wananchi kiasi cha shilingi bilioni 10.5. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mazoezi ambavyo pia kwa kiasi kikubwa vitasaidia katika kupunguza magonjwa yasiyoambukiza ambayo yameendelea kuwa chanzo kikubwa cha vifo nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, ujenzi huu ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 aya ya 243(c) inayoeleza azma ya kuboresha michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi. Mwanazuoni Robin Sharma amewahi kusema; *If you don't make time for exercise, you will probably have to make time for illness.*

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kulinganisha bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa (Kielelezo Na. 7) na imebaini yafuatayo:-

- (a) Wakati bajeti ya matumizi ya mengineyo (*OC*) ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 5.43, bajeti ya matumizi mengineyo ya Fungu 96 imeongezeka kwa asilimia 30;
- (b) Wakati bajeti ya maendeleo ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 2.76, bajeti ya maendeleo ya Fungu 96 imeongezeka kwa asilimia 157;
- (c) Wakati bajeti ya mishahara ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia tano, bajeti ya mishahara ya Fungu 96 imepungua kwa asilimia tisa;
- (d) Kwa ujumla wakati bajeti ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa asilimia 3.95, bajeti ya Fungu 96 imeongezeka kwa asilimia 35.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa pamoja na ongezeko dogo la bajeti ya Taifa, bajeti ya Wizara hii imepewa kipaumbele zaidi. Hata hivyo, tunaona suala la mishahara halijapewa uzito kutokana na kutokupandishwa vyeo kwa watumishi na pia kutokuwa na ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri, mapendekezo ya Kamati; maoni ya jumla:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli; matarajio ya ukusanyaji wa maduhuli yalikuwa kufikia Februari ukusanyaji uwe umefikia asilimia 66, lakini hali halisi ya ukusanyaji ni asilimia 36.87. Kamati inashauri Wizara kuboresha mifumo ya ukusanyaji na kuhakikisha inafikia malengo iliyojiwekea.

(b) Mheshimiwa Spika, sanaa na burudani; Kamati imebaini kuwa sekta hii ina changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika ukuaji, Kamati inashauri yafuatayo; moja, mifumo ya ukusanyaji wa mapato iboreshwe ili kuvutia watumiaji, lakini pia kuongeza mapato ya nchi; pili, kutokana na muingiliano wa shughuli za Taasisi ya *BASATA*, *COSOTA*, Bodi ya Filamu na *TCRA*, ni vyema Wizara ikaweka *One Stop*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Centre ili kurahisisha utoaji wa huduma na hivyo kuchochea ukusanyaji wa mapato.

(c) Mheshimiwa Spika, michezo; mafanikio katika michezo yanachochewa na vitu mbalimbali. Mwanamiereka kutoka Marekani Dan Gable amewahi kusema; " *Gold medals are not really made of gold. They are made of sweat, determination and a hard to find.*" Nchi yetu ikitaka kufanikiwa katika michezo haina budi kuwekeza katika michezo ikiwa ni pamoja na moja, kuandaa mkakati wa kubadili na kuboresha mfumo wa michezo nchini ili iendane na hali halisi ilivyo kwa sasa kwa kuwa michezo zama hizi ni ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhakikisha kunakuwepo viwanja na vifaa bora vyta kutosha kwa ajili ya michezo mbalimbali; tatu, kuanzisha *sport academy* ili vijana wenye vipaji waweze kuibuliwa na kufundishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Utangazaji la Taifa yaani *TBC*:

(a) Serikali iongeze bajeti ya miradi ya maendeleo ya *TBC* ili iweze kusaidia usikivu ili ufikie asilimia 100 hasa maeneo ya vijijini na pembezoni kwani kwa sasa usikivu ni asilimia 63 tu;

(b) Mikakati iwekwe ili wadeni wa *TBC* waweze kulipa madeni yao, aidha, madeni yasiyolipika ni vyema mchakato wa kuyafuta ukafuatwa;

(c) *TBC* iwe na ubunifu wa kuweka burudani na michezo ambayo itasaidia kuvutia watazamaji na wasikilizaji ili baada ya Taarifa ya Habari waendelee kuangalia channeli hiyo ya Taifa;

(d) *TBC* iweke mikakati kuweza kujitangaza duniani kote ili isaidie pia kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA); itakumbukwa kuwa lugha ya Kiswahili imechaguliwa kuwa ni moja ya lugha za mawasiliano katika nchi za Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara yaani SADC na nchi mbalimbali kama Afrika ya Kusini zimeanza kutumia lugha ya Kiswahili. Kutokana na umuhimu wa lugha hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) BAKITA iweke mkakati wa makusudi wa kuzalisha wakalimanis wengi zaidi wenye uwezo wa kufahamu lugha zaidi ya moja kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa vyao;

(b) Ili kufanikiwa kubidhaisha Kiswahili, Serikali ianzishe Dawati la Kiswahili katika kila Ubalozi kama nchi za wenzetu ikiwemo China walivyofanya. Aidha, tutumie *exchange program* na nchi nyingine ili kubidhaisha Kiswahili;

(c) Serikali iweke mkakati wa kuunganisha yaani *link* ya Kiswahili na utalii.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa Tanzania yaani BASATA; kutokana na umuhimu wa Baraza la Sanaa katika sekta ya sanaa nchini, Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) BASATA ianzes kutoa mafunzo kwa wasanii ili waweze kuwa na uelewa wa kutosha wa kanuni ili kupunguza makosa ya kufungiwa;

(b) BASATA iweke mikakati itakayowezesha kuongeza mapato kutokana na fursa zilizopo;

(c) Uanzishwe mfumo wa kielektroniki utakaowezesha wasanii kulipia vibali vya safari bila ya kwenda kwenye Ofisi za BASATA ili kuepuka baadhi yao kuzuiliwa kusafiri au kulazimika kurudi nchini kuomba vibali hivyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Filamu Tanzania; filamu zina nafasi kubwa katika kuchochea utalii na hivyo kuchangia katika ukuaji wa Pato la Taifa. Kwa mujibu wa Utafiti wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mwaka 2018 wa *Travel Competitive Intelligence*, watalii wa kimataifa milioni 80 Ulimwenguni walitembelea sehemu kama *La La Land, Narcos, Pirates of the Caribbean, Buddies in India, Manchester by the Sea* mnamo mwaka 2017 walitokana na ushawishi waliouona kwenye filamu.

Mheshimiwa Spika, aidha, *United Nations World Tourism Organization Awarded Research Agency* inataja maeneo ambayo yamekuwa kivutio cha watalii kutokana na kuyaona kupitia filamu kuwa ni Los Angeles, London, Scotland, Columbia, Florence, New-York, Dubai, Paris, Berlin, New-Zealand kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8.

Mheshimiwa Spika, kamati inashauri Bodi ya Filamu iweke mfumo utakaowezesha filamu zetu kuandaliwa au kutengenezwa katika maeneo ambayo yatavutia watalii na hatimaye kuchangia katika ukualji wa pato la Taifa na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo Tanzania yaani BMT; mkakati uwekwe utakaowezesha kuboresha viwanja vyaa michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuingia ubia na sekta binafsi.

(b) Wizara ionne namna ya kutoa hamasa kwa Maafisa Michezo kuanzia ngazi ya kata hadi mikoa ili kuweza kusimamia vyema jukumu la kukuza michezo katika maeneo yao;

(c) Vibali vyaa usajili wa wachezaji wa kigeni vitolewe ili kuongeza pato la Taifa;

(d) Wizara iweke mkakati wa kusaidia vilabu nchini viweze kuijendesha badala ya kuendelea kutegemea *gate collections* au wawekezaji binafsi;

(e) BMT isimamie kila klabu iweze kuwa na mtaalam wa lishe atakayesaidia kukuza afya za wachezaji wetu ili waweze kushiriki vizuri kwenye Michezo na kuleta matokeo chanya.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania (*TSN*); Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Kutokana na magazeti kuchelewa kufika kwa wakati hasa maeneo ya vijiji, *TSN* iweke mkakati wa kuondoa changamoto hii;

(b) *TSN* wawe wabunifu ili waweze kushindana katika karne hii ya kiteknolojia;

(c) Serikali iiwezeshe *TSN* kupata kiasi cha shilingi bilioni 16 ili iweze kununua mtambo mpya wa kisasa wa uchapaji ambao utasaidia katika kufanya kazi kibiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (*COSOTA*); Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Kutokana na uwepo wa vyanzo vingi vya mapato ambavyo havijatumika vizuri na hivyo kusababisha upotetu wa mapato na hususan katika biashara ya mtandao (*online businesses*), ni wakati sasa *COSOTA* ianze kutumia fursa za mapato ili nchi na wasanii waweze kunufaika;

(b) Mkakati uwekwe wa kuzuia na kudhibiti uharamia kwa kazi za wasanii nchini. Aidha, faini kubwa zitolewe kwa watakaokamatwa kuibia kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*); adhabu zitolewe, ziangaliwe ili zisiumize sana wasanii pia kulikosesha Taifa mapato;

(b) Mkakati uwekwe wa kuwa na *aggregator* wa *YouTube* nchini ili kuwezesha Serikali kupata mapato ambayo imekuwa ikiyakosa kutokana na wasanii kutumia *aggregator* wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa mara zote na hivyo kurahisisha utendaji na wamekuwa wakishiriki vyema katika shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuchambua bajeti ya Wizara hii ya Fungu 96 na maandalizi ya taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa na aliyekuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa sasa Mheshimiwa Pauline Gekul kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati. Pamoja nao, nawashukuru watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbas na Naibu Katibu Mkuu ndugu Dkt. Ally Possi kwa ushirikiano waliyoipa Kamati ikiwa ni pamoja na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano. Aidha, namshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano alioutoa kwa Kamati. Aidha, nampongeza Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge, Kamati inamuahidi ushirikiano wa kutosha na tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja naye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Makatibu wetu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo na Nyamwanja Chilemeji na Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama

yalivyowasilishwa na mtoa hoja Fungu 96 jumla ya shilingi 54,741,802,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO  
MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA  
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/  
2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sana'a na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**1.1      MUUNDO WA TAARIFA**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu matatu ambayo ni kama ifuatavyo:-

- a) Mapitio ya Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa bajeti wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yenye kujumuisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa, hatua iliyofikiwa katika ukusunyaji wa maduhuli pamoja na hali ya upatikanaji wa fedha;

- b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 inayojumuisha makadirio ya makusanyo ya maduhuli na maombi ya fedha za matumizi ya kawaida na za kutekeleza miradi ya maendeleo; na
- c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

### **SEHEMU YA PILI**

## **2.0 MAELEZO KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Upanuzi wa Usikivu TBC (*Expansion of TBC Coverage*) ambao katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilitengewa kiasi cha **Shilingi 5,000,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa, kiasi chote cha fedha jumla ya **Shilingi 5,000,000,000.00** sawa na **asilimia 100** kimepokelewa na TBC na mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

**a) Shilingi 2,480,000,000.00** zinalenga kuboresha Upanuzi wa Usikivu (ujenzi wa mitambo ya FM ya kurusha matangazo ya redio katika maeneo 7 ya nchi ambayo ni Kasulu, Nkasi, Bunda, Karagwe, Sikonge, Same na Kahama) ambapo utambuzi wa maeneo ya kufunga mitambo unaendelea na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2021. Mradi huu ukikamilika pamoja na mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote(UCSAF), inatarajiwa usikivu wa redio utaongezeka kutoka **asilimia 63** ya sasa hadi **asilimia 74** kwa Tanzania nzima;

**b) Shilingi 1,852,067,840.00** zinalenga kufanya ukarabati wa studio za redio (TBC-Taifa, TBC-FM na TBC-*International*) kwa kufunga mitambo na vifaa vya kisasa. Mradi upo katika hatua

za maainisho ya mifumo na vifaa na kazi ilitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2021;

c) **Shilingi 100,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na studio za redio na televisheni Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma;

d) **Shilingi 144,933,160.00** zimetumika kulipa fidia kwa wananchi 5 waliosalia ambao wametoa maeno yao kupisha Mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya TBC jijini – Dodoma katika eneo la Vikonje; na

e) **Shilingi 422,999,000** zimetumika kwa ajili ya kulipa kodi ya kuingiza vifaa katika Mradi wa ujenzi wa studio za televisheni Mikocheni Dar es salaam unaofadhiliwa na Korea Kusini ambapo gharama yake ya kodi kwa ujumla ilikuwa ni **Shilingi 680,581,211.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea Mradi wa ujenzi wa studio za Televisheni ya Shirika la Utangazaji la Taifa- TBC na kushuhudia kazi nzuri ya ujenzi wa Jengo la studio ambao unafadhiliwa na Serikali ya Korea Kusini ambapo hadi kukamilika kwa jengo pamoja na mitambo ya studio awamu ya kwanza gharama za mradi zimefika **shilingi 2,379,850,000.00** na Serikali ya Tanzania imetoa Jumla ya **Sh 422,999,000.00** kati ya **Shilingi 5,000,000,000.00** zilizoainishwa hapo juu kwa ajili ya kulipia kodi mitambo ya studio za Televisheni. Aidha, awamu ya pili ya mitambo na vifaa vya studio imepokelewa nchini toka Korea kusini tarehe 21 Januari, 2021. Gharama ya mitambo na vifaa vilivyopokelewa ni **shilingi 413,354,008.34** na Serikali ya Tanzania inatarajia kulipia kodi ya mitambo na vifaa hivyo kiasi cha **Shilingi 200,106,311.45** fedha hizi pia ni kati ya zile **Shilingi Bilioni 5** zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati ilielezwa kuwa, kazi ya kufunga mitambo na vifaa inatarajiwa kuanza mara baada ya malipo ya kodi kufanyika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mradi huu, Kamati ilitembelea pia mradi wa ujenzi wa redio ya jamii makao makuu Jijini Dodoma eneo la Uhindini (**Namba ya Mradi 4279**)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

unaofadhiliwa na UCSAF na kushuhudia kazi ya kufunga mitambo ya studio ikiwa imekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hii Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya kijinsia kama ifuatavyo:-

- i) Uwiano wa wanawake na wanaume katika ngazi za uongozi umezingatiwa; na
- ii) Ukosefu wa Miundombinu kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwani Jengo lenye ghorofa moja halikuwa na *Lift*.

**Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zote za mradi wa usikivu nchini kiasi cha shilingi Bilioni 5. Aidha, inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika kwa wakati ili usaidie katika kuongeza usikivu nchini.**

### **2.1 MATOKEO NA MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

- a) TBC iendelee kuboresha maudhui ili yaendane na mahitaji ya walaji;
- b) Kwa kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge tayari zimetolewa kiasi cha **shilingi Bilioni 5**, TBC ianze utekelezaji wa Mradi huo wa usikivu kwa maeneo yaliyotengewa fedha hizo mara moja ili wananchi waweze kupata habari;
- c) TBC ishirikiane na Balozi zetu ili channel za TBC ziweze kuonekana nje ya nchi;
- d) Channel ya Utalii ya Safari Channel iboreshwe ili kuongeza vipindi vya lugha mbalimbali ili kuvutia watalii ambao wanatoka maeneo mbalimbali duniani;
- e) TBC ipewe haki na uwezo kurusha mechi za mpira ndani na nje ya nchi ili wananchi waweze kunufaika na chombo chao cha Umma badala ya kutegemea vyombo binafsi;

- f) TBC iweke mkakati utakaowezesha kuwalinda watumishi ambao imewatengeneza kwa muda mrefu wasihamie kwenye vyombo vingine nya habari;
- g)TBC iwezeshwe na Serikali kupata haki za kutangaza ligi za ndani na nje ya nchi yakiwemo mashindano ya UMITASHUMTA, UMISETA n.k. maana huko ndiyo kunakopatikana vipaji;
- h)TBC iboreshe ofisi za Kanda ili ziendane na mabadiliko makubwa yaliyopo kwa sasa; na
- i)TBC ihakikishe inafanya kazi kibiashara (Mfano: matangazo ya mpira, kutengeneza tamthilia kama vile "isindingo" kwa kuhusisha wasanii wa ndani.

## **2.2 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilichambua bajeti ya Wizara hii **Fungu 96** na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kuzingatiwa na Wizara. Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 28 Machi, 2021, Wizara iliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati, lakini pia iliwasilisha Taarifa ya namna ilivyotekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yenye kujumuisha hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli na hali ya upatikanaji wa fedha kama ifuatavyo:-

## **2.3 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 22 Aprili 2020 ilikuwa na jumla ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo Sita (6). Katika Taarifa ya Wizara iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Waziri mwenye dhamana kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati, tumbaini

kuwa, kwa kiasi Wizara imetekeleza maoni ya Kamati. Aidha, baadhi ya maoni bado hayajatekelezwa kikamilifu kama vile kutotolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo ya 2019/2020, utendaji wa TSN pamoa na ukusanyaji mdogo wa maduhuli. **Kamati itaendelea kusititiza utekelezaji wa maoni hayo katika taarifa hii.**

#### **2.4 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, makadirio ya Wizara yalikuwa ni kukusanya **Shilingi 41,631,184,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo ni Idara zilizo chini ya Wizara kiasi cha **Shilingi 960,000,000.00** sawa na **asilimia 2.3** na Taasisi **Shilingi 40,671,184,000.00** sawa na **asilimia 97.7**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Imejulishwa kuwa, kufikia Februari 2021 Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 15,350,626,257.00** sawa na **asilimia 36.9** ya lengo. Kati ya makusanyo hayo, **Shilingi 478,879,282.00** sawa na **asilimia 49.9** zimekusanywa kutoka Idara za Wizara na **Shilingi 14,871,746,975.00** sawa na **asilimia 36.6** zimekusanywa kutoka Taasisi saba zilizo chini ya Wizara<sup>1</sup> kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, makusanyo madogo zaidi yanatoka kwenye Usajili wa Magazeti kwani kati ya **Shilingi 55,000,000.00** zilizokadiriwa, ni **Shilingi 2,000,000.00** tu ndiyo zimekusanywa sawa na **asilimia 3.6** ya lengo. Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo madogo na ilielezwa ni kutokana na wateja wachache waliojitokeza kusajili na kuhuisha leseni za mwaka za magazeti. Si hivyo tu, pia ukuaji na ufanisi wa teknolojia ya mawasiliano ya kielektroniki katika kupashana habari na kutangaza biashara kumeathiri soko la bidhaa za magazeti na majarida.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuishia hapo, ilihoji sababu za makusanyo madogo kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara na hususan Kampuni ya Magazeti ya Tanzania (TSN) na Baraza

la Sanaa Tanzania (BASATA) ambazo makusanyo yao ni chini ya **asilimia 30** ya lengo. Kamati ilielezwa kuwa, ukusanyaji huo mdogo unatokana na sababu mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Kwa TSN, mapato yake yalitarajiwa kutokana na huduma za uchapaji ambapo TSN ilitarajia kuwa na mtambo mpya wa uchapaji. Hata hivyo, mtambo huu haukuweza kupatikana kama ilivyotarajiwa. Aidha, uchakavu wa mtambo uliopo umeathiri biashara ya matangazo na mauzo ya nakala za magazeti ambayo ndiyo chanzo kikuu ya mapato ya Kampuni; na

b) Kwa upande wa BASATA, makadirio ya makusanyo yalitegemea kuzinduliwa kwa mfumo wa kielektroniki wa usajili na vibali ambao ulichelewa kutokana na zoezi la upembuzi yakinifu wa mahitaji ya mfumo (*System requirement specifications*) kuchukua muda mrefu kulkiko ilivyotarajiwa.<sup>2</sup>

#### **Kielelezo Na. 1: UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA 2020/2021 - FUNGU 96**

CHANZO	MAKADIRIO	MAKUSANYO	ASILIMIA
WIZARA	960,000,000.00	478,879,282.00	49.9
TAASISI	40,671,184,000.00	14,871,746,975.00	36.6
JUMLA	<b>41,631,184,000.00</b>	<b>15,350,626,257.00</b>	<b>36.9</b>



#### **Chanzo: Randama ya Fungu 96 na Usanifu wa Kamati**

<sup>2</sup> Majibu ya Wizara (Fungu 96) katika Hoja zilizotolewa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilipokutana na Wizara tarehe 28 Machi, 2021

## 2.5 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, iliidhinishiwa na Bunge Iako Tukufu jumla ya **Shilingi 40,480,641,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, mishahara iliidhinishiwa **Shilingi 20,979,231,000** sawa na **asilimia 52**, matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 11,446,410,000.00** sawa na **asilimia 28**, na miradi ya maendeleo **Shilingi 8,055,000,000.00** sawa na **asilimia 20**.

**Mheshimiwa Spika**, kufikia Februari 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 24,308,869,745.00** sawa na **asilimia 60.1** ya lengo. Kati ya fedha hizo, mishahara **Shilingi 11,227,649,745.00** sawa na **asilimia 53.5**, matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 7,581,220,000.00** sawa na **asilimia 66.2** na miradi ya maendeleo **Shilingi 5,500,000,000.00** sawa na **asilimia 68.3<sup>3</sup>** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.2.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati ilitarajia kufikia Februari 2021 upatikanaji wa fedha uwe umefikia angalau **asilimia 66**. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara ya Watumishi ni **asilimia 53.5**. Kamati ilihoji ni kwa kiasi gani upatikanaji huu ambao haujafikia lengo umeathiri watumishi? Kamati ilielezwa kuwa, bajeti ya mishahara iliyotengwa katika mwaka 2020/2021 ililenga upandishwaji vyeo kwa baadhi ya watumishi pamoja na ajira mpya. Hivyo basi, kutokana na kutotoka kwa fedha hizi hadi Februari, 2021 mishahara ya Wizara iliyotoka ilikuwa haijazingatia upandishwaji wa vyeo uliokusudiwa pamoja na ajira mpya zilizopangwa katika mwaka 2020/21.

**Kamati inatoa Rai wa Serikali kuhakikisha inatoa fedha hizi za Wizara ili Watumishi wanaostahili kupandishwa vyeo waweze kupandishwa lakini pia wale walipangwa kuajiriwa waajiriwe ili kuondoa changamoto ya uhaba wa Watumishi ambayo Wizara na Taasisi zake inakumbana nayo.**

---

<sup>3</sup> Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara (Fungu 96) kwa Mwaka 2020/21 na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2021/22 (Randama Ya Bajeti)

## Kielelezo Na. 2:

### UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021 FUNGU 96



Chanzo: Randama ya Fungu 96 na Usanifu wa Kamati

### SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kuwa, bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 imeandaliwa kwa kuzingatia pamoja na mambo mengine, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025, Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22, Mpango Mkakati wa Wizara (2020/21-2025/26) na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022 katika eneo la makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha makadirio hayo na ya mwaka 2021/2022 pamoja na bajeti ya matumizi na miradi ya maendeleo vilevile kama ifuatavyo:-

### 3.1 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya makusanyo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 yanatarajiwa kutoka katika vyanzo mbalimbali na jumla ya **Shilingi 34,826,444,000.00** zinakadiriwa kukusanywa. Kati ya makadirio hayo, **Shilingi 960,000,000.00** sawa na **asilimia 3** zinakadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vilivyopo chini ya Idara mbili za Wizara (Idara ya Maendeleo ya Michezo **asilimia 2** na Idara ya Habari Maelezo **asilimia 1**) na **Shilingi 33,866,444,000.00** sawa na **asilimia 97** zinakadiriwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya Taasisi saba zilizo chini ya Wizara kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3

#### Kielelezo Na. 3: MAKADIRIO YA MADUHULI 2021/2022 FUNGU 96



Chanzo: Randama ya Fungu 96 na usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha makisio ya makadirio ya maduhuli kati ya mwaka 2021/2022 na mwaka 2020/2021 na kubaini kuwa, makadirio ya mwaka 2021/2022 yamepungua kwa **asilimia 16.35** kutoka **Shilingi 41,631,184,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 34,826,444,000.00** mwaka 2021/2022. Upungufu huo ni katika vyanzo vya Taasisi na hususan katika Shirika la Magazeti (TSN) kwa **asilimia 36.77** kutoka **Shilingi 22,684,519,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 14,343,823,000.00** mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji sababu za kushuka kwa makadirio ya makusanyo ya TSN na ilielezwa ni kutokana na ukweli kuwa, chanzo kikuu cha mapato ya Kampuni ni uuzaji wa nakala za magazeti, hata hivyo mtambo uliopo ni chakavu na mtambo mpya bado haujapatikana kwani kinahitajika kiasi cha **Shilingi Bilioni 16** kuweza kununua mtambo huo. Kamati llielezwa kuwa, Wizara inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha hizo kwa ajili ya kununua mtambo mpya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ikiwa ni pamoja na kufuatilia madeni ya takribani **Shilingi Bilioni 9** ambayo TSN inazidai Taasisi mbalimbali nchini<sup>4</sup>. **Kamati inaendelea kusisitiza Serikali (Wizara ya Fedha) kuhakikisha madeni haya yanahakikiwa mapema ili kuweza kupata kiasi hicho cha fedha Shilingi Bilioni 9 na fedha nyingine ziongezwe na Serikali ili mtambo huo mpya na wa kisasa uweze kununuliwa na hivyo kusaidia katika kuongeza mapato ya TSN.**


**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuishia hapo, ilifanya uchambuzi zaidi na kubaini kuwa, makusanyo ya Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) kwa mwaka 2020/2021 kufikia Februari 2021 ni **asilimia 28** tu (**Shilingi 394,033,971.00** kati ya **Shilingi 1,382,193,000.00** zilizokadiriwa). Lakini cha kushangaza zaidi ni kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 makadirio hayo yameongezeka kufikia **Shilingi 1,480,919,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 7.14**. Kamati ilihoji sababu la ongezeko hilo licha ya lengo katika mwaka 2020/2021 kutofikiwa na ilielezwa kuwa, maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili na vibali yapo katika hatua za mwisho na mfumo unatarajiwa kuanza kutumika kabla ya mwezi Juni, 2021 na hivyo utasidia kuongeza mapato ya BASATA. Ni imani ya Kamati mfumo huu **utaaanza kutumika na lengo hili la makusanyo litafikiwa**.

---

<sup>4</sup> Majibu ya Wizara (Fungu 96) katika Hoja zilizotolewa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilipotokana na Wizara tarehe 28 Machi, 2021

#### Kielelezo Na.4

#### ULINGANISHO WA MADUHULI YA FUNGU 96 KWA MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022.




Chanzo: Randama ya Fungu 96 na usanifu wa Kamati

#### 3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 54,741,802,000.00**. Mchanganuo wa fedha hizo unajumuisha Mishahara ya watumishi **Shilingi 19,146,653,000.0** sawa na **asilimia 35**, Matumizi mengineyo **Shilingi 14,880,149,000.00** sawa na **asilimia 27**; na Miradi ya maendeleo **Shilingi 20,715,000,000.00** sawa na **asilimia 38** kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 5

Kielelezo Na. 5:

SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022



Chanzo: Randama ya Fungu 96 na usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, bajeti ya **Fungu 96** imeongezeka kwa **asilimia 35.2** kutoka **shilingi 40,480,641,000.00** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **shilingi 54,741,802,000.00** mwaka 2021/2022. Ongezeko zaidi linaonekana katika fedha za matumizi mengineyo kwa **asilimia 30** kutoka **shilingi 11,446,410,000.00** hadi **shilingi 14,880,149,000.00**. Aidha, fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 157.2** kutoka **shilingi 8,055,000,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **shilingi 20,715,000,000.00** mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 6.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo limechangiwa na bajeti ya ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzika wananchi kiasi cha **Shilingi Bilioni 10.5**.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mazoezi ambavyo pia kwa kiasi kikubwa vitasaidia katika kupunguza magonjwa yasiyoambukiza ambayo yameendelea kuwa tishio na kuwa chanzo kikubwa cha vifo nchini. Aidha, ujenzi huu ni

utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 aya ya 243 (c) inayoeleza azma ya kuboresha michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi na kuanzisha vilabu nya michezo na matamasha ya mazoezi ili kuboresha afya zao na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.<sup>5</sup> Mwanazuoni Robin Sharma amewahi kusema "*If you don't make time for exercise, you'll probably have to make time for illness.*"

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko la fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa, mishahara ya watumishi imepungua kutoka **Shilingi 20,979,231,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 19,146,653,000.00** mwaka 2021/2022 sawa na upungufu wa **asilimia 8.7**. Kamati ilihoji sababu za upungufu huo na kwa kwa kiasi gani utaathiri stahili za watumishi. Kamati ilielezwa kuwa, ni kutokana na kupungua kwa idadi ya watumishi kutoka 225 hadi watumishi 217 kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, upandishaji cheo umepungua kutoka nafasi 79 mwaka 2020/21 hadi nafasi 31 mwaka 2021/22. Pia, ajira mpya zimepungua kutoka nafasi 36 mwaka 2020/21 hadi nafasi 27 mwaka 2021/22<sup>6</sup>


---

<sup>5</sup> llani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

<sup>6</sup> Majibu ya Wizara (Fungu 96) katika Hoja zilizotolewa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Ilipokutana na Wizara tarehe 28 Machi, 2021

### Kielelezo Na. 6:

#### ULINGANISHO WA BAJETI MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022



**Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuishia kwenye uchambuzi wa kulinganisha bajeti ya Wizara kwa Miaka hiyo miwili, ilifanya uchambuzi zaidi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa (Kielelezo Na. 7) ili kuona ni kwa kiasi gani ongezeko au upungufu wa bajeti ya Taifa unaathiri bajeti ya fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati imebaini yafuatayo:-

- a) Wakati bajeti ya matumizi ya mengineyo (OC) ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 5.43**, bajeti ya matumizi mengineyo ya Fungu 96 imeongezeka kwa **asilimia 30**;
- b) Wakati bajeti ya maendeleo ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 2.76**, bajeti ya maendeleo ya Fungu 96 imeongezeka kwa **asilimia 157**;
- c) Wakati bajeti ya mishahara ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 5**, bajeti ya mishahara ya Fungu 96 imepungua kwa **asilimia 9**

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

d) Kwa ujumla wakati bajeti ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 3.95** kutoka **Shilingi Triliioni 34.8** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi Triliioni 36.2** mwaka 2021/2022, Bajeti ya Fungu 96 imeongezeka kwa **asilimia 35** kutoka **Shilingi Bilioni 40.4** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi Bilioni 54.7** mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, bajeti hizi mbili zinatupa tafsiri kuwa, pamoja na kuwa kuna ongezeko dogo la bajeti ya Taifa, bajeti ya Wizara hii imepewa kipaumbele zaidi hasa katika Miradi ya maendeleo yenye lengo la kuongeza viwanja vya mazoezi pamoja na Matumizi Mengoinyoyo. Hata hivyo, tunaona suala la mishahara halijapewa uzito kutokana na kutokupandishwa vyeo kwa watumishi na kutokuwa na ajira mpya.

### Kielelezo Na.7:

#### ULINGANISHO WA BAJETI YA TAFIA DHIDI YA FUNGU 96

ULINGANISHO WA BAJETI YA TAIFA 2020/2021 NA 2021/2022 (KWA MILIONI)				
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA	BAJETI KUU YA TAIFA	PUNGUFU/ONGEZeko	%
OC	3,741,137	3,944,164	203,027	<b>5.43</b>
MISHAHARA	7,762,389	8,150,509	388,120	<b>5.00</b>
MAENDELEO	12,899,433	13,255,855	356,422	<b>2.76</b>
MALIPO MADENI	10,476,834	10,663,278	186,444	<b>1.78</b>
MAHITAJI YA TANAPA, TAWA NA NCAA	0	245,000	245,000	
JUMLA	<b>34,879,793</b>	<b>36,258,806</b>	<b>1,379,013</b>	<b>3.95</b>

ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 96 KWA MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022				
CHANZO	2020/2021	2021/2022	PUNGUFU/ONGEZeko	%
MISHAHARA	20,979,231,000	19,146,653,000	- 1,832,578,000	- <b>9</b>
MATUMIZI MENGINEYO	11,446,410,000	14,880,149,000	3,433,739,000	<b>30</b>
MAENDELEO NDANI	8,055,000,000	20,715,000,000	<b>12,660,000,000</b>	<b>157</b>
JUMLA	<b>40,480,641,000</b>	<b>54,741,802,000</b>	<b>14,261,161,000</b>	<b>35</b>

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2021/2022 na Randama ya Fungu 96

### SEHEMU YA NNE

#### 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi huo, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

## 4.1 MAONI YA JUMLA

### a) Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, hali ya ukusanyaji wa maduhuli wa **Fungu 96** siyo wa kuridhisha kama inavyoonekana kwenye uchambuzi wa Kamati ambapo ukusanyaji ultarajiwu kufikia Februari uwe **asilimia 66.6** lakini hali halisi ya ukusanyaji ni **asilimia 36.87**. Kamati inashauri **Wizara kuboresha mifumo yake ya ukusanyaji na kuhakikisha inafikia malengo iliojiwekeea.**

### b) Sanaa na Burudani

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa ukuaji wa Sekta ya Sanaa na burudani ni mkubwa. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22, kati ya shughuli za kiuchumi zillzokuwa na ukuaji mkubwa katika kipindi cha mwaka 2019 ukiacha madini na ujenzi, sanaa na burudani imeshika namba 3 kwa ukuaji wa **asilimia 11.2**. Ukuaji huu umeongezeka kutoka **asilimian6.2** mwaka 2015<sup>7</sup>. Kamati inaona ukuaji huu unapaswa kwenda sambamba na kuongezeka kwa mapato. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, Sekta hii ina changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika ukuaji wake na katika kuchangia pato la Taifa. Kutohana na hali hiyo, Kamati inashauri yafuatayo:

- i) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato iboreshwe ili kuvutia watumiaji lakini pia kuongeza mapato ya nchi; na
- ii) Kutohana na muingiliano wa shughuli za Taasisi ya BASATA, COSOTA, Bodi ya Filamu na TCRA, ni vyema Wizara ikaweka *One stop Centre* ili kurahisisha utoaji wa huduma na hivyo kuchochea ukusanyaji wa mapato.

### c) Michezo

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Michezo inakumbana na changamoto nydingi ambazo zimekuwa kikwazo kwa ukuaji

---

<sup>7</sup>Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

wake. Ikumbukwe kuwa, mafanikio katika michezo yanachochewa na vitu mbalimbali. Mwanamiereka kutoka Marekani Dan Gable amewahi kusema "*Gold medals aren't really made of gold. They're made of sweat, determination, and a hard-to-find alloy called guts*". Nchi yetu ikitaka kufanikiwa katika michezo haina budi kuwekeza katika michezo ikiwa ni pamoja na:-

- i) Kuandaa mkakati wa kubadili na kuboresha mfumo wa michezo nchini ili iendane na hali halisi ilivyo kwa sasa kwa kuwa michezo zama hizi ni ajira kwa vijana wetu;
- ii) Kuhakikisha kunakuwepo viwanja na vifaa bora vyta kutosha kwa ajili ya michezo mbalimbali; na
- iii) Kuanzisha *Sport Academy* ili vijana wenyewe vipaji waweze kuibulisha na kufundishwa.

### **4.2 SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA TAIFA – TBC**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Shirika hili, lakini kuna changamoto ambazo zimeendele kuwa kikwazo katika utendaji bora wa TBC. Hivyo, Kamati inashauri:-

- a) Serikali iongeze bajeti ya miradi ya maendeleo ya TBC ili iweze kusaidia kuongeza usikivu ili ufikie **asilimia 100** hasa maeneo ya vijijini na pembezoni kwani kwa sasa usikivu ni **asilimia 63** tu;
- b) Mikakati iwekwe ili wadeni wa TBC waweze kulipa madeni yao. Aidha, kwa madeni yasiyolipika ni vyema mchakato wa kuyafuta ukafuatwa;
- c) TBC iwe na ubunifu wa kuweka burudani na michezo ambayo itasaidia kuvutia watazamaji na wasikilizaji ili baada ya Taarifa ya Habari waendelee kuangalia Chaneli hiyo ya Taifa; na
- d) TBC iweke mikakati ya kuweza kujitangaza Duniani kote ili isaidie pia kuvutia Watalii.

#### **4.3 BARAZA LA KISWAHILI TANZANIA (BAKITA)**

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa lugha ya Kiswahili imechaguliwa kuwa ni moja ya lugha za mawasiliano katika nchi za Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC) na nchi mbalimbali kama Afrika ya Kusini zimeanza kutumia lugha ya kiswahili. Kutokana na umuhimu wa lugha huu, Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) BAKITA iweke mkakati wa makusudi wa kuzalisha Wakalimani wengi zaidi wenye uwezo wa kufahamu lugha zaidi ya moja kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa vyao;
- b) Ili kufanikiwa kubidhaisha Kiswahili, Serikali ianzishe Dawati la Kiswahili katika kila Ubalozi kama nchi za wenzetu ikiwemo China walivyofanya. Aldha, tutumile *exchange program* na nchi nydingine kubidhaisha Kiswahili;na
- c) Serikali iweke Mkakati wa kuunganisha (*link*) Kiswahili na Utalii.

#### **4.4 BARAZA LA SANAATANZANIA (BASATA)**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa Baraza la Sanaa katika Sekta ya Sanaa nchini, Kamati inashauri:-

- a) Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la mwenendo wa ufungiaji wa wasanii nchini kunakosababishwa na makosa mbalimbali, Ni vyema BASATA ianze kutoa mafunzo kwa wasanii ili kupunguza makosa ambayo wamekuwa wakiyafanya kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kutokuwa na uelewa wa kutosha wa kanuni na taratibu hali inayopelekea baadhi yao kufungiwa;
- b) BASATA iweke mikakati itakayowezesha kuongeza mapato kutokana na fursa zilizopo ili wasanii pamoja na Taifa liweze kunufaika; na
- c) Uanzishwe mfumo wa Kielektroniki utakaowezesha wasanii kulipia vibali vya safari bila ya kwenda kwenye Ofisi za BASATA

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ili kuepuka baadhi yao kuzuiliwa kusafiri au kulazimika kurudi nchini kuomba vibali hivyo.

### **4.5 BODI YA FILAMU TANZANIA**

**Mheshimiwa Spika**, Tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa, Filamu zina nafasi kubwa katika kuchochlea utalii na hivyo kuchangia katika ukuaji wa Pato la Taifa. Kwa mujibu wa Utafiti wa mwaka 2018 wa *Travel Competitive Intelligence*, Watalii wa Kimataifa milioni 80 Ulimwenguni walitembela sehemu kama La La Land, Narcos, Pirates of the Caribbean, Buddies in India, Manchester by the sea mnamo mwaka 2017 walitokana na ushawishi waliouna kwenye Filamu. Aidha, The UNWTO-Awarded Research Agency inataja maeneo ambayo yamekuwa kivutio cha watalii kutokana na kuyaona kupitia filamu kuwa ni Los Angeles, London, Scotland, Columbia, Florence, New-York, Dubai, Paris, Berlin, New-Zealand kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.8.

**Kamati inashauri Bodi ya Filamu iweke mfumo utakaowezesha Filamu zetu kuandaliwa/kutengenezwa katika maeneo ambayo yatavutia Watalii na hatimaye kuchangia katika ukuaji wa pato la Taifa na Uchumi kwa ujumla.**

**Kielelezo Na.8:**

#### **Maeneo yanayovutia Watalii baada ya kuyaona kupitia Filamu**



**Chanzo: UNWTO-Awarded Research Agency, 2018**

#### **4.6 BARAZA LA MICHEZO TANZANIA (BMT)**

- a) Mkakati uwekwe utakaowezesha kuboresha viwanja vyatia michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuingia Ubia na Sekta binafsi;
- b) Wizara ionetra namna ya kutoa hamasa kwa Maafisa Michezo kuanzia ngazi ya Kata hadi Mkoa ili kuweza kusimamia vyema jukumu la kukuza Michezo katika maeneo yao;
- c) Vibali vyatia usajili wa wachezaji wa kigeni vitolewe ili kuongeza Pato la Taifa;
- d) Wizara iweke mkakati wa kusaidia Vilabu nchini viweze kuijiendesha badala ya kuendelea kutegemea *Gate-collection* au wawekezaji Binafsi;
- e) BMT isimamie kila Klabu iweze kuwa na Mtaalam wa Lishe atakayesaidia kukuza afya za wachezaji wetu ili waweze kushiriki vizuri kwenye Michezo na kuleta matokeo chanya.

#### **4.7 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI TANZANIA (TSN)**

- a) Kutokana na magazeti kucheleva kufika kwa wakati hasa maeneo ya vijijini, TSN iweke mkakati wa kuondoa changamoto hii;
- b) TSN wawe wabunifu ili waweze kushindana katika Karne hii ya Teknolojia; na
- c) Serikali iiwezeshe TSN kupata kiasi cha **Shilingi Bilioni 16** ili iweze kununua Mtambo mpya wa kisasa wa uchapaji ambao utasaidia katika kufanya kazi kibiashara.

#### **4.8 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)**

**Mheshimiwa Spika**, COSOTA ina wajibu wa kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, wachapishaji, na hususani kukusanya na kugawa mirabaha au ujira unaotolewa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kulingana na haki zao zilizofafanuliwa katika Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999. Kamati imebaini kuwa, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Taasisi hii lakin bado kuna changamoto ambazo zimekuwa kero na kikwazo katika ukuaji wa maendeleo ya sanaa nchini. Hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Kutokana na uwepo wa vyanzo vingi vya mapato ambavyo havijatumwa vizuri na hivyo kusababisha upotevu wa mapato kwa hususan katika biashara ya mtandao (*online business*). Ni wakati sasa COSOTA kuanza kutumia fursa za mapato ili nchi na wasanii waweze kunufaika; na
- b) Mkakati uwekwe wa kuzuia na kudhibiti uharamia (pirates) wa kazi za Wasanii nchini hali ambayo inawavunja moyo wasanii wetu. Aidha, faini kubwa zitolewe kwa watakaokamatwa wakili ba kazi za wasanii.

### **4.9 MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuondoa changamoto wanazokutana nazo wasanii kutokana na maudhui ya kazi zao, Kamati inashauri

- a) Adhabu zinazotolewa ziangaliwe ili zisiumize sana wasanii na pia kulikosesa Taifa mapato; na
- b) Mkakati uwekwe ili kuwa na *Aggregator*wa Youtube nchini ili kuwezesha Serikali kupata mapato ambayo imekuwa ikiyakosa kutokana na wasanii kutumia *aggregator* wa nje ya nchi.

### **5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu vyema.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa mara zote na hivyo kurahisisha utendaji kazi wa Kamati. Nawapongeza sana kwa namna ambavyo wamekuwa wakishiriki vyema katika shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na uchambuzi bajeti ya Wizara ya Fungu 96 na maandalizi ya Taarifa hii. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Hajji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Francis Leonard Mtenga, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Jumanne Abdallah Sagini, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Latifa Khamis Juwakali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb- MJumbe
17. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
18. Mhe. George Ranwell Mwensongole, Mb-Mjumbe
19. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Hassan Ziddu Kungu, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb- Mjumbe
26. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb), aliyekuwa Naibu Waziri Mhe. Abdallah Ulega (Mb), Naibu Waziri wa sasa Mhe. Pauline Gekul (Mb) kwa ushirikiano

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati. Pamoja nao, nawashukuru watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Dr. Hassan Abbas na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ally Possi kwa ushirikiano wanaoipa Kamati ikiwa ni pamoja na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano. Aidha, namshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano aliokuwa anaipa Kamati. Aidha, nampongeza Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge, Kamati inamuahidi ushirikiano wa kutosha na tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake. Pamoja nae namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Makatibu wetu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Nyamwanja Chilemeji na msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja **Fungu 96** jumla ya **Shilingi 54,741,802,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**

31 MEI, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mbunge wa Kankoko.

Sasa tunaenda katika uchangiaji kama nilivyosema Mwenyekiti wetu wa *Bunge Sports Club* atuanzishie. Tujaribu dakika kumi/kumi kwanza halafu tutaona tunavyoenda, Mheshimiwa Talimba atafuatiwa na Mheshimiwa Meneja wa *Bunge Sports Club*, Seif Khamis Gulamali.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza kabisa katika hotuba aliyoitao ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nataka niseme kwamba naunga mkono asilimia mia moja hotuba hii na ninataka nimpongeze kwa kazi nzuri, hotuba nzuri ye ye mwenyewe binafsi pamoja na wasaidizi wake wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nichangie katika maeneo mawili makubwa; eneo la kwanza, ni uendeshaji wa mpira wa miguu katika nchi hii na eneo la pili, nataka nizungumzie kuhusu timu yetu ya Taifa ya mpira wa miguu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mazungumzo haya naanzisha kutoka kwenye *page* namba 46 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri pale ambapo amevitaka vyama vya michezo nchini kuendeshwa kwa mujibu wa taratibu za utawala bora, kufuata kanuni zao na vilevile kuhakikisha kwamba michezo inaleta tija na kuleta maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na kutokana na hili nilitaka nizungumze kwanza upande wa mpira wa miguu. Mpira wa miguu ndio michezo unaopendwa sana katika Tanzania, ipo michezo mingine, lakini mpira wa miguu ndio unaoshika namba moja na kutokana na hali hiyo mpira wa miguu umekuwa ni ajira, umekuwa ni biashara, lakini vilevile imekuwa ni maeneo ambapo watu wanapata burudani na kuwaliwaza wale ambao wanapata matatizo ya aina fulani na kwa fulani. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati mbaya sana uendeshaji wa michezo hii umekuwa mara nyigi sana kumekuwa na changamoto za ajabu, mara nyigi uendeshaji hauridhishi, wadau wanalamika na utakuta mambo mengine ambayo yanatufanya tulalamike wala hayana sababu ya kulalamika. Kwa mfano unakwendaje kubadilisha ya mchezo mzito kabisa, mchezo ambao watu wamewekeza kwa hali na mali kwenye furaha zao, wengine wametoka mbali sana wametoka Dodoma kuja kule Dar es Salaam, unakwenda kutubalidilishia mchezo mwisho mwisho wa siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naambiwa kuna watu walichungulia katika darubini zao wakaona wanakwenda kupigwa mabao basi wakaenda kufanya mipango ya kuweza kupeleka mbele mpira ule, sasa tarehe mpya inakuja tuone watasogea tena? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, viongozi wa klubu wamekuwa wakipewa adhabu za..., nitatumia neno ambalo siyo zuri, za hovyo hovyo kabisa, hakuna *standard*, leo huyu akifanya makosa yaleyale anapona mwingine akifanya makosa yaleyale anaadhibiwa kesho yake na adhabu za kutisha kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda mbali zaidi unakuta hata waamuzi wameathirika nao, wamejiingiza katika mambo kama hayo, wanafanya mambo ya upendeleo wa dhahiri uwanjani, wanakosesha klubu nydingine ushindi kwa sababu tu ya mapenzi yao wakijua kwamba watafungiwa mechimoja au mbili halafu wanarudi tena uwanjani. Mambo kama haya yanaleta taabu na kwa hali hiyo utakuta malalamiko yanapelekwa *TFF* leo, kesho yanapatiwa majibu, mengine yanakaa miezi miwili mpaka miezi saba, *standard* ipo wapi na hapa napata mashaka kwamba ndani ya chama chetu kile au *federation* hakuna uadilifu hata siku moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na yanapeleka mpaka mwisho yanafikia *very personal*, mnakutana katika sherehe, kwa mfano kama juzi kulikuwa na sherehe ya *first division*, watu

wanapeana mikono, sijui ni jana, sijui watu wanapeana mikono wengine wanakataa kutoa mikono, wanatuunesha nini? Kwa sababu tu ya mapenzi yao. Mpira wa miguu umekuwa *tentedvibaya* sana Mheshimiwa Waziri. Tusafishieni mpira wa miguu katika nchi hii ili uweze kutuletea matumaini yanayotarajiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na haya mambo yanayofanyika sasa hivi yanaathiri vilevile timu yetu ya Taifa, timu ya Taifa ya Tanzania haina matumaini, haina matumaini kabisa utafikiri timu ya Uingereza bwana! Uingereza ndiyo nchi za kwanza duniani ambazo zimewahi kucheza *international competition*. Mwaka 1872 wakicheza na Scotland wakatoka zero-zero, hebu fikiri timu kama hiyo imeshiriki na kupata ubingwa wa *World Cup* mara moja katika miaka yake yote, walipata mwaka 1966, lakini wana timu nzuri sana, timu zao za binafsi zile moja moja kina *Chelsea*, kina *Manchester United* na *City* wanacheza mpira mzuri sana kwa sababu gani, wao wameamua ku-*commercialize* ligi yao.

Mheshimiwa Spika, ligi yao ni nzuri sana katika dunia, wachezaji wote wazuri wanakimbilia kule. Lakini timu yao ya Taifa haioneshi ule ukali wa ligi yao, *so it is the opposite*, inavyotakiwa ligi ya nchini kwako hasa *premier league* ndio iakisi timu yako ya Taifa. Sisi timu zetu ziko kali, zina ligi, ligi yake inaanza kuendelea kuwa vizuri zaidi, lakini *where is local talent*, iko wapi *local talent?* Tunaletewa wachezaji wengi wa nje, timu zetu zinafanikiwa, lakini zinafanikiwa kwa sababu ya wachezaji sana wa timu za nje ambao pia nao ni wa mashaka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini wa mashaka, wewe ukiangalia naomba niitaje baadhi ya timu, ukiangalia pale kwetu *Young African* kwa mfano, tunao wachezaji wa nje wengi tu, lakini hawaisaidii *Young Africans* mpaka iingie kina Kaseke na kina nani ndio watuletee magoli. *Simba Sports Club* wachezaji lukuki wamo mle ndani sijui, wachezaji saba mpaka nane kwa timu moja wanaocheza uwajani, akiingia Boko ndio analeta maneno. (*Makof!*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, sasa *point* yangu ni nini, *point* yangu ni kwamba ili tuweze kupiga hatua ningependa *intervention* ya Serikali kwa maagizo kwa TFFkwamba bwana sasa ni wakati wa kuangalia suala zima la wachezaji wa nje na jinsi gani ligi zetu zinaweza zikaibua *local talents* na timu yetu ya Taifa iweze ikasimama. Bila wachezaji wa ndani kupata nafasi za kutosha, wakacheza katika timu zao, tusahau kupata mafanikio katika timu ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mpira wa miguu kama nilivyo sema ni mchezo ambao unaotegemewa sana. Sasa kama utakuwa na *premier league* ambayo haiakisi mafanikio ya timu ya Taifa tutaendelea kubakia kama England. Sisi tumeshiriki mashindano ya ubingwa wa nchi huru za Afrika nafikiri mara mbili, Nigeria na juzi hapa Misri, lakini kote huko hatujapiga hatua, kwa sababu gani; hata uchaguzi wetu wa makocha, kocha akija hapa akikaa mlezi sita ameshatimuliwa tayari, *continuity* unaipata wapi Mheshimiwa Waziri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wanatakiwa kustahamili na hiyo imeathiri mpaka kwenye klubu zetu sisi za mjini humo. *Young Africans* sijui katika msimu huu wameondo makocha wangapi! Hata makocha wazuri huwezi ukamjua kama huyu mzuri kwa sababu ndani ya miezi mitatu hata hajapoteza mechii nakumbuka ameondolewa. Ukiwa *Simba Sports Club* nako ni hivyo hivyo, ukienda kwenye klubu nyiningine ndogo ndogo ni hivyo hivyo. Hebu watanzania tuwe na tabia ya kustahamili tunapowapa makocha timu zetu kutulelea na hili nalitaka sana kwenye upande wa timu ya Taifa Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwamba timu ya Taifa muisaidie na katika kuisaidia sio kuwapa fedha tu, wapeni maelekezo yanayofaa na najua Serikali haitakiwi iingilie masuala ya mpira, lakini jina la Tanzania ndilo linalotumika. Tukifanya vibaya nchi yetu kama nchi ndio inayopata *ratings* mbovu, tusikubali Tanzania ipate *ratings* mbovu kwasababu ya viongozi ambao hawajitambui. Hawa viongozi wasiojitambua wanaopewa mamlaka ya kuongoza TFF, Mheshimiwa Waziri

wawekeeni taratibu ngumu sana ili hata kupima uadilifu kwa timu zetu za Taifa, kupima uadilifu wao kwa Tanzania uwe ni moja ya vigezo vyta kupata viongozi wa namna hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sio tu kura, msiangalie sana suala la kura, kama mtu tunamuona akienda kwenye kupigiwa kura atashinda, muondoeni. Mbona wangapi wamekatwa katwa katika nafasi chungu mzima, kwani kuna lazima wawe ni wao wao tu? (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri naomba nikuunge mkono katika mipango yako ambayo umeizungumza ya mwisho. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na pole sana kwa engineyo.

Mheshimiwa Seif Hamis Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo. (*Makof/Kicheko*)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi siku ya leo kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi ambazo wanazozifanya. Michezo duniani ndio inayotumika kutangaza nchi na utalii, leo ukizungumza Brazil, ukisema Brazil unajua kuna ile timu ya Taifa ya Brazil, lakini Brazil imetangazwa kuititia michezo. Ukizungumza Ujerumani hata mtoto mdogo wanawajua wachezaji wa zile timu, ukizungumza Afrika unaweza ukajua Misri, ukajua Nigeria, ukajua Ghana kwa *performance* nzuri. Michezo inatangaza

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nchi, hata kuongeza utalii na kipato cha nchi ni michezo, kwenye michezo hatujawekeza vyakutosh, hatujawekeza kwa manufaa ya Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukitaka tufanikiwe kwenye michezo na tukitaka tufanikiwe kwenye kupata kipato kupidia michezo, uwekezaji kwenye michezo unatakiwa uwekezwe kwa namna moja ama nyingine. Moja, tuondoe au tupunguze kodi kwenye vifaa vyamichezo, tukipunguza kodi kwenye vifaa vyamichezo itasaidia wananchi wengi kuweza hata kununua mpira. Mpira mmoja ambao ni bora shilingi 60,000, vijana wa vijijiini kwetu wanatumia masandarusi, wanawezaje kukuza na kukilinda kipaji chake kama vifaa havipatikani? (*Makof*)

Mheshimwia Spika, na kuvipata ni kwenye watu wenye uwezo, lazima tupunguze kodi kwenye vifaa vyamichezo. Tunayo ile *sport center* pale Dar es Salaam ya Jakaya Kikwete ni moja Tanzania nzima, halafu unatakiwa michezo ikue, *sport center* zile zinatakiwa ziwepo kila mkoa katika nchi hii na ikiwezekana kila Wilaya. Utakuza sekta ya michezo, utaibua vipaji vinginevyo, tutakuwa tunazunguka na kudanganyana, ni lazima tuondoe kodi tuwarahisishie, kwa sababu sekta ya michezo haiwekezwi na Serikali itawekezwa na watu binafsi ambao wataweka hizi *sport center*, wataweka *academy*, wataweza kununua vifaa vyamichezo, *jersey*, mpira na vitendea kazi pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, turahisishie kuondoa kodi, tuwarahisishie wawekezaji wa sekta binafsi wawekeze kuwa na *academy* nyingi, tutazalisha hawa vijana wengi. Sio kwenye mpira wa miguu tu hata michezo mingine, ukipunguza kodi itaturahisishia kusonga mbele, *otherwise* tutakuwa tunapiga *mark time*.

Mheshimiwa Spika, binafsi niwapongeze wasanii wanafanya vizuri, nimpongeze Diamond, nimpongeze Ali Kiba, nimpongeze Harmonize, nimpongeze Lava lava na wengineo. Hawa vijana tunatakiwa hata tuwape nishani katika Taifa, hawa vijana kupidia muziki wamekuwa maarufu

Afrika, kupitia muziki wameitangaza Tanzania. Leo Kiswahili kinaweza kuimbwa Afrika, hawa wanafanya kazi nzuri na kubwa, lazima tuangalie vijana hawa wanavyofanya vizuri kwenye sekta hii ya sanaa ya kuimba, sasa huku wamefanya vizuri, je, wamewezeshwa? (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Seif, pokea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kumpa taarifa mchangiaji hususani anavyowapongeza wasanii ni jambo zuri sana, lakini pia tuwakumbuke waasisi kina Inspekte Haroun, kina Juma Nature, kina Lady Jaydee, kina Profesa Jay, kina Sugu wao walianza halafu wadogo zao wakafuatia. Kwa hiyo, hawa wanaofanya vizuri tukumbuke kwamba kuna wengine ambao walianzisha kufanya vizuri pia. (*Makofi*)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, haya, nakushukuru sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Unapokea taarifa Mheshimiwa Seif.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, hiyo yote kila mmoja ana mchango wake kwenye sekta hii, ndio maana tunasema wasanii mpaka wamefika hapo, wamefanya vizuri sana hasa kwa sababu ya vipaji vyao. Wanatutangaza, leo ukienda nchi zingine Tanzania utasikia Diamond, Ali Kiba, Harmonize, wanatutangaza hawa vijana na kutangazwa ni unaitangaza nchi. Hata watalii kuja tunapata kipato lazima tuangalie tunawekezaje kwenye sekta ya michezo kuhakikisha kwamba tunatangaza Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nikikuambia katika Afrika ziko *derby* tano bora, maarufu Afrika; ya kwanza ni *Cairo derby-Zamalek* na *Al-Ahly*; ya pili *Casablanca derby - Raja*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

*Casablanca na Wydad Casablanca; ya tatu ni Tunis derby, Club Africanna Es Tunis; ya nne, ni Soweto derby kati ya Kaizer Chiefs na Orlando Pirates; ya tano ni Kariakoo derby, Afrika derby tano. Kariakoo derby ipo Simba na Yanga. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanatoka Kenya, watu wanatoka Uganda, watu wanatoka Congo, Zambia, watu wanatoka hata Ulaya kuja kuangalia *derby* ya Simba na Yanga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tusizichezee hizi timu, tuziimarishe, tuziboreshe, zinatangaza nchi zetu. Kitendo kilichotokea juzi hatukifurahii sana kwa sababu mechi ilikuwa inatambulika inachezwa saa 11. Timu moja ikaingia mitini, sasa hii na yenye we ni tatizo, mtu anatoka Kenya anajua mechi saa 11 unabadilisha inakuwa saa mbili usiku. (Makofi)

### **TAARIFA**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, hili suala nikuombe...

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Seif Gulamali, Taarifa.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, Simba haikuingia mtini ila walifuata maagizo yaliyokuwa yametolewa, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif pokea taarifa inasema kwamba Yanga walitia mpira kwapani. (Makofi)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, unaweza ukaona jinsi gani ambavyo..., tusipoteze ladha ya michezo hii kama tunaweza kuwatoa watu nchi za watu kuja hapa, wewe unaahirisha kienyeji enyeji sio kitu rahisi, mechi ile ni mechi kubwa. Leo unaona uwekezaji wa Azam kwenye tasnia

hii ya michezo hasa kuonesha ligi kuu, kwanza binafsi nampongeza sana Azam kwa kitendo chake cha kuwekeza mzigo mkubwa shilingi bilioni 225. Hili ni jambo la kupongezwa na tunahitaji kumlinda kuhakikisha kwamba anafanya kazi hii kwa uzalendo mkubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kutangaza ligi yetu inaonekana Rwanda, Zambia, Burundi ndio maana unapata watu wanakuja, isingeoneshwa watu wasingekuja. Kwa hiyo, unaweza kuona *impact*, sasa Serikali na wadau lazima tuone.

Mheshimiwa Spika, kingine kimegusiwa hapa namna gani ambavyo mpira unavyoendeshwa, lazima tuwe na shirkisho ambalo halina unazi. Mimi naweza nikawa na timu yangu, lakini inapofika suala la kusimamia michezo, usiweke unazi wako kwenye michezo, usipendelee. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tumeona baadhi ya viongozi wa shirkisho wamekuwa na upendeleo kwenye kusimamia ligi, tumeona kesi zikisimamiwa, wengine wakishtakiwa, kesho wanakaa kikao, hukumu inatoka, wengine wakipeleka kesi mzee mpaka leo, kuna kesi ya Morrison ilipelekwa na Yanga pale mpaka leo miezi saba hamna hukumu, hamna kikao, viongozi wanajifanya kama hawaoni vile.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la aibu hatuwezi kuona jambo hili linaendelea kuendeshwa kienyeji enyeji kama vile shirkisho la timu moja, haiwezekani. Lazima shirkisho lisimamie haki za timu zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jana tumeona wanaenda kupewa zawadi viongozi na vilabu vilivyopanda ligi kuu. Wakati kocha mmoja anakwenda pale amekuwa kocha bora wa ligi daraja la kwanza, anatoa mkono kwa kiongozi mkubwa wa shirkisho, kiongozi yuko *busy* na mambo yake, hataki kutoa mkono. Amebeba zawadi anaenda kumpa tena mkono kiongozi yuko *busy*, mara ya kwanza *it is okay*, mara ya pili tena! Tena kiongozi mkubwa wa shirkisho, ni aibu tusiweke unazi kwenye mashindano yetu, hii haiko sawa ni ubaguzi. (*Makof!*)

## TAARIFA

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nipende kusema...

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif kuna taarifa unapewa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kitendo hicho anachokisema ni kocha aliyekuwa ameshinda kuwa kocha bora katika ligi la kwanza na timu yake ya *Geita Gold Mine* imepanda inaingia ligi kuu Tanzania Bara. Wakati anapewa ushindi wake, kombe lake Rais wa *TFF* mara mbili amekataa kumpa mkono na tafsiri yake ulimwenguni kote michezo huwa hairuhusu kabisa masuala ya ubaguzi.

Kwa hiyo, tungependa kufahamu je. kwa sisi Tanzania tunachukuliaje masuala ya kibaguzi kwenye mchezo ambao unatuunganisha Watanzania? Ahsante. (*Makofii*)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo.

Mheshiwi Spika, tupunguze upendeleo, tupunguze unazi, hata marefa sasa wamekuwa inabidi ukipendelea timu fulani una halali, ukichezesha mechili fulani unakuwa na wakati mgumu, hatuwezi kwenda. Ili kuleta ubora wa ligi yetu haki inatakiwa itendeke na isimamiwe.

Mheshimiwa Spika, kingine, kwenye hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona kuna mashindano ambayo *CAF wameya-launch* hivi karibuni ya *Interschool Championship*. Ni mashindano ya Kiafrika ambayo shule za sekondari zitashiriki mashindano hayo kwa Afrika, sisi nafasi yetu kama

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Tanzania tumeji-position viyi kuweza kuchukua hii fursa na kuweza kupeleka vijana wetu kwenda kushiriki kwenye mashindano hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na timu yako lichukueni hili sijaona kwenye hotuba yenu, lakini chukueni hili mkalifanyie tafiti ili muweze kuona mnapeleka hizi timu ambazo zinashinda kwenye timu za UMISETA. Mpeleke hizo timu kama ikiwa Dar es Salaam, kama ikiwa Tabora mpeleke, naamini Tabora mwaka huu tutachukua hili kombe la UMISETA kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho napenda kuchangia, niwaombe tu Wabunge wenzangu kwamba kipindi cha kukaribia kampeni huwa tunachezesha sana ligi za mpira kwenye majimbo yetu. Niwaombe hii tusiilache, tuiendeleze, itatusaidia kuinua kiwango cha michezo kwa vijana wetu hasa tunakotoka. Tuwe na mashindano kama tutashindwa kwa mwaka mmoja basi, baada ya mwaka mmoja tunafanya. Ligi za vijiji, ligi za kata, ligi za wilaya zitasaidia kuboresha. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu na nakushukuru sana kwa muda wako. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri tunakushukuru sana. Naona Yanga wanalamika sana, hawataki mtuacheze tarehe 3 Julai, 2021. Baada ya mkuki wa juzi wa Namungo sasa wanahangaika kweli kweli, Mheshimiwa Seif pole sana. (*Makofi/Kicheko*)

Nilimtaja Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, ajiandae. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kuwapongeza sana *Simba Sports Club*, kwa kuweza kufika katika nafasi ya robo fainali ya kombe la Afrika kwa maana ya *African Champions League* na hili nichukue fursa hii vilevile kuwapongeza *Young African* kwa sababu kwa kitendo cha Simba kufika katika robo fainali itawafanya Yanga kama watafanikiwa, basi na wao kuwa na nafasi ya pili kwa maana ya kwenda katika mashindano ya *Champions League*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni nafasi ambayo imetengenezwa na Simba, kwa hiyo, niwapongeze sana na wao kama watafanikiwa basi wajue kwamba Simba imefanya kazi nzuri na wao kupata nafasi ya kwenda *Champions League*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee tu kuwaambia watu wa *CAF* ikiwezekana wabadilishe kanuni kwamba, anayefanikiwa kusababisha timu nyingine kwenda kwenye mashindano hayo, waangalie hizi kanuni upya isiwe nafasi ya pili ikiwezekana huyu aliyeshinda ndio achague nani wa kwenda naye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu haiwezekani mtu anayekuzomea, anapokea wageni ambao ni maadui zako ye ye ndio anawapokea *airport* na kuwa-*support* halafu mwisho wa siku tukishinda ye ye apate nafasi ya kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tutawaomba *CAF* waangalie namna nyingine ya kupanga kwasababu, haiwezekani anayetuzomea twende naye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niendelee na mchango wangu, niwaombe tu Watanzania wote, niwaombe Wabunge na watu wote kwa ujumla. Tunawanamuziki wazuri sana Afrika, lakini Diamond

ameonesha kuwa ni mwanamuziki ambaye ameonekana duniani kote na leo ametajwa kuwa ni mmoja wa wanamuziki bora duniani wanaokwenda kupigiwa kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Diamond katika ile *BET Award* yaani *Black Entertainment Award* ametajwa kwamba ni mmoja wa *nominee* yaani wanaopendekezwa wapigiwe kura. Na niseme tu walijotajwa duniani yuko mwanamziki anaitwa Aya Nakamura wa Ufaransa, Burna Boy wa Nigeria, Diamond wa Tanzania, Emicida wa Brazil, Headie One wa UK, Wizkid wa Nigeria, yaani sijui na nani mwingine huyo wa UK. Kuna Youssoupha wa Ufaransa. Kwa Afrika wapo watatu na kwa Afrika Mashariki ni mwanamuziki mmoja tu kutoka Tanzania ambaye ni Diamond Platinum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha ameanza kupata vikwazo tena kutoka kwa watanzania wenyewe na kibaya zaidi wanaingiza hadi masuala ya kisiasa, na kibaya zaidi wanamsema kwa sababu ali-support CCM, wana-CCM mliomo humu na wana-CCM Tanzania wote tumpigie kura Diamond. Sasa hivi sio suala la chama, hili ni suala la Tanzania, tumpigie kura nyingi, tumpigie kampeni aweze kushinda na hii atakuwa amekwenda kutanga nchi yetu katika nyanja za muziki duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niendelee na mchango wangu vilevile kuhusiana na masuala haya ya *TBC*. *TBC* wamefanya kazi nzuri, niishukuru Serikali imeweza kutoa shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuongeza usikivu wa *TBC*. Tunawaomba *TBC* hizo shilingi bilioni tano mlizopewa mzifanyie kazi usikivu uongezeka, wananchi wanataka kusikia habari za uhakika kutoka *TBC*. Kuna mikoa ambayo ipo pembezoni mwa nchi yetu usikivu sio mzuri wa *TBC*, watu wanasikia redio za nchi za jirani. Tunaomba muongeze usikivu ili kusudi watanzania waweze kupata habari za uhakika kutoka *TBC*.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo Mheshimiwa Tarimba alikuwa analiongea hapa kuhusiana na masuala ya mpira wa miguu. Ni lazima tufike sehemu tuamue kuna timu ya Taifa na mashindano ambayo yanashirikisha timu za

Taifa, lakini kuna ligi za ndani pamoja na *champions league* katika mabara yetu. Sisi Tanzania tuna Simba na Yanga zimejtangaza vizuri kuna Azam na timu nyingine. Vilevile kuna timu za Taifa ambazo kwa mfano timu za Nigeria na nchi nyingine wamekuwa na timu nzuri sana za Taifa. Niombe tu kueleza kwamba timu za ligi zinazocheza ligi, hii siyo mpira wa kawaida inaitwa *commercial football* ni mpira wa kibiashara. Uingereza leo hana timu nzuri kweli *World Cup*, lakini amejitangaza kwa maana ya ligi yake imekuwa ni ligi maarufu duniani na amejikita hapo tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo tunaona timu za Waingereza zimeingia fainali *champions league*, Chelsea na Manchester City na wanaingiza fedha nyingi sana. Hata sisi Afrika, Simba tumekomea robo fainali sawa, lakini Simba ingechukua ubingwa wa *champions league* ingeingiza fedha nyingi, ingetangaza Tanzania. *No matter what* katika timu ya Taifa hatuna timu nzuri, lakini tunapojikita kwenye *commercial football*/tunaangalia kwenye *champions league* tunakwenda kufanya nini. Sasa niwaomba *FFF*, niwaombe na Wizara msilimii sana wachezaji kuajiri wachezaji kutoka nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama Azam, kama Simba, kama Yanga amekwenda kwenye *commercial football* ambayo ni ligi kuu hapo ni biashara hata kama angeweza kuleta wachezaji kutoka sehemu nyingine alete lengo lake ni kwenda kushinda *champions league* ili aingize fedha atangaze na nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia timu kwa mfano ile timu ya Congo ile TP Mazembe ambayo ilikuwa inakwenda kushinda inakwenda kwenye *champions league* ilikuwa inaingiza wachezaji, ilikuwa inasajili wachezaji wakati mwingine hata timu nzima, angalia Real Madrid alikuwa anasajili wachezaji sio kutoka Spain, alikuwa anasajili wachezaji kutoka Portugal na maeneo mengine analenga kwenda kwenye *champions league* kwa sababu akishinda tayari anaingiza fedha na ameitangaza Spain.

Mheshimiwa Spika, sisi Simba tukishinda ni Tanzania *no matter* Morison anatoka wapi? Sasa tukitaka kutengeneza timu ya Taifa twende kwenye *football academy*.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, tutengeneza *football academy* hizo zitakwenda kutengeneza timu ya Taifa.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Unapewa taarifa Mheshimiwa Haroon Nyongo.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchangiaji kueleza vizuri sana lakini lengo la Serikali nakupa taarifa tu, ni kuimarisha ligi yetu na kuhakikisha vijana wetu ndio wanakuwa na uwezo mzuri kabisa kwa ajili ya soka letu hili badala ya kuleta vijana wengine kutoka nchi zingine. Nadhani lengo ndio hilo.

**SPIKA:** Je, uko tayari na vijana wa Tanzania wasiende nje pia kwenye nchi za wenzetu? Kwa taarifa hiyo unapewa Mheshimiwa Haroon Nyongo. (*Makofii*)

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana umeuliza swali la msingi zuri sana, kwamba je, wachezaji wetu wasiende nje?

Mheshimiwa Spika, leo Mbwana Samatta amekwenda kucheza huko nje, amekwenda kucheza hadi Aston Villa naomba niwaeleze mbona Samatta angepeleka Aston Villa ingekwenda kucheza *champions league* ya Ulaya ina maana ile timu ingeshinda wale wangejitungaza kama Waingereza wala siyo Mbwana Samatta kutoka Tanzania. *The same* na sisi timu yetu ikifika huko tutaitangaza kwamba ni Tanzania, Simba imeshinda au Yanga imeshinda iliyoshinda *champions league* ni timu kutoka Tanzania *no matter* hawa wachezaji waliomo humu wanatoka nje ya nchi nyiningine.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kingine timu ya Taifa ninachotaka kusema, tutengeneze *football academy* nzuri mzuri ni Zambia ilipopata ajali kule Gabon watu walivyofariki karibu timu nzima wale makocha walirudi kwenye *football academy* zao wakawa kumbe tayari wana-*infrastructure* nzuri ya kutengeneza wachezaji wao, wakatengeneza timu nyingine ikaenda kwenye mashindano hayo hayo na timu ile ikafika hadi fainali, ikaenda kufungwa na Nigeria. Wasingekuwa na *football academy* nzuri wasingekuwa na timu bora hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niwaeleze hakuna timu ya Taifa inayotengenezwa na timu za ligi, timu ya Taifa inatengenezwa na Serikali kwa kutengeneza miundombinu mizuri na walimu wazuri wanaoweza kutengeneza na ukishapata wachezaji wazuri utawauza sasa kwenye ligi yako ya ndani kwa maana hiyo inayochezwa *champions league* na wachezaji wengine utawauza nje ya nchi ikacheze kwenye vilabu vingine. Ukzungumzia timu ya Taifa ndio maana leo utaizungumzia Brazil na Ujeruman, lakini ukzungumzia ligi bora inayoweza kuifikisha timu kwenye *champions league* ni Uingereza. Watu tubadilishe *mindset* zetu, tuangalie kama tunaamua kwenda kwenye *commercial football* twende na kama tunaamua kutengeneza timu Taifa ni jukumu la Waziri na Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana mchezo wa Simba na Yanga; amezungumza kidogo Mheshimiwa Gulamali hapa. *Derby* ni mechii za watani wa jadi na hizi mara nyingi zinakuwa na sifa ya kukusanya watu wengi na kuteka hisia za watu. Ukichukua *ten derbies* za Afrika; ya kwanza alikuwa anajinanii hapa ya kwanza Al-Ahly pamoja na Zamalek; ya pili ni *Kaizer Chiefs* na *Orlando Pirates*; ya tatu ni *Club Africana* na *Esperance* ya Tunisia; ya nne ni *Wydad Casablanca* na *Raja Casablanca* za Sudan; ya tano kwa Afrika ni Simba na Yanga ambayo ni *Kariakoo derby* inafuatiwa na ya sita ya kule Kenya wanajiita *Mashemeji derby*. Hizi zinabeba hisia za watu na mara nyingi huwa zinasababisha fujo na sintofahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali ina jukumu la kulinda hizi mechi, mechi ya Simba na Yanga sio suala la vilabu ni suala la Serikali, lazima muangalie usalama, muzipe usalama na ulinzi wa kutosha. Kwa sababu hizi mechi zinavuta hisia za watu wapenzi wa mpira ndani na nje ya nchi. Kuna wapenzi kutoka Zambia, Kenya, Rwanda, Burundi walikuwa tayari kuangalia ile mechi ikasogezwa mbele, mimi nakubali kuwa Yanga walichukua uamuzi sahihi, lakini na wao wawe wazalendo ilisogezwa kwa masaa mawili wangevumulia tu wapate kichapo chao. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Hanje atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi nichangie na mimi katika Wizara ya Michezo na nitachangia kwenye upande wa maendeleo ya sekta ya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, tukizungumza michezo kwenye Taifa sio tu ni sehemu ya kujenga afya ya mwili, lakini michezo pia ni sehemu ya kutangaza nchi, lakini pia michezo ni sehemu ya kuimarisha umaja na mshikamano wa nchi; lakini pia michezo ni ajira hasa hasa kwa vijana kwa sababu tunajua hata wanamichezo wapo ambao wamekuwa wakipunguza muda wao ili waonekane kama ni vijana kwa sababu inaonekana michezo pia ni kwa ajili ya vijana, hasa *football* na mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa nchi yetu *TFF* ndio wamekuwa wasimamizi kwenye upande wa michezo wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mpira wa miguu Tanzania. Kwa hiyo, haitakuwa busara kama hatutazungumza yaliyopo kwenye *TFF*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 Tanzania ilikuwa mwenyeji kwenye mashindano ya vijana Barani Afrika - *AFCON* ambako Mheshimiwa Rais, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliatoa shilingi bilioni moja na mashirika mengine na taasisi walichanga kwa ajili ya kusaidia kufanikisha mashindano ya *AFCON* 2017. Lakini pia baada ya wageni kuja kulifanyika vitu vingi sana ambavyo kimsingi vililetta taharuki kwa *TFF* kiasi kwamba TAKUKURU waliingilia kati kwa ajili ya kwenda kuchunguza ubadhirifu wa fedha ambazo zilichangwa pamoja na fedha iliyotolewa na Mheshimiwa Rais kipindi kile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU walichunguza mpaka leo hatujajua nini kinaendelea, hatujapata *feedback* kujua nini kilionekana huko kwamba walikutwa na hatia au hawakukutwa na hatia. Naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha aeleze nini kilitokana na uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU kwa *TFF*ili kujua matumizi ya zile fedha, kwa sababu mpaka sasa hivi Hoteli ya *Holiday Inn* ambayo wachezaji walikwenda kufikia pale baadhi waliotoka nje inadai shilingi milioni 80. Kwa hiyo, nitapenda Waziri atuletee *feedback* nini kiliendelea ili Watanzania wajue, kwa sababu *TFF* kiukweli inalalamikiwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini mwezi Julai, *TFF* inakwenda kwenye uchaguzi; sasa hivi wamebadilisha Katiba yao, kinyume na Katiba ya nchi, kinyume cha *FIFA*, kinyume na *CAF* wameweka kigezo cha elimu cha juu kuliko inavyotakiwa. (*Makofii*)

Sasa tunapata dukuduku kidogo kuona kwamba kwa nini wanakaribia uchaguzi halafu wanabadilisha badilisha katiba bila ya kufuata utaratibu. Na Wizara hatujaisikia ikisema chochote kwenye hilo yaani *TFF* imekuwa kama ni dude kubwa hivi ambalo ni ligumu kulifikia, ni kama wanalindwa fulani nisiende huko sana, lakini tunataka tusikie Wizara inazungumza nini kuhusiana na *TFF* kubadilisha Katiba

yake kwenye suala la elimu, wameweka kiwangu tofauti kabisa hata na utaratibu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, lakini *TFF* imeonekana ikiwaonea baadhi ya viongozi wa michezo kwenye nchi. Nitatoa mfano wa Mwakalebela aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Yanga. Ukionekana unakosoa *TFF* unakuwa *labeled* kama mtu ambaye uko *against TFF* na wanakushughulikia vizuri. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat nimesikia kama kuna Taarifa. Aaah basi endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa *TFF* nitapenda Wizara wakati inafanya hitimisho itoe majibu kwenye hayo kwa kweli ni sehemu ambayo inaleta mtanziko mkubwa kwa watu ambao ni wapenda michezo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitazungumza kuhusiana na kukuza vipaji vyta wanamichezo wetu kwenye nchi. Tumezungumzwa kuhusiana na *sports academy*. Mimi nina fikra tofauti kidogo kwa sababu mimi ni muumini wa Tanzania, ninapenda michezo lakini pia ni muumini wa timu ya Taifa ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba timu ya Taifa inakuwa *constituted* na vilabu yaani na vilabu, kwa sababu ni miaka mingi tumezungumza tumesema kwamba tutengeneze *sports academy* kwenye nchi, lakini haifanikiwi, ninachojaribu ni kutoa *solution* ya tunaweza kufanya nini kutokana na *experience* ya nchi nyigine. Nigeria inaonekana inafanya vizuri sana kwenye michezo, lakini Nigeria hata zile *private sector* wana *football academy* nyingi na zinafanya vizuri na ndio Serikali inategemea huko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri badala ya kuimba kila siku tutaweka *football academy* ya *Taifa Stars* na haifanikiwi, nafikiri kuna haja ya kuwezesha hizi *sports academy* za *club* kama Namungo, Ruvu JKT huko kwa sababu tunategemea wanamichezo wetu watoke kwenye hizo klabu. Ni kweli

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwamba tunategemea pia nchi zingine kutuletea wanamichezo kwetu, lakini pia mimi nafikiri tutengeneze ndani zaidi kwa sababu ndio tunaowategemea na tuna-*feel proud*kama tutapata kina Samatta wengi zaidi maana yake ni faida pia kwa Taifa, kwanza anatangaza Taifa, lakini pia inaleta hamasa kwa vijana wengine ambao wanafanya michezo Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiri sasa Serikali kuna *sports academy* Tanzania nitazitaja na najua Waziri either anazifahamu au kama hazifahamu aangalie namna ambavyo unaweza kuzisaidia. Kwa upande wa shule, shule ya *Fountain Gate Academy*, *sports academy* wanafanya vizuri sasa hivi wameingiza timu ya wasichana *under 17*. Wanafanya vizuri sana na mnajua kuna *football academy* Morogoro na hapa ya *Fountain Gate*, *they doing very great* na hapa kwa kweli kwenye hilli nawapongeza pia *Simba Queens* chini ya uongozi wa Fatma Dewji kwa kweli wanafanya vizuri pamoja na kwamba mimi mwenyewe Simba tunawapongeza Simba wale. Lakini *Simba Queens* kwa sababu wanafanya vizuri sana *this time* tunawapongeza pia na nafikiri wanahitaji kupewa *support* kwa namna moja ama nyininge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna *sports academy* kama *Roho Sports Academy*, *Gymnastic Sports Academy*, *Dar es Salaam International Academy*, *A Future Stars Academy*, *Football Academy Arusha*, *Street Children Sports Academy*, *Faome Highway and...*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa Mbunge anayeongea sasa kwa kuwa amesema kwamba timu ya *Simba Queens Sports Club* inafanya vizuri sana na kwa misingi hiyo mimi nilikuwa nataka niseme kwamba angeendelea kuongelea kwamba hii timu

walau sisi Wabunge tungewachangia ili kuwatia motisha waendelee kufanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa msingi huo nimuombe Mheshimiwa Nusrat atoe hoja ili sisi tuiunge mkono na hawa vijana wetu, mabinti zetu waweze kupata motisha ili waweze kufanya vizuri zaidi. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Unapokea hiyo hoja Mheshimiwa Nusrat. (*Kicheko*)

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naipokea na kimsingi hili ni suala tunaweza pia kusema ni la Kibunge zima, kwa hiyo, Yanga pia watulie ikifika na wao hatua yao, kwa kweli hili kama itabidi tuweke utaratibu mzuri ili watu waichangie *Simba Queens*, kwa hiyo naipokea. Nafikiri niendelee kuchangia.

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu ya kukuza vipaji kwenye Taifa kwa masikitiko makubwa sana...

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Taarifa, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko upande gani.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Ipo hapa.

**SPIKA:** Haya nimekuona, endelea.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi naomba nimpe taarifa Mbunge anayechangia kwamba anapoipongeza Simba kufanya vizuri ajue kwamba kuna mwanamke lazima ampongeze pia Barbara kwamba wanawake sasa hivi hata Yanga wakimuweka mwanamke wanaweza wakafanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat unapokea taarifa hiyo kwamba wanawake mnaweza?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naipokea na nilimtaja Fatma Dewji kwa sababu ndio anasimamia *Simba Queens*, lakini Barbara ndio *top in charge* mwenyewe kwa hiyo tunampungeza. Yanga tulieni! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upande huo huo wa kukuza vipaji...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Hajaongea bado, subirini aongee ndio mumpe taarifa.

**MHE. NUSRAT SH. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naomba niende pia hapo hapo kwenye kukuza vipaji nasikitika sana kuna dada anaitwa Hadhara Charles Mjeje alishinda mashindano ya *football free style* ya danadana mnamfahamu, alishinda na anatoka Tanzania mpaka Rais Donald Trump alim-post, alifanya *video call* na Messi, walimpungeza sana na kuna baadhi ya makampuni walijitolea kuingia naye kwenye *contract* kwa ajili ya kutangaza bidhaa zao za michezo kwa sababu *she is really good*.

Mheshimiwa Spika, lakini nasikitika sana alikuwa amepata *deal* ya *ten years* akafanye na kampuni moja ya kutangaza bidhaa za michezo *South Africa*, lakini inaonekana Serikali iliomba ile kampuni ibadilishe muda isimuwekee *ten years* mpaka tunapozungumza yupo mtaani na juzi alikuwa anahojiwa, ana maisha magumu mno.

Mheshimiwa Spika, ina-*demoralised*, inashusha morali na ari ya vijana na wote watu wa Tanzania ambao wanajituma sana na wanavipaji ambavyo wamebarikiwa. (*Makofii*)

Sasa kuna siku moja ulizungumza kuhusu *less government* kwenye *intervention*, Serikali ni sehemu moja wapo ya kuweka *link* katika wananchi na yenyewe Serikali kwa maana ya utaratibu, lakini isiwe kikwazo cha kusaidia vijana wetu na wana michezo wetu kufanya vizuri kwenye Taifa. Kwa hiyo, nafikiri huyu sasa kwa sababu pia umri pengine umekwenda na nini, lakini ikitokea vijana wengine wana uwezo wa kufanya vizuri, tunahitaji sana kuwasaidia. Tunategemea Wizara iwe sehemu ya kuwa *-link* na kuwasidia kwa sababu wanatangaza nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi uki-*google* unaandika Mtanzania aliyepostiwa na Donald Trump, unaweza kusema ni kitu kidogo, lakini Tanzania imeshaingia kwenye hiyo *statement* Tanzania imeshaingia, lakini pia *is our very own*, ni wa kwetu, kwa hiyo vitu vya kwetu lazima viwe *protected* sasa *in the same spirit* tunaomba Diamond Platinum asaidiwe kuhakikisha kwamba anashinda tuzo anayogombea kwa sababu *in the name of the country*, ukiachana na hivi vitu vyote, kwanza ukweli usiopingika anafanya vizuri, huo ndio ukweli anafanya vizuri, *very good*. Kwa hiyo tuna sababu pia kila sababu ya kumsaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimalizie kwenye upande wa wasanii wetu, namna gani tunaweza tukalinda kazi za wasanii wetu na kwa kweli pamoja na mambo yote Serikali imekuwa ina mkono mzito sana kwenye kuwabana wakifanya vibaya. Lakini kwenye kuwasaidia imekuwa ni changamoto kubwa sana. Nashauri kuundwe chombo maalum ambacho kitakuwa kina waratibu wasanii wao, najua kuna vyombo vingi huko, lakini kuna mgawanyiko na ninyi mnajua kuna madudu mengi sana yanaendelea huko, wana mambo yao wenyeewe ndani wanajua kina Mwana FA.

Mheshimiwa Spika, lakini nafikiri pia kuna namna ambavyo hata kupiga kazi zao. Nashauri Serikali itoe mwongozo asilimia 80, yaani asilimia 100 ya kupiga nyimbo za wanamuziki duniani basi asilimia 80 zipigwe za Watanzania,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

zipigwe za kwetu. Hilo suala mnaliweza, ni suala tu la kutoa mwongozo.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji vijana wetu wanaofanya muziki wapate *coverage* kubwa na wajisikie fahari kufanya sanaa Tanzania. Ukweli ni kwamba Afrika Mashariki nchi ambayo inafanya sanaa nzuri ya uimbaji ni Tanzania. Wakenya wapo wanapiga tu kazi zetu kwenye *club* zao, redio zao na *television* zao kwa sababu tunafanya muziki mzuri. Kwa hiyo, ikawe pia ilete tija. Kamati imeshauri kuhusu *aggregation* na mimi nashauri na naongezea hapo hapo kwamba ili wapate kipato, wekeni utaratibu mzuri kuwasiliana na Wizara ya TEHAMA kuona namna gani wasanii wetu wanaweza wakapata faida kutokana na kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nategemea majibu ya maswali niliyowauliza Wizara kwenye masuala ya *TFF*, kwa kweli ni *very important*, tunahitaji kusikia mnazungumzaje kuhusu *TFF*. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Taletale na Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa ustawi wa Taifa letu la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hoja yake kwa umahiri mkubwa. Sambamba na hilo niwapongeze wasaidizi wote ambao wameifanya hii kazi na ikawa nzuri. (*Makofi*)

Sasa mimi nataka kuchangia katika maeneo makubwa mawili; eneo la kwanza la michezo na eneo la pili ni kuhusiana na suala zima la lugha ya Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikianzia na michezo, Wabunge wengi na kila Mbunge ambaye amesimama hapa

anazungumzia suala zima la michezo na lazima tukubali kwamba michezo ndiyo inayowapa raha Watanzania na ndiyo inayowapa raha watu mbalimbali duniani kote. Kila aliyesimama hapa amezungumzia Simba na Yanga. Hata humu kwenye Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, timu kubwa ambazo tunazungumzia, zinazungumziwa kama sio Simba, itazungumziwa timu ya Yanga. Kwa hiyo, niwapongezeni sana, tena sana kwa hoja nzito ambazo mmezitanguliza kuzitoa. Tunafarijika sana Watanzania hasa Yanga na Simba zinapoingia uwanjani. Hatimaye mmoja akashindwa na mmoja akashinda au mmoja akashinda na mwingine akashindwa, lakini baada ya hapo tunakuwa kitu kimoja udugu wetu unaendelea kustawi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la michezo kwenye suala la vifaa na wataalam. Tunajua kwamba kuna kitu kinaitwa UMISETA na kuna kitu kinaitwa UMITASHUMTA. Sasa tukianzia na UMITASHUMTA, ni ngazi ya mwanzo kabisa kule kwenye shule za msingi hasa zile shule zetu za awali. Sasa tukienda kule kitu ambacho ni changamoto kubwa ni vifaa, vifaa kule hakuna. Hakuna mipira, hakuna mikuki kwa ajili ya kurusha, hakuna visahani kwa ajili ya kutupa, hata viwanja vyenyewe ni mtihani mkubwa sana kwenye eneo la michezo. Kitu kikubwa na cha kushangaza mpira wa miguu ndiyo mpira unaopendwa, ukienda kwenye zile shule hata magoli hakuna. Ukienda wewe kama Mbunge unaambiwa sasa Mbunge tuletee magoli, Mbunge tuletee mpira, sasa mpira hiyo hata ukipeleka, magoli hakuna. Wanacheza nini? Hakuna cha kucheza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwenye bajeti hii ambayo imeidhinishwa, kwa ushauri wangu ni lazima tuangalie kwenye shule zetu za msingi na za sekondari kupeleka mipira pamoja na vifaa vingine vitakavyowasaidia watoto au wanafunzi kucheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hiyo ukiachana na vifaa vyatia michezo wa mpira, hakuna wataalam. Kwenye shule zile za msingi hata sekondari hakuna

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hata mwalimu wa michezo, yaani mwalimu tu mtafute huko mtaani au wapi sijui ndipo aende. Tunazungumzia leo timu ya Taifa, kama wale wasingekuwa na wataalam, hiyo timu ya Taifa ingeweza kupatikana? Au timu ya Yanga isingekuwa na wataalam wangefikia pale walipofikia? Au timu yetu ya Simba isingekuwa na wataalam wangefikia pale walipofikia? Isingewezekana! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujenga kitu, anzia kwenye ngazo ya shina kule. Hata Cchama chetu cha Mapinduzi watu wako shinani kule mpaka huko Taifani. Sasa tuanze kwenye shina kule kujenga hii michezo ili tuibue vipaji kwa ajili ya watoto hawa waendelee mbele ya safari. Hili ni muhimu sana katika ustawi wa michezo yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuchangia kwenye hilo eneo la michezo nataka nizungumzie kwenye suala la lugha. Tulizungumza hapa, lugha ni sauti za nasibu zinazobeba maana na zilizokubaliwa na jamii ya watu ili zitumike katika mawasiliano. Kwenye lugha hakuna lugha iliyokuwa bora zaidi ya lugha nyingine, isipokuwa lugha huongeza msamati wake. Lugha inakua na lugha inakufa, kufa kwa lugha ni kwa kutotumiwa na watu wengi duniani na kupunguza msamati wake. (*Makof!*)

Leo tukizungumzia suala la Kiingereza, sio lugha bora kulikoni lugha ya Kiswahili isipokuwa watu wengi wanazungumza. Tukizungumzia hali kadhalika Kifaransa, Kifaransa sio bora kuliko lugha nyingine isipokuwa Kiswahili chetu ni lugha bora na ziliwekwa hizo lugha kwa sababu ya kututawala. Sasa kama tuna lugha yetu kwa nini tusiitumie hiyo lugha yetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kutumia lugha ya Kiswahili na tuisikie tuna raha, amani kwamba tuna lugha yetu ambayo itazungumzwa ndani ya Bara letu la Afrika na watumiaji wa lugha hii ni wengi kweli. Siku hadi siku wanaongezeka duniani kote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mantiki hiyo au kwa muktadha huo kuna suala la wakalimani. Tumemsikia Mheshimiwa Waziri hapa anatueleza, wakalimani walipo wote jumla yake ni 45 tu na kati ya 45 hao 20 ndiyo wataalam, 25 wanahitaji usaidizi. Kwenye eneo hili ni lazima tutengeneze mkakati muhimu kuhakikisha kwamba wakalimani hawa wanaongezwa. Kwa mfano leo, Afrika nzima ikisema tunahitaji wakalimani wawili kila nchi, au hata mmoja tu ina maana kwamba hatuwezi kutosheleza mahitaji ya wakalimani kwa sababu tuna nchi zaidi ya 56 na wakalimani walipo ni 45. Tufafika kweli? Lugha ni biashara, wakalimani hawa ni biashara. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tukiongeza wakalimani bado tutaongeza fursa ya biashara ndani ya lugha yetu ya Kiswahili. Naomba hili lizingatiwe kwa umakini mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimesema nitachangia katika maeneo mawili tu wala sio mengi; la mwisho, kama tunavyofahamu na tunavyotambua Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli alisisitiza sana suala la lugha na sasahivi tunae Mama Samia Suluhu Hassan.

Ninachoomba na kushauri, katika wasaidizi wake, Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan kuwe na msaidizi maalum wa lugha ya Kiswahili kama walivyo washauri wengine katika eneo la siasa, uchumi na maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete. Mheshimiwa Hamisi Taletale atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman ajiandae. (*Makofii*)

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nashukuru, leo kwa mara ya kwanza

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

na mimi nachangia kwenye Wizara ambayo imenilea. Ni Wizara ambayo upande wa sanaa najua madudu wanasema kindakindaki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze na *COSOTA*. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri sisi tunafahamu wenzetu wa michezo wanaongoza michezo, mpira alikuwa kocha, alikuwa mchezaji lakini huku kwenye *COSOTA* sijui msomi kaoka wapi huko anakuja anaongoza *COSOTA*, hajui sheria ye ye yuko *busy* tu kutung'ang'aniza wananchi tuseme tunafuata sijui utamaduni. Sawa, hakuna mtu asiyetaka kuufuata utamaduni wa nchi yetu, lakini *COSOTA* tumewekewa mapolisi ambao wanakwenda kuua utamaduni wa nchi, wanakwenda kuua muziki wetu.

Mimi nina mfano mmoja ambao mwaka jana, hapa kidogo na-*declare interest*, mwanamuziki wangu Diamond Platinum wimbo wake wa *Hallelujah* ulizuiliwa usipigwe na *COSOTA*, mwaka huo huo mwishoni waandaaji wa filamu ya *Coming to America* wakauchukua ule wimbo kama wimbo bora. Sasa wimbo umeenda kuwa bora nje ya nchi, nchi yenye yenyewe yenyewe wimbo imeikataa. HaPa kuna walakin kwenye BASATA. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho naomba nzungumzie, wasanii wamekuwa wakilia sana sijui mirabaha, nini, hawalipwi. Leo hii *media* inalipa ili wasanii walipwe lakini *COSOTA* hawalipi. Mimi zamani nilikuwa napata pesa kutoka kwenye taasisi ya *MCSK* ipo Kenya na taasisi nyingine ya *SAMBRO* iko *South Africa*, *COSOTA* walipoenda kujejunga na *SAMBRO*, *MCSK* wasanii nchini hawalipwi. Hivi vitu viwili leo namwambia Waziri, nitamshikia shilingi mpaka nijue wasanii wanaanza kulipwa lini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo mimi kiukweli linaniuma kwa sababu sisi ambao tunafanya burudani za viwanjani tumekuwa tukipigia simu sana kwa babu zetu vijijini, leo ziba mvua, zuia mvua. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, suaona aseme kwamba kuna *sports arena* inakwenda kutengenezwa. Tumechoka kufanya *event* za wazi,

tunahangaika kuwapigia simu mababu vijijini wazuie mvua. /  
*am from Africa bro! (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo hii Rwanda ni nchi ambayo mpya tu leo hii wana *sports arena* yao, watu wa *NBA* wanakuja. Sisi hapa hatuna *sports arena*, sio tu hivyo wasanii wa Tanzania ni moja ya wasanii wakubwa *East Africa*, tunaongoza kwenye kila kitu. Tunapokosa kuwa na *sports arena* tunategemea kwenda kufanya *show* viwanjani, tunakosa kukuza sanaa yetu.

Leo hii nchi yetu Tanzania, hakuna asiyejua Afrika kama sisi ni *corona free*, wananchi wanaingia, tunakusanyika, hakuna tuzo za *MTV South Africa* kwa sababu watu hawakusanyiki. Wamekuja wanatuomba waje Tanzania lakini sisi tunawaambia hatuna *sports arena*. Wanashangaa, hee, hiyo nchi gani? Ni nchi ambayo ina uhuru, ina amani, viongozi wake tumekuwa tukiahidiwa tu tutajenga *sports arena*. Leo hii tumeenda kutafuta wawekezaji jamni twendeni tukatengeneze *sports arena* nchini kwetu. Lakini hivyo vigingi vilivyotokea hapo katikati. Sasa sijui ni Waziri hutaki tupate na sisi sehemu yetu ya kujistiri au samahani ingawa sio mtani wangu, lakini sijui na wewe unapenda tukakae vilingeni tuzuie mvua bila sababu. Kwa sababu kama unafanya *show* Dar es Salaam, Morogoro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka tulifanya *show* hapa uwanjani mwanzo mwisho ilikuwa ni mvua. Sasa inakuwa shida. Mimi nikumbushe kitu kimoja, mwaka juzi tulifanya *show* Sumbawanga, nakumbuka Mkuu wa Mkoa alinipa mganga wa mkoa, huyo mganga wa mkoa akaniambia hapa mvua itafungwa usiwe na wasiwasi. Ndani ya uwanja kulikuwa kuna wananchi 7,000; nje nina watu kubao. Sasa tukitaka kutoka na wasanii kwenda uwanjani ile mvua inatufuata shiiiiii, tukitaka kurudi inarudi. (*Makofi*)

Mheshimia Spika, tuliingia uwanjani kama unakumbuka ile *show* ambayo wasanii wangu walidumbukia, watateleza, wakadondoka. Hivi ni vitu ambavyo vinatumiza sisi, naongea kama natania, lakini Mheshimiwa Waziri

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

umezungumza bajeti yako yote sijakuona ukizungumzia *sports arena*. Mimi ni mmojawapo ambao nitakataa kuunga mkono bajeti yako kwa sababu naona hauungi mkono maendeleo ya muziki wa Tanzania. Kwa sababu hatuwezi, leo muziki umekua. Tunatoka hapa wasanii wanakwenda kufanya *show nje*...

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika. Taarifa.

**SPIKA:** Kuna Taarifa. Endelea.

### **T A A R I F A**

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa mzungumzaji kwamba Sumbawanga hatuna shida hiyo, siku nyingine akija, afuate utaratibu tu mambo yatakwenda sawa. (*Makofi*)

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa nimeipokea na kweli, shida hawana ila balaa lilikuwepo. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa kule Sumbawanga wake za watu tu, basi! Endelea. (*Kicheko*)

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, hivi ni vitu ambavyo vinatokea kwenye sanaa yetu. Kama Serikali inakosa kutufikiria kwenye suala zima la kuwa na ukumbi na Serikali inaandaa bajeti inakuja kutusomea bajeti mpaka inamaliza hajjatamka wala hajaonesha dhamira ya kwamba leo hii tutakuwa na sehemu ya sisi wasanii kwa ujumla kupata sehemu ya burudani, hii inasikitisha sana Mheshimiwa Waziri. Mimi nikuombe, nashindwa kukuambia uende ukajipange tena, ila jipange na Wizara yako tunahitaji kupata *sports arena* nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kuna kipindi nilizungumza na Katibu Mkuu wa Wizara yetu akaniambia wanapigania kuwa na *sports arena* Dodoma, Hee! Mheshimiwa siiombei hata Morogoro Kusini Mashariki wala Morogoro, iko wazi

kabisa mji wa burudani na starehe ni Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunatakiwa kama tunawaza kuwa na *sports arena*, lkakae Dar es Salaam. Isiende Morogoro, isije Dodoma lkakae Dar es Salaam. Lakini ikitokea leo hii tunakaa hapa, Mheshimiwa Waziri amesimama, amezungumza mpaka amemaliza bajeti yake sijaona azungumzie hicho kitu. Mimi inaniumiza, hakuna msanii asiyejua kama mimi ndiye ninayeongoza kufunga mvua. Kwa sababu ya mila zetu za Kiluguru, mimi ni mziwanda, mziwanda ndiyo mfunga mvua sio uchawi wa ushirikina, *I am from Africa!* Hilo liko wazi. (*Makofi*)

Naomba unipunguzie hii kazi Mheshimiwa Waziri, naomba unipunguzie hii kazi, inatuchosha. Mpaka unamaliza bajeti yako unazungumza sijaona ukizungumza kuhusu viwanja. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaomba tupate kiwanja na sisi wasanii wawepo *indoor*, wafanye burudani zao na usituletee kiwanja cha watu sijui 20,000/30,000 ikiwa tunakwenda nje ya nchi kama Mali na kadhalika tunajaza viwanja vya mpira leo hii tunataka kiwanja kikubwa cha burudani nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, cha mwisho kabisa hawa Marais wetu, kuna sijui Rais wa Ngumi, sijui Rais wa nini. Nchi yetu ina Rais mmoja tu, R ni moja tu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Waziri naomba hawa Marais, sijui wa Shirikisho, sijui *TFF*, zitoke wawe na vyeo vyao. Wanapunguza heshima ya neno Rais na wanaitoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu unamuona Rais kabisa Rais ana vumbi. Rais hawesi kuwa na kiatu kina vumbi. Tunatakiwa tuheshimu neno Rais. Eti Rais wa Wasafi! Hawesi kuwa Rais! (*Makofi*)

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amar nimekuona.

## TAARIFA

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji, kwa kweli, hili suala la Rais, hata sisi kule tuna Rais wa Wachimbaji, hili linakera sana. Nilikuwa nampa Taarifa hiyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa kweli jambo hili linakera. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa Marais, hata Yanga wana Rais wa Yanga, hii haiwezekani! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Babu Tale endelea bwana! (*Makofi*)

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, hili suala la Marais kwa kweli linakera. Tuache maana ya Rais ibakie kuwa moja, nchi ina R moja tu. Tuna Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anatokea Rais anasimama eti ye ye ni Rais, ana kiatu kina vumbi, ina maana Rais! Tuheshimu majina tunayopeana, ndio maana mimi nimejita babu, kwa sababu nikijua kabisa kama babu ni mzee, mimi ni mzee kwenye *industry* yangu ya *bongo fleva*, ni mzee kwenye *industry* ya *music in general*.

Mheshimiwa Waziri, milango yangu iko wazi, nakukaribisha ukihitaji ushauri wowote, ila nitakuonea huruma sana na wewe ukiwa katika watu ambao eti wasanii wakifanya kiki zao ninyi mkaziingilia mkazitamka. Nilimuona Mheshimiwa Naibu Waziri akizungumzia kiki ya mmoja wa wasanii wangu. Ilinisikitisha sana na nilikuambia kama nisingekuwa Mbunge angeona rangi ya pili ya tabia yangu. Lakini kwa sababu naona ah! Marekani kuna msanii anaitwa Sixnine Tekashi, ni mmoja ya wasanii kichaa, lakini moja ya msanii ambaye anatengeneza pesa kuliko wasanii wengine wote kwa kipindi hiki. Lazima tujue kutofautisha kiki ambayo inatengeneza pesa, kiki ambayo isiyotengeneza pesa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa wasanii wetu wanatuletea heshima, kikubwa wasivunje maadili. Ukiwa

kama Waziri au Naibu Waziri ukawa wewe sasa unakwenda kumzuwia msanii asifanye kile ambacho kinamtengenezea faida yake, wewe upo *busy* kama mtu unaonekana kama sasa unapinga maendeleo ya sanaa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe, nikuombe Mheshimiwa Waziri, hakuna kitu ambacho kinawaliza wasanii kama hiyo *system* yenu ya BASATA ya kumuona kila msanii kumfungia. Hii ni taasisi, tunaomba ipewe watu ambao wanahusiana na sanaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuunga mkono hoja mpaka ninapoona uwanja, *arena*. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamis Taletale, ahsante sana. Ahsante kwa makofi hayo.

Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ambayo hata mimi pia ni Wizara ambayo nimehusika kwenye kufanya kazi, kwa maana ya sekta ya michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili ya kuchangia kwenye Wizara hii, jambo la kwanza ni suala la soka, lakini suala la pili ni suala la BASATA.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza mwekezaji mkubwa aliyeingia kwenye mpira wa miguu, kwa maana ya *Azam Media Group* kwa kile kitendo alichokifanya ndani ya nchi yetu. *Azam Media Group* wamewekeza zaidi ya shilingi bilioni 225 kwenye soka la Tanzania na ndio kitu cha kwanza kimefanyika kwenye *East Africa*, hakuna nchi yoyote ambayo haki ya matangazo imepata shilingi bilioni 225 kwa wakati mmoja ni Tanzania tu imetokea, lakini tu kitendo hiki hakiipi manufaa soka, kitendo hiki kinaipatia Serikali shilingi bilioni 34 kama kodi, kitu ambacho kwa miaka yote hakijawahi tokea. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kattika kufanya hilo nataka nizungumzie suala la viwanja. Mwekezaji huyu amewekeza fedha zote hizi kwenye soka la Tanzania; ana tv production yenye quality nzuri kama tunaangalia premier league Uingereza, lakini viwanja tulivyonavyo vinatimua vumbi. Inatia hasara sana kwa sababu gani, leo hii tunazungumzia shilingi bilioni 34 ambayo Bakhresa anaenda kuipatia kama kodi nchi hii, bajeti ya Serikali ni shilingi bilioni 54 ya mwaka mzima ya Wizara ya Michezo, lakini bado Serikali haioni haja ya kuhakikisha viwanja hivi vinaenda kuwekwa mkeka ambayo Tanzania nzima tungekuwa tunajivunia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe mahesabu machache tu; kiwanja kimoja kuweka mkeka ni shilingi milioni 300; kwenye shilingi milioni 300 maana yake unazungumzia shilingi bilioni tatu ni viwanja 10 na shilingi bilioni sita ni viwanja 20 ambavyo unakuwa umemalliza nchi nzima. Tuiombe Serikali na hapa Mheshimiwa Waziri na nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na njiombe Serikali na nimuombe Rais, kama tumeweza kupata shilingi bilioni 34 kwa wakati mmoja tunashindwaje kutenga shilingi bilioni sita tu katika shilingi bilioni 34 tukaweka mkeka nchi nzima na tukawa tumefuta historia ya viwanja katika Taifa hili? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, inatia hasira na inasikitisha sana. Utakuja na hoja hapa kwamba hivi viwanja vinamilikiwa na CCM, inawezekanaje baba ambaye ni CCM anashindwa kuongea na mtoto ambaye ni Serikali ili Watanzania waweze kupata nyasi nzuri kwenye Taifa hili? Inawezekanaje? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kubaki kwenye michakato, michakato, michakato kuhusu viwanja. CCM kwenye sera yake/kwenye ilani inasema; tutaboresha mazingira ya michezo nchini. Michezo ipi nchini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na ukienda pia kwenye Sera ya Michezo ya mwaka 1995 inazungumzia suala la kuboresha viwanja nchini. Serikali inazungumzia kuboresha viwanja, CCM inazungumzia kuboresha viwanja, lakini nenda Jamhuri pale

Dodoma angalia, Wabunge tunafanya mazoezi kwenye vumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuiombe Serikali na nikucombe Rais, shilingi bilioni 34 atupe bilioni sita tu. Haya mambo ya *negotiation* kati ya CCM na Serikali yabaki kwao sisi tuone nyasi zinacheza, watoto wa Kitanzania wacheze mpira sehemu nzuri. (*Makofi*)

Mimi nikucombe Mheshimiwa Waziri una fursa ya kuandika historia kwenye Taifa hili, una fursa ya kufanya vijana wote wa Tanzania wakusifie, nenda ongea na Rais, ongea na Wizara ya Fedha wakupatie shilingi bilioni sita, weka viwanja...

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa. Endelea nimekuruhusu.

## TAARIFA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji katika hoja yake ya viwanja. Yaani hivyo viwanja vya mpira ndio vimegeuzwa pia sasa viwanja vya kila maonesho, viwanja vya bongo *flavor* kama anavyosema Babu Tale, viwanja vya *gospel*, yaani kila mtu anayetaka kufanya kitu chake anaenda kwenye hivyo viwanja vya mpira. Na matokeo yake ndio haya ambayo tunaona sasa fedha imewekezwa, lakini wapi tutachezea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa yake kwa sababu ni kweli na amesahau tu kusema pia hata gwaride la majeshi linafanyikia kwenye viwanja hivyo hivyo. Tungekuwa na viwanja ambavyo vina nyasi za bandia, mnazungumza viwanja vyenye nyasi za bandia visingekuwa vinaharibika kama ambavyo vinaharibika hivi. Leo hii ukipanda nyasi kesho kutwa JKT wameingia wanapiga gwaride, nyasi zimekanyagwa zote zimeisha. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, tuiombe Serikali angalieni haja, michakato kati ya CCM na Serikali isituumize Watanzania tunaopenda mpira kwenye Taifa hili. Tunaomba shilingi bilioni sita katika shilingi bilioni 34 ambazo mmezipata Serikali mtuwekee viwanja *carpet* tumalizane na nyie endeleeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alijenga viwanja Taifa hili kila kona. Leo wakikwambia utafute uwanja kama wa Jamhuri hapa Dodoma ujenge, utapata sehemu gani ya kujenga uwanja mkubwa kama ule? Nenda Mkwakwani, nenda Sokoine, nenda Ali Hassan Mwinyi pale Tabora, lakini nenda CCM Kirumba wakwambie leo jenga, Nyerere alijenga, sisi Taifa la leo tunashindwa? Watu milioni 55 tunashindwa kuweka nyasi za bandia kwenye Taifa hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Nyerere ameweke majengo yote yale tunakaa. Kwa kweli, niombe Mheshimiwa Waziri, nitashika shilingi kama haya mambo hamtayaafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nipende kuzungumzia, sitakuwa na mambo mengi; jambo lingine ni suala la BASATA. Ukiangalia BASATA ni Baraza la Sanaa la Taifa, lakini saa hizi imegeuka ni Mahakama ya Sanaa ya Taifa, kitu ambacho mimi niseme kitu kimoja, wasanii wa nchi hii asilimia 90 wamejipambania wao wenyewe hadi pale walipofikia na si kwa jitihada za sekta ya Wizara ya Michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo Diamond ametoka si kwa sababu alipita Chuo cha Bagamoyo, leo Ali Kiba ametoka si kwa sababu alipita Chuo cha Muziki Bagamoyo, ametoka kwa jitihada zake, lakini BASATA wanatengeneza urasimu wa kwamba waanze kuweka kwamba wimbo kabla haujatoka lazima upitie kwao, ukaguliwe ili waangalie ubora wa huo wimbo. Hiki kitu ni mlango, hili ni dirisha la kuwaumiza wasanii; ndio maana nasema ni mahakama, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, leo hii kama kuna mtu ana bifu (ugomvi) na Ali Kiba, Ali Kiba akitoa wimbo huyo mtu anazunguka BASATA anawapa hela BASATA wanazuia ule wimbo. Tunatengeneza wizi, katika hili nimheshimu Mheshimiwa Waziri kwa sababu alilingilia kati akajenga heshima kwenye nchi, hali imetulia. Msingefanya vile mnataka kumgombanisha Rais na wasanii wa Tanzania hii kwa uzembe wa BASATA. BASATA kazi zake ilizonazo, kazi ambazo BASATA wanazo ni kusimamia maendeleo ya muziki wala sio kufungia wasanii na wala sio kufungia muziki kwenye Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, unapomfungia Diamond, diamond peke yake unapomfungia maana yake umefungia wasanii wengine walioko nyuma yake, maana yake umefungia *producer* wa muziki, maana yake umefungia *bodyguards* wake, maana yake umefungia shughuli nyingi asimame asifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa tutakuwa tunazalisha wasanii au tunaonesha? Ndio zile sheria ambazo ulisema ni za kikoloni, zimejikita kwenye kudhibiti kuliko *ku-facilitate* wasanii wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuombe BASATA hawana jukumu lingine la kufanya Taifa hili zaidi kusimamia muziki uwe bora. Diamond amefika pale si kwa ajili ya nguvu ya BASATA, leo hii Ali Kiba amefika pale si kwa ajili ya nguvu ya BASATA, wala Harmonize alipo si kwa ajili ya nguvu ya BASATA. BASATA wasimamie tu maudhui kama wimbo ni mbovu wausimamishe, waurekebishe uendelee kufanya kazi, lakini hili jambo ambalo nyie BASATA mnalifanya hatutawaacha, hatutawaacha salama...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, nimekuruhusu Mheshimiwa Saashisha.

## TAARIFA

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka kumpa msemaji tTaarifa kwamba pamoja na mchango wake mzuri na kule kwetu Hai tuna vipaji vya kutosha, wasanii wa kila aina, lakini mpaka sasa hivi BASATA imeshindwa kutusaidia. Sasa nilikuwa namwambia tu kwenye hoja yake aiombe Serikali, BASATA wawekwe pembeni tutafute chombo ambacho kinaweza kutusaidia, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Unapokea Taarifa hiyo Mheshimiwa Sanga?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, BASATA hawana *manpower* ya kuchunguza huo muziki ni bora au sio bora. BASATA hawana miundombinu yoyote ya kuchunguza huo muziki ni bora, wanatengeneza dirisha la kuwaonea wasanii wetu katika nchi hii na mimi naungananae kwamba tutafute chombo kingine ambacho kitakuwa na *manpower* inayojua muziki, imesomea muziki, kitakuwa na watu wataalam wanaojua muziki ili wawzeze kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini mambo mengine sina la kuzungumza, zaidi niungane na Mbunge wa Morogoro kwamba, nchi hii bila *arena* ni ukoloni. Bila *arena* nchi hii tunakuwa tumbaki sehemu ambayo haina maendeleo. Dare es Salaam tunahitaji *arena* ya michezo, *sports arena*, Dar es Salaam ya watu 60,000; watu 50,000. Rais akitaka kuongea na Taifa hili Uwanja wa Taifa, mvua ikinyesha watu wanaanza kukimbia. Tafuteni *arena* ambayo Rais akitaka kuongea na watu mnaingia mle ndani mvua inyeshe au isinyeshe Rais anazungumza na wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pli, leo *boxing* inakua, mtafanya sehemu gani? Vikumbi vyenyewe vya watu 2,000/ watu 1,000. Tafuteni *Tanzania Arena*, andikeni hata *JPM Arena*

au *Samia Arena* halafu mwisho wa siku Watanzania watawakumbuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante, lakini sitaunga mkono hoja hadi pale ambapo mtatupa majibu kuhusu BASATA na kile ambacho wanakifanya. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Wasiojua *arena* jamani ni kitu kama, hii ndio *arena* ya Spika hii. Eeh, hii *arena* mojawapo hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, utafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kuwa mionganoni mwa wachangiaji kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Kwa niaba ya watu wa Chakechake na mimi ninaunga mkono hoja hii kutoka mwanzo wa uwasilishaji wangu, lakini nitakuwa na ushauri kidogo kwa Wizara hii kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kwenye ushauri wangu binafsi nichukue nafasi hii kwanza kutoa pongezi kwa bondia Hassan Mwakinyo kutokana na ushindi alioupata juzi baada ya kumpiga bondia Muangola kwa *KO*. Analipeperusha bendera ya Tanzania vizuri, Watanzania tuko nyuma yake na tunamuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili nitoe pongezi kwa msanii wa kizazi kipywa wa Tanzania, Nasib Abdul *a.k.a.* Diamond Platnumz kwa kuwekwa kwenye *nomination* ya *Best International Act* kwenye tuzo za *BET*. Nayo ni hatua kubwa na ya kupigiwa mfano. Na mimi niahidi kwamba nitampigia kura na kuwashauri Wabunge wenzangu tuungane kwa pamoja na Watanzania wote tumpigie kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, simpigii kura kwa sababu ni msanini tu, Diamond ni *icon* inayoamsha *dreams* za vijana wengi walioko nje ya muziki; ndio *definition* ya *hard working*,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

vijana wengi wanapotaka kujifunza kuhusu *hard working* na *commitment* kwenye tasnia au fani zao wanaweza wakamuangalia Diamond kama mfano. Kwa hiyo, hiyo inanipa mimi hiyo hamu ya kutaka kupiga kura kumpigia kura, ili apate kushinda imtie moyo kuendelea zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la tatu natoa shukrani kwa uongozi mzima wa *GSM* jinsi unavyoendelea kuishika Yanga na kutushika mkono kwenye kipindi hiki cha mpito, tunaelekea kwenye mabadiliko ya uongozi wa klubu wameeendelea kut-support kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, pongezi pia ziende kwa *Mr. Ghalib Salim Said* na uongozi mzima wa *GSM*, Mungu awajalie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za nne ziende kwa *Azam Media Limited*, wameuheshimisha mpira wa Tanzania. Mkataba wa shillingi billioni 225.6 unaenda kuongeza thamani ya ligi kuu ya Tanzania. Unaenda kuvitendea haki vilabu vyote vinavyoshiriki ligi ya Tanzania, vilabu 16, sio tu timu kubwa za Simba na Yanga. Vilabu vyote vinavyoshiriki ligi ya Tanzania sasa kutohana na mkataba huu vitakuwa vina uwezo wa kupokea shillingi milioni 500 kabla ya msimu, hizi ni nyngi na zitawasaidia vilabu vidogo hasa ambavyo vipato vyao bado viko chini kuweza kujikimu na kuondokana na umasikini wa vilabu vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia wameutendea haki mpira wa Tanzania kwa sababu kwa mujibu wa mkataba huu *coverage* ya uoneshaji wa mpira inaenda kuwa asilimia 99 sasa. Kwa hiyo, tunaenda kuungalia mpira wa Tanzania kwa asilimia 99, hii ni heshima kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na niipongeze *TFF* kwa kukubali hiyo *tender* na mkataba huu kuingia na *Azam* ni *media* ya nyumbani, kodi inarudi nyumbani kwa hiyo, ni heshima kubwa sana kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka mchango wangu nijikite kwenye mpira wa miguu. sisi wengine kileo chetu, hatuna starehe nyngine, kileo chetu ni mpira, aidha tuchaze

au tuangalie, tuzungumzie, yaani kitu chochote kinachohusiana na mpira, kwa hiyo mpira umekuwa ni sehemu ya maisha yetu tunavyotoka mpaka tulipo sasa. Moja katika kitu kinachotusononesha sana ukiaa ni kuangalia timu yetu ya Taifa, kwa kweli hatufanyi vizuri kwenye *football*, lakini nakusudia, hatufanyi vizuri. Tunapata *progress*, lakini haiendi kwa kasi tunayoitarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ili tupate maendeleo kwenye mpira ni lazima tukubali kuwekeza kwenye mpira, nakusudia *investment* kwenye mpira. Hatujawa *serious* kwenye kufanya *investment* kubwa kwenye mpira. Wenzetu wa Burundi na Mauritius wanapiga maendeleo makubwa kwenye soka, wanaleta *revolution* kubwa kwenye soka. Baada ya miaka mitano mbele tutakuja kushangaa watakafokia na yote ni *investment*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpira ni *profession*, ni fani kama *u-engineer*, kama udaktari, kama ualimu, tusipowekeza tutakuwa tunajidanganya. Kama tuna uwezo wa kuchukua madaktari wetu kuwapeleka Urusi wakakae miaka mitano tunawalipia kwa pesa za Bodi ya Mikopo, kama tuna uwezo wa kuchukua *ma-engineer* kuwapeleka Japan, China, kuchukua madaktari kuwapeleka India wakakae miaka mitano ili tuje tubadilishe fani ya udaktari tuwe na *ma-professional* kwenye fani, *the same ina-apply* kwenye mpira. Hakuna ubabaishaji, tukitaka *shortcut* ndio tunapoharibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Burundi wanachukua watoto wa miaka 11, wameingia mkataba na nchi za Scandnavia pamoja na Algeria, wanachukua watoto wao wenye *talents*, vipaji vyta mpira wenye umri wa miaka 11 mpaka 14 wanapelekwa Algeria na Scandnavia, wanakaa huko kuchenza, wako *academy* huko na *federations* ndio zinalipia gharama za kuwaweka huko. Tunalilia hatuna *academy*, hatujajenga *academy*, lakini wako duniani watu wanazo *academy*, tuwachukue hawa vijana wetu tuwapeleke kwenye hizo *academy* zilizoko duniani. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, ukichukua vijana watano ukawapeleka *academy PSG* - Ufaransa, watano wenyе umri wa kati ya miaka 14, 15, 16, baada ya miaka mitano unapata watoto wasiopungua 30 wacheza mpira *professional* ambao watakuja kuipa nguvu timu yetu ya Taifa. Na sisi ifike wakati tuwe na timu ya Taifa ukikaa nyumbani kutizama timu ya Tanzania inacheza, una soda, unakunywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sasahivi moyo, sisi wengine tuna maradhi ya moyo. Sisi wengine tuna maradhi ya moyo, yaani hatutabiriki, mara unapata maradhi. Leo tunacheza vizuri, kesho pasua kichwa. Maana yake sisi tunataka kuziba ma-gap kwa kuweka viraka viraka, mpira ni uwekezaji, ni *professional*, hakuna *shortcut*. Ni lazima tuweke *strategy* za muda mrefu, bora tuumie miaka mitano hii, lakini baada ya miaka kumi tuje kustarehe... (*Makofi*)

**SPIKA:** Poleni sana Yanga, ugonjwa wa moyo jamani. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, baada ya miaka kumi tuje tukae tukistarehe tukiangalia timu yetu ya Taifa. Sasa hivi mpira unachezwа na vijana wenyе umri mdogo ndio wenyе *market*. Ukisema mpira duniani sasa hivi unazungumzia uchumi. Wachezaji unalipwa kwa wiki *pound* laki moja, ni fedha nyingi. Watu ni *fulltime job*. Soka imekuwa *fulltime job* za watu hawafanyi kazi nyingine yoyote, ni mpira tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nikiiliza Wizara wanajua nini kuhusiana na Kevin John? Wanaweza wasiwe na majibu.

Mheshimiwa Spika, Kevin John kapelekwa Genk, alipofika Genk wameshindwa kuingia nae *senior contract* kwa sababu ya umri. Wamemchukua wenyeewe Genk wamempeleka Uingereza, *Leicester School*, akae Leicester, asome lugha na vitu vingine ajue, apate ile *general knowledge*, halafu muda ukifika wa kuingia *contract* atarudi Genk. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapolalamika kwenye mifumo na sera zetu za elimu, baadhi ya wakati na ajira za vijana wetu tunaweza tukaweka *academy*, sio lazima tusome *chemistry*, tuwalazimishe watoto wasome *physics*, wasome, unaweza ukawaweka *academy* ukawapa *general knowledge* ya kuyainua maisha tu na lugha. Yaani wakawa wamebobeia mtu anajua lugha tano, sita, ikamtosha yeye kuwa aki-*fail* kwenye mpira anarudi huku kumsaidia kwenye maisha yake ya kawaida hizo lugha sio lazima tung'ang'anie vijana wetu lazima... (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ramadhan Suleiman.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Pole sana Mheshimiwa Ramadhani kwa mioyo, mioyo ina na ndio maana leo ninawapa nafasi zaidi Yanga. Sasa anaafuata Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Yanga mwingine. (*Kicheko/Makofii*)

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii; la kwanza ambalo ninataka nianze nalo naiomba Serikali sasa ni wakati muafaka kwa kuanza kutenga bajeti kuzisaidia timu zetu za Taifa. Ukienda duniani kote Serikali inazibeba timu za Taifa, ni Tanzania peke yake kwa sisi hapa Afrika ambapo timu ya Taifa inakwenda kwenye mashindano makubwa pasipokuwa na utaratibu maalum wa kuwasaidia kufika huko, wanakwenda kwa kuunga unga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo ninaiomba Serikali ione haja ya kuanza kutenga bajeti kubwa wafanye uwekezaji mkubwa msiishie kuwapa bendera tu wakati wanaondoka lakini msimamie pia na maandalizi yao. Nchi nyingi zinasaidia timu zao, Mheshimiwa Waziri nikuombe katika hili kama kweli tunataka *Taifa Star* na timu nyingine zifanya vizuri lazima tuwekeze, wakienda hivi wanavyoenda kila siku tutakuwa tunawaita kichwa cha mwendawazimu na vilevile tutakuwa hatuwatendei haki kwa sababu maandalizi yao hayaendani

na kile ambacho sisi tunakitarajia. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri katika hili m jitahidi sana kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya timu zetu mbalimbali za Taifa, hii itatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili naomba niungane na hoja ya Mheshimiwa Sanga na Wabunge wengine wote waliochangia juu ya miundombinu ya viwanja vyetu. Ninaanza kwa kuwapongeza kwanza Azam kwa uwekezaji mkubwa sana ambao wameufanya, Azam hivi sasa ukiangalia mpira ukioneshwa Azam kwenye *HD* ni kama unaangalia ligi ya Uingereza kwa namna ambavyo kamera wanazozitumia na uwekezaji mkubwa ambao wameufanya ni uwekezaji mkubwa sana, lakini ukienda katika aina za viwanja vyetu ukiondoa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam; ukiondoa uwanja wa Kaitaba, Kagera, hivyo ndivyo viwanja ambavyo mpira unaweza ukachezwa watu wakauna vingine vyote mpira una kuwa *unpredictable* kwa sababu mchezaji huwa anajua mpira ukidunda hapa unadondokea pale, lakini kwa aina ya viwanja tulivyonyavyo huwezi kujua mpira unadondokea wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na muda mwingine unaweza ukawalaumu watu wa viwango vibovu kwa sababu ya aina ya miundombinu ya viwanja tulivyonyavyo. Haiwezekani tukawa tunaonesha ligi ambayo viwanja vyake vina vumbi hatueleweki, niiombe Serikali la kwanza kabisa kama Mheshimiwa Sanga alivyochangia tuiombe Wizara mkae na Chama cha Mapinduzi ambao ndio wanamiliki viwanja hivi mzungumze kwa pamoja ili tuone namna nzuri ya ujenzi wa viwanja hivi kupitia nyasi za bandia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa hakuna mtu anaweza kuleta nyasi za bandia hapa nchini isipokuwa Azam, Mo Dewji na watu wengine wenye uwezo mkubwa kwa sababu ya ghamama kubwa. Kodi ya nyasi za bandia zinawavunja watu moyo na ukiangalia katika vyanzo vya mapato, mapato ya kodi ya nyasi bandia siyo ni chanzo kikuu sana kwa Serikali, hata leo mkiondoa haina athari hasi katika mapato ya Taifa letu, kwa sababu katika miaka mitano

anaweza akaingiza mtu mmoja nyasi bandia, lakini leo mtu akiingiza nyasi bandia hapa nchini Tanzania za shilingi 200,000,000 ikiwa gharama yake hiyo maana yake lazima alipe asilimia 42 ya tozo ikiwemo *excise duty* na VAT.

Mheshimiwa Spika, *excise duty* ni asilimia 25 ya manunuzi ya ile bidhaa, lakini na VAT ni asilimia 18, kwa hiyo, mtu akitaka kuingiza leo majani ya nyasi bandia kwa ajili ya uwanja maana yake ni lazima akiwa na shilingi milioni 200 atafute shilingi milioni 84 nyingine kwa ajili ya kodi tu, hakuna mtu anayeweza kufanya hii.

Niombe Serikali na bahati nzuri Wizara ya Fedha ipo chini ya Mheshimiwa Mwigulu mwana michezo, Naibu Waziri vilevile Masauni ni mwana michezo kaeni mliangalie hili, twendeni tukatoe kodi kwenye nyasi bandia. (*Makofii*)

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

## TAARIFA

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumpa taarifa mzungumzaji anachokizungumza ni kitu sahihi na bahati nzuri ni kwamba kwenye sera ya michezo ukurasa namba 43 unasema vifaa vya michezo pamoja na malighafi za kutengenezea michezo zitozwe kodi nafuu, kwa hiyo, ninampa taarifa kwamba hili linawezekana Wizara ya Michezo na Wizara ya Fedha zikiamua.

**SPIKA:** Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Anthony.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea kwa mikono miwili niombe sana Serikali iliangalie hili ili tuboreshe viwanja yetu vya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni *sports arena* Mheshimiwa Waziri na mimi nilitegemea ningeona kwenye hotuba yako, dunia ya leo ndio imekwenda huko Mheshimiwa Waziri na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

bahati nzuri Mheshimiwa Innocent wewe una *exposure* kubwa sana umekaa Marekani unafahamu hizi vitu, duniani kote ndio tunaelekea huko hivi sasa, leo *Kigali arena* yenye uwezo wa kuingiza watu 10,000 tu leo ndio mashinano ya ligi ya *basketball* ya Afrika yanafanyikia pale Rwanda ambayo yameitangaza Rwanda dunia nzima inajua Rwanda kwa sababu ya arena tu ya watu 10,000 pale Amahoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rwanda wamejenga kwa kutumia kampuni kutoka Uturuki, ni *PPP*, ni Shirika la Nyumba la Rwanda Wizara na ile kampuni wamejenga arena hiyo leo Rwanda inafahamika dunia nzima kwa sababu ya *basketball* na *NBA* wale wanaoandaa mashindano kule Marekani wametia mkono wao, kwa hiyo, hivi sasa zaidi ya *viewers* milioni 450 wanafuatilia mashindano ya *basketball* pale Rwanda. Hii ni sehemu yetu pia na sisi kujitangaza kama tunalipa fedha nyingi kwa ajili ya kujitangaza kwenye utalii huu ndio utalii wenyewe. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tuone namna sasa ya kwenda huko na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, amesema Mheshimiwa Babu Tale hapa, matamasha yetu mengi yanafanyikia katika viwanda vya wazi na Mheshimiwa Waziri bahati nzuri tulikuwa wote siku zile katika *Urithi Festival*, mvua ilitunyeshea Uwanja wa Jamhuri tukakimbia wote, tulijibanza wote Mheshimiwa Waziri kwenye vibanda vya maonesho kwa sababu ya mvua, tutoke huko tuingie katika *sports arena* na mimi nitafurahi kuona katika bajeti hii...

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Anthony.

## **T A A R I F A**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, mdogo wangu Mheshimiwa Anthony Mavunde ninasema kwamba lile eneo la kujenga *sports arena* liko Temeke pale Mwembe Yanga, lipo tayari, karibuni sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anthony taarifa hiyo.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa niiombe Serikali kwa ajili ya utekelezaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kupitia hivi vitu ndio tunaitangaza nchi yetu hata kwenye utalii leo nataka niwapongeze sana timu ya *Simba Sports Club* kwa kuva tu *visit Tanzania*, Afrika wameiona Tanzania. (*Makof!*)

Kwa hiyo, Serikali mnayo nafasi kubwa sana mkikaa pamoja katika kuhakikisha kwamba hata kwenye utalii tutumie michezo pia na wasanii wetu leo Diamond ana *followers* milioni 12 kwenye *instagram*, Diamond ndio msanii pekee Tanzania amefanya Tamasha Ouagadougou, Burkina Faso ya kuzaja watu 100,000 akarudia mara mbili ndani ya masaa 24; huyu akienda pale na nembo ya Tanzania. Tanzania inajulikana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba mliangalie hili, mkae pamoja katika kuhakikisha kwamba pia michezo inakuwa sehemu ya utalii ouagadougou

Lakini Mheshimiwa Waziri nimeangalia katika hotuba yako ukurasa wa 46 umesema kwa uchache sana kuhusu uwanja wa mpira wa miguu Dodoma pale Nzuguni. Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini pia mambo yote ya michoro yamekamilika, ujenzi wa uwanja mkubwa wa mpira wa miguu pale Nzuguni, uwanja huu ukijengwa utakuwa mkubwa kuliko yote Afrika Mashariki na Kati, kwa hivi sasa ni viwanja viwili tu vinauvezo wa kubeba watu 60,000 kwa wakati mmoja ni uwanja wa Moi Kasarani pale Kenya na Uwanja wa Benjamin Mkapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini uwanja wa Dodoma ukijengwa utakuwa una uwezo wa kuwakalisha watu 80,000 kwa wakati mmoja. Nikuombe Mheshimiwa Waziri sijaona namna yoyote ambapo jambo hili linakwenda kutekeleza isipokuwa tu mmesema mnaratibu katika ukurasa 46 wa

hotuba yako. Wananchi wa Dodoma wana hamu sana kusikia hatua ya uwanja huu imefikia wapi, nitakuomba ukija ku-*windup* utuambie sisi wananchi wa Dodoma tujue uwanja huu wa mpira wa miguu umefikia wapi ili tupunguze adha ya uwanja wa Jamhuri ambao hivi sasa tunavyozungumza hivi sasa kuna maonesho pale ya *NACTE* na *TPSF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, majukwaa yamekaa mpaka katika *pitch* ya kuchezea mpira ambayo ni changamoto kubwa sana kwa sisi kwetu ambaao tunaosimamia uwanja ule. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri uwanja huu ukijengwa mwingine utakuwa na manufaa makubwa sana, lakini vilevile itafanya nchi nyngine zije zicheze hapa kufanya mazoezi; Brazil walishakuja kucheza katika uwanja wa Benjamin Mkapa mkiwa mna viwanja vizuri maana yake pia ni sehemu ya kutangaza nchi yetu ya Tanzania na watu wakaja kutumia viwanja hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nichukue fursa hii kuendelea kutoa rai kwa watu wengi zaidi kuwekeza kwenye michezo, uwekezaji wa kwenye michezo ndio utakaotutoa hapa kutupeleka mbele, ni ukweli ambaao upo dhahiri kabisa kwamba hatuwezi kuendelea pasipo uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii niwashukuru wafuatao ambaao wameleta chachu kwenye uwekezaji hapa nchini, wa kwanza nataka niwashukuru sana kampuni ya Azam kupitia Said Salim Bakhresa kwa uwekezaji mkubwa sana ambaao ameufanya, lakini la pili nataka nimpongeze sana Mohamed Dewji kwa uwekezaji mkubwa ambaao ameufanya kupitia Klabu ya Simba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nimpongeze sana Ghalib Said Mohamed wa *GSM* kwa uwekezaji mkubwa sana alioufanya katika Klabu ya Yanga, lakini pia nataka niipongeze jiji la Dodoma kwa uwekezaji mkubwa sana walioufanya katika timu ya Jiji la Dodoma ambalo leo ninaiona timu yetu inacheza vizuri sana na kwa kweli katika timu ambazo zinakuwa hivi sasa katika kandanda safi ni

Dodoma Jiji na hata mechi yetu ya mwisho kule uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam mnaweza mkaona Simba walipata taabu kidogo ingawa walituzidi mbinu tu, lakini timu ipo vizuri ni kwasababu ya uwekezaji mkubwa ambao unafanyika. (*Makofi*)

*Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nguvu kubwa aliyoweka pale Namungo, ingawa juzi mlitupa furaha mpaka dakika 78 kuendelea mbele ikawa majanga. (Makofi/Kicheko) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze sana KMC kwa uwekezaji mkubwa sana ambao wameufanya lakini vile vile nimpongeze Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Alexander Mnyeti kijana mdogo amefanya jambo kubwa sana pale Gwambina pale Misungwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya makusudi kwamba ili michezo iendelee lazima tufanye uwekezaji leo ligi yetu imebadilika, mimi ni mshabiki wa Yanga, lakini nitakuwa sijitendei haki kama sitasema ukweli, uwekezaji wa Mo Dewji umeibadilisha Simba, unaiona Simba leo jinsi ilivyo wanajitahidi wanacheza vizuri, lakini na sisi pia kupitia GSM tunakuja. Tunakuja na lengo letu ni kuleta ushindani mkubwa kwa sababu michezo haiwezi kuendelea bila uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niyaomba makampuni mengine pia izibebe hizi timu, hizi timu hizi ukiacha tu fedha wanazopata kutoka Azam kuendesha timu ni gharama kweli kweli, mimi kipindi fulani nilikuwa ninaimiliki hapa nilikuwa ninaisimamia Dodoma jiji hapa niliwahi kuweka reheni nyumba yangu kwa ajili ya kulipa mishahara, ni jambo gumu kweli kweli mpaka Mheshimiwa Kunambi amekuja kunisaidia kupita Jiji la Dodoma. Lakini tunaomba wawekezaji waje wengi zaidi ligi iwe ya ushindani, Simba akienda kucheza na Gwambina watu wasiyajue matokeo, uwe mchezo ambao hautabiriki, lakini leo ni gumu sana. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na kwa haraka kabisa napenda kutumia nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan alipokuja kulihutubia Bunge alieleza sasa nia ya Serikali kuanza kutenga fedha kidogo kidogo kugharamia timu zetu za Taifa na hata timu za wanawake napenda kutoa pongezi sana, lakini pia napenda kutoa pongezi kwa Azam kwa uwekezaji waliouweka ambaao kwa kweli unasaidia tu sio sisi kuangalia mpira, lakini pia ni sehemu ya ajira. Ukienda huko kwa wananchi wetu kuna kitu kinaitwa vibanda umiza, unakuta mtu ana banda lake anaonesha mpira, anauza vinywaji, anapata kipato na maisha yanaendelea, kwa hiyo ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitoe wito kwa vilabu wasibweteke tu na uwekezaji huu na wenyewe pia watafuta wadhamini wengine, lakini pia napenda kutoa pongezi wa wachambuzi wote wa michezo hususan zamani tulikuwa tumezoea vipindi vya michezo unasubiri jioni, lakini siku hizi kuna vipindi vya michezo hata katika stesheni za redio kama Wasafi, EFM TBC Fm unapata habari za michezo muda wowote, kwa hiyo nao napenda kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya pongezi hizi watu wengi wamesema kuhusu michezo kweli michezo pamoja na kuwa ni burudani inatuondolea *stress* na kadhalika lakini kama ambavyo siku zote mimi nimesema michezo ni sehemu ya ajira ni mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, michezo, sanaa na burudani ni kitu kikubwa katika uchumi wa nchi na hasa kwa kuendelea katika uchumi wa kutumia sayansi na teknolojia, *digital*

economymichezo ina nafasi kubwa sana, lakini sasa michezo ili uweze kukupa hiyo tija sasa lazima kuwe na usimamizi bora, nitatoa mfano hapa tarehe 5 Mei, 2017 nilitoa mchango wangu hapa nikasema *TFF* ambao ni *Tanzania Football Federation* imegeuka sasa kuwa *Tanzania Football* fungia fungia kwa sababu ya kufungia fungia yaani jambo dogo tu unamfungia mtu, yawezekana kweli ni kanuni, mimi ninashauri, unajua unapomfungia mtu kama Mwakalebelia ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa *TFF* ile ya Tenga ambayo ndio imejenga msingi wa mpira huu tulionao leo kwa kweli *you have to think twice* mimi kwa mawazo yangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yawezekana ni kanuni ni taratibu zao lakini wajaribu kuziangalia kuwe na adhabu ambao kidogo ni *friendly* ambao unaweza kumjengea mtu kurekebika kuliko kumfungia, unamfungia Mwakalebelia miaka mitano, huyu mtu ambaye katika *football*, katika michezo ni mtu ambaye amekuwa na mchango mkubwa sana kwa hiyo ndio maana kunakuwa na lawama nydingi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Leo hii sisi katika *FIFA ranking* Tanzania tupo wa 137 hata Libya ambao wako kwenye kupigana wako wa 119 sasa hata Mama alipokuja hapa kwenye Bunge alisema tumechoka na mimi nasema tumechoka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu tumechoka mimi ninashauri unawezekana ukawa ushauri sio mzuri na haitakuwa mara ya kwanza, sisi kwanza timu yetu ya Taifa kwanza ipumzike, tujipange, tujipange hata miaka mitano. Ghana wamefanya hivyo, Cameroon wamefanya hivyo, Comoro wamefanya hivyo, wamejipanga, leo hii tunajua Cameroon wako wapi, Ghana wako wapi, hata Comoro ambao vilabu vyao vilikuwa vikija hapa tunawafunga 12 kwa sifuri sasa hivi wameshatuacha katika *listya* Afrika, yaani kama ile ambayo *easy way of doing business* sisi wa 141 katika *East Africa* Uganda ya 84; Kenya ya 102; Sudan ya 123; kwa kwa maana ya ile *CECAFA* Rwanda ya 129 yaani tuliovazidi sisi ni

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Burundi tu kwenye mazingira ya kufanya biashara pia tuliowazidi sisi ni Burundi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaweza ukaangalia hivi vitu ni kama vile sijui kama vinashabihiana, sasa ukienda katika mpira wa Uingereza, Spain na Ujerumani wale wote ukienda *Man U* wawekezaji wametoka Amerika ukienda Chelsea - Abramovich ametoka Russia, ukienda Arsenal kwa nini wale watu wanakuja? Kwa sababu kuna mazingira bora ya kuwekeza katika mpira. *Man City* wanatoka Arabuni *Leicester City* wanatoka Singapore kwa sababu gani? Kwa sababu kuna mazingira bora ya nini ya kuwekeza, sasa mazingira bora yanatoka wapi, yanatoka kuanzia kwenye usimamizi wa watu wenye mpira ambao ni *TFF*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi huwa ninasema maisha ni ujanja, sio ujanja ujanja, lakini *TFF* inavyoendeshwa ni *full ujanja ujanja* ndio maana tunakosa nini uwekezaji, kweli leo hii wamekuja hao wa Azam, Azam wamewekeza pia nao kwa sababu watapata faida kwa kuuza ving'amuzi na kadhalika. Lakini kama tunataka *serious* watu wawafuate Azam ni lazima kwakweli mazingira ya uwekezaji kama yale tunayosema kwenye biashara katika mpira wetu yaboreshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa watu wanazungumzia kujenga viwanja Serikali hii bajeti iliyokuja hapa bilioni 54, uwanja tu kama wa *Abuja National Stadium* bilioni 800 ambao unaweza kufanya mambo ya mpira na mambo hayo aliyokuwa anasema Mheshimiwa Babu Tale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo hapo Serikali haiwezi, Serikali iwe *facilitator* na vyombo vyake vyta michezo, wawekezaji waje wawekeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitapenda kuzungumzia kuhusu *COSOTA*, *BASATA* na Bodi ya Filamu; hii mimi nimelisema miaka minne tunawashukuru wameviunganisha wamesema *One Stop Centre*. Ukienda *EWURA* ukienda *NEMC* hivi *regulator authority* unazikuta hadi ngazi ya kanda, ninashauri Serikali,

ione uwezekano tuache kumsumbuu msanii kutoka Kongwa, kutoka Itimbo Mafinga kutoka Tandahimba kuja Dar es Salaam akae siku tatu gharama za usafiri na kadhalika, haya siyo mazingira bora ya kuwawezesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninakuomba Mheshimiwa Waziri jaribu kama utaona ni gharama tumia Maafisa Utamaduni uwe japo na ngazi ya Kanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakuja Shirika la Magazeti ya Serikali; kama ambavyo tunasema tuwe na *national career* kwa maana lazima kama Taifa uwe na shirika la Ndege kama Taifa uwe na Shirika la Utangazaji, Shirika la Magazeti ya Serikali ni chombo muhimu sana katika dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, magazeti yale ya *Daily News*, Habari Leo ndiyo chanzo kikuu ukitaka kusema cha taarifa za Serikali, lakini *TSN* mimi nimekaa *newsroom*, nimefanya kazi ya uandishi wa habari kwa miaka nane hali ya *TSN* siyo nzuri, wameomba bilioni 16 wanunue mtambo ambao utachapisha siyo magazeti yao tu, lakini utafanya uchapishaji mpaka kutoka watu wa Congo ita-*generate income* leo hii ukibeba gazeti la *Daily News* tunasema washindani, hawawezi kwasababu watu hawa hawana nguvu hiyo, hatujawawekezea. Sasa kama tumeweza kuweka nguvu kwenye Shirika la Ndege la Serikali, *TBC* mmeona kazi waliyofanya wakati wa mazishi ya Mheshimiwa JPM ni kwa sababu wamewezeshwa.

Mheshimiwa Spika, Leo hii *TBC* wamepewa shilingi bilioni tano; ninashauri tuiangalie sana Shirika la Magazeti ya Serikali ili liweze kushindana na akina *The Guardian*, liweze kushindana na akina Mwananchi, kwa sababu hiki ndiyo kisemeo cha Serikali. Tufumbe macho tuiwezeshe *TSN* ili kusudi hili gazeti la *Daily News*, *diplomatic community* kabla hajasoma chombo chochote cha habari anaanza kusoma *Daily News*, sasa *Daily News* haina uwezo tena wa kujichapisha kushindana na *The Guardian* matokeo yake hata mtangazaji anayepeleka matangazo hawezi kupeleka kwasababu halina mvuto. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hawa watu *TSN*wanaidai Serikali nadhani *almost* shilingi bilioni 11 lakini na wao wanadaiwa na *suppliers* mbalimbali pesa nyingi tu. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali na baadaye naweza nikashika shilingi inakuja na mkakati gani kuisaidia kitu ambacho ndiyo kisemeo cha Serikali, ili wasaidiane na *TBC*, wasaidiane na *TBC Radio* wasaidiane na vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuhitimisha tu, mimi narudia tena, ili tuvutie wawekezaji katika sekta ya michezo, burudani na sanaa ni lazima tugeuke kuwa *facilitators*, wala tusiwaze sisi kama Serikali tutawekeza leo hii kama nilivyosema tulienda nakushukuru sana katika miaka mitano ulijitahidi sana *Bunge Sports Club* imeshiriki kwenye michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki tumeenda pale Burundi, tumekuta unaenda asubuhi uwanja wa mazoezi, kuna timu ina wachezaji 31 ni magoli kipa tu wana-*train* ugolkipa tu, na leo hii tunaona kuanzia Namungo kule golikipa ni Mrundi yule wako makipa wengi tu ni Warundi.

Mheshimiwa Spika, leo hii ligi yetu ina wachezaji kutoka Burundi wako wengi tu. Tumeenda pale Kampala watu wamewekeza sasa ili ukisimamia bora nitakwambia kwa kumalizia kitu kidogo tu, hata waamuzi sisi hapa hatupeleki waamuzi kwenye michezo, hawapati nafasi kwa sababu usimamizi siyo mzuri nitakwambia katika *CHAN* hii ambayo tulienda kushiriki hii katika waamuzi 47, 19 wa kati, wasaidizi walikuwa 20 na wale wa *VAR* (*Video Assistant*) walikuwa nane mionganoni mwao wakiwepo akinamama wawili Lydia Abebe kutoka Ethiopia na Bernadeta Kwimbila kutoka Malawi. Sisi hapa kama hauna menejimenti nzuri ya mpira utakosa hata waamuzi.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu bajeti hii ni ya leo tu

mimi naomba tuvumiliane niongeze wachangiaji kidogo, lakini kwa dakika tano/tano wachache, hawatazidi wanne kwa dakika tano tano ili jioni wanaobakia jioni tuweze kuwapata wote kama walivyo katika orodha yetu, asibakie mtu hata mmoja, wa jioni wao watachangia dakika 10/10; lakini hawa nitakaowaita watatu/wanne watachangia dakika tano/tano. Tuanze na Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda ikilia tu kengele moja ndiyo hapo hapo.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii. Napenda sana kuipongeza Wizara hii chini ya Waziri pamoja na mdogo wangu Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Kwa sababu nina dakika tano mimi naomba nichangie katika eneo la utangazaji.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu suala la utangazaji au habari; ufikishaji habari ni haki ya kila na hata katika ilani yetu ya chama pia tumejjipambanua kwamba kila mwananchi ana haki ya kupata habari sahihi. Sasa nitaenda moja kwa moja kusema kwamba katika *channel* zetu za *tvupatikanaji* wa habari bado hautoshelezi na usikivu wa *channel* hasa *channel* ya *TBC* ni *limited* na kama tunavyofahamu katika maeneo ya pembezoni sehemu kama Ngorongoro ambayo ni eneo kubwa, lakini upatikanaji wa habari kwa sehemu hii kwa kweli ni hafifu na maeneo kama Namanga, maeneo kama Longido na Bukobwa zile sehemu ambazo ziko pembezoni wale wananchi hawapati habari.

Mheshimiwa Spika, habari ni muhimu sana, kwa mfano kama hotuba za Rais ni muhimu kila mwananchi akaisikia. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali iweze kuangalia hili kwa sababu habari ni muhimu katika kulinda nchi yetu, jambo lolote la hatari litakapotokea ni vyombo vyaya habari ndivyo vitakavyotumika kusambaza habari na mambo kama ujenzi wa uzalendo, mambo kama utamaduni wetu vyote hufikiwa kwa habari. Kwa hiyo usikivu wa *channel* ambao kwa mgano tuna *channel* yetu ya *TBC* ambayo ni asilimia 63 na ni *channel*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ambayo ni ya Taifa tunaomba hii iwekewe mkazo iweze kufikia watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili kwa haraka niende kusema kwamba naiomba Wizara iangalie suala la wasanii wetu waweze kutengeneza tamthilia. Kwa sasa hivi tumejikita zaidi katika sinema zetu na unakuta hazifurahishi kwa sababu nyingi sinema ni fupi na kwa sababu hata wale wanaocheza sinema wengi wanajitegemea, hawana pesa za kutosha mtu ukiangalia filamu unajua itaishiaje.

Kwa hiyo hata hupati mvuto wowote unajua tu hii sinema imeanza *climax* yake itaishia hivi. Kwa hiyo haupati ile hamu ya kuangalia. Lakini filamu kama Isidingo na filamu zingine za nje ni nzuri kwa sababu zinakupa hata mtu umechoka kusikiliza.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara iangalie kutengeneza tamthilia ndefu kama Isidingo, lakini iwe inaakisi tamaduni zetu, lugha yetu na itaweza kujenga Taifa kwa ubora na watu watakuwa na hamu ya kuiangalia mara kwa mara kwa sababu mtu hatajua inaishiaje na hivyo basi pia tutatengeneza uchumi na itaweza kuwajenga vijana kuwa na weledi wa kuweza kutengeneza filamu zenye ubora kuliko sasa hivi ambazo tunaangalia nyingi zimejielekeza katika mapenzi na mambo fulani fulani ambayo ni kwa ajili tu ya kupata kipato kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine naomba kusisitiza juu ya mambo ya *channel* ya utalii. *Channel* ya utalii bado hajakaa vizuri, *coverage* yake bado haitoshi utalii wetu unatakiwa utangazwe sana waandishi wa habari nimepata habari walipata semina kutoka Tanzania nzima, lakini unakuta wanapokwenda kutengeneza filamu za utalii pesa haitoshi, wanakwenda katika mbuga za wanyama au sehemu mbalimbali wanakaa siku tatu. Siku tatu utatengeneza filamu gani? Haiwezekani na yote hayo ni kwa sababu ya pesa, ili utengeneze filamu nzuri inatakiwa muda na vitu vyote vile vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kifupi siwezi nikasema lakini naomba *channel* hii ya utalii hata watalii wenyewe wanapokuja wakati mwinge kutokana na usikivu kuwa hafifu wanaulizia *channel* za utalii, mtu hajui nakumbuka mimi nilipokuwa Marekani mtalii mmoja alikuja akasema mimi nimengalia *channel*, lakini sijaona mlima Kilimanjaro je, wewe umeuona? Nikamwambia nimewahi kuuona, akanikumbatia, akaniambia daktari nafurahi nimemshika mtu ambaye amepanda Mlima Kilimanjaro. Lakini Mlima Kilimanjaro ungetengenezewa *channel* nzuri ungeweza kuleta watalii kwa wingi zaidi. (*Makof*)

Kwa hiyo naomba kusitiza kwamba hii *safari channel* na *channel* zingine ziwepo na zitengewe pesa ya kutosha ili ziwe na *coverage* nzuri yaku-capture utalii wetu na uweze kusambaa dunia nzima na iwe ni *channel* ambayo ni imara zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la mwisho sasa labda kwa ajili ya muda haraka napenda kusemea juu ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Paulina Nahato.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Maimuna Mtanda atafatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi, awali ya yote niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo kwa uwasilishaji pamoja na timu yake yote. Lakini pia Kamati; lakini kipekee kabisa niipongeze Serikali kwa mwaka huu wa 2021 kwa kupeleka michezo ya UMITASHUTA pamoja na UMISETA katika Mkoa wa Mtwara kwa sababu kwa kufanya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hivyo inafungua milango ya fursa kwa Wana Mtwara, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye mchango, Tanzania wote tunatambua kwamba imekuwa ikishiriki mara nyingi kwenye michezo mbalimbali ya kitaifa pamoja na kimataifa. Kuna wakati huwa tunafanya vizuri, lakini kuna wakati hatufanyi vizuri sana. Lakini ukiangalia ni kwa nini hatufanyi vizuri sana kuna sehemu kuna *gap*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na Serikali yake kwa ujumla imekuwa ikiwekeza fedha nyingi katika maandalizi ya michezo ya UMISETA, pamoja na UMITASHUTA jambo ambalo nijema kwa sababu tunataraji wanamichezo hawa ambao wanaenda kucheza michezo ya kimataifa watokane na maandalizi ambayo yanafanyika katika michezo ya UMISETA pamoja na UMITASHUTA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukianglaia Serikali inatenga shilingi 600 kwa wanafunzi wa shule za msingi kila mwanafunzi mmoja kwa ajili ya maandalizi ya UMITASHUTA na shilingi 1,500 kwa ajili ya wanafunzi wa shule za sekondari, ni jambo jema tunawashukuru na kwa kweli wanafunzi wanahamasika na wanafanya vizuri. Niwapongeze *TFF* kwa sababu wakati wa michezo hiyo wamekuwa wakiwabaini wanafunzi wanaofanya vizuri wanawaweka kwenye *database* yao pamoja na CHANETA na watu wa *basketball*.

Mheshimiwa Spika, lakini pale michezo ambayo inashindanishwa ni mingi ipo pia michezo ya ndani wale wa michezo ya ndani sijaona mkakati madhubuti wa Serikali kuwashirikisha au kuwachukua katika *database* yao ili waweze kuwatumia baadaye. Nishauri sana Serikali kwamba michezo ya ndani ni sehemu ya michezo na yenyewe ichukuliwe kwa uzito wake Watoto wale nao wapate kushiriki katika michezo mingine hapo baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wale wanafunzi wanaomaliza wanaoshiriki michezo ya UMISETA pamoja na UMITASHUTA wakishamaliza shule hakuna wanakoelekea,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wamejitatihidi wamefanya vizuri, wamemaliza masomo yao wanarudi wanakaa nyumbani hakuna muendelezo wa michezo kwa wanafunzi wale. (*Makof*)

Sasa swalii la kujuliza ni kwamba Serikali iliwekeza kwa kiasi kikubwa, wanafunzi wakajitoa, maandalizi yakafanyika, lakini mwisho wa siku fedha za Serikali ambazo zimeenda kuwekeza katika michezo hiyo hazileti tija kwa sababu wanafunzi wanapomaliza hakuna wanakoelekea tena ukiondoa wale wachache wa *football*, *netball* pamoja na *basketball*.

Kwa hiyo, niombe Serikali sasa iwe na mkakati madhubuti wa kuhakikisha wale wanafunzi wanaomaliza shule wanachukuliwa au wanaendeleza michezo yetu mbalimbali ili baadaye iweze kutuletea tija katika Taifa katika fani hiyo ya michezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini niongelee pia suala la utamaduni; hii ndiyo Wizara ambayo inasimamia kwa ujumla masuala yote ya utamaduni, utamaduni kwa maana ya vyakula, maadili na mambo yote yale ambayo yanakusanyika huko, lakini tumeona mmomonyoko mkubwa sana wa kimaadili sasa hivi katika nchi yetu. Niombe Wizara kwa sababu ni Wizara ambayo ina vyombo vyahabari; ina *television* pamoja na magazeti na radio kwa kupitia vyombo vyake vyahabari waanze kurejesha au watoe elimu kuhusiana na suala la maadili katika nchi hii, hali iliyoko ni mbaya hata Mheshimiwa Rais alisema wakati anaongea na wazee wa Dar es Salaam, mwanafunzi au kijana amekaa kwenye kiti, lakini hampishi mama mjamzito wala wazee na hiyo inatokana na mmomonyoko wa maadili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutumie vyombo vyetu tulivyo navyo kutoa elimu ili suala la maadili liweze kuendelezwa katika nchi hii. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea kumalizia sasa Mheshimiwa Ester Bulaya atafatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza na mimi nikiri ni mwanahabari, nilikuwa *newsroom* takriban miaka sita magazeti ya Uhuru, Mzalendo na burudani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimeona watu wengi wamejikita katika michezo lakini pia Mheshimiwa Waziri waandishi wako wa habari wanalipwa vibaya sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi na Waheshimiwa Wabunge waandishi wa habari wamekuwa wakifanyakazi kubwa sana na Taifa letu linawategemea waandishi wa habari kuelimisha jamii, lakini waandishi hawa wamekuwa na maslahi madogo sana, nani waandishi wa vyombo vya habari vyote vya Serikali na vyombo vya habari binafsi, siyo walioajiriwa tu mishahara yao midogo haiongezwi, hata *correspondent journalist* na wenyewe wanalipwa vibaya sana hapo nimezungumzia *correspondent* kwenye *print media*, sijazungumzia kwenye *electronic media*/ watangazaji nimezungumzia tu kwneye magazeti. Lakini wote wanalipwa vibaya sana na hawana watu wa kuwasemea.

Mheshimiwa Spika, sisi wanahabari kazi yetu ni kusemea wengine, lakini Bunge hili linapaswa kuwasemea waandishi wa habari wanatumia kalamu zao, wanatumia midomo yao kuhakikisha wananchi wanajua taarifa mbalimbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Iakini Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Sera dada yangu pale Jenista baadhi

ya vyombo nya habari havipeleki michango. Kwa hiyo, hatma ya waandishi wa Habari baada ya kumaliza kazi zao haieleweki nimekutana tu na baadhi ya wanahabari hapo wachache nje na wenyewe imebidi waanze kufuutilia kama michango yao inaenda, michango yao haiendi kwenye mifuko ya hifadhi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mbali ya maslahi madogo kile wanachokatwa hakipelekwi, hilo nalo naomba ulifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri tabia ya kufungia fungia vyombo nya habari, tukubali/tukatae vyombo nya habari ni CAG mwingine, tusitake tu kutolewa habari za kufurahisha, lazima tukubali na kukosolewa zote ni habari za kujenga Taifa letu. Kwa mfano unakuta unafanyiwa *interview* mwandishi wa habari anakwambia Ester usiende huko tutafungiwa sasa unafungiwa wazo nililolitoa mimi? (*Makofi*)

Kwa hiyo, kuna shida na ukweli soko la magazeti limekuwa, sasa hivi hamna mtu ambaye wengi hawanunui magazeti kwa sababu anaona habari zile zile, habari za uchunguzi saa hivi zimepungua makala za uchunguzi zimepungua hebu hata ukienda kwenye mijadala angalia tathmini mbalimbali zinapotolewa watu wanatoa kwa hofu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hatusemi kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka, lakini tukiwahakikishia hawa waandishi wetu wa habari wafanyakazi zao kwa weledi hata kama wanapotukosoa magazeti haya hayafungiwi fungiwi hovyo, Mheshimiwa Waziri ukifungia gazeti moja ina maana umesimamisha zaidi ya familia 50; zaidi ya wafanyakazi 50 hawana ajira ina maana watoto hawaendi shule unawaweka hizo familia katika hali ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tuzungumzie faini imekuwa kama chanzo cha mapato, watu walikuwa wanazungumzia upande wa michezo, hata huku kwenye

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

magazeti, kwenye vyombo vya habari kuna shida, unamtoza mtu faini kubwa mtoze faini kidogo ajirekebishe, lakini siyo faini ikiwa chanzo cha mapato.

Sasa natolea tu mfano mlifungia Wasafi pale Babu Tale Mbunge anajua alivyofanya mpaka Wasafi ikafunguliwa, lakini je, hizi *media* zingine ambazo hazina watetezi? (*Makofi*)

### **T A A R I F A**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Babu Tale, *declare interest.*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, dada yangu Ester sijafanya chochote ni utaratibu umefanywa na Serikali ndiyo maana tumefunguliwa, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Pokea hiyo taarifa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nimetolea mfano lakini anajua tulipokuwa tunakunywa *canteen* alisemaje.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hizi faini zisiwe chanzo cha mapato mnapofungia gazeti moja mbali ya kumuathiri yule mwenye chombo, lakini mnawaathiri hawa waandishi wengine ambao mbali tu ya maslahi yao madogo, lakini pia unamfanya sasa anakosa kabisa kazi, anashindwa kuendeleza maisha yake. (*Makofi*)

Kwa hiyo nilikuwa naomba maslahi ya waandishi wa Habari tabia ya kufungia fungia vyombo hebu acha waandishi wa habari wafanye kazi kwa uhuru, tukosolewe, tujenje taifa letu, tusipongezwe tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia mmezungumzia hapa mpira, mmoja tu ndiyo amezungumzia timu ya wanawake, tena amegusa tu, hapa mnapozungumzia uwekezaji kwenye mpira wa miguu timu ya mpira wa miguu ya wanawake

imekuwa kama mtoto yatima kwenye Taifa hili mbali ya kufanya vizuri timu ya Taifa ya Wanawake imekuwa ikichangiwa changiwa, albu. (*Makofii*)

Lakini Mheshimiwa Waziri kwenye kurudisha michezo mashulenii hakuna programu ya timu ya mpira wa miguu ya wanawake hivi kweli ndiyo tunataka timu zetu zikashindane na Brazil, tukashindane na Senegal ambazo zinaenda *compete* kwenye kombe la dunia. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ester Bulaya. Mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza naomba nichukue nafasi hii nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji katika Wizara hii ya Habari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninalotaka kuliongelea kwenye Wizara ya Habari kwanza ni kuwapongeza namna utendaji wao wa kazi za kila siku hasa kupitia vyombo vyetu vya Serikali ikiwemo *TBC*. Vyombo vya habari vya Serikali vinafanyakazi kubwa sana, lakini pamoja na kazi kubwa inayofanywa bado ipo haja kwa Wizara ya Habari kuona wanafanya kila jitihada kuangalia waandishi wa habari kwa vile wao ndiyo waelimishaji wa jamii ndiyo ambao wanapasha umma katika habari mbalimbali za nchi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia waandishi wa habari hawa wana kazi ya kuelimisha umma, wana kazi ya kuburudisha, wana kazi ya kuonesha namna gani wanamichezo na sanaa wanafanya katika nchi yao. (*Makofii*)

Mimi ningeongelea jambo moja kwa waandishi wa habari, bado waandishi wa habari wanapaswa kuenziwa, wanapaswa kulindwa katika masuala mbalimbali yakiwemo maslahi yao, lakini pia yakiwemo masuala la *overtime* kama tunavyofahamu waandishi wa habari wanafanyakazi sana hasa wa vyombo ya Serikali. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari hawa ni mashahidi sisi wote kwamba wanafanyakazi bila upendeleo lakini wanajituma usiku na mchana sjui Wizara ina mpango gani kuona inaandaa fidia maalum pale waandishi wa habari wanapopata ajali wakiwa kazini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba kuunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

Jioni tutakaporudi saa 11.00 kama nilivyoahidi kwamba wale wote ambao tunao kwenye daftari letu watapata nafasi akiwa ni Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mheshimiwa Martha Neema Gwau, Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mheshimiwa Hassan Mtenga, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Mwantumu Muzamil Zodo, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya (Mheshimiwa Keisha) na shughuli zingine zitaendelea tunaamini tutahitimisha hoja hii jioni ya leo, ni vizuri tukarudi ili tuje tufanyie uamuzi mzuri ifikapo jioni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri tunakupongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri timu nzima ya wataalamu michezo ni eneo ambalo lina wadau wengi tena vijana na lina washabiki wengi. Ni eneo ambalo ukigusa huku watafurahi na kushangilia lakini wakati huo huo kuna wanaosema aaa ukigusa upande wa pili hivyo hivyo ni eneo lina lawama nydingi. Kwa hiyo, mvumilie tu ndiyo mwendo wenyewe, lakini mimi ninachowenza kukushauri ni kwamba uwe karibu sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimwia Waziri Mkuu katika masuala haya ya michezo na hasa mpira wa miguu yeye ni gwiji kabisa kabisa, Wizara mkitumia usoefu wake na uono wake katika eneo la *football* na hata michezo mingine tunaweza kabisa kwa kipindi hiki tukaifikisha nchi yetu mbali sana kwenye michezo. Kwa hiyo kuweni karibu tu, msikae mbali maana ana shughuli

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nyingi pamoja na michikichi na katani mvute kidogo na kwako na wewe kwenye michezo kidogo uvune vune kidogo kutoka kwake. (*Makof*)

Basi Waheshimiwa Wabunge naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 07.25 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA  
HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mheshimiwa Martha Gwau atafuatiwa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, ajiandae.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na mimi niweze kuongeza senti 50 zangu kwenye bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi wakati wa michango, moja ya wachangiaji dada yangu Ester Bulaya aliongelea wanahabari na kidogo kukawa na lawama ya kwamba Wabunge wote ambao walitangulia kutoa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

michango hawakuwa wamewaongelea wanahabari.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hili ni suala ambalo tumekuwa tukilifiria kwa muda mrefu ya kwamba Wizara hii ina matawi mengi kiasi kwamba matawi mengine yanafichwa sana. Ningetoa pendekoz heshima kwa mamlaka husika kuona kama tunaweza kuipunguzia matawi Wizara hii kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano habari imekaa sana kama inafanana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na hali kadhalika utamaduni umefanana sana na Maliasili na Utalii ili tubaki na Michezo na Sanaa ambavyo kusema kweli asilimia 98 ya michango iliyotoka leo ilikuwa inaelekea huko, kama itazipendeza mamlaka kwa hisani yao naomba wallangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nitoe pongeze kwa Serikali na *Azam Media* kwa mkataba mzito wa haki za *television* za ligi yetu kuu, mkataba ule ambao haujawahi kutokea kwa nchi za Afrika Mashariki ni mkubwa sana na sisi watu wa mpira tunaimani kwamba unakwenda kusaidia mpira wetu. Watu wa mpira tunafahamu masuala ya fedha yalivyokuwa yanaathiri ubora wa ligi yetu, timu nyngi zilikuwa haziwezi hata kusafiri zenyewe mpaka zichangishe washabiki wake na hili lilikuwa linafanya michezo mingi lamuliwe siyo kwa sababu ya ubora wa michezo yenyewe, ubora wa wachezaji na ubora wa timu, isipokuwa kwa uwezo ama kutokuwa na uwezo wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana unaskia kila siku kuna maneno maneno mara huyu anasema ametaka kupewa milioni 40, hivi vitu ni vya kweli na ninaamini sasa Azam kwa namna moja ama nyngine wamekwenda kuzirekebisha. Kule kwetu tunasema kila harusi inamshenga wake na sisi tunaamini ya kwamba *Azam Media* ndiyo washenga wa mpira wa nchi hii, kwa hiyo, hii naomba nichukuwe nafasi hii kuitia Bunge lako Tukufu kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu kwa Wizara ni iwekeze nguvu zake kwenye kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya kuwekeza kwenye ngazi za chini, mashulen na huku kwenye *field*. Ukienda majimboni moja ya matatizo makubwa ambayo unaulizwa kila siku na vijana ni vifaa nya michezo na viwanja; hawataki nyasi, hawataki viwanja nya milioni 300 kama alivyopendekeza ndugu yangu *Senator Sanga* asubuhi wanataka tu viwanja vinavyotosha kuweza kufanya kazi vipaji walivyojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kusema ukweli ni gharama kubwa, naona Wabunge hawana uwezo wa kuyamudu hayo. Mimi mara ya mwisho kuna kata inaitwa Kwaibada katika jimbo la Muheza vijana waliniomba niwasaidie wakati *TARURA* wakienda kule wawasaidie kuchonga/kurekebisha uwanja wao ambaa umekaa upande mmoja uko mlimali, upande mmoja uko chini, nilivyowaomba *TARURA* wakaniletea *bill*/ya milioni 13 kwa ajili ya kurekebisha uwanja ule, nikaona sasa *TARURA* nao hawataki uwanja utengenezwe bado nawaza namna ya kuwasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nipendekeze kwamba Wizara ione namna ambayo kama inaweza kupeleka fedha zaidi mashulen na majimboni ikiwezekana kwa ajili ya vifaa na kurekebisha viwanja hivi sehemu za vijana kufanya michezo hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ushiriki wa wachezaji wa nje kwenye ligi zetu, ukiangalia ligi yetu na idadi ya wachezaji wa nje ambaa wanatupa burudani kubwa naweza kuwataja wengi hasa walioko katika timu ya Simba unaweza kuona kabisa kwamba kama siku moja wachezaji wale wa nje wataondolewa kwenye ligi yetu, ligi yetu itakuwa na ladha tofauti na itakuwa kwenye kiwango kidogo kuliko ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa wachezaji wa nje ni mzuri sana, unawapa changamoto wachezaji wetu, lakini niiombe tena Serikali namna ya kulifanya hili ni kuhakikisha

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kwamba tunapeleka nguvu huku chini ili na sisi tutengeneze wachezaji ambao wanaweza kucheza nje ya nchi ama ambao peke yao kama wataweza kucheza kwenye ligi yetu basi ligi yetu itakuwa na msisimko kama ilionayo sasa hivi. Lakini bila Serikali kutilia mkazo michezo ngazi hizi za nchini, uwezo wa timu yetu ya Taifa utaendelea kuwa dhahifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hili jambo la BASATA; kwanza niseme kwamba mimi bado niko kwenye majukwaa mengi ya wasanii na asilimia 98 ya wasanii wa nchi hii tunakubaliana mambo mawili; aidha, BASATA inahitaji *major reform* ama sheria inayowekwa kuundwa kwa BASATA iondolewe kabisa tuwe na chombo kingine kwa ajili ya kulea wasanii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza hili liliundwa mwaka 1984 kwa sheria namba 23 na liliunganisha Baraza la Muziki Tanzania - BAMUTA na Baraza la Sanaa la Taifa kwa wakati huo, na malengo yake ukiyasoma kwenye sheria ya mwaka 1984 ambalo ililiunda unaweza kuona kabisa hayakuwa na walakini, hayakuwa na viashiria, hayakuwa na maelekezo ya moja kwa moja kwamba baraza hili linakwenda kuwa polisi kama ambavyo liko sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1984 kazi za baraza ni pamoja na kufufua na kukuza maendeleo na utengenezaji wa kazi za sanaa, kufanya utafiti wa maendeleo kutoa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi kwa ajili ya maendeleo na shughuli za biashara na sanaa, kupanga na kuratibu shughuli za sanaa na ny inginezo nyingi, lakini hakuna mahali popote kwenye sheria hii ya mwaka 1984 ambapo baraza lilikuwa na kazi ya kusajili na kuhakikisha kwamba linapitia na kuitisha mashahiri ya nyimbo kama linavyofanya sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine tumefanya muziki kwa takribani miaka 19; sijawahi kukaguliwa wimbo wangu na sijawahi kufungiwa wimbo wangu kwamba nimewahi kutumia lugha ya matusi. (*Makof*)

Sasa tunajua umuhimu wa kuangalia maadili na hatuna wasiwasi nao, hatuna matatizo nalo, lakini suala la Baraza kujipa jukumu ambalo linatuongezea urasimu, ambalo linafanya kazi yetu iwe ngumu, wakati halina msaada wowote kwenye maisha ya msanii wa Kitanzania wala sanaa lenyewe ni suala ambalo sisi halikubaliki kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuombi haki ya kutukana kwenye nyimbo, wala hatuombi haki ya kuchochea, kuleta uchochezi kwenye nyimbo, tunachoomba ni haki ya kutengeneza muziki, kufanya sanaa yetu bila kuwa na vikwazo vingi ambavyo baraza hili kwa sheria hii ya mwaka 2019 linajaribu kuifanya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ninachoona ni kwamba Baraza linajaribu kwa nguvu nyingi sana kuichonganisha Serikali na wasanii, hiki kitu wasanii wote nchi hili wamekikataa na tunashukuru hekima za Waziri na Katibu Mkuu wetu wa Wizara hii ambao walikwenda wakahamua kukisimamisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachikiomba ninajua sheria bado ipo na Waziri na Katibu Mkuu wameisimamisha kwa hekima zao kuona namna ambavyo kitu gani kinaweza kufanyika kuirekebisha.

Sasa mimi sitaki kuhitumia hii kama *ground* ya kushika mshahara wa Waziri, ninachoomba ni *commitment* ya Waziri wakati hakija kufanya majumuhiшo kuonesha *commitment* ya Serikali kwamba sheria hii inarekebishwa *road map* ya marekebisho ya sheria hii ili isiende kuendelea kuwakwaza wasanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho ni suala la *COSOTA*. Nimefurahi kwamba *COSOTA* sasa inaanika na pamoja na mambo mengine inaanza kukusanya *blanks up levy* ambayo ni kodi inayokusanya kwa sababu ya vifaa vyote ambavyo vinaweza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. HAMISI M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** Haya malizia.

**MHE. HAMISI M. MWINJUMA:** Sasa tunachoomba sisi kwa Wizara kuwe na mgawanyo *separation* ya *copyright office* na *collective management organization*, kwa sababu Serikali najua mnaanza kuchukua fedha kutoka *media houses* mbalimbali, sisi tunaomba tukusanye fedha kutoka sehemu nyingine ambazo zinatakiwa kupewa leseni ya kutumia kazi za sanaa kama mahoteli, kama mabasi, *hair saloon* na *barber shop*. Sheria ya Namba 7 ya mwaka 1999 imeshasema haya waziwazi na kabisa hata uki-*charge* shilingi 7,000/8,000 kwa haya maeneo haya yote na tumeshafanya *research* unaweza kujikuta na bilioni 54 kwa *units* ambazo zipo zinazotakiwa kukusanya mapato haya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunaomba wakati Serikali inatusaidia kukusanya kwenye *media houses*, sisi tukusanye kwenye haya maeneo mengine na tuisaidie Serikali pamoja na mambo mengine kukusanya kodi yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme nina *grounds* kadhaa ambazo naweza kuzitumia kushika mshahara wa Waziri lakini sitaki kuzitumia ninachoomba..

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, dakika niliyokuungeza imeisha. Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, atafuatiwa na Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mheshimiwa Hassan Mtenga, ajiandae.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii uliyonipa na mimi ya kuchangia Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii kwa ajili ya kusaidia vijana wetu, lakini na Taifa kwa ujumla. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kwenye sanaa, najua wenzangu wamechangia michezo naomba niongelee Sanaa na Sanaa inavitu vingi kuna mziki, kuna *movie* na vingine. Naomba nijikite kwenye upande wa *movie* peke yake. Sanaa ni kazi, sanaa inasaidia vijana wetu wanapata ajira, sanaa inasaidia kuitangaza nchi yetu nchi mbalimbali, lakini sanaa hii itasaidia utalii na vitu vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu zilizopo watoa huduma ambaa ni wasanii wetu na walaji kidogo kunakuwa na kupishana au kidogo kunakuwa na walaji wanaona kwamba hawapati ile wanaohitaji kutoka kwa watoa huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kumekuwa na wimbi kubwa sana la watu hapa hapa Tanzania kuangalia *movie* za Kinajigeria, kuagalia *movie* kutoka kwenye *channel* tofauti tofauti *netflix* na zingine. Sasa huwa naijuliza kwa nini hatupendi vya kwetu? Kuna tatizo gani kwa nini tuisiangularie *movie* za kwetu na tuangularie *movie* za watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikagundua tatizo lipo kwa upande wa Serikali pia, Serikali imejikita sana kwenye habari na michezo nadhani sanaa haiipi uzito mkubwa na ukiangalia ndiyo inayoajiri vijana wetu kwa asilimia kubwa, wanahangaika kutoka chini lakini mpaka watafika juu.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba nimepitia ripoti ya Waziri kwa kweli wamejitahidi sana pamoja na timu yake nzima kuainisha kwenye upande wa sanaa kwa mwaka wa fedha ujao watafanya nini, ameainisha ataanzisha tuzo za kitaifa, mikopo mbalimbali kwa wasanii, ameainisha mengi mazuri ambayo atawafanya Sanaa ili iweze kukuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata Kamati pia wamekiri kwamba kuna ukuwajuwaji wa asilimia kubwa kwenye sanaa kwenye nchi yetu toka mwaka 2015 wamesema ilikuwa asilimia 6.2, lakini sasa imekuwa mpaka asilimia 11, kwa hiyo tumeona kuna tija ya Serikali kuwekeza

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

zaidi kwenye sanaa ili wavijana wetu waweze kujajiri, lakini pia waweze kutengeneza vitu ambavyo vitakidhi matakwa ya malaji ambayo ni *customer* kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la sanaa yetu, tatizo la *movie* zetu za Tanzania zinakosa ubunifu, lakini zinakosa uhalisia kwa sababu ni kwanini watu wengi wanapenda kuangalia *movie* za nchi nyingine kama India, China, lazima tuijulize sababu ni nini, wale wana ubunifu na wana uhalisia; kwa hiyo na sisi tujikite kusaidia vijana wetu waje na ubunifu, lakini waje na uhalisia kwa sababu ni ukweli usiopingika sanaa ni *another digital economic*, mtu anaweza aka-*act movie* Tanzania ikaangaliwa Marekani na wakalipia *netflix*, tunalipia movie za kinaijeria kwanini vijana wetu wasiweze ku-*act* na nchi nyingine wakalipia wakapata kuangalia *movie* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna tatizo lazima tuangalie jinsi ya kulitatua, lakini lazima tuangalie jinsi ya kuli-*facilitate*. Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba mashindano ya kitaifa, ya kimataifa, mikopo kabla ya kumpa mtu mkopo, kabla ya kumpa huyu mtu kufanya tuzo mbalimbali tuangalie *ground, ground* ya tatizo ni nini, kwa sababu uwezi ku-*solve problem* kama ujajua tatizo la problem nini tukitajiwa tatizo la *problem* tunaweza tuka *solve problem*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema *movie* zetu hazina uhalisia na watu wengi hawapendi kuangalia kwa sababu ya vitu wanavyo *act* baadhi ya *movie* hizo hazivutii hata kutazama, lakini tukiongeza haya ya ubunifu na uhalisia kwa vijana wetu kwa kusaidiana na Serikali watafika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kuna mataifa kama Korea, kuna mataifa kama Turkish wamefanya *investment* kwenye sanaa kwa sababu walitambua kwamba sanaa inaajiri vijana wengi sana wakawekeza kwenye taaluma mbalimbali, wakawekeza kwenye ubunifu mbalimbali na kwenye vitu mbalimbali ambavyo vitakuza hivi vipaji vya watu, lakini watoa huduma watoe huduma ambayo inakidhi matakwa ya mlaji ambayo ndiyo *costomer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na ushauri mdogo tu kwa Serikali ambao nahisi kwamba itakuwa ni *solution* labda kwa soko letu la *movie* au wasanii wetu wa *movie* au wasanii wetu wa *movie* kwa ujumla. Unapotaka ku-solve problem kuna *long term solution* na kuna *short term solution*, mimi naona Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo waje na *long term solution* hata kama itatuchukua miaka mitano, hata kama kumi, lakini mwisho wa siku tuje na kitu ambacho mtu akiangalia wanasesema kweli hii ni Tanzania imebadiiliya ya sanaa, *long term plan* ndiyo inatakiwa na wala siyo *short term plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukifanya *long term plan* utaanza kufanya kuanzia *ground* tatizo ni nini? *Solution* itakuwa ni nini? Na mimi kwa kufanya uchambuzi mdogo tu japokuwa na yapo mengi zaidi, lakini uchambuzi nillouona cha kwanza tufanye *investment*, Serikali lazima wawe *willing* kufanya *investment*, *investment* unaweza uka-invest leo *return* yake ikawa baada ya miaka 10, baada ya miaka mitano, *but* ikisha-turn around inakuja kuwa *the best* inakuja ku-solve tatizo lote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tu-*invest* katika ku-*empower* watoto kuanzia wakiwa wadogo. Mataifa mengine wanakuwa kuwafundisha watoto kuongelea na miaka mitatu, anamfundisha mtoto kukimbia anamiaka mitatu huyu mtoto akifika hakija kuwa *the best performer* hakuna miujiza imetumika ni *training* aliyopata kutoka chini, hawa ma-*actor* na ma-*actress* wakubwa wanaoingiza milioni za pesa kwenye nchi za wenzetu hawajatokea tu ukubwani kama mimi niende ku-*act* kesho wamepikwa kuanzia chini wakafundishwa, wakasaidiwa na Serikali yao kwa namna moja au nyingine kesho hakiwa anafanya vizuri ni matokeo ya *investment* ambayo imefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna shule za msingi, tuanzie kwenye shule za msingi tusiongelee kwamba tuna kuna chuo watoto wataenda kusoma, huyu mtoto wa maskini hatatokaje kule vijijini aende kwenye kile chuo, tukianza kufandisha masomo ya sanaa, lakini pia tukasaidia kuboresha

hata kama yapo, wakaja mwisho wanamaliza la saba wanajua kuna kipaji cha huyu mtoto, wale watu wa sarakasi wanachukua, wa ku-*act* wanachukua, wa sehemu tofauti wanachukua, kunakuwa na *designated* sekondari moja kwenye kila kanda zitakuwa nne kwa mfano unasema Singida tunasema shule fulani tunaiweka inakuwa masomo ya kawaida, lakini na masomo ya sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mtoto akimaliza darasa la saba ataenda *form one* mpaka *form six* kwenye shule ambayo inatoa masomo ya kawaida, lakini inatoa na masomo ya sanaa pia. Kwa hiyo, akitoka hapo hata akichuliwa kwenda ku-*actatakuwa the best* kwa watakaishia pale, lakini watakaoendelea na chuo wataenda Bodi ya Mikopo na itawapa mikopo. Hizi programu za *fine art and performing designing* watakuwa *the best*, wanaenda kupewa mikopo watamaliza tukitoka hapo sasa tutazaa kizazi kipyaa cha *bongo movie* kwa sababu waliomaliza ndio watakwenda kuleta mapinduzi ya ubunifu, wataleta mapinduzi ya uhalisia, kwa sababu kaanza kuanzia chini kujifunza na hata atakuja kuleta uhalisia na watu watapenda vya kwao kama ilivyo sasa tofauti watu wanapenda vya nje kuliko vya kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kwa sababu Serikali isipoingilia katika kusaidia hili suala kwa *long term solution* tutaimba wimbo ule ule kila siku na tutaendelea kufaidilika mataifa mengine tunaona Azam analipa pesa nyingi sisi tunaangalia *movie* zimekuwa *translated Kiswahili*, kwa nini tuisiangularie za kwetu? Kwa nini ile pesa iende kule badala ya sisi tuipate hapa? Ni *reform* tu inayotakiwa kwenye suala la sanaa ambalo litasaidia vijana wetu waje na ubunifu mpya, waje na mbinu mpya tofauti na sasa hivi ukiangalia *movie* mtu anaweka sumu, anakoroga na anaonja; kweli utavutika kuangalia hiyo *movie*? Hapana, na *movie* hazina hisia. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo soko hili ni kubwa lakini linaleta mamilionea na mabilionea wengi na tunawajua sitaki kuwataja, tuna tatizo gani tuisitengeneze mabilionea

hana Tanzania au mamilionea ma-acter na *maactress* ambao watafanya kazi Tanzania zitauzika sehemu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ulikuwa mchango wangu kwa leo, lakini naiomba Serikali ije na *long term solution*, tukifanya *short term solution* atakuja Waziri mwingine ataimba Wimbo wa Taifa huu, atakuja mwingine ataimba huu kwa sababu kwa mfano mzuri tu, hawa waliiomaliza *bachelor of fine art and performing* Mheshimiwa Waziri labda ni takwimu alizonazo ni wangapi wameajiriwa walipomaliza hizi shule? Unakuta hakuna, lakini hata bodi ya mikopo hii *field ambayo* ni muhimu kwa sasa hivi kwa *digital economy* je, hao wanafunzi wanapewa mikopo asilimia 100 inavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ndio hii tunasema tunasoma *degree* hazina faida lakini *degree* ya *performing art* ina faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono, ahsante (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nikawa najiuliza hawa vijana wetu wa kuigiza sijua itabidi waigize kwa kutumia lugha gani hasa maana sisi wenyewe humu ndani tuna changamoto kweli Kiswahili chenyewe sisi wenyewe hapa hatukijui Kiingereza hatukijua wale watoto wetu sijui wataigiza nini huko nje, lakini ni mambo ya kujipanga Mheshimiwa Waziri nadhani mpango wa muda mrefu utakuwa ni pamoja na kujifunza lugha, kwa sababu zile tunazoangalia za nje mtu akiamua kuzungumza Kiyoruba ni Kiyoruba mwanzo mpaka mwisho, akizungumza Kiingereza ni mwanzo mpaka mwisho na ndio maana wanaweza kwenda sehemu mbalimbali zikatafsiriwa.

Sasa sisi hapa tukishafanya ule mchanganyiko wa mambo sijui tunategemea nani atusaidie kutafiri Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mheshimiwa Hassan Mtenga atafuatia Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama salama hapa, na kuchangia Wizara ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Katiba ya *TFF* kifungu 2.7 inaeleza *TFF* itashirikiana na Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar kwa yale mambo ya kimataifa na ndio kipengele pekee ambacho kipo katika Katiba ya *TFF*, yenye page 64 lakini cha kushangaza kifungu hiki hakifanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakifanyi kazi kwa sababu kunako mwaka 2017 Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar lilijiunga na uanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika *CAF*. Kwa muda mfupi Shirikisho la Miguu Zanzibar likaondolewa uanachama huo, lakini chakusikitisha na chakushangaza Chama cha Mpira wa Miguu - *TFF* hakikushiriki lolote juu ya kadhia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili *FIFA* inatoa mgao kwa wanachama wake kila mwaka usiopungua dola milioni mbili, lakini miradi hiyo yote ipo Tanzania Bara tu kwa mfano Kigamboni Dar es Salaam na Tanga; Zanzibar hakuna mradi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika,...

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ravia kuna taarifa, Mheshimiwa jitambulise.

## **TAARIFA**

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa naitwa Mheshimiwa Sima Hassan Sadiki, Mbunge wa Jimbo la Nungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa ndugu mchangiaji kwamba wakati wa uongozi wa

Mheshimiwa Tenga alipokuwa Rais wa *TFF* Zanzibar iliwahi kunufaika na huo mradi ambao anazungumzia kwa kujengewa uwanja wa Gombani, Pemba kule kuwekewa nyasi bandia, lakini toka kipindi hicho si chini ya miaka minane hakuna mradi mwingine wowote wa kimaendeleo uliwhi kufanyika kwamba kwa kutumia fedha hizo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ravia unaipokea taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Sadiki.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo na niunge mkono hoja na huo uhalsia ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Zanzibar haiwezi tena kuwa mwanachama wa *CAF* wala *FIFA*, kwa hiyo naomba niishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zikutane Wizara mbili za michezo kati ya Zanzibar na Tanzania Bara hili kulijadili mustakhabali mzima wa kadhia hii kwa wakati huu; pili, yafanyike marekebisho ya Katiba ya *TFF* na ndani ya Katiba ya *TFF* isomeke Zanzibar kitu ambacho kipo mstari mmoja; Makamu mmoja wa Rais *TFF* atoke Zanzibar; kuwe na Wajumbe wa Kamati Tendaji wa *TFF* ambao wanatoka Zanzibar; kuwe na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa *TFF* watoke Zanzibar na isiwe kama sasa hivi Rais wa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar na Makamu ni mwalikwa tu wa Mkutano Mkuu, aende pale akasinzie tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia turejeshe ligi ya Muungano ili tupate wawakilishi sahihi wa Tanzania na tupate kutengeneza timu ya Taifa ya Tanzania Bara yenyе ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kama haya hayatekelezeki naomba Bunge lako Tukufu liridhie na liwaruhusu Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar wawaarifu *FIFA* kipengele cha 2.7 cha Katiba ya *TFF* hakitekelezeki. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**NAIBU SPIKA:**Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Mtenga atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niseme nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara ya Habari, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumza suala la michezo ndani ya nchi yetu inawezekana tukazungumza kwa mapana na mrefu sana kwa muda mrefu lakini bila kuelewa changamoto tulizokuwa nazo au kupata tija juu ya michezo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nianze kwenye masuala ya mchezo wa mpira. Hatuwezi kuzungumza kwamba tunakwenda kucheza mpira bila kujiandaa, lakini mara nyingi nimekuwa nasilikiza hotuba za viongozi wetu wanatueleza kwamba Tanzania ni kichwa cha mwendawazimu, lakini haya yote yanakuja kwa sababu hatuna maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la viwanja hatuwezi kulibenza, inawezekana tukawa na *academy* nyingi za kutosha, lakini kama hatuna msingi wa kutengeneza viwanja vyta kutosha, hizi *academy* zitakwenda kuchaza wapi mipira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunavyo viwanja vyta Chama cha Mapinduzi, viwanja hivi mimi nadhani nimeshiriki wakati niko Hai nilijenga kiwanja pale kikubwa cha mpira na nadhani kiwanja sasa hivi kiwanja kile kinatumika, lakini nilivyofika Iringa niliboresha kiwanja cha Iringa pale. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja hivi vinahitaji kugharamiwa, lakini ukiangalia mapato yanayopatikana kwenye viwanja vile CCM nadhani inapata kwenye asilimia 20 ya mapato. Lakini tunapoingia sasa kuvikarabati viwanja

vile mzigo unabaki kwa Chama cha Mapinduzi. Sasa angalizo langu tuna fedha sisi ambazo zinatoka *FIFA* kwa ajili ya kuboresha masuala yote ya mpira katika chama chetu cha mpira, lakini tuijangaliea na tuangalie kwamba je fedha hizi zinatumikaje kwenye suala la mpira? Lakini leo tuna vilabu timu nyingi zinakwenda kwenye awamu ya kwanza zikishapanda daraja, awamu ya pili timu zile zinatemka daraja. Lakini timu hizi zinatemka daraja kwa sababu tayari hatujafikia malengo ya kuzilea hizi timu kwa mfano mimi ninayo kule timu ya Ndanda, toka inacheza ligi kuu inatoka Mtwara timu ya Ndanda wanasesfiri kuja Dar es Salaam lazima ungo utembee, lakini kuna wafadhili ambao wanaifadhili *TFF*, lakini ukiangalia kwenye kasma za fedha ambazo wanapewa kila klabu kwenda kuendeleza suala zima la mpira hawawezi ku-*move* kwenye suala zima la mpira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo langu leo Azam wametoa fedha nyingi sana, fedha hizi Mheshimiwa Waziri usipokuwa nazo karibu, hizi fedha zitaishia mikono ya watu, kama kuna fedha za *FIFA* zinakuja kwetu kwa ajili ya kuboresha mpira na fedha ni nyingi sana inayokuja Tanzania, lakini vilevile tumeshindwa kabisa hata kui-*maintain* timu yetu ya Taifa tutaweza haya mabilioni ya Shilingi yanayokuja, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli nikuombe kwenye suala hili la mpira kwetu Tanzania kwanza tuangalie kwenye viongozi wa *TFF*, hawa wanaweza wakatuvusha? Lakini la pili kuangalia mfumo wenyewe wa mpira tunaocheza Tanzania, tunazungumza kuhusu wachezaji wa kigeni, hatuwezi kuwakwepa wachezaji wa kigeni, wachezaji wa kigeni lazima waje na lazima wacheze kwa sababu hatuja waandaa wachezaji wetu humu ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mchezaji wa Kitanzania akishaingia amecheza Simba, amecheza Yanga na jina lake tayari limeshakuwa kuwa kubwa siku kesho anakwenda kuchenza mpira leo anatafutwa yuko baa, kwa namna moja au nyingine wachezaji wetu hili lazima tulizungumze bado hawajitambua kama mpira ni ajira. Wachezaji wa wenzetu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wa kigeni wanakuja kucheza mpira Tanzania kwa sababu wanaelewa mpira ni ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Wizara ijielekeze sasa kwenye kuangalia mazingira yote ya mpira, ukiangalia pale Brazil kuna wachezaji wa zamani, lakini wale wachezaji wote wa zamani wanapomaliza muda wao wa kustaa fu wanakuwa kuna chombo mahsus ambacho kinawawe ka kwa ajili ya kuwa makocha. Lakini leo ukiangalia Tanzania timu zote kubwa ukienda Namungo, Simba, Yanga na timu zingine zote kuna makocha ambao si wa zawa ni makocha wa nje, lakini timu za Brazil mnazoziona wanacheza mpira tunaziita *samba* wale kule kuna wazawa wenyewe ambao kuna chuo pale kinafundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi niombe tujielekeze na sisi sasa kufundisha makocha tunaposema sasa tunataka tusome lazima tuwe na walimu, hatuwezi kuzungumza kwamba tunataka tusome wakati hatuna darasa, walimu tunasema tunakwenda kusoma kusomea mpira, ni kitu ambacho hakiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumza kuhusu *academy*, *academy* hizi zina gherama kubwa sana katika bajeti hii ya Wizara niliyoiangalia suaona sehemu ambayo Wizara inakwenda kujikita kwenda kuendesha haya madarasa ya chini ya watoto wetu ili waweze kupanda. Leo ukiangalia inawezekana tukamzungumzia Messi amekulia kwenye *academy* ya Barcelona na amekaa pale na wachezaji kadhaa, ameletelewa, amefundishwa mpira toka akiwa na miaka mitano leo hii anaonekana mchezaji mkubwa duniani ambaye analipwa fedha nyingi duniani. Tunashindwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni mambo ambayo Mheshimiwa Waziri anatakiwa afanye sasa maamuzi kwamba sasa tunaingia, tutengeneze *academy* na vijana wetu waweze kucheza mpira. Mimi nina imani sana kubwa mtoto ukimfundisha akiwa mdogo ni mwepesi sana kushika

kile kile unachomfundisha, lakini sasa sisi bado hatujajajiwekeza huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza kuhusu BASATA; kama kuna chombo ambacho kinawezekana baadaye kikaenda kuua mziki wa kitanzania ni BASATA. Hili inawezekana Wabunge tukazungumza hapa na hatuzungumzi kwa mapana na marefu sana, lakini chombo hiki hakipo kwa ajili ya kuwa-*accomadate* wanamuziki, lakini chombo hiki kipo kimaslahi zaidi na matendo yao wanayoyafanya, yako ambao wanayafanya hata wanamuziki wenyewe, wasanii wenyewe wamekata tamaa na chombo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa na chombo yaani leo tunampishi anasema anampikia Mtenga ugali, lakini Mtenga anatoka anakotoka akienda kwenye sahani anasema ugali huu mimi siwezi kula, ni vitu ambavyo haziwezekani. (*Makofi*)

Kwa hiyo tuangalie Mheshimiwa Waziri afike mahali aiangalie hii BASATA, lakini arudi tena kwa upande wa *TFF* nenda pale ukaangalie viongozi wako wengine wana miaka 20 pale *TFF* hawa waliokuwa miaka 20 ndio *leadership*, wale wanapanga viongozi, wanajua mambo yakufanya, wanajua *deal* ziende wapi. Lakini wanajua mpira wao wanataka kuuendesha kwa namna gani, hatuwezi kumove kwa viongozi wale ambao ni watendaji pale *TFF* hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tunajidanganya, hivyo leo kama tuna *premier league* tuna timu zaidi ya 12 au 14, lakini timu hizi kama tungkuwa tuna watu wenye uwezo wa kufikiri tungefika mahali tukasema bwana kila timu kwa mfano kwangu mimi kule tuna timu ya Ndanda pale tuna Dangote; *TFF* wangekwenda kuzungumza na kampuni ya Dangote, wakafanya makubaliano wakawa mdhamini namba moja, lakini kuna *Breweries*, sijui Kilimanjaro kuna kampuni gani; vilabu vyote tusifike mahala hapa tukamsifia Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho inawezekana Waziri Mkuu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

inawezekana akasema jamani nguvu zimeniishia za kufanya hii kazi ya mpira nani anamsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tutengeneza sasa *impact* ya kujua kwamba tunawatafuta wawekezaji na hili ni suala la kulibeba Serikali sio suala la vilabu hivyi, kwa sababu vilabu vinakotokea mpaka vinapanda madaraja haya wanakwenda hawa kwa kuchangishana fedha zao. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha ahsante sana.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii, mimi nitazungumizia upande wa ngumi kwa sababu toka asubuni suaona uwakilishi kwa watu wa ngumi. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ngumi kama ilivyo michezo mingine ni ajira kwa vijana na mara nyingi sana na kwa muda mrefu ngumi iliyoonekana wapiganaji ngumi ni wakorofi, ngumi ni uhuni, ngumi sio kitu sahihi, ninamshukuru kipekee, Mheshimiwa Waziri aliyejita Mheshimiwa Mwakyembe alijitahidi sana na hasa baada ya kumpa ushauri wa karibu aliweza kuitengeneza tasnia ya ngumi angalau kuonekana ipo katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ngumi Waziri aliyejitaliza muda wake aliamua kuweka Kamisheni ya Ngumi, siku za nyuma watu wa ngumi wachache wajanja walikuwa wanachukua vijana kwenda kupigana nje ya nchi, unafahamu ili uweze kupanda daraja kwenye ngumi ni lazima umpsige adui yako ndipo unapanda cheo. Hivyo wale

tunawaita wasimamizi wa ngumi ikiwepo ma-*promoter* walikuwa wanachukua vijana wetu wanawapeleka nje ya nchi wakilua kabisa hawana uwezo wa kwenda kupambana na wale wanaoenda kuwagombanisha ili tu wale watu wa nje wapande daraja kwa kutumia vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ulikuwa uuaji na ilikuwa ni tabia mbaya sana. Sasa Mheshimiwa Waziri nina kuomba sana ninajua kwamba wako wachache waliobaki wanachukua vijana wetu wanapeleka nje kuwachezisha kwa mchezo ambao hawajakidhi kwa maana ya *kilogram*. Wapiganaji ngumi huwa tunapimwa uzito wako na uzito wa kwako na mwingine ndio unakuwa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakuchukuwawewe wa kilo 59 wanakupambanisha na mtu wa kilo 70 wa Uingereza *promoter* apate fedha wakati mpambanaji toka Tanzania anakuwa ameumizwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia hii Dkt. Mwakyembe aliikomesha, lakini bado inaendelea; ninaomba kiongozi wa sasa aisimamie na kuiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kamisheni ya Ngumi, mtu mmoja asubuhi amengumza habari ya majina ya Urais, sijui nani wa Kamisheni, mimi ninafikiri naunga naye mkono kwamba huyo anayejita Rais wa Ngumi iweze kubadilishwa. Kwa hiyo, ninaomba Wizara muangalie Katiba ya wanangumi ibadilishwe, maana utendaji wao ubabaishaji bado unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni *promoter* pia, baada ya kuacha masumbwi, umri umekwenda sasa nimetuwa *promoter*. Katika u-*promoter* wangu nimejikita sana kwa mabondia wa kike akina Feliche, akina Asha Ngedere na wengineo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabondia hawa hawajui mikataba ambayo wanakwenda kuchezeshwa *promoter* amelipwa shilingi ngapi; huo ndiyo ugomvu wangu mimi na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ma-*promoter* wengine, hata mkisikia natukanwa, juu kwamba mimi ninapambana. Sisi ma-*promoter* lazima tuoneshe mikataba na wale tunaoingia nao ili mcheza ngumi akienda kupigana ajue anapigania nini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mcheza ngumi anatolewa Tanzania anapandishwa basi kwenda Zambia na wala siyo ndege, anafika amechoka, anakwenda kupambana ngumi kwa kutumia nguvu zake, halafu unamlipa shilingi 200,000; hii siyo sawa. Ninaomba Wizara isimamie hilo. Na hasa ma-*promoter* wa mabondia wanawake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa unacheza ngumi ukishapigwa kwa *KO* mara nydingi thamani yako inashuka, unazeeka hata nyumba hujajenga. Leo hii mimi nimekuwa Mbunge, nashukuru angalau lakini wengine, mabondia wenzangu waliko nje, hawana hata nyumba kwa sababu ya kipato kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua *Tulia Trust* inasaidia sana, ninakuomba sana waone mabondia wa kike, ili uweze kuwasaidia kama ambavyo unasaidia wengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba bima za afya kwa mabondia. Serikali tunawaomba kama ikibidi mtulazimishe sisi ma-*promoter* tuwakatie bima mabondia wetu. Maana wasipokuwa na bima kuna wakati unapigwa ngumi moja unarudi chini ya ulingo hata pesa ya kujitibia huna. Ninaomba ma-*promoter* sasa waweze kuwalipia mabondia bima ya afya kwa faida ya maisha yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka kwenye ngumi, sasa nije kwenye *TBC*. Televisheni hii ni Televisheni ya Taifa na ina manufaa kwa Watanzania wote. Lakini nimekuwa nikimpigia simu Mkurugenzi wa Shirika hili; kuna wakati vyama vya siasa ambavyo ni walipa kodi na wana uhalali na *tv* hii pamoja na redio, lakini wanapokuwa na shughuli zao ni vigumu sana kukubaliwa kutoka *live* kama ukiwa chama mbadala na wala siyo chama tawala. Ninaomba sana

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mkurugenzi ufikirie, *tv* hii pamoja redio ni ya Watanzania, tuhudumiwe kwa usawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, usikivu hasa mipakani, bado unasumbua. Ninaomba Serikali iongeze fedha ili tuweze kuongeza usikivu kwa ajili ya Televisheni ya Taifa pamoja na Redio Tanzania ya kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niweze kuzungumzia Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kila mtu ana haki ya kupata habari, ya kutoa maoni, lakini kwa nyuma kidogo kulikuwa kuna ugumu wa kutoa maoni kwenye mitandao ya kijamii, kwenye redio na vitu kama hivyo. Lakini tunamshukuru Rais, amesema vyombo vyote viwe sawa na akaruhusu baadhi ya vyombo vilivyofungiwa virudishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nitumie nafasi hii kuiambia Wizara irudishe magazeti yote, irudishe vyombo vyote kwa...

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Taletale.

## TAARIFA

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa *promoter*, kabla Mheshimiwa Waziri hajarekebisha hilo neno la rais, ukisema rais sema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mnavyosema Rais tunajua Rais wa Ngumi, ahsante. (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaikubali taarifa hiyo, ni Rais wa Jamhuri ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Muungano wa Tanzania, ni mmoja, lakini Rais wa Ngumi, Rais wa Yanga, wote hao wafutwe abaki Rais wa Simba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema vyombo vyote vilivyofungiwa virudishwe na mimi nakubaliana naye, nami ninasema leo hii kwenye Wizara hii, ninaomba kabisa zile sheria ambazo zililetwa hapa tukazipitisha, kama ikiwekezana Wizara ilete tuweze kurekebisha baadhi ya sheria tulizozipitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ile sheria ya kukubali haki ya vyombo vyaa habari irudiwe, marekebishi ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vyaa Habari ile ya 2016, kama inawezekana iletwe tena tuone kama kuna sehemu ya kurekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Makosa ya Mtandao pia nafikiri kuna haja iletwe sasa tuweze kuirekebisha. Dunia ya sasa mtandao uko kiganjani, tukianza kushikana kwa *cybercrimes* kwamba umeongea kitu hiki *facebook*, umefanya hivi, haiwi sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nizungumzie suala la BAKITA. Tunafahamu kwamba Kiswahili ndio lugha yetu ya Taifa, na Marehemu Rais Nyerere, wote hao walizungumzia sana suala la Kiswahili. Leo hii ukienda nchi zingine, kwa mfano Afrika Kusini ilitaka shule zake, vyuo vyake viweze kuwa vinatumia lugha ya Kiswahili. Lakini walioshinda tenda ya kufundisha ni Wakenya ambaao wao ni wanafunzi wetu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba sana BAKITA ni lazima mchukue nafasi ya kuwasaidia Watanzania fursa mbalimbali ambazo zinajitokeza, muwe wa kwanza na mfanye kwa haraka kuhakikisha hatuachwi nyuma kama waanzilishi wa lugha hii ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafahamu wengine wamezungumza habari ya sanaa, ni kweli wasanii, wakiwemo

waimbaji wa maigizo, wamekuwa wakijitumikisha wenyewe na kufika mahali tunawasifia, ni baada ya wao kutumia jitihada zao binafsi kufika hapo walipofika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wamezungumza habari ya kuweza kumpigia kura Diamond. Mimi nafahamu yupo mtoto anaitwa Sonia wa Monalisa. Huyu ni binti wa sekondari lakini ameingia kwenye kuchaguliwa na ametaka wananchi tumchague, ni juhudzi za bibi yake anatoa *Instagram*, na mimi ninayemfuatilia ndiyo ninaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara inafanya nini kuwasaidia vijana kama hawa? Wizara inafanya nini kumsaidia Diamond kuweza hata kutangaza kwenye *TBC*, ndiyo kazi ya Televisheni ya Taifa, wala siyo kusikiliza taarab, ni vyema tukaangalia vitu vya msingi kuliko kuweka vitu ambavyo ni vya kujiburudisha na wala havijengi wala kusaldia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sanaa; mwingine amezungumza, vijana wetu kwa sababu ya kutokuwa na ajira, lakini wakati mwingine wana vipaji, wamekwenda kuingia kwenye sanaa. Leo mtu anaigiza amekaa chini ya mwembe lakini inadondoka nazi, ni kwa sababu ya kutokuwa na elimu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuwasaidie. Ninaomba Wizara itumie fursa ya makusudi kuwasaidia. Wanahitaji kuigiza, lakini hawana elimu, hawana msaada kutoka kwenye Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba, siyo kuunga mkono, lakini ninaomba Serikali ihakikishe inasimamia hayo bila kusahau kuwasimamia ma-boxerwangu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya ajiandae.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naomba nishukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia Wizara hii muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kujikita kwenye habari baadaye nitakwenda kwenye michezo na kama muda utaniruhusu, nitamalizia kwenye utamaduni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa habari naomba niongelee hili Shirika letu la Utangazaji la Taifa - *TBC*. Maeneo mengi ya Mkao wetu wa Tanga hayana usikivu, kwa mfano kwa maeneo kama vile ya Mkinga, Mlalo na Bumbuli wanasikiliza sana redio za Kenya kuliko za Tanzania. Kwa hiyo hali hii ni ya hatari sana, wale watu wanakosa mawasiliano kabisa na kama tunavyojua, mawasiliano ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la *TBC* kwa maeneo hayo walifunga minara yao kwa Kata za Mnyuzi na Kwemshai maeneo ya Korogwe na Lushoto. Lakini sasa maeneo ya Mlalo na Bumbuli yako nyuma ya mlima, kwa hiyo hayapati mawimbi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri waliopita walikwenda mara kadhaa wakaahidi kushughulikia suala hilo lakini mpaka sasa halijashughulikiwa. Kwa hiyo, niiombe Wizara itukumbuke watu wa Mkao wa Tanga kwa maeneo hayo ambayo hatuna usikivu waende wakarekebishe mitambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia cha kushangaza ni kwamba hapo awali maeneo hayo yalikuwa yanakamata lakini baada ya kutoka kwenye mfumo ule wa *analogue* kwenda kwenye mfumo wa *digital*/wa *fm* ndiyo yamepoteza usikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo nashindwa kuelewa, kwa nchi nyingine wakitoka kwenye mifumo ya zamani wakiwa wanaboresha mifumo yao kwenda kwenye

mifumo mipya ndiyo wanafanya vizuri zaidi. Lakini sasa ni tofauti sisi kwa nchi yetu, yaani tulivyokuwa kwenye *analogue* maeneo yale yalikuwa yana usikivu na tulikuwa tunakamata vizuri hizo redio. Lakini baada ya kufanya marekebisho yale kutoka kwenye hizo *short waves* kwenda kwenye *fm*, maeneo yale yamepoteza usikivu. Kwa hiyo niiombe Wizara iende katika maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kwenye Shirika letu hili la Utangazaji la *TBC*, naona kama bado vifaa vyao vingi si vya kisasa; naomba wapatiwe vifaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waandishi wetu wa habari naona maslahi yao bado ni madogo mno, tuangalie namna ya kuongeza maslahi ya waandishi wa habari. Wanafanya kazi kubwa na ni kazi ngumu mno. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona hata tunapokuwa kwenye misafara ya viongozi, wakati viongozi wanakimbia na zile *V8* nao wanakimbia na magari yao na wanatakiwa kuwahi pale tukio likitokea, kila kituo mnachohama yaani unaona wanavyopata taabu na wanavyoomba *lift* kwenye magari ya viongozi. Kwa hiyo, naomba sana pia waandishi wa habari waangaliwe kwa upande wa maslahi na upande wa vifaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye michezo. Michezo ni ajira, michezo ni afya na michezo ni uwekezaji pia. Lakini nimesikiliza vizuri hotuba ya Wizara hapo asubuhi, hoja yao moja kubwa, walisema mkakati mmoja wapo wa Wizara ni kuongeza ushiriki wa michezo kwenye ngazi za shule na jamii. Nafikiri ndiyo mkakati wao mmoja mkubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa kuongeza ushiriki tu peke yake haitatosha kama Wizara haitashirikiana na Wizara nyingine kama vile TAMISEMI na Wizara ya Elimu. Kwa sababu samaki mkunje angalia mbichi; vipaji vinaandalialiwa watoto wakiwa bado wadogo na watoto wetu hawa kwa muda mwangi huwa tunawakabidhi shulen, tunawakabidhi

kwenye Wizara ya Elimu. Mpaka mtoto yule anaporudi kwako, kama mara nyingi anavyosema Mheshimiwa Jumanne Kishimba ambaye leo nafikiri hayuko hapa anasema tunakukabidhi mtoto yule akiwa mdogo unakuja kunirudishia mtoto akiwa mkubwa na hajui chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sasa huku shulenii kuna michezo na kwenye shule zote za Serikali huwa kuna pesa zile za *capitation*. Pesa zile zinaingizwa kila mwezi na ni pesa nyingi sana ambazo kama tungezisimamia vizuri, Wizara ya Michezo nayo ingekuwa inafuatilia, wakashirikiana na Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI, nafikiri tungeibua vipaji vingi vya watoto wakiwa kuanzia wadogo mpaka tukawaendeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu, tuchukulie tuna shule za msingi na za sekondari 20,000 zote jumla, na ziko zaidi ya hizo, na kila shule kwa mfano mimi nilikuwa mwalimu, kwa mwezi shule yangu ilikuwa inapokea shilingi 243,000 pesa za michezo kila mwezi kwenye kila shule ya Serikali ni asilimia kumi, unatenga pbeni, pesa ile ya *capitation* ambayo ilikuwa ni kama elfu ishirini na kitu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukichukua tu ile 20,000 mara shule 20,000 ni pesa nyingi sana, ni *millions of money* na huo ni mwezi mmoja, sikwambii mwaka mzima, sikwambii miaka mitano. Ni *billions of money* tunapeleka pesa za michezo kwenye kifungu kile cha *capitation* lakini hakuna vipaji vinavyozalishwa huko kwa sababu kwanza hakuna vifaa, hakuna viwanja na wale wanafunzi hawana lishe, hawawezi wakashiriki michezo wakiwa na njaa, tutakuwa tunajidanganya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapohapo kila mwaka tuna mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA. Yale mashindano yapo toka enzi kwa hiyo sasa hivi yamekuwa tu ni kama mazoea. Tulitarajia pia kupitia mashindano yale ya michezo shulenii kila mwaka, pale ndiyo tungekuwa tunaibua wanafunzi ambao wanapenda michezo, ni rahisi sana kuwasoma pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini mashindano yale huwa yanaanza ngazi za shule Tanzania nzima, yanakwenda ngazi ya Wilaya Tanzania nzima, ngazi za Kata, ngazi ya Kkoa na baadaye wanafunzi wanapelekwa Taifani. Na maeneo yote humo inakopita kwenye hiyo michakato wanafunzi huwa wanalala kambini na wanachangiwa chakula na baadaye wanafunzi wanafika mpaka mwisho Taifani tunapata washindi wa Kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini baada ya kupata wale washindi wa Kitaifa kila mwaka, hawaendelezwi na wala Serikali haitambui chocchote. Na ukimuona kama kuna mchezaji ambaye ameibuka yaani ni yeye mwenyewe juhud zake mwenyewe, usifikiri kwamba kuna jitihada za Wizara pale, hapana. Kwa asilimia kubwa wanaoibuka; si wasanii, si wachezaji, si kwenye vikundi nya ngoma, ni jitihada zake mwenyewe. Ni mwanafunzi tu alikuwa na *interest*ya michezo, akitoka shule anakwenda kwenye viwanja nya vumbi, anacheza na baadaye anakuwa mchezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni wakati sasa wa Wizara hizi tatu kushirikiana, hizo pesa zisipotee. Tunaweza kuibua wachezaji wengi sana kuititia pesa zile na Wizara yenye ikifanya jitihada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Wizara, tunaweza tukajenga shule za kanda; ni ngumu sana kujenga shule za michezo katika kila mkoa, Iakini tunaweza angalau tukaanza na kanda. Kwa hiyo, wale wanafunzi tukishakuwa tumewachagua kwenye zile UMITASHUMTA na UMISETA, ni vizuri sasa wale wakawa historia yao vizuri, ndiyo mana nasema hizi Wizara zishirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wizara ya Elimu ndiyo yenye watoto, Wizara ya TAMISEMI ndiyo yenye miundombinu ambayo ndiyo tunaweza tukawaomba baadaye wakatusaidia kujenga shule hizo. Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali tunaweza tukafikiria kujenga shule hizo za kikanda Iakini pia tunaweza tukaboresha viwanja vyetu shuleni pamoja na kuboresha lishe ku-promote michezo.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana kuangalia huku mbele, ukiona *microphone* imewashwa basi unaangalia sentensi ya mwisho.

Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa mara ya pili leo kuinuka kwenye kiti changu na kuweza kuzungumza na kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza ninapenda kujikita kwenye michezo na baadaye kama nafasi itaruhusu basi nitaongelea pia upande wa habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza nashukuru na kuwapongeza uongozi mzima wa Wizara ya Michezo kwa namna ambavyo imekuwa ikishirikiana vizuri na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*) na ningependa nijitambulishé uhusika wangu kwenye michezo, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho wa Mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*), lakini pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mpango na Fedha ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania. Na nimekuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa *TFF* kwa miaka 14 hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kwanza kupongeza ushirikiano uliopo kati ya Serikali na *TFF*, Serikali imetusaidia mambo mengi katika kuboresha mpira wetu wa nchi hii ya Tanzania. Tumeshuhudia mwaka juzi wakati

tunajiandaa na mashindano ya *Under Seventeen* Barani Afrika iliweza kujitolea jumla ya shilingi bilioni moja, kwa kweli zilitusaidia sana na zimeboresha mambo mengi katika yale mashindano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na ushirikiano uliopo ndani ya miaka minne iliyopita tumeweza kushiriki mashindano ya *CHAN* pamoja na mashindano ya *AFCON* kwenye *senior teams*. Lakini vilevile tumetoa mataji tisa kwenye mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo mataji kwa timu za wanawake na vijnaa, lakini vilevile tumekuwa na mafanikio makubwa kwenye ligi yetu ya Tanzania Bara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ligi yetu miaka minne iliyopita ilikuwa kwenye nafasi za ishirini huko, lakini kutokana na ushirikiano mzuri kati ya Serikali, wawekezaji kwenye *football*, lakini na *TFF* basi sasa ligi yetu inashika nafasi ya nane kwa ubora Barani Afrika. Tunazididi nchi za Nigeria na Algeria ambazo kwa miaka mingi zilikuwa kwenye nafasi tano za juu, sasa zinashika nafasi ya tisa; ya kumi na kuendelea, sisi nafasi ya nane. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kutokana na maboresho ya ligi ambayo tunayo ndiyo maana vilabu vyetu ambavyo vinatuwakilisha katika mashindano ya kimataifa vya Simba na Namungo vimetuwezesha kufika katika hatua nzuri ya mafanikio kuliko kipindi chochote tangu Uhuru wa nchi hii. Hii inatokana na ubora wa ligi ambayo inaendeshwa katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kuwapongeza Klabu ya Simba ikiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye ni Mbunge wa Jimbo langu mstaafu, Ally Murtaza Mangungu pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, pamoja na Mtendaji Mkuu wa Club ya Simba, Dada yangu Barbara Gonzalez. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitakuwa mchache wa fadhila kama nisipoipongeza timu ya Namungo kwa kazi

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nzuri ambayo wamefanya hasa msimu huu uliopita, katika msimu wake wa kwanza klabu ya Namungo imeweza kufanya vizuri katika ligi kuu pamoja na mashindano ya FA na hatimaye ikaweza kutuwakilisha katika mashindano ya kimataifa kwenye kombe la shirikisho kwa mafanikio makubwa na mafanikio haya yaliongozwa na kaka yangu, rafiki yangu Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, Mheshimiwa Hassan Ziddu, hongera sana Mheshimiwa Hassan Ziddu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ningependa sasa kushukuru kwa namna ambavyo hotuba ya Wizara, lakini pia hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu alipofika hapa Bungeni kwa kuonesha nia ya dhati ya *ku-support* timu zetu za Taifa. Katika nchi za jirani ambazo zimepiga hatua kuliko sisi kwenye *rank* za sifa na mambo mengine tumeshuhudia zikiwa *zina-support* timu zao kwenye mambo mengi kwenye *training session* zao, lakini vilevile zinapokwenda kushiriki mashindano mbalimbali katika maeneo ya kuwapa usafiri wa kwenda kwenye mashindano hapo Kenya tu na Uganda wamekuwa wakifanya hivyo kwa miaka mingi hivi sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye masuala ya *accommodation* wanapokwenda kucheza mashindano nje ya nchi, lakini pia kwenye posho za kujikumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba tu kwa kuanzia Serikali yetu niishauri iwekeze kwenye hayo maeneo katika *kuzi-support* timu zetu za Taifa. Lakini vilevile pamoja na mafanikio ya timu ya Simba kulikuwa na wimbi la watu wengi kujaribu kuipiga vita timu ile, wamekuwa wakipokea wageni jambo ambalo mimi sijawahi kuliona katika nchi yoyote wakati nilipokuwa naongozana na timu ya Simba kwenda katika mashindano mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi nilipata nafasi ya kuwa *head of delegation* wakati timu ya Simba ilipokwenda kucheza na timu ya *Nkana FC*, lakini pia ilipokwenda kucheza na timu ya *Saura* kule Algeria, tulipofika Algeria tulioneshwa vidole saba, kwa sababu mwaka

uliotangulia timu yetu ya Taifa ilifungwa goli saba kule Algeria, Algiers. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulipofika Zambia kule Kitwe tulivyotua na ndege tu pale Ndola tulikuwa tunaonyeshwa vidole vinne kwa sababu kwa mara ya mwisho Simba ilipokwenda Zambia ikacheza katika uwanja wa Ndola ilifungwa goli nne, lakini cha ajabu na cha kusikitisha katika nchi hii wametokea watu hivi sasa timu ngeni zikija zinapata kupokelewa na ukiangalia yale mapokezi huwa yanaratibiiwa na watu ambao wana akili zao, siyo wale washabiki wa kule Uzuri kwa Mfugambwa au kule Somanga, Kilwa. (*Makofi*)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ningeomba Serikali ijikite katika kuwafundisha uzalendo wananchi wetu ili mwakani tunapokwenda kucheza timu nne basi hizi vurugu vurugu zisiwepo timu zetu ziweze kufanikiwa vizuri.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa hivi kwanza moja atumie lugha ya Kibunge anapochangia na kuzungumzia juu ya kutoa lugha ambazo zinaonesha kama vile hao wanaouna timu zingine, lugha hizo ambazo anatumia si nzuri. Lakini kingine...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali ngoja lugha gani iliyotumiwa, kwa sababu mimi hapa nasikiliza Wabunge wote wanaochangia, lugha gani ya Kibunge aliyoisema?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ambayo imetumika ni kuonesha kama vile timu

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ambayo wanayoizungumzia kwa mapenzi yake yeye ni kama timu ya Taifa ya Tanzania. Kwa hiyo, timu ni moja tu ya Tanzania ambayo ni uzalendo kwa watu wote ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali nisikilize kwanza, nisikilize kwanza, ulipewa nafasi ya kuchangia wewe kuhusu timu yako na yeye anachangia kuhusu timu yake kwa hiyo wewe ulisema unataka kumpa taarifa sasa sioni kama unataka kutoa taarifa naona unataka kukosoa uchangiaji wake. (*Makofi*)

Alikuwa amekaa hapa Mheshimiwa Spika wewe ulipata fursa ya kuchangia ukamaliza mchango wako, kuhusu timu yako kwa hiyo muache na yeye amalizie kuhusu timu yake hakuna lugha ambayo si ya kibunge aliyoizungumza.

Mheshimiwa Ndulane malizia mchango wako. (*Makofi*)

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, mimi siipokei taarifa yake kwanza, nazungumza kama Mbunge, lakini pili nazungumza kama mmoja kati ya wanafamilia ya mpira katika nchi hii, kwa hiyo na-*balance story* yangu, nai-*balance*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningependa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane kuna taarifa nyingine simuoni Mbunge akisimama, ni wapi.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu spika, nipo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba siku zote unaposema ukweli unauma sana hasa kwa mtu ambaye anaguswa na jambo lake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane unapokea taarifa hiyo.

**MHE. FRANCIS N. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea kwa mikono miwili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yote ambayo tumeyapata vilevile kunachangamoto kwenye utambuzi wa mchezo wa mpira wa miguu kama *profession* na nina fikiri hapa ndipo tunapokwama. Mpira ni *profession* kama zilivyo *profession* nyingine kwa hiyo zinatakiwa zitengenezewe msingi imara wa kufundishwa, lakini vifaa nya ufundishaji vipatikane na vilevile mafunzo yawezwe kuendeshwa kama mafunzo ya *profession* zingine, hapa ndipo tunapo-fail. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningelomba Serikali yangu pamoja na kuwekeza kwenye *national team* pia iweze kuwekeza kwenye mafunzo kuanzia watoto wadogo kule wanakosoma kwenye shule za msingi na shule za sekondari, twende tukafundishe walimu wengi wa mpira na michezo mingine, lakini vilevile twende tukahakikishe kwamba watoto wanafundishwa angalau kila Halmashauri kuwe na kituo kimoja cha uendelezaji wa soka la vijana ili vipaji vyote viweze kukusanya na viweze kuendelezwa na hatimaye tuweze kupata wachezaji ambao wanafaa kutusaidia kutuvusha katika mashindano mbalimbali. (*Makafi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachezaji ambao tunao hivi sasa wanatokea *from nowhere*, wanaokotwa okotwa tu halafu mwisho wa siku unaskia tayari wanacheza *national* timu kwa hiyo hawana zile *ethics* za uchezaji mpira. Kwa hiyo, naomba Serikali iwekeze kupeleka fedha kwenye halmashauri kwa kusudio maalum kama tulivyofanya kwenye miradi mingine na kwenye mradi huu maalum uwepo wa kuendeleza vipaji nya watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa vilevile kuchangia kwenye changamoto. Shirikisho letu la mpira Tanzania limekuwa likiendeshwa kwa shida sana, wakati fulani

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Shirikisho letu lilikuwa na deni la jumla ya shilingi milioni 10.18 wakati wa utawala wa Tenga, Malinzi na hata sasa wakati wa utawala wa Wallace Karia. Deni limelipwa kwa kiasi cha kutosha kama nusu ya deni sasa hivi *TFF* inadaiwa kodi jumla ya shilingi bilioni 5.009, ndani ya deni hilo lipo deni la shilingi bilioni 4.55 linalotokana na kodi zilizotokana na michezo mbalimbali ambayo ilifanyika hapa Tanzania ya kimataifa na kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwaka 2010 timu yetu ya Taifa ya Tanzania ilipocheza na timu ya Taifa ya Brazil ile mechili aliyeialika timu ya Taifa ya Brazil haikuwa *TFF* na hata mapato yaliyopatikana pale uwanjani ambayo yalivunja rekodi ya mapato hayakwenda *TFF*, lakini mwisho wa siku lile deni la *VAT* lilipelekwa *TFF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna fedha za kuwalipwa makocha zimekuwa zikilipwa na Hazina tangu enzi za akina Marcio Maximo, kuna mkusanyiko wa *pay as you earn* kulikuwa na jumla ya shilingi bilioni 1.3, lakini *TFF* imehangaika kulilipa limebaki jumla ya shilingi bilioni 1.049.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kawaida ya malipo ya mishahara kwa watumishi wa Serikali ambao vilevile wale makocha walikuwa wanapitia kama Marcio Maximo alikuwa analipwa na Hazina, lakini wakawa wanalipa ile *net figure* halafu deni bado linabaki la kodi na yale makato mengine ya kisheria yalikuwa yanabaki kwa *TFF*, kwa hiyo *total* sasa hivi ya deni liliobaki ni jumla ya shilingi bilioni 5.809.

Kwa hiyo, ningeiomba Serikali ijitahidi kuifutia *TFF* deni hili ili waweze kuongeza ubora wa kusimamia mpira wa nchi hii, ili tuweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa habari ningeomba kwanza niishukuru Wizara yetu kwa kufanya kazi nzuri, nikianza na Mkurugenzi wetu wa Habari, kwanza Waziri, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Mheshimiwa Bashungwa pamoa na Mheshimiwa Gekul. Lakini vilevile kuna Mkurugenzi

Mkuu wa Habari Ndugu Gerson Msigwa kwa kweli amekuwa akifanya kazi kubwa ya kutujuza taarifa mbalimbali zinazohusu Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nivipongeze vyombo vyaa habari vyaa TBC, ITV, Azam Tv, Redio Abood, Redio Mashujaa kule Lindi na Mtwara, Millard Ayo, pamoja na Clouds FM. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya atafuatiwa na Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae. (*Makofii*)

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbwe wote ambaye amenipa uhai wa leo hii kusimama leo na kuzungumza sekta yangu na sekta ya maisha yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii naomba nizungumze na umma huu wa Wabunge pamoja na Taifa hili. Sanaa ni maisha yetu vijana na kama Serikali ina mpango mzuri wa kuongeza ajira kwa vijana basi sanaa ni sehemu nzuri sana ya kuongeza ajira. Msanii kama msanii anayeimba, kuna anaye-produce, kuna director, kuna mpiga picha, kuna kila aina ya kazi, sasa hivi hadi mabaunsa wamekuwa wanaajiriwa kuititia sehemu ya sanaa. Kwa hiyo sanaa ni jambo muhimu sana na tukilizungumza hapa tuzungumzie kwa u-serious wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye upande wa mirabaha; mirabaha kwa wasanii ni jambo la muhimu sana, leo hii Keisha nitazeeka, siasa nitastaafu, lakini kuititia hii mirabaha tutaweza kupata pesa

mpaka tunakufa na watoto wetu wataendelea kula hela, kama ambavyo mimi sasa hivi bado naendelea kula hela ya muziki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii hela ya muziki tunayokula, tunakula kupitia *caller tune, ringtones*, lakini tunataka *COSOTA* wasimamie mirabaha. Hii mirahaba itatusaidia sisi ku-*generate lot of money*, yaani pesa nyingi sana ambazo hizi pesa zitatusaidia sisi wasanii kutengeneza kazi zenye ubora ili tuweze kushindina kimataifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mirabaha ninayoizungumiza hapa kuna sehemu za starehe nyingi sana ambazo wewe huwezi kwenda kwenye starehe kama hauwezi kusikiliza muziki, kwa hiyo mirabaha hii tunayoizungumza sehemu za starehe, sehemu za mabasi, sehemu za *hotels* hawawezi kupiga muziki wetu bila kulipla pesa, ina maana tunapata pesa nyingi sana, lakini vilevile na Serikali inakusanya mapato mengi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna mapato mengi ambayo yanakosekana kwa Serikali kwa sababu ya kutokusimamia vizuri mirabaha ya wasanii katika hii nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine naomba nizungumze juu ya masuala ya maadili, mimi ni mfuasi mzuri sana wa maadili ya wasanii. Ni mfuasi mzuri sana na ni mfano mzuri sana kwa maadili ya wasanii. Leo hii mimi nisingefika hapa kama ningekuwa sina maadili, lakini maadili gani tunayozungumza hapa, maadili ya kufungia nyimbo za wasanii bila kujua hawa wasanii wanatakiwa waimbe nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba Wizara iwaite hawa wasanaii, ikae nao, iseme wanataka nini katika hizi kazi, lakini siyo wasanii peke yao hata hivi vyombo vya *televisions, media* zote wawaite, *media* ziambiwe ni nyimbo gani na nyimbo gani zinatakiwa kupigwa kwa muda gani, kwa sababu kuna muda amba Watoto wamelala,

hawasikilizi nyimbo zingine, lakini kuna hata kwa hawa watu wa filamu wanaigiza filamu na zinawekwa masharti pale chini ya miaka 13 hapaswi kuangalia hii filamu, chini ya miaka 18 anapaswa kuangalia, hivyo, kwa hiyo tuweke utaratibu ambao hawa wasanii watajua ni namna gani wao wanapaswa kuongoza kazi yao ili waweze kufanya kazi zao za sanaa kwa uhuru vizuri. Kwa sababu mwisho wa siku utamfungia huyu msanii ana familia yake, ana maisha yake, ana ndugu zake wanamtegemea hebu tuangalie hili suala kama Wizara ione namna gani ya *ku-deal* na wasanii katika masuala haya *especially* masuala haya ya maadili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimefurahi sana kuona kwamba katika hii hotuba ya Waziri imezungumza kuhusu masuala ya tuzo. Tuzo ni muhimu sana, mimi nimekuwa msanii kwa kipindi cha muda mrefu na nimekuwa nimeshika tuzo mbili za mwanamuziki bora wa kile Tanzania, lakini nimeshika tuzo ya albamu bora ya Zuku. Hizi tuzo zilinifanya mimi niwe *motivated* kufanya kazi sana. Kwa hiyo leo hii kama Wizara imeona umuhimu wa kuanzisha tuzo hizi basi ione umuhimu wa kuruhusu tuzo zingine za watu wengine kuendelea kufanya kazi kuliko kuwawekea vizingiti vingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mtu akianzisha tuzo anaambiwa kipengele fulani usiseme, kipengele fulani usiseme, sasa hizi tuzo zitaendeshwaje, hizi tuzo mnataka ziwe nydingi ili *zi-motivate* wasanii wetu. Wasanii wapo kila sehemu na wanafanya vizuri na kila msanii ana ubora wake na katika kazi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikwambie jambo moja ambalo wasanii wanahangaika, wasanii wamepata bima za afya, lakini wasanii wanataka bima ya maisha. Tunashukuru sana Wizara, wameweza kutuwezesha kupata bima za afya, lakini wanataka bima za maisha ili wajihakikishie maisha yao hawa wasanii, tunaomba sana sana hili jambo liendele, liwekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba pia nizungumze juu ya masuala ya maadili ya mavazi, hili suala

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

jamani naomba sasa Serikali ituambie ni mavazi gani msanii anapaswa avae. Je, akienda kufanya *video* kwenye *swimming pool* anatakiwa avae baibui au nikabu? (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize ni mavazi gani haya ambayo yanahitajika kwa wasanii wavae? Je, tuangalie asili ya Mtanzania vazi lake ni nini? Turudi tena huko kwenye tamaduni zetu, tuangalie Mtanzania anapaswa kuvala nguo ya aina gani, ili akifikisha ujumbe ajue anafikisha ujumbe kwa namna gani. Wenzetu tunawaona nje wanavaa *swimming costumes* kwenye *swimming pool* kwa sababu ndivyo utamaduni wao unavyosema. Basi na sisi tuangalie kwenye *swimming pool* tuvae nini, tuvae nikabu au tuvae *skin tight* au tuvae nguo gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni suala la uhalisia, leo hii tutawalaumu wasanii wanaenda kurekodi nje *South Africa* wapi, kwa sababu wanafuata *facilities*, hizi *facilities* zinawasaidia wao kuonesha uhalisia katika kazi zao. Sasa leo hii kama *facilities* hapa Tanzania haturuhusiwi kutumia nguo za polisi, haturuhusiwi kutumia sijui mahakama, sasa tutafanyaje kazi kama wasanii? Uhalisia utatoka wapi? Tutashindana vipi kitaifa na kimataifa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Diamond kusema kweli, Diamond anatuwakilisha vizuri sasa hivi Diamond anagombea tuzo ya *BET*. Ningombwa Wabunge wote hapa wam-support Diamond kwenye ma-group yao ya maeneo yao wapige kura kwa ajili ya Tanzania. Diamond hayuko pale kwa sababu ya Diamond au kwa ajili ya Wasafi au kwa sababu ya Babu Tale hapana, Diamond yuko pale kwa ajili ya Watanzania na anawawakilisha Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba Bunge hili wahamasishe wananchi wao huko wanakoenda, wampigie kura Diamond aweze kuleta tuzo hii Tanzania *proudly* kabisa na sisi tuone kwamba tumepata hii tuzo ya mwanamuziki ambaye anaiwakilisha vizuri Tanzania hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache na Bunge lako hili Tukufu, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini naomba niunge mkono hoja endapo haya mambo yatatekelezeka, lakini nilisahau jambo moja la mwisho samahani kweli muda wangu haujaisha. Kuna suala hili la *arena*. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *arena arena arena*, Babu Tale umesahau kuwaambia kwamba...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keisha muda wako umekwisha.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kupongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya chini ya Waziri Bashungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mchango mfupi sana kwenye Wizara hii ya Michezo, jambo la kwanza ni makato yanayofanywa na Serikali baada ya mechi. Tunafahamu wote kwamba kuandaa timu au kuandaa mchezo ama mchezo ni gharama kubwa, lakini inasikitisha sana baada ya mechi, Serikali mmekuwa mkivamia hayo mapato na kuanza kuyakatakata vipande vipande. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoandaa mechi tatizo la Serikali wanakwenda kuangalia nini kimepatikana siku ya mechi. Hawaangalii umetumia shilingi ngapi kuandaa hiyo mechi. Tafsiri yake ni kwamba wanakuja wanakatakata

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mpaka wanakula mtaji halafu kesho timu zinashindwa kuandaa mechi. Serikali haijui mchezaji ili ahudhurie mechi moja anahitaji kula, kuvaa, kutibiwa, kunywa maji, kwenda mazoezi na kufundishwa na mwalimu aliyebolea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hayo Serikali hawayajui na hawataki kuyasikia. Siku ya mechi utawaona wako getini *TRA* wanakata asilimia 18, Halmashauri wanakata asilimia 10, BMT wanakata asilimia tatu, pasipo kujua umewekeza shilingi ngapi mpaka kufika siku ya mechi. Sasa kwa mfano, unatumia shilingi milioni nane kuandaa mechi moja, halafu getini unapata shilingi 2,100,000. Lakini fedha zote hizo Serikali inaziangalia na inakwenda kuzikata pasipo kujua umetumia shilingi ngapi kwenye kuandaa hiyo mechi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona huu ni uonevu na kwa stahili hii hatuwezi kuendeleza mpira wa miguu kwa namna yoyote ile, vinginevyo kama tunapiga *story* ili muda uende hakuna, haitawezekana. Hii kuandaa timu imekuwa ni kama watu wanapiga *story* sio jambo rahisi kama tunavyofikiria. Wachezaji hawa wanakula, wanatibiwa, wanaumwa, *ankle*, magoti, sijui visigino vimefanya nini. Ukimtibu mpaka kumpeleka kwenye mechi ni gharama kubwa, lakini inasikitisha sana wakati unafanya hayo yote Serikali haipo. Unawatibu wachezaji Serikali haipo, unalipa kocha Serikali haipo, Serikali inakuja kuonekana siku ya mechi inataka asilimia 18. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akaliangalie hili vizuri akae na wenzake muone mnawezaje kusaidia hivi vilabu ambavyo vinasuasua havina hata shilingi ya kuendesha huu mpira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tunampongeza sana Azam kwa udhamini mkubwa wa mwakani ambaao ameufanya, lakini si tu mwakani, Azam hata mwaka huu, mwaka jana, mwaka juzi walau chochote ameweka kwenye mpira huu wa miguu na tayari ameanza kwenye michezo mingine kama ngumi, *netball* na michezo mingine. Tunampongeza sana huyu mwekezaji, mwekezaji

mzawa tunaomba aendelee kufanya hivi kwa sababu ndio njia pekee ya kuinua soka la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimuombe Mheshimiwa Waziri kuna mdhamini mwengine anaitwa Vodacom ambayo ligi inayokwisha sasa ambayo bado mechi tatu, nne kuisha. mdhamini huyu ndio mdhamini mkuu kwenye ligi ya Vodacom. Nasikitika kukujulisha mpaka sasa hajawahi kuweka hata shilingi 10 pamoja na udhamini huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila vilabu vinapouliza jambo hili limekuwa likipigwa chenga. Mheshimiwa Waziri ingilia kati, saidia hivi vilabu vipate haki yao hata kama anaacha, lakini haki ya vilabu vimepatikana ili waendelee na mpira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, najua hili linaweza likachelewa sana kueleweka lakini ndio ukweli, tukizungumza siasa ya mpira katika nchi hii tunazungumza siasa ya Simba na Yanga, lakini Simba na Yanga hawana msaada wowote kwenye kuunda timu ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuisubiri matokeo ya timu ya Taifa ifanye vizuri halafu akili zetu na nguvu zetu zote tumeelekeza kwenye Simba na Yanga. Simba na Yanga hapa wote tunajua ina nguvu kubwa, ina *political mileage* kila mtu anashabikia na wengine tuko humu tunashabikia ni sawa kabisa. Lakini tusiulize kwa nini timu yetu ya Taifa haifanyi vizuri, ni kwa sababu akili zetu na nguvu zetu zote tumeelekeza kwenye Simba na Yanga, tumesahau vilabu vidogo ambavyo ndivyo vyenye mchango kwenye timu yetu ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikutolee mfano mmoja, ukiongelea habari ya Simba, juzi Simba wamecheza robo fainali ya Kombe la Afrika tunawapongeza sana. Lakini nikutolee mfano mmoja kule, *lineup* ya Simba wachezaji watatu tu ndio Watanzania golikipa, namba mbili na namba tatu basi. Namba nne Mkenya, namba tano Ghana, namba sita Mganda, namba saba Mozambique, namba nane

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Zambia, namba tisa Congo, namba 10 Zambia, 11 Rwanda. Huwezi kupata timu ya Taifa kama wachezaji wa Simba na Yanga wote *lineup* wanatoka nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule Yanga, mara sijui Tusiletusinde, mara Tunombetunombe, mara Mandama, sijui vitu gani. (*Kicheko*)

Nataka nikuambie tunajenga Simba na Yanga kwa nguvu kubwa lakini hatujengi timu ya Taifa kwa sababu tunapoita wachezaji wa timu ya Taifa hatuwaiti wale kwa sababu wanatoka nje ya Taifa letu. (*Makofi*)

Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri kama kweli tunataka tujenge msingi wa mpira katika nchi hii, haya mambo ya Simba na Yanga tungeweka baadaye ikawa ni *second option*. Kipaumbele ikawa ni wachezaji wetu wa kitanzania wazawa, ambao tunaweza tukawatumia kwenye timu yetu ya Taifa na wakaleta tija kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kwenye Taifa letu kila mtu ni Simba ama ni Yanga; anayejua mpira yuko Simba ama Yanga. Simba Yanga, Simba Yanga, Simba Yanga *nonsense*, hatuvezi kila saa hapa tunaongelea mambo ya Simba Yanga, Simba Yanga, *which is Simba and Yanga*. Kama tunazungumza habari ya maendeleo ya mpira ya miguu kwenye Taifa letu, Simba na Yanga ziwe *second option*.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, tuunde wachezaji wetu wa kizawa wanaoweza kuleta tija kwenye Taifa letu, tofauti na hapo tukiendelea kupiga hizi *story* tutapoteza muda na hakuna tutakachopata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii na mimi niishie hapo hapo alipoishia mzungumzaji wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na timu ya Taifa madhubuti tukiziweka akili zetu kwa kutegemea kwamba Simba na Yanga ndio zitakazofanya timu ya Taifa iwe bora tutakuwa tumechelewa sana. Taifa lolote duniani linawekeza katika sera na katika michezo Taifa lenyewe na Taifa kama Senegal, Mali na mengine yote yaliyoko katika ukanda wa Magharibi yamewekeza katika tasnia ya ufundi, lakini pia yakawekeza katika *academy*. Hili ndilo jukumu la msingi la Serikali, lakini hatuwezi tukaviachia vilabu jukumu la kuendesha timu ya Taifa hiyo haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema wakati Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita anahutubia Bunge lako Tukufu alieleza wazi hapa kwamba sasa ataanza kutenga fedha kwa ajili ya kuziwezesha timu zetu za Taifa. Huku ndio tunakopaswa kuelekea, hatupaswi kuelekea kuzisubiri Simba na Yanga kwamba ndio zitakuja kututengenezea timu ya Taifa, ni lazima uwekezaji ufanyike kwa maana kwamba tuandae wakufunzi waende wakapate mafunzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuandae uwezeshaji wa kisera wa kuwezesha *academy* ziweze kufanya kazi, lakini pia na uwekezaji katika tasnia nzima ya michezo uweze kuwa wenyewe kueleweka kama ambavyo kwenye Klabu ya Simba sasa hivi tunaanza kuona matunda ya uwekezaji wetu baada ya miaka minne ya mwekezaji wetu Mohamed Dewji - Mo, ambaye sasa anatupeleka katika hatua ya *champions league* katika kipindi cha misimu mitatu, mara mbili tumefika hatua ya robo fainali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka kuchangia eneo lingine ambalo limezua mjadala kidogo katika Bunge lako Tukufu. Nataka niseme katika historia ya mpira wetu tangu mwaka 1961 ambapo Taifa hili limepata uhuru, huko nyuma hatukuwahi kuwa na wachezaji wa kigeni hebu tujiulize

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ukiondoa mwaka 1980 ambao tumekwenda *AFCON*, ni wakati gani mwagine tumewahi kufika hatua hizo wakati huo hatukuwa na wachezaji hawa wa Kimataifa. Isije ikawa watu wanapaliwa na hili biriani ambalo Simba inacheza ndio wanaanza kuleta hoja nyepesi nyepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba mpira ni uwekezaji kuna mtu pale ataweka bilioni 20 kuwekeza ni lazima aoneshe mchezo wake katika uwanda mzima wa kibashara. Kwa hiyo, hili jambo tuliweke katika mawanda hayo.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hassan.

### **TAARIFA**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayeongelea kuhusiana na wachezaji wa kigeni. Wachezaji wa kigeni sio tu wanaleta ubora wa ligi yetu ya Tanzania bali wanaongeza kipato cha nchi. Mfano, mchezaji mmoja ambaye ni wa nchi za *SADC* ili uweze kumsajili maana yake unahitaji kutumia dola 4,700 ambapo ni sawa na shilingi 11,128,880 huyo ni wa nchi za *SADC*. Mchezaji wa Afrika Mashariki ili uweze kumsajili mchezaji mmoja unatakiwa utumie dola 3,260 sawa na shilingi 7,621,880. Kwa hiyo, kwa timu moja ikiweza kusajili wachezaji wa nchi za *SADC* kumi maana yake Taifa linakwenda kupata kipato cha shilingi 111,880,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ikiweza kusajili wachezaji 10 wa Afrika Mashariki maana yake Taifa linakwenda kupata kipato cha shilingi 76,218,800. Kwa hiyo, wachezaji waruhusiwe kuja kwa wingi kutoka nje ya nchi ili Taifa liweze kupata kipato. Ahsante kwa taarifa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Zidadu ambaye ndiye Mwenyekiti wa timu ya Namungo, anaelewa hiki ninachokizungumza. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa taarifa hii pia nimuombe Mheshimiwa Zidadu, juzi wakati lile goli la Bernard Morrison linafungwa wanafunzi wa shule ya Nyangao walishangilia sana, tumeputa taarifa kwamba wale wanafunzi wana kesi kidogo kule kwa hiyo, wanafunzi wale wasamehewe. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni kuhusu *TFF*. *TFF* hii tutende hakilimefanya kazi kubwa sana, nadiriki kusema ukiondoa *TFF* ya Leonard Chila Tenga hii ndio inayofuata kwa kusimamia mpira. Sasa hivi timu zote *under 17*, *under 20*, timu za wanawake pamoja na ligi ya wanawake inachezwa hapa nchini ni kwa sababu ya *TFF* hii chini ya Karia pamoja na Wilfred Kidau wanafanya kazi nzuri sana. Huwezi ukafananisha na *FAT* ambayo ilikuwa na Mheshimiwa Mhata pale na hii *TFF* ya leo, wanafanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kakunda.

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Shangazi kwamba kwa mara ya kwanza tangu dunia iumbwe Tanzania imetoa mchezaji wa mpira wa miguu mwanamke kwenda kucheza mpira wa kulipwa nje ya nje. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na hiyo ndio kazi ambayo anaisimamia Wallace Karia pamoja na Wilfred Kidau.

Waheshimiwa Wabunge lazima tujikumbushe tunapokimbilia kwenye kanuni, haswa tukizingatia mchezo namba 208 ambao kuna watu wanajificha kwenye kanuni; kanuni hizi hizi katika msimu wa mwaka 2016 kuna timu moja illipa nauli kwa timu ya *Ndanda FC* itoke Mtwara jje icheze mechi ya mwisho uwanja wa Taifa Dar es Salaam. Wakati kanuni inataka kwamba mechi ikachezwe uwanja wa ugenini kule Ndanda wakati ule kanuni hazikuwepo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna timu moja imemsajili mchezaji wa timu ya Taifa Kelvin Yondani akiwa kwenye jezi ya timu ya Taifa kwenye hoteli ya TANSOMA pale gerezani kanuni zikiwepo. Kuna mchezaji anaitwa Mbuyu Twite amesajiliwa kwa kanuni hizo hizo kwa milango ya uani na Mheshimiwa Tarimba, yote hayo unayajua leo mbona tunamhukumu Karia kwa kuvunja kanuni? (*Makofii*)

### **TAARIFA**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tarimba Abbas.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba afute kauli yake kwa sababu mimi habari hizo sizitambui, ili zisiwepo katika *Hansard* tafadhalisana. (*Makofii/ Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Rashid Shangazi uzifute taarifa zinazomhusu Mheshimiwa, ama ufute jina la

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Abbas Tarimba kwa sababu yeye hizo taarifa unazosema hana taarifa nazo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi taarifa anazo na anafahamu kwamba wakati Mbonye Twite anasajiliwa yeye alikuwa wapi na ni mdau mkubwa sana wa michezo. (*Makofii*)

Sasa nilitaka tu niseme kwamba *TFF* kama kuna mapungufu ni mapungufu ya kibinadamu, lakini kazi inayofanyika pale ni kazi nzuri tunapaswa tuwapongeze. Hata hii hatua ya Simba na Namungo kufika hatua ya robo fainali hatuwezi tukazipongeza hizi vilabu bila kuitaja *TFF*, wala bila kugusa tasnia nzima ya michezo kwa namna ambavyo imeshiriki. (*Makofii*)

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge taarifa zimeshakuwa nydingi sana na muda wangu unakimbia taarifa hii itakuwa ya mwisho. Mheshimiwa Katani Katani.

## TAARIFA

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua wewe ni mtaalam wa sheria na kwenye sheria wanasema kutenda kosa ni kosa kurudia kosa ni uzoefu wa makosa. Sasa kilichofanywa na Klabu kubwa ni kuwanyoosha watu wasimamie sheria, nampa taarifa mzungumzaji. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa vizuri kwa sababu Bernard Morrison alisajiliwa na Yanga tarehe 17 Januari wakati dirisha la usajili limefungwa tarehe 15 Januari, amepita dirisha gani kusajiliwa ndio maana ilikuwa rahisi kutoka Yanga kwenda Simba. Kwa hiyo, mpokee

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

haya machungu wakati tunaendelea kuboresha, lakini ukweli ndio huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Pauline Gekul achangie ambaye yeche na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika Wizara yetu hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. (*Makofi*)

Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa nafasi ya upendeleo ya kutupa afya njema sisi Wabunge wa Bunge lako Tukufu ili kuendelea na majukumu yetu ya kulitumikia Taifa Mwenyezi Mungu tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini tena na kunitfea kuwa miongoni mwa wasaidizi katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuwa naomba nimuahidi Mheshimiwa Rais kwamba nimepokea kwa mikono miwili kazi hii na nitaifanya kwa moyo wangu wote kumsaidia Mheshimiwa Waziri na kuisaidia Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Niwashukuru wana Babati kwa jinsi ambavyo wameniamini kuwa Mbunge wao wa Jimbo kwa awamu ya pili. Niwashukuru sana na niwaahidi kwamba nitaendelea kuwa mtumishi mwema kwao na msikivu ili tuweze kufikia yale malengo ambayo tumejiwekea ya maendeleo katika jimbo letu. (*Makofi*)

Kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Innocent Bashungwa amekuwa akitupa ushirikiano katika Wizara yetu, lakini amekuwa akitupa

maelekezo mbalimbali ili kutusaidia kufikia malengo ya Wizara yetu pamoja na malengo yaliyoanishwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025; Mheshimiwa Waziri nakushukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za dhati pia kwa Katibu Mkuu pamoja na timu yetu ya Wizara, Dkt. Hassan Abbas, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ally Possi pamoja na watendaji wetu wa Wizara na wadau wa Wizara hii wamekuwa msaada kwetu, lakini wamekuwa wakitupa ushirikiano mkubwa sana. (*Makof*)

Niwashukuru wadau wote wa sekte hii tumekuwa tukishirikiana kwa karibu lakini pia niwashukuru viongozi wa dini ambao wamekuwa wakiendelea kuombea Taifa letu la Tanzania na kumuombea Mheshimiwa Rais wetu na Watanzania kwa ujumla; nchi yetu imeendelea kuwa salama na amani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru wale wote wenye mapenzi mema, familia yangu, nawashukuru wanangu nawaona hapo juu Irene pamoja na wenzako kwa maombi ambayo mmekuwa mkituombea mama yenu pamoja na Tanzania na tunawashukuru kwa maombi hayo yaendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Niwashukuru kwa namna ya pekee Wabunge wote wa Bunge hili waliochangia hoja ya Mheshimiwa Waziri kaka yangu Bashungwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maoni mazuri ya Kamati ya Bunge lakini Wabunge walioongea humu ndani ni Wabunge 25, walioandikia kwa maandishi ni Wabungu wanne, jumla Wabunge 29 wameweza kuchangia hoja hii iliyoko mezani. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Wabunge hawa sisi tumepokea kama Wizara na imekuwa michango ya afya sana kwetu kwa ajili ya kazi hii ambayo ipo mbele yetu. (*Makof*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara inayogusa ajira za watu, ni Wizara inayogusa hisia za watu, ni Wizara inayoelimisha lakini ni Wizara inayohabarisha Watanzania. Bila vyombo vya habari maana yake taifa letu tunakuwa kwenye giza. Wizara hii imekuwa ikihabarisha inafanya kazi kubwa ya kuunganisha Watanzania. Lakini Wizara hii kupitia michezo ni Wizara ambayo imekuwa ikisaidia Watanzania kujenga afya zetu lakini kuisaidia pia na Wizara zingine na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na afya njema na hata itasaidia pia kupunguza matumizi kwa upande wa Wizara ya Afya kwa bajeti ya dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukuhakikishie kwamba maoni yao yote tumepokea na tutaendelea kuzingatia na kwa sababu ya muda kwa kuwa nina dakika 10 naomba nizungumzie hoja kadhaa ambazo zimebekwa mezani na nianze kuhusu hoja hii ya kukuza michezo katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge wamezungumza suala zima la kuhakikisha suala la michezo linapewa kipaumbele. Tunashukuru mnafahamu kazi kubwa inayofanywa na *academy* mbalimbali kwa ajili ya kukuza vipaji. Sisi kama Wizara tunaona kwamba hili ni la msingi na ndio maana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge Wizara yetu ikishirikiana na Wizara ya Elimu, Wizara ya TAMISEMI, tuliunda Kamati Maalum ambayo pia itapita huko kwenye ngazi za chini kuboresha michezo katika Halmashauri zetu na katika shule zetu za sekondari na za msingi ili vipaji vya Watanzania hawa ambao wanahitaji michezo hii vikuzwe kwa kuwapatia walimu bora, lakini pia mazingira mazuri ya viwanja pamoja na miundombinu ipatikane kwenye ngazi za chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuwahakikishieni kazi hii ambayo mmtupa na maoni ambayo mmetupa kuhakikisha michezo tunaboresha kuanzia ngazi za chini tumeshaanza kufanyia kazi na Kamati hii karibuni inakamilisha pia kupitia *combinations* mbalimbali ambazo zinafundishwa kwa shule za *form five* na *form six* kuhakikisha kwamba watoto wetu hawa ambao wanatoka

huku chini, lakini wanafikia kidato cha tano na cha sita waweze pia kusoma masomo ya michezo ambayo tunaishukuru Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu wameshafikia hitimisho kuhusu hili na kuanzia mwakani sasa udahili utafanyika ili hao watoto wetu waweze ku-*specialized* katika masomo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili Chuo chetu cha Malya pia Waheshimiwa Wabunge katika bajeti hii tunakwenda kukiboresha. Ukiangalia kwenye bajeti yetu ya mwaka huu ambaa unaisha mwezi Juni tumetenga zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya Chuo chetu cha Malya na maana yake fedha hizo zitakwenda kule zitaboresha. Lakini kwenye bajeti hiyo ambayo leo tunaomba ridhaa Waheshimiwa Wabunge kwenu Serikali kupitia Wizara hii tumetenga fedha shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya Chuo chetu cha Malya. Maana yake hao watoto wakianzia huku chini watakapofika kwenye chuo hiki na masomo ya juu wanakuwa wamebobea katika masuala ya michezo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuhakikishieni kazi hii tunaendelea kuifanya vizuri na kusimamia pia michezo kwa wanawake. Tunaomba mtuamini na hilli tuendelee kulifanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu vijana wetu kupata mafunzo kule walipo, tumeshauri sana kuhusu taasisi yetu ya *TaSuBa*. Tumeshauri pia ndani ya Serikali tuendelee kushauriana na TAMISEMI, Wizara ya Elimu pia kuhakikisha mafunzo ya vijana wetu ya usanii yanapatikana kwa Wilaya zetu kupitia *VETA*, tunategemea kuanzisha ushirikiano pia na *VETA* ili vijana wetu wapate mafunzo hayo katika wilaya zao ambako *VETA* zipo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa hili pia itasaidia sana vijana wakipata elimu hawatakuwa wanafungiwa fungiwa maana tumeona pia sio kuwafungia fungia tu ndio kazi yetu, lazima tuhakikishe pia vijana wetu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wanapata elimu. Kwa hili tupeane ushirikiano na mambo yatakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka niende kwenye suala la *TBC*. Tunashukuru maoni yenu Waheshimiwa Wabunge kwa upande wa kuboresha *TBC*, lakini pia Wizara yetu inaishukuru Wizara ya Fedha kutupatia fedha za *TBC* zilitolewa zote kwa ajili ya kuimarisha usikivu katika maeneo mbalimbali ambako usikivu haujafika, ni *TBC Television* pamoja na radio zake. Nikuhakikishie kwamba Wizara yetu itaendelea kufanya kazi hii na katika bajeti hii pia tunaomba shilingi bilioni tano na tunahakikisha kwamba tutazimamia kwamba fedha hizi zifike kwenye mikoa na wilaya ambazo kwa kweli usikivu bado haujafika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwenye hotuba yetu mmeona kwamba ni maeneo mbalimbali kama Kasulu, Tanga, Ngorongoro, Kahama, Bunda, Karagwe na maeneo mbalimbali usikivu bado tu. Tuwahakikishieni mpaka sasa tumeshafika Wilaya 102 lakini lengo letu ni kufikia Wilaya 119 kati ya 161 kupitia hizi shilingi bilioni tano ambazo mtatupatia Waheshimiwa Wabunge tuwahakikishie tutazimamia na usikivu utapatika kupitia radio *television*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini jingine ni suala la madeni ya *TBC*; Waheshimiwa Wabunge wameshauri kwamba *TBC* madeni yao yalipwe. Nikuhakikishie *TBC* wameshaanza kulipwa madeni yao *1.8 billions* zimeshaanza kuingia na Wizara imeshawaandikia wale ambao tunawadai na kazi inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la *TSN*. Tumekaa kwa karibu sana *TSN* kuangalia kwanza kwa nini makusanyo yao yameanza kushuka. Kuna suala la UVIKO 19 lakini kuna suala pia la mitambo chakavu. Waheshimiwa Wabunge mmelizungumzia hili ndugu zangu, sisi Wizara yetu pamoja na Wizara ya Fedha tunashukuru fedha hizi ambazo *TSN* ilikuwa inadai zimeanza kulipwa na mmeshauri mtambo ununuliwe. Hili tumeshaanza kulifanya kazi kwenye zile shilingi milioni 495 ambazo zimeshaingizwa kutoka Hazina

tumeshaelekeza mchakato uanze wa ununuzi wa mtambo huu ili *TSN*sasa waweze kuchapisha magazeti ambayo yana ubora na yaweze kufika kwenye maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mtambo utakaponunuliwa maana yake magazeti haya sasa yatakuwa na ubora, lakini pia yatafikia Watanzania kwa wakati. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuwatoe wasiwasi, uhakiki wa madeni unaendelea lakini pia kupitia Wizara ya Fedha, tuishukuru Wizara ya Fedha wamehakiki madeni ya *TSN*na wameendelea kufuatilia na ndio maana walipohakiki walihamua kutupatia kiasi fulani. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi hii inaendele na *TSN* watanunua mtambo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa kabla hoja haijaja kuhitimishwa hapa na Mheshimiwa Waziri nitoe ufanuzi wa jambo moja.

Waheshimiwa Wabunge, wakati mkitoa michango mbalimbali kuhusu timu zetu zinazotuwakilisha kimataifa kwa maana ya Simba na Namungo, wako Waheshimiwa Wabunge wanafikiru ukisikiliza michango yao wanafikiru timu ya Namungo ni timu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Timu ya Namungo siyo ya Waziri Mkuu na siyo Waziri Mkuu ambaye anaiendesha hiyo timu kifedha au kwa namna yoyote ile. Basi kama kuna mchango anatoa anatoa tu kama Mbunge mwingine ambaye kwenye jimbo lake kunaweza kukawa na timu. Lakini timu ya Namungo siyo timu ya Waziri Mkuu wala siyo yeye anaiendesha hiyo timu na kama mlivyosikia kiongozi wa timu yupo humu ndani Mwenyekiti wa timu ya Namungo. Mwenyewe ameshainuka kabisa kabla sijamuita, Mheshimiwa Hassan Ziddu Kungu huyu ni Mbunge wa Tunduru. Huyu ndiyo Mwenyekiti wa Timu na ni

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mwenyekiti wa hiyo timu ambayo kimsingi inamilikiwa na wachimbaji wa Namungo. (*Makofi*)

Sasa hao wachimbaji imetokea wapo jimboni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa hilo lazima tutenganishe maana Mheshimiwa Waziri Mkuu timu zote zake na hata mimi kule kwangu zipo timu nyingi tu nilitaka nimpelekee Mheshimiwa Waziri Mkuu maombi sasa kumbe hata ya kwake ina wadau wengine.

Kwa hiyo ni vizuri Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri, timu ya Namungo inagharimiwa na *Sports Pesa* na nadhani Mheshimiwa Tarimba hapo anafahamu hivyo lakini pia *Vodacom* na *GSM* ambayo mara nyingi huwa anatajwa sana kwenye Yanga, lakini hata Namungo pia anawasaidia *GSM* na pia Benki yetu ya *CRDB*. (*Makofi*)

Kwa hiyo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge kuyaelewa mambo haya. Kwa mukhtadha huo Taarifa zetu Rasmi za Bunge ili zikae vizuri michango iliyokuwa inaashiria timu hii ni ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani kuna Mbunge mmoja/kama wawili waliozungumza kwa namna hiyo mtaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge ili taarifa zetu zikae vizuri mtu asije kusoma miaka kadhaa hiyo ijayo huko mbele ikaonekana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa ana timu. Labda anaweze anaweza akatengeneza timu lakini ni wazi timu ya Namungo siyo ya kwake. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Innocent Lugh Bashungwa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aje ahitimishe hoja yake. (*Makofi*)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nguvu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuhitimisha hoja ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Pia nitumie nafasi hii kukushukuru wewe, Naibu Spika wetu na Mbunge wa Mbeya Mjini, juzi nilikuwa Mbeya kwa kweli nilifurahi kuona kauli chanya za Wana Mbeya Mjini wengi kukupongeza kwa kazi nzuri unayofanya. Hongera sana Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, mama mahiri, mchapakazi tunampongeza kwa kazi nzuri anayoifanya kuiongoza nchi yetu. (*Makofi*)

Nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango kwa kazi nzuri anayoifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutimiza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa kwa miongozo na maelekezo anayotupatia Mawaziri katika kutimiza majukumu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kauli, kwa maandishi na kwa *support* kwa ujumla Bunge zima toka asubuhi kwa kweli imekuwa ni furaha tupu. Waheshimiwa Wabunge tunawapongeza kwa *ku-support* michezo, sanaa, utamaduni na habari toka asubuhi yaani muda ungekuwa unatosha kwa kweli michango tungepata mingi sana kwahiyoo tunawashukuru wale 29 ambao mmechangia hoja yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Nyongo na Makamu Mheshimiwa Kamamba na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa maoni na ushauri ambao mmekuwa mkitupatia. Na niwaahidi Wizara yangu kwa maoni na ushauri ambao mmetupatia tutauekeleza kwa asilimia 100. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa njibu hoja zilizotolewa kutoka kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge na nianze kwa kumshukuru Naibu Waziri Mhehimiwa Pauline Gekul kwa ufanuzi mzuri wa hoja za Wabunge. Na nianze kwenye Tasnia ya Habari; kumekuwa na hoja kwamba Serikali tusaidie wanahabari kwenye stahiki zao na hoja hii ilichangiwa na Wabunge kadhaa, Mheshimiwa Bulaya pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ningependa kuwaondolea wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, Serikali ndio maana kwenye Sheria Na. 12 ya mwaka 2016 ukiangalia moja ya malengo ya sheria ile ni kuhakikisha stahiki na maslahi ya wanahabari yanazingaitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachowea kuwahakikisha pamoja na Wabunge sheria ile imeelekeza kuanzisha Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Wanahabari na vyombo hivi viwili moja ya majukumu ni kuhakikisha vinasimamia maslahi ya wanahabari. Na sisi Serikali kwa vile tunajali maslahi na stahiki za wanahabari tutahakikisha tunatumia sheria hii kuhakikisha mambo mazuri kwa mfano, bima kwa wanahabari, mambo ya pensheni na mazingira bora ya kazi yanazingatiwa kwa wamiliki wa vyombo vya habari kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, ningependa kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanahabari kote nchini Serikali tupo pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja pia kwamba Serikali hufungia vyombo vya habari ambavyo vinafanya kazi za kiuchunguzi. Sheria Na. 12 ya mwaka 2016 kifungu 52(2) kinasema kwamba si kosa kuikosoa Serikali. Kwa hiyo, Serikali haijawai kufungia chombo chochote cha habari eti kwa vile kinafanya kazi za kiuchunguzi. Kwa vile magazeti ambayo yalifungiwa yalikuwa ni mambo ya kimaadili na uvunjifu wa Sheria ya Habari, lakini sio kwamba wanafanya kazi ya kiuchunguzi, hiyo si kweli.

Kwa hiyo, pamoja na Waheshimiwa Wabunge nitoe wito kwa wanahabari na wadau wote wa tasnia ya habari waendelee kufuata Sheria na Maadili ya Habari na Utangazaji. Nia ya Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ili kazi

zao ziweze kufanyika vizuri, lakini lengo la Serikali siyo kufungia vyombo vya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye upande wa michezo; na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kuipongeza Azam kwa mkataba ambao walisaini na *TFF* kwa kweli mkataba huu utaleta mchango na mageuzi makubwa katika maendeleo ya sekta ya soka nchini. Lakini Azam tumewaona wakisaidia pia tasnia ya ngumi kwa hiyo nitoe wito kwa wadau wengine wafanye kama Azam ili tushirikiane pamoja na Serikali kuhakikisha tunaendeleza michezo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la utawala bora katika michezo na Waheshimiwa Wabunge sana sana wamejikita katika kuelezea changamoto zillizopo za utawala bora upande wa soka hasa hasa *TFF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba kwa utaratibu wa *FIFA*, Serikali inatakiwa iwe *eyes on, hands off* katika masuala ya michezo. Lakini pia Serikali tunatambua kwamba hata *FIFA* inashirikiana na Serikali kote inakofanya kazi katika kusimamia masuala ya michezo.

Kwa hiyo, kwenye suala la utawala bora Serikali tuko *serious*, zipo sheria za nchi ambazo zinasimamia masuala ya utawala bora na katika hili Waheshimiwa Wabunge, Wizara imepokea malalamiko, kwa hiyo, nikiri kwamba malalamiko haya na sisi tumeyapokea na tayari nimeelekeza Baraza la Michezo Tanzania kufanyia chambuzi malalamiko haya ili tuweze kuyafanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwenye suala la utawala bora Serikali tuko *serious*, tutahakikisha sheria na taratibu za nchi zinasimamiwa. Kwa hiyo, ningependa kutoa wito na nilishatoa wito huu kwa *TFF* waendelee kuzingatia misingi ya utawala bora hapa nchini katika suala zima la maendeleo ya soka.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna suala la rushwa. Kwamba, TAKUKURU ilikuwa inachunguza jambo ambalo limechukua muda mrefu. Nimefuatilia jambo hili na kwa vile bado liko kwenye uchunguzi basi niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa TAKUKURU italitolea ufanuzi wake pale uchunguzi utakapokuwa umekamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge ningependa kuzungumzia changamoto ambazo zimetajwa kwenye maendeleo ya michezo nchini kwa kutumia mfano wa *pyramid*. *Pyramid* ukiiangalia upande wa chini inakuwa ni pana halafu kadri unavyopanda inakuwa ni nyembamba. Sasa kwenye maendeleo ya michezo nchini kwenye hotuba yangu nimesema kuna mpango mkakati wa maendeleo ya michezo ambaao tunauzindua Julai, 2021 yaani mwezi wa saba na katika mkakati huu Waheshimiwa Wabunge, kwenye hotuba yangu nimesema *sports for all*, kwamba lazima tuhakikishe shule za misingi na sekondari watoto wote wawe kwenye shule za msingi za umma au binafsi, shule za msingi na sekondari wanapata fursa ya kucheza michezo shulenii kama wanavyopata fursa ya kusoma masomo mengine. Jambo hili tayari tumeshashirikiana na Wizara ya Elimu, namshukuru Mheshimiwa Profesa Ndlichako pamoja na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Jafo kipindi kile, lakini hata Mheshimiwa Ummy tumeendelea kushirikiana katika jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeunda utatu wa kushirikiana kuhakikisha masuala ya UMITASHUMTA na UMISETA tunajipanga upya kuanzia mwaka huu na ndio maana Waheshimiwa Wabunge mtaangalia mkakati wa UMITASHUMTA na UMISETA wa mwaka huu uko tofauti na miaka iliyopita. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 8 Juni ataenda kutufungulia mashindano kule Mtwara. Lakini kuanzia mwaka huu kwenda miaka inayokuja Waheshimiwa Wabunge mtaona tofauti kubwa. Tumejipanga kuhakikisha kuititia UMITASHUMTA na UMISETA watoto wetu wanapewa mazingira mazuri ya kufanya michezo lakini pia tunashirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha watoto wanaofanya vizuri kuititia michezo hii basi tunawaendeza badala ya kuacha

UMITASHUMTA na UMISETA imeisha basi wanapotea mpaka mwaka unaofuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia miaka ya nyuma watoto walikuwa wanacheza unakuta wiki moja kabla ya UMITASHUMTA na UMISETA ndipo wanaandalishi kwenda kushiriki kwenye michezo. Safari hii kuititia TAMISEMI tayari maelekezo yameshatolewa kwenye shule za msingi na sekondari kote kwamba somo la michezo ni somo muhimu kama masomo mengine. Kwa hiyo, tutaendelea kusimamia hili ili kuendelea kutengeneza vipaji kwa watoto wetu kuanzia shule za msingi na sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, sambamba na hili tuanshirikiana na TAMISEMI kubainisha shule ambazo zitakuwa ni shule maalum za michezo kwenye shule za msingi kila mkoa na sekondari. Zoezi hill tumekubaliana likamiliike kufika mwezi huu mwishoni ili kwenye mipango ya Serikali ya miaka ya fedha inayokuja, basi fedha iwe inatengwa tunahakikisha shule hizi maalum zinapata vile vifaa vyta lazima ili watoto wanaofanya vizuri wenyi vipaji wanaenda kwenye hizi shule maalum sambamba na *combination* ambazo zitakuwa zinatolewa *form five* na *six* ili kuandaa walimu wa michezo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kutumia hii *pyramid approach* vipaji tutakavyoinua kuititia shule za msingi na sekondari katikati ya *pyramid* kuna upande wa sekta binafsi pia kushiriki kwa kujenga *academies* na tumeona *academies* mbalimbali hapa nchini. Tunaipongeza Serikali na kuwaunga mkono wawekezaji hawa na tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha suala la kuibua vipaji kutoka kwenye shule za msingi na sekondari basi hapa tunakuwa tuna *sports academies*nyingi na sisi Serikali ili kuonesha mfano tumetenga shilingi bilioni 1.3 kwenda kwenye Chuo cha Malya ili kuwe kuna *sports academy*, wale wanachuo wanaojifunza michezo wajifunze kwa vitendo huku wakifundisha kwenye shule hii ambayo itakuwa inaendeshwa na Serikali. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo kwenye *pyramid* mwisho inakuwa nalo hapo ndiyo unakuta vilabu kama Simba, Yanga, Namungo, Ihefu na vilabu vingine. Lakini hapo ndipo tunaenda kwenye *professional sports* yaani wachezaji wa ndani kwenye vilabu, lakini na wachezaji wa nje. Tukitumia *approach* hiyo mimi sina shaka kwa namna Serikali ambavyo tumejipanga tutafanya vizuri na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri ambayo itatupa muelekeo na kusaidia kuboresha haya niliyoyataja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo mapitio ya sera, sheria na kanuni ili kuhakikisha mkakati huu tunaenda vizuri na unakuwa na matokeo ambayo mmetushauri. Katika hili mimi namshukuru Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, ametuelekeza kwamba pamoja na mikakati yote hii angependa kuona wanawake katika michezo nao wanafanya vizuri. Haiwezekani tukawa tuna mama mahiri, shupavu Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, nina Naibu Waziri mwanamke, halafu timu za wanawake zinafanya vibaya. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nawahakikishia kwenye hili tutahakikisha michezo inaenda sawia wanaume na wanawake na timu za wanawake zinafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, hoja ya viwanja vya CCM ni kwamba Wizara yangu imeratibu jambo hili; Azam, *TFF* na Chama cha Mapinduzi wako katika maongezi ya kuangalia namna ya kushirikiana ili kuendesha viwanja vya Chama cha Mapinduzi nichini. Katika hili niwaelekeze *TFF*, sauti ya Wabunge ni sauti ya wengi, katika fedha ambazo wanazipata kutoka *FIFA* pamoja na vyanzo vingine hebu tuanze kuangalia na kuweka nyasi bandia kwenye viwanja ambavyo viko kwenye mikoa mbalimbali. (*Makofii*)

Kwa hiyo, *TFF* kwenye hili najua mnajenga uwanja wa kisasa pale Kigamboni na Tanga lakini kwenye vipaumbele kuanzia mwaka huu ambaeo na mimi naomba nипитишиве

fungu basi *TFF* tuanze kushirikiana kuhakikisha nyasi bandia kwenye viwanja mbalimbali mikoani basi tunashirikiana katika kuvijenga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni suala la wachezaji wa kigeni *vs local content* kwa maana ya kukuza vipaji ndani ya nchi ni suala ambalo lina mjadala na lina pande mbili. Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, mwaka jana mlituelekeza tushirikishe wadau ili tuweze kulipatia mwelekeo. Baada ya kuwashirikisha wadau, mwongozo unasema *maximum* ya wachezaji wa ndani kwenye klabu ni wachezaji wasiozidi kumi.

Kwa hiyo, kama kutakuwa na ushauri na maboresho katika hili sisi tuko tayari kupokea ushauri wenu ili tuone namna ya kulipeleka lakini nia hapa ni *ku-balance import substitution* ni jambo zuri ili tuweze kutengeneza vipaji vya hapa ndani. Lakini hiyo isiweze kuathiri malengo ya vilabu katika kutafuta wachezaji wazuri. Katika hili nipende kusisitiza na kuelekeza wale wanaoleta wachezaji kutoka nje basi leteni wachezaji ambao wana-profile ambazo zinaeleweka na zitaleta mageuzi katika kufundisha vijana wetu ambao wanacheza hapa ndani. Ipo kasumba unakuta mchezaji ametoka nje lakini akija anacheza, anazidiwa na wachezaji wa ndani. Sasa hiyo inakuwa na maana gani? (*Makof*)

Kwa hiyo, ningependa kuwasisitiza vilabu pamoja na wadau wa mchezo wa soka tuangalie *profile* za wachezaji tunaowaleta ili watakapokuja kweli waweze kutoa chachu kwa wachezaji wetu wa ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna hoja ya uwanja wa michezo hapa Dodoma ambao uliahidiwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliuliza Mheshimiwa Mavunde. Ningependa kumhakikishia kwenye hili tuko katika hatua nzuri. Eneo la kujenga tumeshalibainisha na Serikali kuititia Wizara ya Fedha maana mkakati wa Serikali ni kuititia mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwenye *corporate social responsibility* hapo ndipo tutapata fedha za kujenga

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

uwanje huu. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali iko pale pale na jambo hili tutalisimamia katika utekelezaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna suala la Muungano. Ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge michezo inatuunganisha, ni sehemu ya fursa ya kujenga Muungano wetu. Kwa hiyo, changamoto zilizopo *TFF* na *ZFF* tutawaelekeza na kuwasihî waendelee kushirikiana kwa sababu michezo na sanaa ni maeneo ambayo yanatuunganisha vizuri sana katika Muungano. Kwa hiyo, mimi kama Waziri mwenye dhamana nitaendelea kuhakikisha kupitia michezo *ZFF* na *TFF* wanashirikiana katika kuleta mageuzi ya maendeleo na michezo Bara na Visiwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa Sanaa niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza mdogo wangu Naseeb Abdul *a.k.a* Diamond. Nami niendelee kutoa wito kwa Watanzania, katika hili tumuunge asilimia 100 ili kijana wetu ashinde. Hii ni heshima kwa nchi yetu, lakini katika hili pia niwapongeze vijana wetu waliopata tuzo za *AFRIMMA* ya mwaka 2021 alikuwepo Diamond, Nandy na Zuchu, na wenye tunawapongeza. (*Makofii*)

Katika hili niendelee kusisitiza iwe kwenye michezo, sanaa, timu au mtu anapoliwakilisha Taifa letu hebu turudi kuwa wamoja kama Watanzania tuweke ushabiki wetu pembeni. Kwa hiyo, hata hili la Diamond, najua kwenye muziki pia kuna ushabiki, kuna timu fulani na timu fulani. Ningependa kutoa wito kwa wadau na Watanzania kwenye hili tuungane na tumuunge mkono kijana huyu akifanikiwa kupata *award* ya *BET* inaleta *inspiration* na hamasa kubwa kwa vijana wengine wanaochipukia katika sanaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *sports and arts arena*; Serikali inachukua jambo hili kwa uzito sana Waheshimiwa Wabunge. Ningependa kuwatoa wasiwasi. Sasa hivi kwenye bajeti tumetenga shilingi milioni 20.9 yaani milioni 20 na laki tisa kwa ajili ya kumlipa mtaalam elekezi aweze ku-*design* mchoro na kusanifu ili tuweze kujua

gharama halisi ya kujenga hii *sports and arts arena*. Kwa hiyo, kwenye bajeti inayokuja ya mwaka unaokuja tutakuwa tumeshajua gharama halisi ni nini ili tuweze kuziombea fedha kwenye bajeti inayokuja. Kwa hiyo, kwenye mwaka huu tumetenga hela ya kumlipa *consultant* afanye usanifu halafu mwaka unaokuja tutaweza kujua gharama halisi ni kiasi fulani ili tuweze kuiombea fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la BASATA. Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili Wizara tuko na ninyi. Tunatambua hata kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi fursa ziko kubwa sana katika tashia ya sanaa kutengeneza ajira kwa vijana wetu. Lakini sambamba na hili, tutafanya kila linalowezekana kuweka mazingira wezeshe. Ndiyo maana nilielekeza kanuni ya 25 tu-*withdraw*, tushirikishe wadau tuweze kufanya maboresho, kwa sababu lengo la Serikali ni ku-*promote sector* itengeneze ajira na kuchangia Pato la Taifa, lakini tusifanye hilo kwa *cost* ya kudidimiza maadili. Kwa hiyo, hata kanuni tunayoandaa tunatafuta *balance* ya ku-*promote sector* kama llani ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza, lakini sambamba na hilo, maadili lazima tuyalinde. Katika hili tumeenda mbali, tupo tunaandaa mwongozo ambao tutashirikisha ma-*producer* na Idara za Muziki kwenye redio na tvili kila mmoja katika eneo lake ajue kwamba jambo hili tumekubaliana ni katazo kwa hiyo hata mimi ninawajibika kulisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninaamini tukifanya hivyo tutaondoa urasimu unaolalamikiwa lakini tutasaidiana katika kuhakikisha maadili hatuyadidimizi kwa gharama ya kuangalia tu ku-*promote sector*. Hakuna Taifa ambalo halina maadili, Taifa lolote linajivunia na utambulisho wake ni mila na desturi zake. Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwa wasanii wetu waendelee kuipa ushirikiano Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na tuangalie na tusaidiane kuhakikisha mwongozo tutakaoutoa wote tunashirikiana katika kuusimamia pamoja na Kanuni mpya ambayo niwahakikishie hatutachukua muda mrefu kuikamilisha ili iweze kuingia katika utekelezaji. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa kuna hoja pia kuhusu *COSOTA*, suala ya mirahaba. Nilivyoangalia kiasi ambacho *COSOTA* imekusanya nikaona ni kidogo sana, lakini pia nikaangalia *potential* ya kukusanya mirahaba kupitia *COSOTA* nikaona ni kubwa sana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tulichokifanya katika hili *TCRA* kwa teknolojia iliyopo muziki ukipigwa kwenye redio au *tv*, hata ukipigwa kwa sekunde 15 tunajua redio fulani imepiga muziki wa msanii fulani. Kwa hiyo, *TCRA* inashirikiana na *COSOTA* kutengeneza mfumo ambao tutautumia kuboresha mfumo wa ukusanyaji mirahaba kwa wasanii wetu. Mimi ningependa siku tunawaita wasanii, tunagawa bilioni kadhaa sio milioni 199 ambayo iko hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ningependa kuwaomba mtupe muda mpaka mwisho wa mwaka ili jithada hizi nillizotitaja tuziweke katika utekelezaji angalau tutakapoandaa tukio la kutoa mirahaba kwa wasanii, hata ukimkaribisha Mheshimiwa Rais au Makamu wa Rais au Waziri Mkuu aje kuzindua hilo tukio liwe linaendana na hadhi yake. Lakini huwezi ukamkaribisha Mheshimiwa Rais au Makamu wa Rais au Waziri Mkuu aje kugawa mrhaba wa milioni 190. Kwa kweli mimi kwa ninavyotazama fursa ya kukusanya mirabaha hii, najua mpaka kufika mwisho wa mwaka tutakuwa tumepiga hatua nzuri. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mtuamini katika hili na wasanii tutafanya vizuri. Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunatumia mifumo na teknolojia katika kuwasaidia wasanii kupata mirahaba na haki zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili ni suala la *aggregate* ambalo limetajwa; tunafanya mawasiliano na tunajadiliana na wasanii, Mheshimiwa Babu Tale, Mheshimiwa Mwana FA mmekuwa washauri wazuri katika hili. Tutaangalia namna bora ya kulipeleka hili ili liweze kuwasaidia wasanii wasinyonywe kama ilivyo hivi sasa. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini mimi kama nilivyosema hapo mwanzo, nikiri kwamba tumepokea na hoja zote tutaziwasilisha kwa maandishi na niwashukuru sana, hii Wizara ni Wizara ambayo kazi kubwa ni kuratibu. Kwa vile tunawasikia na mnatupa ushauri mzuri mimi niwahakikishie nitaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yangu ya Wizara ili kuratibu mawazo na ushauri mzuri ambaa Bunge hili tukufu mnatupatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, natoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YANJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa hivyo, tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu. (*Makofi*)

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 96 – WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI,  
SANA'A NA MICHEZO**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 4,960,535,000

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Fungu hili ndilo lenye mshahara wa Waziri na ninayo orodha ndefu kabisa hapa ya Wabunge wanaotaka ufanuzi wa mambo ya kisera kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kupatiwa ufanuzi wa kwa Serikali kuhusiana na viwanja vya michezo katika shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vyetu nchini kwa sababu shule nyingi hazina viwanja vya michezo. Tuna haja ya kutafuta vipaji vya watoto, lakini bila kuboresha viwanja vyetu nchini sidhani kama tutaweza kweli, kupata hivyo vipaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile michezo ni kiwanda kama viwanda vingine. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anipatie ufanuzi mkakati gani unafanyika kuhakikisha kwamba viwanja vya shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vyetu vinakuwa viwanja ambavyo vinaweza vikafanyiwa hata mashindano kwa sababu sasa hivi watoto wetu wanashindwa kucheza michezo? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa hoja yake ni hoja ambayo hata sisi Serikali tunakubaliana nae na kama nilivyosema kwenye maelezo yangu katika kuhitimisha hapo mbele, nilizungumzia utatu ambaao tumeunda kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Na katika utatu huo moja ya maelekezo ambayo tumeyatoa kwa Halmashsuri zote nchini kuitia kwa Waziri Mheshimiwa Ummy ni kwamba Wakurugenzi kote nchini wahakikishe shule zetu za msingi zinatenga maeneo na maeneo hayo yanalindwa dhidi ya uvamizi au kubadilishwa kwa matumizi yake, huo ni mkakati mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mwingine ni tumetoa mapendekezo kwa upande wa Wizara ya Fedha na Mipango namna ya kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ambao uko chini ya Baraza la Michezo Taifa, *Sports Betting* fedha ambayo inaenda Hazina asilimia fulani iende kwenye huo mfuko ili iweze kusaidia maendeleo ya timu za Taifa pamoja na kusaidia kujenga vipaji kwenye shule za msingi na sekondari. Sambamba na hilo ombi lingine ambalo tumepeleka Wizara ya Fedha ni kurudisha Bahati Nasibu ya Taifa ili asilimia 50 ziende kwenye kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo, lakini pia na Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sina shaka na kwa vile kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu yuko hapa ninaamini yuko analifanyia kazi na mbele ya safari huko kwenye *Finance Bill* pengine tunaweza tukapata kauli ya Serikali, lakini hiyo ndio mikakati ambayo iko ndani ya Serikali katika kuhakikisha tunaendeleza michezo nchini, hasa hasa kwenye ngazi za chini kwa shule za msingi na sekondari upande wa miundombinu.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ritta naona ameridhika.

Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hasa ukurasa wa 46 amezungumza kwamba Wizara yake pamoja na Wizara ya Fedha wanaangalia uwezekano kwamba michezo ya kubahatisha iweze kuchangia katika maendeleo ya michezo nchini.

Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi, je, haoni ni busara katika hayo majadiliano ama hayo mazungumzo kwamba badala ya kufikiria kutoza tozo jipya wachukue asilimia 50 ya kodi ambayo inakusanywa sasa hivi ya *Gamming Tax* ili kwenda moja kwa moja kugharamia michezo hiyo? Ahsante.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ufanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Sekta, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kwa majibu fasaha aliyo yatoa na kwa hotuba yake nzuri. Na niombe nimhakikishie Mheshimiwa Tarimba kwamba maadam bado tuko hatua za mwisho kabisa za kukamilisha migawanyiko ya hivi vyanzo, kipi kinaenda wapi, kitakuwa cha kiasi gani, aridhie tufikie hatua ya mwisho na ashike ahadi aliyotolewa na Waziri wa Sekta kwamba tutaitoa kauli wakati tunaleta hivyo vyanzo.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa sababu kwa utaratibu na michakato ya kawaida ya vyanzo vya mapato kwa hatua hii bado hatujafikia hatua ya kuweza kuvitangaza kipi ni kipi. Kwa hiyo, ye ye achukue tu kwamba tunalfanyia kazi hilo na tutakuja na kauli wakati wa hotuba ya Serikali na wakati wa *Finance Bill* tutakapokuwa tunabainisha vyanzo vipi vinaenda katika mfuko gani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba ameridhika. Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante.

Kwanza nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuwa na wazo kidogo kwenye lile suala langu la *sports arena*. Najua Serikali ina mkakati mzuri, lakini je, kwa nini Serikali isiweze kukubali na kushirikiana na sekta binafsi kwenye hilo suala?

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa sababu tunaamini kwamba, tykisema mwaka huu tuna shilingi milioni 28 tunasubiria mpaka mwakani. Bajeti ya mwakani hapa nahofia Mheshimiwa Bashungwa tutaanza kutafuta hata shilingi milioni 30 nyingine; tutamaliza miaka hii mitano hatujaacha *legacy* kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Uwanja wa Mkapa, tumeuita Benjamin Mkapa, na sisi tunahitaji kwamba tuwe na *Mama Samia Sports Arena* na inawezekana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utujibie kwenye hilo eneo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri uafanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale kwamba mawazo aliyopendekeza ni sehemu ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan katika *ku-promote* uwekezaji tunamaanisha hata sekta ya michezo, habari na sanaa. Kwa hiyo, hata katika hili Mheshimiwa Taletale nikushukuru kwa wazo hili na tumelichukua, ni wazo zuri, ipo mifumo mbalimbali, kuna mifumo ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kutumia fursa hii kutoa wito kwa wadau ye yote ambaye yuko tayari kukaa na Serikali tuangalie namna hii *consultancy* ya *design* ikikamilika na kiasi gani kinahitajika basi twende kwenye uwekezaji kupitia *modality* mbalimbali ikiwemo mfumo wa *PPP*. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya, nataka kuamini tunalo neno katika Kiswahili la *sports arena*. Mheshimiwa Almasi Maige sijui yuko kona gani.

Mheshimiwa Cosato David Chumi, eeh, Mheshimiwa Almasi naona amenyoosha hapo. Eeh, *sports arena* inaitwa nini Kiswahili?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Na hili ninaloliezea ikiwa Waziri hajanipa maelezo ya kutosha nitashika shilingi.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma dira ya Wizara na dhima ya Wizara, kwanza dira inasema kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri. Dhima pamoja na mengine kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Shirika la Magazeti ya Serikali (*TSN*) katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba magazeti yale yanashindwa kufika vijiji kwa wakati na pia shirika linashindwa kushindana kiteknolojia. Sasa katika ukurasa wa 14 pia amekiri kwamba jithada zinaendelea kupata mtambo na kwa sasa kwa jinsi mtambo ulivyo hata matangazo yanatoka hafifu na hivyo kulipunguzia shirika uwezekano wa kupata matangazo ya biashara na hivyo kuijendesha, lakini ile dhima sasa ya kuhabarisha Taifa kwa chombo hiki muhimu cha Serikali inashindwa kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba chombo hiki cha Serikali cha kupata habari kinakuwa madhubuti na kinafanya kazi kwa weledi? Nitashika shilingi nisipopata maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, Mheshimiwa Chumi hoja yake hii ni ya msingi sana na wakati natoa ufanuzi niliizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TSN* tunatambua kazi kubwa wanayoifanya kuhabarisha na kuelimisha Taifa, lakini sisi kama Wizara tumekaa na *TSN* kuona ni wapi wanakwama na ndio maana mionganoni mwa mahitaji yao ilikuwa pia ni vyombo vyaa usafiri. Mheshimiwa Chumi tukuhakikishie hata kwenye bajeti hii *TSN* tumewatengea zaidi ya shilingi milioni 300 kwa kuwasaidia katika masuala ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama hilo halitoshi Mheshimiwa Chumi, rafiki yangu na kaka yangu, nimeeleza

kuhusu uhakiki ambao unaendelea Wizara ya Fedha kuhakiki madeni ya *TSN*, lakini pia wameandikiwa taasisi ambazo wanadaiwa hayo madeni, lakini yale madeni yalipoanza kulipwa zaidi ya shilingi milioni 495 tumeelekeza kule sasa inunue ule mtambo ambao ulikuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu kusaidia *TSN* ifanye kazi yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Chumi tunakuomba usichukue shilingi hii, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Tukuhakikishie *TSN* watakwenda vizuri na mtambo huu utanunuliwa na pia madeni yake yatakapokuwa yamelipwa basi *TSN* itafanya kazi kwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba ukitupitishia fedha hizi na Waheshimiwa Wabunge, *TSN* itakwenda kuimarika. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Chumi bado umesimama.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TSN* madeni wanayodai asilimia kubwa ni kutoka Serikalini, zaidi ya shilingi bilioni 11, Mheshimiwa Waziri anasema wamewalipa shilingi milioni 400. Mtambo unaotakiwa kununuliwa ni shilingi bilioni 16, hebu tuangalie huo uwiano. Mimi narejesha shilingi, lakini sioni *seriousness*. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Sehemu ya pili huwa sio sehemu ya mchango, wewe unaeleza tu kama hoja yako unataka watu wakuunge mkono, unatoa hoja, watu wanakuunga mkono. Kama unarejesha shilingi basi unasema tu, mimi maelezo yaliyotolewa nimeridhika, si ndio Mheshimiwa?

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui nisemeje, lakini nahitaji *seriousness* ya Serikali. Naomba...

**MWENYEKITI:** Nadhani ndicho alichokisema Naibu Waziri kwamba wanaendelea kukusanya madeni. Kama unataka Bunge lijadili, hilo ni suala lingine, lakini sehemu ya pili ukisimama hautoi tena maelezo kwa kirefu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi wakusanye kwa speed. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana. Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwenye mchango wangu nilizungumzia suala la viwanja nchini na nikasema kwa wakati mmoja Serikali imeweza kupata faida, kwa maana imepata kodi ya shilingi bilioni 34 kutokana na mkataba ambao Azam wameingia na nikataja *statistics* kwamba, tukitumia bilioni sita tunaweza kuweka viwanja 20 *carpet* na shilingi bilioni tatu ni kama viwanja vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amenijibu kwamba, kuna majadiliano ambayo yanaendelea kat i ya watu watatu, kwa maana ya Serikali, CCM na huyo mwingine ambaye amemtaja, lakini haya yamekuwa yakizungumzwa siku nyingi, Mabunge yanaenda. Huyu mtu ambaye ana-*invest* ana *production* nzuri, lakini anachokifanya kuonesha anaonesha vumbi. Sisi hapa ni Wabunge tunafanya mazoezi pale, viwanja vile havina *carpet* hadi leo hii na viwanja ambavyo Mwalimu Nyerere alijenga kwa malengo ambayo Watanzania wavitumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kauli na *commitment* ya Serikali, watoe fedha ambazo *at least* hata shilingi bilioni tatu ili nyasi ziweze kutandikwa kwa sababu CCM ni baba, Serikali ni mtoto. Hawa watu wanaweza wakazungumza jambo moja na wakafikia makubaliano. Sisi Watanzania tusiendelee kuteseka. Kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali na nisiporidhika majibu nitatoa hoja ili watu wawezee kuchangia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Sanga ni mdau mzuri sana wa michezo na tunashukuru kwa

ushirikiano anaotupa katika kazi za maendeleo ya michezo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumuondoa wasiwasi Mheshimiwa Sanga, tumeshakaa mimi na yeze na mikakati ambayo inaendelea kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Fedha nilikudokeza kwamba tunajitahidi kila inavyowezekana, lakini pia lipo suala la maombi ya kuondoa VAT kwenye nyasi bandia na linaendana sambamba na hoja yako Mheshimiwa Sanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa na hili tuliweke kwenye kapu la Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwamba, tunaendelea kulijadili na kwa sababu Sheria ya Bajeti ina taratibu zake, basi muda utakapofika, pamoja na yale ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ame-*commit* kwamba yanafanyiwa kazi na hili pia lipo mionganoni mwa hayo mambo.

Kwa hiyo, ningependa nikuombe sana ndugu yangu Mheshimiwa Sanga unirudishie hiyo shilingi ili tuweze kusimamia mambo mengi ambayo unayasubiri katika utekelezaji wa shughuli za michezo nchini. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, naona umesimama?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu itabidi nikubaliane na kaka yangu, lakini nimwambie Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ana dhamana ya kutoa fedha ili soka linamda pamoja na Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Charles Muguta Kajenge.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nilikuwa na hoja moja kuhusiana na sekta ya michezo.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya changamoto kubwa inayorudisha nyuma maendeleo ya soka letu ni ukosefu wa fedha, hasa katika vilabu vyetu. Je, Serikali haioni haja ya kusaidia angalau vilabu ambavyo viko katika ligi kuu, fedha kila mwaka ili viweze kufanya maandalizi ya kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nishukuru swali la Mheshimiwa Charles, mzee wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba tumefuatilia na Vodacom na hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Mbunge, naamini alikuwa Mheshimiwa Mnyeti, Vodacom wameahidi wiki ijayo watatoa fedha kwenye vilabu ambavyo vimesubiri kwa muda mrefu malipo hayo. Kwa hiyo, katika hili suala la ukosefu wa fedha ligi kuu, ndio maana tumewapongeza Azam kwa ule mkataba ambao wamesaini na *TFF*, ni mkataba ambao utasaidia sana vilabu vyetu nchini kwenye suala la ukosefu wa fedha, moja ya *solution* ni mkataba huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kumuondolea wasiwasi Mheshimiwa Charles kwamba, Serikali kwa kushirikiana na wadau tunaendelea kulifanyia kazi, ili vilabu vyetu vusiwe vinapata changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya, naona amekaa ameridhika.  
Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hasa kwenye sehemu ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tunaelekea kwenye uchaguzi na nilikuwa nataka kupata kauli ya Serikali kwa maana ya Wizara imejipanga vipi, Wizara, BMT, TAKUKURU na wadau wote kuhakikisha kwamba chaguzi

iliyoko mbele yetu ya *TFF*inafanyika kwa haki, inaondoa uhuni, uzandiki, fitina na kuondoa rushwa ambayo husababisha baadhi ya wagombea kuondolewa kwa mazingira tatanishi. Serikali, Wizara na BMT pamoja na TAKUKURU wemjipanga vi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uchaguzi huu umepelekwa Kigoma na Serikali ina mkono mrefu. Je, mmejipangaje kudhibiti uhuni katika uchaguzi unaokwenda kufanyika mwezi wa saba? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Gulamali kuhusu jinsi ambavyo tumejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishie Bunge lako tukufu kwamba Wizara yetu kuitia BMT tuko karibu sana tukifua tililia masuala ambayo yanaendelea katika mashirikisho mbalimbali ya kimichezo. Na kwa mwaka huu *TFF*wanafanya uchaguzi, tunafahamu pia mashirikisho haya wana Katiba zao, sisi kama Serikali ni kuendelea kuona kwamba kama hizi Katiba zinatafuatwa, lakini pia wanachama wao wanaridhika na mchakato na mifumo inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pale tulipoona kwamba kuna ukiukwaji wowote unaojitokeza, Wizara yetu kuitia BMT tumekuwa tukiwashauri na tumehashauri pia kuna mashirikisho mengine ambayo walikuwa wamepanga, mfano uchaguzi ufanyakie Dodoma, lakini unasikia leo umehamishiwa Mtwara, kesho umehamishiwa sehemu nyininge. Tumeendelea kushauri utawala bora uzingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukuhakikishie tuko imara na nitoe rai kwa wanamichezo wote kote nchini kuitia mashirikisho yao kuhakikisha kwamba tunabaki kwenye Katiba zetu mwisho wa siku tuisiwakwaze Watanzania ambao ni wapenzi wa michezo hii, ahsante. (*Makof!*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba maelekezo ya Serikali na *commitment* yao; mara nyingi tumekuwa tukiandaa mechii, michezo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, lakini hatuoneshi *commitment* ya kuwasaidia wale wachezaji, tunaishia kuwapa bendera kwenye viwanja vya ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujuu Serikali inajiaandaa vipi kuhakikisha, ili ushinde uwe na matokeo chanya ni lazima uwekeze toka mwanzo. Tunajua kabisa kwamba tumemaliza lligi hili au tuna olyimpiki mwakani, lazima Serikali ifanye sasa. Ninaomba *commitment* kwa sababu, ninaona hata bajeti mliyopewa ni ndogo. Mnawezaje kufanya kazi ya kuwasaidia wachezaji na hii ni kwa wote, iwe mabondia na haujazungumzia kabisa habari za mabondia Mheshimiwa Waziri; iwe mabondia, iwe wanariadha, iwe michezo yoyote sijaona *commitment* ya Serikali. Ninaomba *comitemtent* ya Serikali, vinginevyo nitashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru naomba nitoe ufanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Sophia Mwakagenda rafiki yetu na mpenzi wa..., ahsante.

Mheshimiwa Sophia nikuhakikishe Wizara yetu imeshalionia hili ndio maana kwenye mwaka huu wa fedha uliokwisha tuna zaidi ya shilingi milioni 200 ku-support timu za Taifa ambazo zinafuzu kwenda kimataifa, nikupe mfano kwa *issue* ya riadha kuna timu yetu ipo kwenye kambi pale Arusha na ni juzi tu tumeona Afisa Michezo kutoka BMT ameenda pale amewakabidhi kiasi kadhaa cha fedha, lakini

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Sophia, dada yangu ndio maana katika bajeti yetu hii umeiona tumependekeza sasa kuwe na mfuko wa michezo ambao utasaidia timu zetu pia za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa kazi kubwa ya mfuko huu ni kuhakikisha kwamba kama tuna timu yoyote, mwanamichezo yejote wa michezo wowote amefuzu anayeiwakilisha nchi yetu asilalamike asisononeke moyoni mwake tumsaidie kama Serikali pamoja na wadau. Kwa hiyo tukuhakikishie hata hili la ngumi Mheshimiwa Sophia ukifuzu pia tutaku- *support. (Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi; mimi ningependa kupata maelezo kutoka kwa Waziri ambayo kwakweli yanasisitisha sana kuhusu Shirika letu la Habari - *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usikivu wa *TBC* ni asilimia 74 tu nchi nzima, kwa hiyo kama kuna tukio kubwa karibu asilimia 30 ya Watanzania hawasikii chochote kuhusu *TBC*. Sasa nilitaka nijue nini *commitment* ya Serikali na kwanini Waziri hii *issue* haikukeri, ni aibu miaka 61 baada ya Uhuru Shirika la Habari Tanzania alisikiki nchi nzima na kwanini mimi nikiwa mjumbe wa Kamati nina *declare interest* wametuambia *TBC* wanahitaji shilingi bilioni 10 tu wakipata hizo *TBC* inasikika nchi nzima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini *commitment* ya Serikali kuhusu hizo shilingi bilioni 10 ambazo *TBC* wanahitaji wapate ili nchi nzima Watanzania wenzetu wafaidike na Shirika la Habari Tanzania? Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ningependa kumuondoa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wasiwasi ndugu yangu, mwana *diaspora*, kaka yangu Mheshimiwa Mwenisongole kuhusu suala la usikivu wa *TBC* Serikali tunalichukua kwa uzito mkubwa sana na ndio maana ukiangalia *trend* ya fedha za maendeleo kwenda *TBC* kila mwaka imekuwa ikitoka shilingi bilioni tano ambazo zilikuwa zimetengwa kwenye mwaka wa fedha 2020/2021 zimeshatoka shilingi bilioni tano zote na tumeomba shilingi bilioni tano nyingine ambayo tunaomba mtupitishie ili suala la kuweka miundombinu ya *TBC* kwenye Wilaya ambazo hazijapata uendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hili Serikali tunawasiliza sana, kuna maelekezo walitupa Kamati kwenye fedha za maendeleo Malya shilingi milioni 300 ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Mwigulu leo ameniwekea kwenye akaunti shilingi milioni 300 kwa ajili ya Malya na *TaSuBa* shilingi milioni 250 Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ameweke leo kwenye akaunti; fedha za ukarabati uwanja wa Taifa shilingi milioni 638 Waziri wa Fedha ameniwekea leo kwenye akaunti. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhi Hassan na Serikali yake ya Awamu wa Sita kwenye *commitment tuki-commit* jambo tunatekeleza, kwa hiyo, ningependa kumuondoa wasiwasi hata hili suala la *TBC* zile *target* ambazo tumeziweka kila mwaka na kwamba kufika mwaka 2025 asilimia 100 ya nchi nzima watakuwa na usikivu mzuri, hilo tutalitekeleza, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza niseme kwamba nimevutiwa sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri nimpongeze, lakini sehemu ya mchango wangu kuhusiana na *COSOTA* na masuala ya makusanyo ya mirabaha alilijibbia upande wa makusanyo kwenye redio na akatuahidi kwamba wataanza kulipa mwezi Desemba, ni muda mrefu kidogo, lakini tutalichukua hilo. Lakini *COSOTA* haionekani kufanya kazi nzuri kwenye

makusanyo ya mirabaha kwenye maeneo ya wazi yanayotumia kazi za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku ndio ambako kwenye hesabu zetu kama kuna *units* nyingi na kuna fedha ya makusanyo makubwa zaidi yanayofanyika sasa mimi nataka *commitment* ya Serikali na kuona kwamba Mheshimiwa Waziri hili amewahi kulitupia macho kwa sababu hajaliongelea kabisa na kuona yeye kama mwakilishi wa Serikali kuruhusu watu binafsi kusaidia makusanyo haya na kuyagawanywa kwa wasanii wahusika. Nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ningependa kwanza kumshukuru Mheshimiwa Hamis Mwinjuma *a.k.a* Mwana FA katika hili mimi nikiri kwamba *concern* yake tumeipokea na kwa vile yeye ni mdau ambaye amekuwa akitupa ushirikiano wa karibu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kama tulivyofanya kukaa na BASATA na wadau wa sanaa kwenye suala la kanuni basi nikuahidi baada ya ninaamini Waheshimiwa Wabunge mkitupitishia bajeti hii jambo la la kwanza kabisa Mheshimiwa Mwana FA litakuwa ni kukaa na wewe pamoja na wadau tuangalie namna ya kushirikiana na *COSOTA* ili tuweze kuboresha mifumo ya ukusanyaji mirahaba. Kwa hiyo ninakuomba sana madogo wangu unirudishie shilingi ili tuweze kuendelea na kazi, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru katika mchango wangu nilizungumzia maslahi ya waandishi wa habari, lakini waandishi wa habari mbali tu wana mishahara midogo na mazingira yao magumu nilizungumzia sala zima la makato yao ya mwezi hayapelekwi na sijasikia kabisa Mheshimiwa Waziri kama amelijibia hili.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye ripoti ya CAG amezungumza waajiri wengi hawapeleki michango na moja ya maeneo ambao waajiri ni baadhi ya wamiliki wa vyombo vyia habari binafsi na vyia umma hawapeleki michango ya wafanyakazi wao na hata wengine wanaopeleka wanapeleka kwa kucheleva. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nakuja jioni kwenye Bunge hili Mheshimiwa Waziri nimekutana na mzee wangu mmoja mwandishi wa habari, *very senior*, amestaafu, ameenda kudai mafao yake ameambiwa chombo chake hakijapeleka, huku mmekusahau mna-deal/kwenye viwanda na maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitaji *commitment* ya Serikali, lini mtavibana baadhi ya vyombo vyia habari ambavyo havipeleki michango, mwandishi anakuwa na *stress* ya mshahara mdogo, mazingira duni na pia hata fedha yake ya msingi baada ya kazi nayo? Ninahitaji *commitment* ya Serikali. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana na niendelee kuwashukuru waheshimiwa Wabunge na nimewasikia Wabunge kadhaa ambao wamekuwa na *concern* hiyo kwanza ya kuhakikisha kwamba tunasimamia mapato halisi yaani ya viwango vinavyokidhi vyia mishahara kwa ajili ya waandishi wa habari, lakini eneo la pili ni hili la mafao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Ester amesema jambo la maana sana kwenye tasnia ya habari kwa kweli tuna matatizo, waajiri wengi wamekuwa wakikiuka sheria za kazi na hasa katika suala zima la kulipa mishahara inayotakikana kwa mujibu wa sheria, lakini pia tumekuwa tukipokea mashtaka mengi baadhi ya waajiri ama wamiliki

wa vyombo nya habari ambao wamekuwa pia hawawasilishi michango hiyo kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikuthibitishie wapo wamiliki wa vyombo nya habari ambao ni sugu katika kuwasilisha michango hiyo na kulipa mishahara kwa waandishi wa habari inavyotakiwa. Nimhakikishe tu Mheshimiwa Ester Bulaya kuwa Serikali inawatambua hawa na tumeshaanza kazi ya kuafuatialia na tumeshaagiza kwa Kamishna Mkuu wa Kazi sasa tuna *operation* maalum ya kwenda chombo kimoja baada ya kingine na ninaomba kuititia Bunge lako Tukufu niwaelekeze kwa kweli wamiliki wa vyombo nya habari kutenda haki kwa waandishi wa habari nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waandishi wa habari nchini wanapokwenda kuwajibika kama wafanyakazi kwenye vyombo nya habari ni wafanyakazi wenyewe haki sawa kama wafanyakazi wengine kwenye Sekta nytingine. (*Makofi*)

Kwa hiyo Mheshimiwa Ester nakuomba tu umwachie Mheshimiwa Waziri mshahara wake, tutashirikiana wakati mwingine na nyie Waheshimiwa Wabunge mtusaidie pia kutambua hayo maeneo ambayo bado ni sugu ili tuendelee kuyafanyika kazi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri nakumbuka ulishatoa ufaanuzi hapa kwamba sio kazi ya mfanyakazi kufuatilia kama mwajiri amepeleka au hajapeleka ni kazi ya chombo husika kwa maana ya Hifadhi ya Jamii ndio sheria wamewapa kufuatilia yale malipo.

Kwa hiyo nafikiri wale watu ambao wanapata changamoto huko waweze kama hivi Mheshimiwa Mbunge kama ana kesi mahsus ni nadhani akikuleta Mheshimiwa Waziri itakuwa rahisi zaidi ili Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii isiwanime watu mafao kwa maana kwamba waajiri wao hajapeleka kwa sababu wao hamna sehemu yoyote wanahuksika kwenye jambo hili. *Guillotine Katibu!*

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**FUNGU 96 - WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI,  
SANAA NA MICHEZO**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management</i> .....	Sh. 4,960,535,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 316,960,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 433,316,000
Kifungu 1004 - <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh. 243,253,000
Kifungu 1005 - <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 221,240,000
Kifungu 1006 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 85,470,000
Kifungu 1007 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 273,418,000
Kifungu 1008 - <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh. 84,018,000
Kifungu 6001 - <i>Culture Development Division</i> ...Sh.	1,344,246,000
Kifungu 6004 - <i>Sports Development</i> .....	Sh. 2,703,049,000
Kifungu 6005 - <i>Arts Development Division</i> ....Sh.	5,617,667,000
Kifungu 7003 - <i>Information Services</i> .....Sh.	17,743,630,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 96 - WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI,  
SANAA NA MICHEZO**

Kifungu 6001 - <i>Culture Development Division</i> .....	Sh. 2,015,000,000
Kifungu 6004 - <i>Sports Development</i> .....	Sh. 12,449,000,000
Kifungu 6005 - <i>Arts Development Division</i> .....	Sh. 250,000,000
Kifungu 7003 - <i>Information Services</i> .....Sh.	6,001,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi zake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja Taarifa.

### **T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake kifungu kwa kifungu kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote kuwapongeza sana Mheshimiwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waziri na Naibu Waziri na watendaji wao walioko hapa kwa kuleta bajeti nzuri ambayo kwa mujibu wa taarifa ambayo Kamati yetu ya Huduma na Maendeelo ya Jamii imeleta hapa nidhahiri kwamba mmesikiliza mawazo yao mengi na mmeahidi kuyafanya kazi na yale ambayo mlikuwa mmeshindwa kuyachukua safari hii tunaamini kwa kadri yalivyoainishwa kwenye ile taarifa ya Kamati ambayo inafanya kazi kwa niaba ya Bunge mtayazingatia katika utendaji kazi wenu.

Kwa kuwa Bunge limepitisha mafungu kadri mlivyokuwa mmeomba nasi tunawatachia kheri katika utekelezaji wa yale yote ambayo mmeyaahidi kuyafanya na sio hayo tu na mengine mengi kama ambavyo Wabunge wamependekeza mabadiliko hapa na pale, mengine sio mabadiliko ya kifedha, kwa hiyo hayahu su bajeti, lakini yanahu su utendaji kazi wenu kwasababu fedha za kurahisisha huo utendaji mmepewa na Bunge ninaamini yale yote waliyoyasema Wabunge mtayatilia maanani na mtayafanya kazi, tunawatachia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mambo machache kwanza ni tangazo la wageni; tunao wageni humu ndani ambao ni watoto wa Mheshimiwa Pauline Gekul na hawa ni Ndugu Irene Silaha sijui yuko wapi Irene Silaha, haya nafikiri ametoka kidogo, lakini yupo Heaven Suleiman na Eliza Manda; haya karibuni sana, nadhani mmemuona hapa mama akiwa kazini, kwa hiyo akichelewa kurudi nyumbani msiwe na maswali mengi sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Jafo anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwamba siku ya kesho kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa na neno ama tamko kuhusu Wiki ya Mazingira kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hii mnakaribishwa kesho baada ya kipindi cha Maswali na Majibu asubuhi mnakaribishwa katika Ukumbi wa Hazina ndiko ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu

ataenda kutoa hilo tamko na Kamati hii ya Bunge wanaalikwa kwenda huko.

Waheshimiwa Wabunge, yamechangiwa mambo mengi hapa na mimi niwashukuru Wabunge mlivyoonesha msisitizo kwa vijana wetu ambao wanajitahidi kutengeneza ajira kwa ajili ya vijana wengine, lakini hata wao wenyewe wamejita futia ajira badala ya kusubiri. Vijana wetu wanaojishughulisha na michezo, sanaa na mambo yote ambayo yapo chini ya Wizara hii wanajitahidi sana na mimi niwaombe Wizara kwa namna yoyote ile kwa sababu hawa vijana wanatumia nguvu kubwa ya kwao wenyewe, ninyi mjitätahidi kuwasaidia wafanye vizuri zaidi kuliko kuweka ngazi ndefu wanashindwa kabisa kupanda kutoka pale ambapo wameweza kujisukuma wao wenyewe. Kwa maana hiyo vyombo vyote vilivyopo chini ya Wizara hii vinavyowasimamia hawa wasanii vilenge kuwasaidla kuliko kuwazuia kufanya kazi zao vizuri zile wanazozifanya.

Sasa ameeleza Mheshimiwa Keisha hapa kuhusu mavazi na mambo kama hayo, nchi nyininge ukienda wameeleza wazi ni maneno gani hayatumiki nchi hiyo, kwa hiyo, mtu akiimba yaani anajikuta haruhusiwi hata kuimba maana hayo maneno nchi hiyo hayaruhusiwi, hapa nimtolee mfano kwa sababu ni ndugu yangu sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo jina Adolf haliruhusiwi Ujeruman, mtoto hawezи kupewa jina la Adolf. Kwa hiyo sasa kule wanajua kabisa hata msanii hawezи kuimba, naona Mheshimiwa Waziri ananiangalia, ama limeruhusiwa siku hizi? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Hapana.

**NAIBU SPIKA:** Ni kwa sababu ya Adolf Hitler. Kwa hiyo watoto kule hawapewi hayo majina kwa sababu hiyo tu. Sasa kule maana yake msanii anafahamu hata angetaka kuremba vipi wimbo wake na *movie* yake na kitu kama hicho hawezи kutumia. Hata hapa kwetu basi tutengeneze huo utaratibusi maneno hayo tuwe tunayaingiza yawe yanakua tunajua kitabu hiki akipewa msanii hayo maneno asiyaseme, kuliko amejipanga ameweka ukamwambia akabadilishe,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wimbo hauwezekani tena kuubadilisha kwa sababu yeye alivyokuwa anapanga beti zake alijua hivyo ndio ataeleweka. (*Makof*)

Kwa hiyo, tujitahidi na sisi na yale ambayo ni ya kawaida sana basi tuyaache yawe ya kawaida, yaani tuisiyafanye ni magumu sana hata maneno ambayo yapo kwenye Kamusi zetu za Kiswahili. Kama yapo kwenye Kamusi maana yake ni maneno yanayoweza kutumika katika hali ya kawaida.

Kwa nafasi hii Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda alileta ombi, lakini sasa kwa sababu mimi sio Serikali kwa hiyo siwezi kujibia humu ndani, lakini ni wazi hoja yake imepokelewa ya kuhusu wanaopigana masumbwi wanawake tutajitahidi ili tuwasaidie. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe kama ambavyo wawakilishi wetu humu ndani wamesema tuwa-*support* vijana wetu, tuwatie moyo, kama kijana wetu Diamond anafanya vizuri na sidhani kama ni sahihi watu kuanza kufikiri anaweza kukaa upande huu au upande huu.

Wakati anachangia Mheshimiwa Taletale ameeleza mambo mengine vijana huyafanya kwa sababu yanawapatia fedha kwa maana ya huko mtaani tunaita kiki. Sasa wewe humu ndani unaweza ukahisi fulani na fulani wanagombana au hata sisi huko nje wakati mwengine mashabiki wanadhani msanii huyu na msanii huyu wanagombana, lakini huenda wao ni marafiki ila ule ugomvi ni lazima uwepo ili mjue kwamba kuna ushindani. Kwa hiyo ni mambo ya kawaida kwenye sanaa yao na sisi tuwasaidie hawa vijana kufanya vizuri hasa wanapofika ngazi hiyo ambayo wanakwenda kuwakilisha nchi yetu. (*Makof*)

Kwa namna hiyo hiyo, sisi kama wawakilishi wa wananchi tujitahidi kuzungumza na wananchi wetu wale tunao wawakilisha, wananchi wenzetu, viongozi wenzetu wajitahidi kuzungumza kwa namna ambayo nchi yetu

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

itapata nayo mwakilishi na sifa nzuri huko nje kwenye mambo kama haya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2:00 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 1 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*